

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 18 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wakati dunia ilipopata msukosuko wa kiuchumi, nchi mbalimbali zilichukua tahadhari kadhaa ikiwa ni pamoja na kuyaangalia makampuni ambayo yamepata hasara, wananchi au taasisi mbalimbali ambazo zimepata hasara, lakini vilevile taathira ambazo zilizokwenda moja kwa moja kwa wananchi.

Hapa kwetu Tanzania imetangazwa *package* ya kuwasaidia au kuwakopesha wafanyabiashara na wenyewe makampuni. Kuna sababu zozote za Serikali kushindwa kutangaza *package* ya hasara waliyopata wakulima wa pamba, karafu, na wafugaji? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu rafiki yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed swali lake kama ifuatavyo; si kwamba Serikali imeshindwa kutangaza, kama kungekuwepo na hasara ya namna yoyote ile, tungetangaza na pengine tungkuwa na mikakati ya namna ya kupata suluhu ya jambo hili.

Lakini kwa kutumia mifano michache aliyoitumia, labda nikiondoa karafuu tu kwa sababu sina takwimu zake. Wakati mtikisiko huu unajitokeza kilichokuwa kimefanyika ni kwamba mazao kutoka kwa mkulima yalikwishanunuliwa yako mikononi ama kwa makampuni yanayohusika au kampuni zingine zinazohusiana na usafirishaji. (*Makofi*)

Ndiyo maana unaona zoezi zima linatazama makampuni haya kwa sababu yamekopa fedha ili kuweza kununua mazao hayo. Na ndiyo maana fidia umeona imelenga kurejesha ama kuahirisha riba kwenye makampuni yanayohusika. Tatizo tunalolipata sasa ni msimu unaokuja baada ya makampuni haya kusaidiwa na kuwezeshwani matumaini ya Serikali ni kwamba yatarejea zoezi la kununua mazao ya msimu huu. (*Makofi*)

Lakini rai ya Wabunge ni kwamba kwa sababu ya mtikisiko inaonekana bei haiwezi kuwa nzuri kama ilivyokuwa msimu uliopita, pamba mathalani wameanza na shilingi 360 lakini msimu uliopita walifika mpaka shilingi 500 kwa kilo na zaidi kidogo. Na ndiyo maana unaona wanaiomba Serikali kidogo kwamba jamani hebu tafuteni njia kama mnaweza angalau bei iongezeke kidogo ndiyo maana kusema kweli hukuona Serikali hatukujikita sana kwenye eneo hilo, sasa sina takwimu juu ya karafu kwa sababu si mtaalam wa eneo hili. Lakini kwa upande wa Bara hivyo ndiyo imetokea kwenye korosho, kwenye pamba na mazao mengine. (*Makofii*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Inaelekea kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hakukuwa na mipango madhubuti ya kuangalia tatizo lenyewe kwa kina.

Kwa mfano inaeleweka kabisa hawa wanunuzi wa pamba, korosho na kadhalika, ambao walikwenda Benki kukopa na hatimaye bei ya dunia bado inaendelea kuwa ndogo, hili lilikuwa linajulikana. Hivyo kama kungekuwa na mipango mizuri tangu mwanzo wakulima hao wangeweza kufikiriwa mapema kwa maana wao watakuwa na taswira ya upungufu wa bei katika mazao yao.

Huoni kama kuna upungufu wa kuliangalia tatizo lenyewe kwa undani zaidi na kwa upana zaidi? Tatizo tunalolipata, tunashughulikia makampuni machache, badala ya kushughulikia wale wazalishaji wakuu wa chakula na mazao mengine? (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Hamad huu ni mtikisiko, ni jambo limetokea katika mazingira ambayo wote tunalazimika kulishughulikia. Ingekuwa kwamba ni jambo ambalo unaliona katika *context*, limeandaliwa, linakuja, mnalionia, mnazungumza, ingekuwa kitu tofauti kidogo.

Lakini kwa hali ilivyo sasa ilibidi tuanze na hatua moja ili tuone itatupeleka wapi maana mimi nachokisema Mheshimiwa Hamad, kama Serikali isingechukua hatua hii ya angalau kusaidia makampuni haya kitu ambacho kingetokea leo, ni kwamba hata kununua bei hiyo kwa shilingi 360 isingewezekana, kwa sababu wangesumbuana, riba wangekuwa wanadaiwa na benki. Ndiyo maana tukasema ili kuwezesha angalau ununuzi kuendelea hata kama ni kwa kiwango hicho cha chini. Lakini angalau kazi hiyo isiachwe pamba ikaachwa ikiharibika au mazao mengine yakaharibika. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi nataka niseme tu kwamba Serikali kwa upande wake imejitahidi sana, suala ambalo tunaweza kuendelea kuliangalia ni hili ambalo limejitokeza sasa kwa sababu bei ziko chini, tunafanyaje? Sasa tungkuwa na mfumo wa mauzo awamu ya kwanza na ya pili mimi ningesema pengine kama hali itaendelea kuboreshwa inawezekana pamba ikapanda zaidi kidogo tukawalipa kwenye mkupuo wa pili. Lakini kwa mazingira ya pamba hilo haliwezekani, korosho tunaweza kwa sababu ile iko *controlled* vizuri sana. Sasa tuiachie Serikali kama itapata uwezo *allhamdulilah* tukikosa

tunakwenda kupiga magoti kwa Mzee Cheyo pale na kumwambia chonde, chonde, kubali liendeleee. (*Makofi*)

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii naomba nimwulize swalilifuatalo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa katika kipindi hiki kifupi cha uongozi wako umeonyesha umejjijengea hazina kubwa sana ya uadilifu na utawala bora.

Na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ameonyesha waziwazi dhamira yake ya kutenganisha siasa na biashara. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unaweza kuliambia Bunge hili kwamba Serikali katika Mkutano huu wa 16 au ujao wa 17 italeta kwa Hati ya Dharura Muswada wa Sheria ya Kutenganisha Siasa na Biashara? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mwambalaswa kwa kuulizia jambo hili lakini labda nianze kwa kusema kwamba unajua masuala ya uadilifu haya, zaidi ni mtu mwenyewe, ni *conscious* yako zaidi kuliko kitu kingine chochote. Unaweza ukaja na sheria nzuri sana za kila aina lakini kama wewe mwenyewe ni mbiniasi bado hata sheria zikipita utafanya tu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi muda wowote nasema rai kwa Watanzania na hasa sisi tuliomo kwenye utumishi wa umma ni vizuri kila mmoja akawa muda wote anasema kabeba dhamana ya watu. Lazima kujitahidi kukataa vishawishi vyakulupeleka huko, tumo kwenye utumishi humu si kwamba hili jambo halina maeneo ambayo tunadhibitiwa, yapo, lakini nyie Wabunge mashahidi, nenda kwenye Serikali za Mitaa, nenda kwenye vituo vingine bado kelele za uadilifu bado zipo. *More so* ni sisi wenyewe, *more so* ni wewe *as a person* wewe biniasi ndiyo kwanza uchukue hilo jukummu la kujisafisha na kukataa baadhi ya vitu hivi. (*Makofi*)

Lakini kuhusu swalilifu lako, ninachosema tu ni kwamba bahati nzuri Serikali jambo hili ni moja ya mambo ambayo Rais aliagiza na tuliahidi kufanya. Hivyo mchakato umeshakwenda mbali, siwezi nikakuahidi kuwa Bunge lijalohi lakini nachowenza kusema kwa uhakika kwamba kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao hiyo sheria itakuwa imeshaletwa, kwa sababu tulilenga Uchaguzi Mkuu ujao hili jambo liwe limekwisha. (*Makofi*)

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, asante. Mheshimiwa Waziri Mkuu yahusu vitambulisho. Mwaka 1986 nchi hii ilipitisha sheria ya kuweza kupata vitambulisho kwa raia wetu, Miaka 22 imepita sasa bado vitambulisho hivyo havipo. Mwaka jana mwezi wa kumi. Mheshimiwa Waziri Mkuu ulituambia kwamba mchakato unaendelea, kwenye Kamati ambayo nami nimo inayohusikana na Wizara hii bado tunaambiwa mchakato unaendelea na waraka unaandalialiwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nia yangu sio kujua nani anayekwamisha na kwa sababu gani na wala Watanzania hawataki kujua hilo, nia yao ni kupata vitambulisho. Ninakuomba, kwa sababu nimeenda kwenye mkutano mmoja wakasema

Watanzania wazuri sana kwa kupanga mipango na kusaidia nchi zingine lakini ya kwenu yanalala imebidi niwahi nikuulize hili swalii. (*Makofii*)

Sasa kwa sababu umesema uadilifu ni mtu mwenyewe na wewe ni muadilifu na wote tunajua na wewe ndiye mwenye mamlaka, unaonaje sasa ukiamua mamlaka hii ambayo ni mamlaka kamili kisheria ihamie ofisini kwako ili kazi ianze na hatimaye Desemba, 2009 tuweze kuwa na vitambulisho? (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mama Shellukindo ni kama anasema kwamba huko iliko hakuna waadilifu. Hapana! Sio hivyo, niseme kwamba ni bahati mbaya sana jambo hili kila linapokwenda, likipiga hatua kadhaa unakuta linasimama kwa sababu moja au nyingine na mnajaribu tena mnaanza upya. Linakwenda, mnarudi tena nyuma hatua moja. Lakini nataka nikuhakikishie tu kwamba tulipofika sio mahali pabaya sana. Hili zoezi limeshakwenda hatua kubwa tu, tunachosubiri sasa ni zoezi hilo lifike kwenye *Cabinet* tufanye uamuzi ili tuweze kukamilisha zoezi hili mapema inavyowezekana. Ni bahati mbaya sana limechukua muda mrefu lakini yaliyopita si ndwele wacha tugange yajayo. (*Makofii*)

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu hayo tumekuwa tukiyapata kwa muda mrefu kwamba tusubiri Baraza la Mawaziri na waraka. Mimi nilikuwa naomba kitu kimoja Mheshimiwa Waziri Mkuu kama utaruhusu kabla ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani tupate taarifa mchakato umefikia wapi ndani ya nyumba hii. (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nilichokisema ndicho atakachokisema Masha, kwa sababu mimi ndiyo nasimamia shughuli za Serikali, ndiyo maana nimekuambia kwamba ukivuta subira jambo hili litaisha. Najua linaudhi wengi kwa sababu limechukua muda mrefu sasa hatuwezi kuacha kusema, tutaendelea kusema na ukiona tunachelewa na wewe utaendelea kusema hivyo hivyo mchakato, mchakato na mimi nasema karibu utakwisha lazima tufike mahali sasa liishe. Ndiyo maana nimesema hatuko mbali na mwisho wa zoezi hili. (*Makofii*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna kauli ambayo ndiyo imeanza kutumika sasa kwamba, “Kilimo Kwanza”.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakulima wa kahawa kwa kupitia waraka uliotoka Wizara ya Viwanda na Biashara wanalamishwa kununua magunia ya Katani badala ya *Jute*. Magunia ya Katani yanauzwa kwa shilingi 3,000 wakati mwingine mpaka shilingi 3,800 wakati magunia ya *Jute* yanauzwa shilingi 800. Wakulima wa kahawa wanalamishwa kununua haya magunia wakati kahawa ikifika kwenye vinu vya kukoboa na ikishatoka kwenye vinu vya kukoboa wakati inapelekwa *Tanga Port* kwa ajili ya kuwa *exported*, magunia yale yakifika Tanga yanatupwa na kahawa inawekwa kwenye makasha maalum.

Sasa swalii Waziri Mkuu, wakulima wa kahawa wamenituma, uwaondolee huu mzigo wa kulazimishwa kununua magunia ya Katani. (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimemwelewa Mheshimiwa Kimaro. Mimi nimekusikia, nimekuelewa sijauona huo waraka lakini inawezekana upo, ukiniuliza kwa nini pengine tumetoa waraka huo naweza pengine nikashindwa kusema kwa uhakika. Lakini inawezekana ni kwa nia nzuri tu na rai ya Wabunge wengi hapa ndiyo lugha mnayoitumia kwamba lazima tutafute kila namna ya kusaidia kulinda viwanda vyetu vya ndani. Inawezekana hilo limefanywa inategemea haya magunia yanatengenezwa wapi. Lakini naamini yatakuwa yanatengenezwa na Katani hapa ndani na pengine na viwanda vya hapa ndani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama mtazamo ni huo tuna kila sababu ya kutafuta njia bora ya kulinda viwanda hivyo ambavyo viko hapa ndani, tungeweza kabisa kwa msingi huo huo hata hiyo unayoiita *Jute* tukaipiga ushuru mkubwa sana au tukapiga marufuku kabisa isionekane hapa nchini ili tuweze kufanya hilo zoezi kwa maslahi ya viwanda vyetu. Lakini hatukufanya hivyo na pengine ndiyo maana unaona tunapata maelezo kwamba *Jute* ni rahisi zaidi kuliko gunia. Sasa nitakuwa sina maelezo ya undani sana pengine niachie na Waziri wa Viwanda na Biashara tujaribu kuona tatizo liko wapi pamoja na Wizara nitazungumza Kilimo na Ushirika halafu pengine tunaweza kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. (*Makofi*)

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu katika mkutano wake wa 12 wakati ambapo unafunga Bunge ulizungumzia kuhusu matatizo ya somo la Hisabati katika shule zetu na ukasema kuwa utafanya utafiti. Je, utafiti huo umefanyika na kama bado kwa nini? Na kama tayari taarifa ya utafiti huo iko wapi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo matatizo ya maswali ya papo kwa papo. Maana Mheshimiwa Zubeir ungekuwa umeni-*tip* mapema ningekuwa nimeshauliza nikajua hivi utafiti umekamilika, maana yako mambo mengi Serikalini humu na Waziri Mkuu kichwa kimoja. Sina jibu la moja kwa moja kwa hilo labda nipe muda nijaribu kuuliza vile vyombo vinavyohusika tumefika wapi halafu baadaye ninaweza nikakupa jibu la uhakika zaidi.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu leo walijitokeza wanne tu na hao wanne wote ni wa CCM, nadhani hii ni ishara kwamba unayajibu vizuri mno kwamba mtu anatafakari sana kabla hajaenda kujiorodhesha jina, ni jambo zuri sana.

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwenye maswali ya kawaida leo swali la kwanza linalekezwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na linaulizwa na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 62

### **Utaratibu wa Kupata Viongozi Wanaoandamana**

## **na Viongozi Wakuu wa Nchi Nje ya Nchi**

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI** aliuliza:-

- (a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuwachagua Viongizi wanaofuatana na Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wanapofanya ziara nje ya nchi?
- (b) Je, ni viongozi wa makundi yapi wameshafuatana na Viongozi hao kwenye ziara zao nje ya nchi?

## **WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, swalii lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika katika kuchagua nani afuatane na Viongozi wa juu wanaposafiri unazingatia vigezo kadhaa kama ifuatavyo:-

Ukiacha wapambe wa Viongozi hao pamoja na Maafisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambaa hawana budi kufuatana na viongozi wetu kwa mujibu wa Itifaki, wapo viongozi wanaoteuliwa kuijunga na misafara hiyo kufuatana na kusudio na madhumuni ya safari hizo.

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa viongizi hao hufanywa na Ofisi za Viongozi hao kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ofisi ya Makamu wa Rais na kwa upande wa Zanzibar Ofisi ya Rais wa Zanzibar na kwa hapa Bungeni pia Ofisi ya Mheshimiwa Spika huhusishwa katika uteuzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika uteuzi huo vigezo kama vile jinsia, uwakilishi kutoka pande zote mbili za Muungano na pia uwakilishi kutoka Upinzani huzingatiwa. Aidha, kila wakati viongizi Wakuu wanaposafiri nje ya nchi Waandishi wa Habari wamekuwa wakijulishwa katika misafara hiyo.

Pale inapotokea kuwa Viongizi wamekaribishwa kutembelea nchi jirani basi Wakuu wa Mikoa inayopakana na nchi hizo huteuliwa kufuatana na Viongozi hao.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kifupi na kwa kuzingatia vigezo nilivyovitaja hapo juu, makundi ya viongizi yanayofuatana na Viongozi Wakuu wa nchi ni Mawaziri mbalimbali kutoka pande zote mbili za Muungano, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watendaji kutoka Idara mbalimbali za Serikali kutegemeana na madhumuni ya ziara hizo.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa masuala ya nyongeza kutokana na makundi ambayo ameyaeleza bado kuna makundi ambayo nilitegemea atayazungumzia.

Mara nyingine husikia viongozi wa juu wakienda ziara za nje husikia wamefuatana na wafanyabiashara wakuu, wanaoshughulika na uchumi na mambo mengine, wale huwa wanakuwaje?

Halafu hata hivyo hatuoni kwamba wakati umefika kwamba pia wachukuliwe mwakilishi kama wa makundi ya vijana, makundi ya wanawake au na makundi ya watu wenye ulemavu? Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, nimemwelewa sana na ningependa kumhakikishia kwamba *ishallah* baada ya muda mfupi tutayazingatia makundi hayo akiwemo yeze mwenyewe. (*Makofi*)

**MHE. MHONGA S. LUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi tuna matatizo ya uchumi kwamba na safari hizo huwa zinachukua watu wengi sana kiasi kwamba matumizi mengine yanakuwa sio ya lazima.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kupunguza ukubwa wa misafara ili pesa zinazoweza kutumika ziwe kidogo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba ukubwa wa misafara inaongeza gharama kubwa za matumizi, katika kipindi cha mwaka 2008 Serikali kupitia Bunge hili ilikuwa imetengewa shilingi bilioni 8 kwa ajili ya usafiri.

Ni kweli kutokana na majukumu makubwa na mazito ya Serikali pesa hizi zinaonekana hazitoshi na sababu moja ni ukubwa wa misafara. Mheshimiwa Rais ameagiza kulifanyia kazi suala hilo na Mungu akitusaidia baada ya muda si mfupi misafara ya viongozi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu yatakuwa na kiwango maalum cha watu wanaotaka kusafiri ili kupunguza matumizi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi nami niongeze swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa moja wapo ya madhumuni ya safari za nje ya nchi kwa viongozi ni kujifunza na kwa kuwa kujifunza kungekuwa na manufaa kama yale mafunzo yanaweza yakaja ndani ya nchi yakaboresha shughuli zetu ndani ya nchi.

Je, ni kwa kiasi gani ziara za nje ya nchi kwa viongozi zimesaidia kuboresha *VIP Lounge International Airport* ili iwe kuwa na hadhi ya kimataifa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba safari zinazofanywa na viongozi nchi za nje pamoja na mambo mengi zinatoa fursa ya watu wanaokwenda huko nje kujifunza namna mambo yanavyokwenda kwenye maeneo kadhaa. Mheshimiwa Spika, kuhusu na itifaki na hadhi na uwanja wa kimataifa nina amini kabisa watu wa Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam, Meya wa jiji la Dar es Salaam na viongozi kadhaa wamekwenda nchi mbalimbali duniani kujifunza mambo yale yanavyokwenda na nina hakika mkatuba mpya wa kampuni ya Kichina ambao utakuwa unaangalia ujenzi wa kiwanja kipywa cha kimataifa cha Dar es Salaam kitazingatia uwepo wa ukumbi mzuri wa VIP.

Hali kadhalika utaangalia hadhi ya sehemu ya mapokezi na ujenzi wa hoteli ya kimataifa itakayohifadhi wageni watakaokuwa wanapita kwa muda. Mambo hayo yanazingatiwa na yanatokana na mafunzo wanayoyapata viongozi wetu wanaposafiri huko duniani. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii baada ya majibu mazuri ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ina mpango madhubuti wa ujenzi wa jengo la mapokezi la viongozi wakuu ama *VIP lounge*, kazi hiyo itaanza ndani ya mwaka huu 2009 na matarajio tutamaliza ndani ya 2009. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante kwa majibu hayo yanatoa mwanga zaidi.

Na. 63

**Tanzania Kufungua Balozi Jijini Jerusalem**

**MHE. LAZARO S. NYALANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa, mataifa mengi duniani yakiwemo yale ya Umoja wa Nchi za Afrika (AU) yamefungua Ofisi za Kibalozi jijini Yerusalem, ambao ndiyo mji mkuu wa nchi ya Israel;

Je, ni lini Tanzania itafungua Ofisi ya Ubalozi katika jiji la Jerusalem ?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBOYA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri a Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu (Singida Kaskazini) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge naomba nitoe ufanuzi kama ifuatavyo; Israel ina miji mikubwa miwili. Mji wa Tel Aviv ambao ni

Makao Makuu ya Serikali ya Israel na hapo ndipo kwenye Balozi za nchi nyingi kutoka Afrika, Ulaya, Amerika ya Kusini na Amerika ya Kaskazini. Mji wa Jerusalem ambao pia ni wa kihistoria, hauna Balozi kamili bali lakini ziko Balozi ndogondogo zipatazo 17 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufanuzi huo, naomba sasa kijibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo uhusiano wa kibalozi kati ya Tanzania na Israel. Lakini Serikali yetu haina ofisi pale Jerusalem, wala haina ofisi pale Tel Aviv. Balozi wa Israel nchini Tanzania anayo makazi yake Mjini Nairobi, Kenya na wenyewe hawana ofisi Dar es Salaam. Balozi wa Tanzania nchini Israel anayo makazi yake Mjini Cairo, Misri na anahudumia shughuli za kibalozi Israel kwa maana ya Tel Aviv Jerusalem. Azma ya Serikali yetu ni kuwa na ofisi za Ubalozi kwenye miji husika hasa zenyeh maslahi na tija taifa letu. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti tunalazimika kutoa huduma za kibalozi kutoka nchi jirani kama ilivyo kesi hiyo ya Israel kutolewa huduma na Cairo.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa kazi kubwa na nzuri na ya kuheshimika anayoifanya nje ya nchi. Naomba nimuulize maswali mawili madogo ndani ya nchi, kwanza uhusiano wetu Tanzania na Israel una significant mbili kubwa. *Significance* ya kwanza ni ya kihistoria, katika Jerusalem, nahii unaweza ukawekwa balozi Tel Aviv au Jerusalem ni kama dakika ishirini tu kwa gari kwa hiyo siyo mbali.

Katika Jerusalem msikiti wa pili demoscrolias upo mji wa Yerusalem, lakini point pili, significance nyingine ni kwa wakristo ni kwa wayahudi na watu wengine kwa hiyo nchi ya Israel kwa ujumla ina umuhimu mkubwa sana uliopo kihistoria duniani, ndiyo maana mataifa mengi yameweka balozi zao pale. Je, Serikali halioni hilo?

La pili, ningetaja nchi kadhaa na ninaomba niitaje Egypt yenyewe. Egypt ilikuwa ni moja ya nchi za kwanza kabisa Afrika kuweka Ubalozi mkubwa sana Israel. Kenya wameweka ubalozi mkubwa sana, *South Africa*, Rwanda na Uganda kwa pamoja zina *Military Cooperation and Technology Transfer, Technology Transfer* kubwa wanayofanya kati ya Israel na haya mataifa.

**SPIKA:** Lenga kwenye swali tadhali!

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Swali langu sasa ni kwamba tukizingatia na historia yetu ya JKT na kadhalka Waziri anaweza akakubaliana na mimi kwamba kuna significance ya kimaendeleo katika uhusiano huu na Israel?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kama ifuatavyo:-

Moja, ni kwa kweli kabisa kwamba umuhimu wa nchi mbalimbali kuwepo Israel umuhimu huo upo lakini kubwa la muhimu ni kuwa na ubalozi na kama nilivyosema Tanzania na Israel tuna *maintain* au tunao uhusiano wa kibalozi na kama nilivyosema hali ya kiuchumi ikeruhusu si vibaya kuwa na Ofisi zetu moja kwa moja pale katika Jiji la Jerusalem.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kuwakumbusha tu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba miaka ya 70 na 80 nchi nyingi za Kiafrika zaidi ya 33 zilikuwa na uhusiano mzuri na Israel mpaka baada ilipotokea vita kati ya Israel na *Egypt* na baada ya *operation* ya kuokoa mateka iliyofanywa na Israel nchini Uganda. Katika kipindi hicho ndiyo Serikali ya *Egypt* ilizomba nchi za Afrika kuvunja uhusiano wa Kidiplomasia kati ya Israel na nchi za Afrika kama njia moja ya kuonyesha mshikamano dhidi ya uvamizi uliokuwa umefanywa na Israel kwenye milima ya Sinai na Golan *Haits*.

Lakini pia baada ya wao kwenda Uganda kuchukua mateka wao nchi nyingi za Kiafrika walikasirika kwamba wali *-violate air space* na kwa hiyo nchi 33 za Kiafrika zilivunja uhusiano na Israel. Lakini baada ya makubaliano ya *Camp David* Kati ya Hanry Kissinger wa Marekani pamoja na *Egypt* pamoja na Israel nchi nyingi za Afrika zimerudisha uhusiano wake na Israel na wanarudisha taratibu na sisi tumeanza kurudisha uhusiano huo.

Lakini kama nilivyosema pindi muda utakapopita tutapata nafasi ya kupatiwa majengo yetu mijini Jerusalem pamoja na Tel Aviv.

Umuhimu wa JKT, nao ni muhimu vyuo vya Kijeshi vya JKT vilianzishwa na Israel na viliungwa mkono na Waisrael na waliongeza sana uchumi hasa kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na nina hakika baada ya Serikali kuamua kurejesha shughuli za JKT hawa ni baadhi ya Wataalamu ambao wangeweza na watasaidia sana kuimarishe JKT katika nchi yetu.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri napenda kumwuliza kama ifuatavyo:-

Katika mambo ya Diplomasia ambao Wataalam wenyewe ndiyo hao akina Mheshimiwa Membe wanapenda sana kutumia *reciprocation*. Taifa la Palestina kwa muda mrefu sasa limekuwa na Balozi katika nchi yetu hivi ni sababu zippi zilizopelekea mpaka leo nchi yetu haina Balozi katika nchi ya Palestina?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa kama ifuatavyo:-

Kama Waheshimiwa Wabunge na Taifa linavyofahamu wenzetu Wapalestina wanayo Mamlaka ambayo inaitwa *Authority* lakini hawana *viable land* hawana mahali unapoweza kusema hii ni nchi yao yenyenye mipaka, utamaduni na *culture* na vita iliyopo sasa hivi kati ya Israel na Parestina na Dunia ni ya kuwaomba Waisrael wawapatie kitu kinachoitwa *a Viable Land* Ardhi ambayo wanaweza wakatengeneza Serikali yao yakawa Makao yao Makuu ya Serikali na kuziruhusu nchi nyingi duniani kuwa na nafasi zake za kufungua ubalozi kule.

Sasa hivi kilichopo ni kwamba wenzetu Wapalestina wana vitu tu sijui kama nitaeleweka hapo yaani itokee kwa mfano unawaita Wapalestina nchini Tanzania halafu unaenda pale Kigoma unawaambia hii ardhi ni yako, unaruka nao kwenda Lindi unawaambia hapa Lindi ni penu pia, halafu unafika Mwanza Nyamagana unawaambia na hapa ni penu.

Sasa sijui wewe unayefungua ubalozi utakwenda kukaa wapi pale. *Land* waliyokuwa nayo pale siyo *viable* ndiyo maana Tanzania pamoja na mataifa mengine yote duniani yanaishinikisha Israel kuwapatia Wapalestina Ardhi yao ambayo wataunda Serikali itakayoitwa *Government* na siyo *Authority* na hilo litakapotokea Watanzania tutakuwa wa kwanza kufungua Ubalozi Palestina.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, huwa tunakupata kwa nadra lakini tukikupata ndiyo hivyo tunakutumia vizuri. (*Makofi*)

Sasa ni zamu ya Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi na swalilinaulizwa na Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, kwa niaba yake jirani yake hapo Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

Na. 64

### **Utaratibu wa Kupata Miliki ya Mashamba**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH (K.n.y. MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, utaratibu wa kupata Hati Miliki za mashamba ni ngumu sana kwa wananchi wa kawaiida.

(a) Je, ni wananchi wangapi katika Mkoa wa Mwanza waliopatiwa Hati za mashamba yao hadi sasa?

(b) Je, Serikali itarahisisha lini taratibu za kupata hati za mashamba ili ardhi iweze kumkomboa mwananchi kutoka kwenye umaskini?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**  
aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, naomba nitoe maelekezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utoaji wa Hati Miliki za Mashamba na Viwanja unatawaliwa na Sheria Na. 5 ya Ardhi ya Vijiji, Sura Na. 114 na Sheria ya Usajili wa Hati Sura Na. 334.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Vijiji kabla ya Wanavijiji kumilikishwa mashamba yao, sharti la kwanza kijiji kiwe kimepimwa, kisha kijiji kipate Hati ya Ardhi ya Kijiji (*Village Land Certificate*) na kisha kijiji kifanyiwe mpango wa matumizi bora ya ardhi. Hatua hizi zikikamilika, ndipo mashamba ya wanakijiji yanaweza kupimwa na kumilikishwa kwa kupewa Hati miliki ya kimila (*Customary Right of Occupancy*) ambayo ina nguvu za kisheria kama Hati Miliki ya viwanja vya mijini (*Granted Right of Occupancy*).

Mamlaka ya utoaji wa Hati Miliki za kimila ni ya Serikali za Vijiji chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya, ngazi hizo zinahitajika ziwe na Masjala maalum za kutunza nakala za Hati hizo ni kumbukumbu zote za mashamba yaliyomilikishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kijibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vigezo vilivyotajwa katika maelezo yangu ya awali, utoaji wa Hatimili za Kimila kwa mashamba ya wanavijiji katika Mkoa wa Mwanza bado hazijaanza kutolewa.

Kazi ya kuandaa Mipango ya Matumizi bora ya ardhi katika kila kijiji na kupima mashamba ya wakulima wote vijijini inafanyika hivi sasa hapa nchini na ina gharama kubwa. Hivyo, imeanza kufanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 Mamlaka ya kuandaa Hati Miliki ya Kimila ni Serikali ya Kijiji na zinatakiwa zitolewe na kusajiliwa kulekule vijijini chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya.

Wananchi wanaohitaji kumilikishwa mashamba yao kwa kupewa Hatimiliki za Kimila wanatakiwa kuomba kuitia Serikali ya Kijiji ambayo nayo itahitaji kupata ridhaa ya Mkutano Mkuu wa Kijiji (*Village Assembly*).

Hata hivyo, hatua hii itawezekana tu endapo mipaka ya Kijiji husika imepimwa, kijiji kimepewa Cheti cha Ardhi ya Kijiji na Kijiji kiwe kimeandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi.

Kwa Mkoa wa Mwanza jumla ya Vijiji 116 tayari mipaka yake imepimwa na kati yake vijiji 134 vimekwishapata cheti cha ardhi ya vijiji. Hivyo kitakachofuata ni mchakato wa kupanga matumizi ya ardhi na upimaji wa mashamba na kumilikisha wanavijiji mara fedha zikipatikana kupitia Halmashauri za Wilaya husika.

Kuhusu utoaji wa Hati Miliki za Viwanda Mijini utaratibu umeharakishwa na kurahisishwa kwa kuanzisha Ofisi za Kanda ambazo zimepewa madaraka ya kutoa Hati Miliki na kuzisajili bila kupelekwa Dar es Salaam, Wizarani kama ilivyokuwa hapo zamani.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali ina mikakati mizuri sana kuhusu kutoa kipaumbele katika masuala ya kilimo hivyo kuwezesha wananchi kuweza kumiliki uchumi na kuwa na maisha bora. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuchelewa kujenga Ofisi hizi ili wanakijiji waweze kupata hati miliki za kimila inawacheleweshea maendeleo katika mambo yao ya kilimo?

Pili, Serikali sasa hivi imetenga Bajeti kubwa sana katika suala la kilimo, na wananchi raslimali yao kubwa ni ardhi waliyokuwa nayo. Je, ni mikakati gani sasa Serikali inaweza ikafanya kuwashirikisha wananchi wenyewe katika kujenga Ofisi hizi kama vile tunavyojenga shule za Sekondari, Msingi na Zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri ana kauli gani kuhusu hilo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika azma ya kuendeleza kilimo katika kutekeleza kauli mbiu ya kilimo kwanza Wizara yangu inao mchango kubwa kwanza kuhakikisha kwamba wanavijiji wanapimiwa mashamba yao na kupewa Hati Miliki kwa sababu wakishapata ile Hati Miliki kwanza anakuba na usalama wa mali yake ya shamba lake lakini vilevile atalilima vizuri, atalitunza vizuri kwa sababu ni mali yake na ana Hati.

Sasa tatizo kubwa kwa kweli si masjala tu kwa sababu masjala hatusemi kila mahali wajenge masjala hizi za kutunza hati miliki. Masjala inaweza kuwa ni Ofisi ya Kijiji iliyopo sasa hivi kikatengwa chumba kimoja wakakiimarisha vizuri ili kikawenza kutunza hizi hati miliki kwa sababu ni mali, inaweza ile hati miliki ukaenda benki ukaweka rehani ukapata mkopo.

Kwa hiyo, hii ya masjala ni jambo muhimu lakini siyo linalokwamisha, sasa hivi kinachokwamisha ni kwamba Halmashauri zetu hazitengi fedha kwa ajili ya kazi hii ambayo inagharama. Hazitengi fedha na baadhi ya Halmashauri hazina hata hao

Wataalamu wenyewe wa kupima hayo mashamba, baadhi ya Halmashauri hazina hata hivyo vifaa vya kupimia hayo mashamba.

Kwa hiyo, tunazungumza na Halmashauri kwamba watoe kipaumbele katika sekta ya ardhi kama wanavyotoa kipaumbele katika sekta nyingine ili tuwasaidie wakulima kuweza kupata mashamba yao, kupata hati miliki ili waweze kuendeleza kilimo kwa uhakika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawapa Wabunge watatu tu. Mheshimiwa Musalika kwa sababu ni Mkoa anaohusika nao, Mheshimiwa Job Y. Ndugai na Mheshimiwa John M. Cheyo.

**MHE. JAMES PHILIP MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, mpango wa MKURABITA unahusika sana na suala la ardhi, na kwa kuwa MKURABITA ipo kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2005 na kwa kuwa, Waziri amesema sasa hivi tatizo ni fedha kuweza kutimiza vigezo vilivyoulizwa. Kama ndiyo hivyo, kwa kuwa, mwaka sasa unaisha wa 2010 wa Ilani Waziri anaweza kuiomba CCM itoe MKURABITA kwenye ilani yake ya uchaguzi mpaka kipindi kinachokuja?

**SPIKA:** Tena swali hili limekwenda pazuri kwa sababu Waziri huyu ndiye Mkuu wa Idara ya Uenezi. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Philip Musalika Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi tumeweka huu mpango wa kurasimisha raslimali za Watanzania na biashara za Watanzania yaani MKURABITA.

Sasa anasema kwamba MKURATIBA tuuahirishe, hatuwezi kuuahirisha MKURATIBA kwa sababu ndiyo njia peke yake ya kuweza kuwasaidia Watanzania kwa sababu raslimali wanazo lakini kwa sababu hazijarasimishwa, hazijatambuliwa kisheria wanashindwa kuzitumia kupata mikopo katika benki.

MKURABITA umeanza haujaenea katika nchi nzima lakini umeanza na katika Mikoa ambapo umeanza umefanya kazi nzuri kwa mfano Dar es Salaam. Mfano mzuri Dar Es Salaam ambapo watu wanazo raslimali za nyumba wamejenga katika maeneo ambayo hayajapimwa, nyumba nzuri kabisa nyingine za ghorofa zipo katika maeneo ambayo hayajapimwa kwa hiyo hazina hati miliki sasa kuitia mpango huuu wa MKURABITA tumeanzisha utaratibu wa kuzitambua zile nyumba, kuzipa leseni za makazi na leseni hizo sasa wanaweza wakazitumia kupata mikopo. Kwa hiyo, MKURABITA umeanza na tunao mpango kabambe kabisa wa kufanya sasa MKURABITA huu uweze kuenea kwa kasi mpya katika Mikoa yote. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, suala la kumiliki ardhi ni jambo muhimu sana kwa hatua za kimaendeleo, na Mheshimiwa Waziri ameelezea hapa kwa kijiji lazima kwenye kijiji pawe na hati ya kijiji. pili, kijiji hicho kiwe kina hati ya matumizi ardhi. Tatu, kijiji hicho kiwe na masjala maalum kwa ajili ya hati hizo.

Lakini mwananchi akitapa kupata hati kwa ekari moja gharama ya upimaji ni kama kati ya shilingi 180,000/= hadi 250,000/= kwa maneno mengine ni gharama kubwa sana, na Wataalamu Wilayani hakuna na vifaa havipo.

Je, sasa kwa vile lengo la kilimo kwanza ni kuwakopesha wananchi matrekta na vifaa vinavyoendana na hivyo na ili wakope ni lazima wawe na dhamana na dhamana rahisi ni ardhi yao. Je, zoezi hili litawezekana kweli?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba namna moja ya kuwawezesha wanavijiji kupata uwezo wa kukopa matrekta na pembejeo mbalimbali ni kupata Hati Miliki ili wazitumie kupata hiyo mikopo ili kuendeleza kilimo chao. Hili katika hii Bajeti ambayo itakuja Wizara yangu, masuala haya yenyе mwelekeo huo wa kwenda kuwamilikisha Watanzania mashamba yameingizwa katika Bajeti ya mwaka huu kwa maana kwanza vile vijiji ambavyo havijapimwa kwa sababu sharti mojawapo la kupata Hati ni lazima kwanza mipaka ya kijiji iwe imeshapimwa. Vile vijiji vyote, ambavyo havijapimwa mwaka huu imewekwa fedha zitakazowezesha kupima mipaka ya vijiji vyote kwa sababu ndiyo sharti la kwanza.

Pili, katika kupata mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji kama moja ya masharti, Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, katika Bajeti ya Serikali ambayo nitakuja nayo safari hii imepewa fedha nyingi zaidi, imeongezewa pesa kwa karibu 20% ili kuongeza kasi ya kuweka mipango madhubuti ya ardhi. Tunachoomba tu Halmashauri nazo vilevile na zenyewe ziunge mkono kwa sababu kwa kweli zenyewe ndizo zenyе jukumu hili, Tume inakwenda tu kuwasaidia ili kwa pamoja tukishamaliza haya masharti mawili sasa itabaki kazi ya kupima hayo mashamba.

Ni kweli ukimwita peke yako waje wakupimie shamba lako hawa Wataalam wakija maana haji mtu mmoja wanakuja kama team kweli gharama ni kubwa. Kwa utaratibu ambao tumeshauanzisha na tumeanza katika Wilaya ya Babati na Bariadi kwamba tukienda katika kijiji tunapima mashamba ya kijiji chote. Kwa hiyo, gharama ambazo ungebeba peke yako sasa mnagawana wanavijiji 300 au 400 au hata 600 zinateremka sana sana. Kwa hiyo, suala la gharama tukianza utaratibu wa kupima vijiji

vyote katika kijiji kizima gharama zitateremka sana kwa sababu mnazigawanagawana watu 600 wa kijiji kizima badala ya kubeba mtu mmoja.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. kwanza nataka kusema kwamba wakulima wa Pamba walishapanda mbegu yao, walishalima kabla ya mtikisiko. Kwa hiyo, waliathirika kabla ya bei kushuka. Serikali haijalewa hili jambo? Naomba walifikirie upya. (*Kicheko*)

Swali juu ya ardhi. Kwa kuwa, maana ya kupima kijiji ni kukiwezesha kijiji hata kupanga matumizi ya ardhi. Je, kwa sehemu kama Moshi ambapo kuna vihamba vyta watu vinavyotawaliwa na mila, unapovipima hivi vijiji na unapokipa kijiji Mamlaka ya kuamua maamuzi ya kuamua matumizi ya hiyo ardhi, Mheshimiwa Waziri anatuambia hapo mbele ya safari hapatakuwa vihamba tena katika sehemu kama za Moshi? Au jambo hili la kupima vijiji ni la sehemu kama za *Wasukuma Land* tu?

**SPIKA:** Ni la Mheshimiwa Waziri na siyo Naibu Waziri. Majibu Mheshimiwa Waziri !

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa John M. Cheyo, Mbunge wa Bariadi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kutumia mafasi hii kuwashukuru wananchi wa Bariadi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wote wawili kwa jinsi walivyopokea vizuri mradi wa kupima mashamba ya wanavijiji katika Wilaya yao na walitueleza pale kwamba katika hili hakuna itikadi tuko pamoja na tutashirikiana na ndivyo inavyotakiwa.

Sasa kuhusu swalii lake, ni kweli kwamba katika kupima mipaka ya vijiji kule Moshi vijiji vimeshapimwa vinajulikana, kupanga matumizi ya ardhi wataalamu wakifika katika kijiji wanaopanga kwa kweli ni wanakijiji wenyewe ndiyo wanaosema hapa iwe hiki, hapa iwe hiki na kadhalika. Ni wanavijiji wenyewe. (*Makofi*)

Sasa kwenye eneo lile ambalo wanaosema hili ni la mashamba na mashamba yao ni vihamba, vipande vidogovidogo hivyo, kila kihamba kitapimwa na kitapewa Hati Miliki. Ukoo ukisema hivi vihamba vyetu 10 kwa pamoja ni vya ukoo mzima na kiongozi wa Ukoo wetu ni fulani. Kwa hiyo, hivyo vihamba kumi (10) vitapewa Hati moja na atakayekabidhiwa ni yule mkuu wa ukoo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, yote mawili yatafanyika kutoa Hati mojamoja kwa kihamba kimojakimoja na kutoa Hati moja yenye vihamba vingi chini ya ukoo kwa ridhaa ya ukoo wenyewe. (*Makofi*)

**SPIKA:** Bado tuko kwenye Wizara hiyo hiyo na swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando.

**Ardhi ya Nchi yetu Kuuzwa kwa Wageni**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo malalamiko miongoni mwa Watanzania kuwa ardhi ya nchi yetu inauzwa kwa wageni:-

- (a) Je, wageni wangapi mpaka sasa wamemilikishwa ardhi hapa nchini na ni kwa kiwango gani?
- (b) Serikali imekusanya fedha kiasi gani kwa utekelezaji wa mpango huo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2005-2008?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sera yetu, ardhi ni mali ya Umma chini ya udhamini wa Mheshimiwa Rais. Kila raia anayo haki ya kumiliki ardhi bila ya kubaguliwa jinsia, kabilia, dini na kadhalika. Raia wa Tanzania wanamilikishwa ardhi kwa mijini kwa utaratibu uitwao *lease* yaani kuwa na haki ya kutumia kwa miaka 33 au 66 au 99. Na kwa upande wa vijijini haki ya utumiaji wa ardhi kwa wanavijiji haina ukomo yaani wao hawajawekewa hii miaka ni haki ya kutumia ardhi ile milele kwa upande wa vijijini. Aidha, Sera na Sheria zetu za ardhi, haziruhusu raia wa nje kumiliki ardhi ila kwa wawekezaji waliopitishwa na Kituo cha Uwekezaji (*Tanzania Investment Centre (TIC)*) ambao hukodishiwa kwa vipindi maalum vya miaka 33,66,na 99 na muda huo ukimalizika wanaweza kuhuisha umilikaji huo, au ardhi hurejeshwa kwa Serikali.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Sheria zetu za ardhi haziruhusu raia wa nje kununua na kumilikishwa ardhi kwa njia ya kawaida (*Granted Right of Occupancy*) bali kwa njia ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*Derivative Right of Occupancy*), chini ya Sheria ya Uwekezaji Na. 26 ya mwaka 1997. Tangu Sheria zetu za Ardhi zianze kutumika mwaka 2001, jumla ya wageni 20 wamemilikishwa ardhi yenye ukubwa wa hekta 66,128 nchini kwa ajili ya matumizi ya Kilimo, Viwanda na Hoteli.
- (b) Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo kwa kipindi cha 2005-2008 jumla ya wawekezaji raia wa nje 15 wamemilikishwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji katika Miradi ya Kilimo, Viwanda na mahoteli; na kupima ardhi, kulipia fidia, kuandaliwa Hati, kodi ya pango la ardhi na kadhalika.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabla ya kuuliza maswali Mheshimiwa Waziri wakati anajibu, jibu A alilolitoa hapo mimi siyo nililopewa kwenye maandishi. Lakini jibu B ni sawasawa na nililopewa kwenye maandishi. Kwa vile ningependa kupata hayo majibu A kwa sababu ndiyo msingi wa swali langu, eneo lenyewe la ardhi ambalo humu halimo. Lakini baada ya wasiwasi huo sasa napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, hiki kiwango cha watu 20. Je, Mheshimiwa Waziri kama ikibainika kuwa kuna maeneo katika nchi yetu ambayo wako watu wamemilikishwa ardhi kwa mujibu wa maelezo yake yeze hayapo katika nchi yetu ambayo wako watu wamemilikishwa ardhi na kwa mujibu wa maelezo yake yeze hayamo katika idadi aliyojupa. Analiaidi nini Bunge hili? Atachukua hatua gani? kwa sababu hali inaonyesha maeneo ya Iringa, Pwani na Arusha kuna watu wengi wanamiliki ardhi. Ninapata wasiwasi kuwa ni watu 20 tu, atachukua hatua gani kama akibaini ziada ipo?

(b) Lakini la pili, moja katika watu wenye hofu kubwa sana na ardhi yao kuwa labda itakodishwa au kuchukuliwa ni watu walioko eneo la Kigamboni Dar es Salaam. Anatoa kauli gani ndani ya Bunge hili juu ya usalama wa ardhi ile kuanzia leo mpaka siku zijazo? Itachukuliwa kukodishwa au vipi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimhakikishie kwamba, yale majibu yangu ya sehemu (a) ambayo yana marekebisho ambayo yeze hana, atapatiwa kwa sababu majibu yenye masahihisho ni haki yake na tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, njiblu maswali yake mawili kama ifuatavyo. Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kwamba, je, kama kuna watu ambao wamemiliki ardhi kinyume cha yale niliyotaja itakuwaje? Sheria inasema, raia wa nje haruhusiwi kumilikishwa ardhi hapa Tanzania, isipokuwa mwekezaji na mwekezaji mwenyewe huyo awe amepitishwa, amepewa *certificate* na Kituo cha Uwekezaji. Sasa kama kuna mtu raia wa nje baada ya sheria hizi mpya kuanza kutumika mwaka 2001, kule nyuma inawezakana hayo yalitokea lakini baada ya mwaka 2001, kama kuna mgeni ambaye amemilikishwa ardhi kinyume cha utaratibu huu, ni uvunjaji wa sheria. Nataka nitumie nafasi hii kuwaambia Watanzania kwa sababu nasikia huko mipakani kuna baadhi ya Watanzania wanauzwa ardhi kwa wageni kwamba, wanavunja sheria. Narudia tena kama kuna Mtanzania anauza ardhi kwa wageni, anavunja sheria na akibainika yule mgeni atanyang'anywa na huyu naye aliyeuza vilevile atapata adhabu kwa sababu wote wawili wamevunja sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu Kigamboni. Kigamboni katika hotuba yangu ya bajeti iliyopita, nilitoa taarifa kwamba, Kigamboni tunapanga uzuri, tunapanga upya lile eneo la Kigamboni kwa kuliwekea huduma za kisasa. Huduma zote kama ni barabara, kama ni maji, kama ni umeme, kama ni kujenga vizuri zaidi kwa kupangilia vizuri zaidi. Nilitoa taarifa hiyo na niliwakikishieni kwamba, katika utaratibu huo, wananchi hawatahamishwa wala ardhi yao haitauzwa kwa mtu mwagine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimepita Kigamboni nimewaeleza hilo, nimefanya mikutano ya hadhara katika mitaa mbalimbali na nimewaeleza juu ya azma hiyo. Juzi wakati Mheshimiwa Rais anazindua kivuko cha Kigamboni, vilevile alitumia nafasi hiyo kuwaeleza wananchi wa Kigamboni kwamba, huu uvumi kwamba ardhi yao inauzwa, wanaondolewa, wanapelekwa sijui Mkuranga, sijui wapi, ni uvumi wa uongo. Marekebisho na maboresho yote yanayofanywa, watakaonufaika wa kwanza ni wao wenyewe na hawatahamishwa. (*Makofi*)

Na. 66

### **Uchache wa Wanawake katika ngazi za Maamuzi**

**MHE. MARTHA J. UMBULA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Tanzania imeweka sera nzuri ya kuelimisha watoto bila ubaguzi wa kijinsia lakini bado wanawake ni wachache kwenye ngazi za maamuzi kama vile, Maprofesa katika Vyuo Vikuu, Idara za Serikali na katika sekta binafsi.

- (a) Je, Serikali imefanya tathmini gani kubaini kuwa tatizo liko wapi?
- (b) Je, Serikali ina mikakati mipya ya kukabiliana na changamoto hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Manyara, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, pamoja na Serikali kutoa fursa sawa ya elimu bila kujali jinsia, bado idadi ya wanawake kwenye ngazi za maamuzi ni ndogo. Kwa mfano, kwenye Vyuo Vikuu vya Umma nchini, idadi ya Maprofesa wanawake ni asilimia 8.8 ikilinganishwa na asilimia 91.2 ya wanaume. Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wanawake ni asilimia 21.2 ukilingaanisha na asilimia 78.8 ya wanaume. Makatibu Tawala wa Mikoa Wanawake ni asilimia 40.9 ukilinganisha na Wanaume ambao ni asilimia 59.1. Wakurugenzi kwenye Idara na Taasisi za Serikali, wanawake ni asilimia 11.2 na wanaume ni asilimia 88.8 na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri wanawake ni asilimia 21.8 ukilinganisha na ya wanaume asilimia 78.2.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu zilizobainika za chanzo cha wanawake kuwa wachache katika ngazi za maamuzi ni kama ifuatavyo:-

Mila na desturi za jamii nyingi za kiafrika, ikiwemo Tanzania ziliwu na mfumo dume uliokuwa ukithamini zaidi mtoto wa kiume kuliko mtoto wa kike. Mfumo huu usio na usawa kijinsia, ulimpa mtoto wa kiume fursa kubwa zaidi ya kupata elimu kuliko mtoto wa kike. Kutokana na mfumo huu, mtoto wa kike alionekana kama msaidizi wa mama nyumbani, akitayarishwa kuolewa ili wazazi waweze kupata mahari na mambo mengine. Kutokana na mfumo huu, watoto wengi wa kike hawakuweza kupata fursa ya elimu kama wenzao wavulana.

Aidha, mfumo wa elimu tuliorithi kutoka kwa wakoloni nao ulikuwa na mfumo dume ambaa haukutoa nafasi sawa za masomo kwa wanawake na wanaume. Wanaume walipewa nafsi nyingi za masomo, ikilinganishwa na wanawake. Hali hii iliendelea hata baada ya uhuru, hivyo wasomi wengi wa miaka ya 1960 hadi 1980 ni wanaume ikilinganishwa na wanawake. Wasomi wa kipindi hicho ndio ambaa wengi wao, wapo katika ngazi za maamuzi, utendaji na uongozi kwa mfano, Maprofesa wa Vyuo Vikuu ambaa wengi wao ni wanaume.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linalofanya wanawake wakose fursa za kielimu, ni mgawanyo usio sawa wa majukumu katika jamii unaotokana na mfumo dume na maumbile ya jinsi ya kike. Kwa mfano, daraja la Uprofesa alilouliza Mheshimiwa Mbunge, ni jukumu na jitihada za mhusika binafsi kulifiki kwa kuwa lina hatua zake ambazo kutokana na majukumu na maumbile (yaani wanawake wanakuwa na maumbile ya uzazi) na malezi ya kifamilia, kunamfanya mwanamke ashindwe kufikia kwa wakati au kutofika kabisa viwango vya kuwa Profesa.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kutambua tatizo hili, ilianza kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia masuala ya kijinsia katika jamii, ilitoa muongozo wa udahili wa wanafunzi kwa uwiano wa kijinsia katika ngazi za Msingi, Sekondari na Vyuo. Aidha kuongeza idadi ya shule hususan shule za bweni kwa wasichana, kulegeza masharti ya viwango kwa wasichana kuingilia kidato cha tano na vyuo vya elimu ya juu. Kuhamasisha wasichana kuchukua masomo ya sayansi kwa kuanzisha programu maalumu kwa wasichana wanaojiunga na masomo ya sayansi katika Vyuo Vikuu. Serikali kwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi, imefuta karo kwa Shule za Msingi, ili kuongeza uwiano wa watoto wa kike na kiume. Katika kuharakisha usawa wa jinsia, Kamati za Shule za Msingi zinatakiwa kuwa na wajumbe wanawake sawa na wanaume. Kulegeza masharti ya mikopo ya elimu ya juu kwa wasichana hadi wale wa daraja la pili waliopata udahili Vyuo Vikuu na somo la jinsia limeingizwa kwenye mtaala wa vyuo vya elimu ya juu.

Hii ni mikakati madhubuti ya Serikali kuwaendeleza watoto wa kike ili wapate elimu na baadaye waweze kushika nafasi za maamuzi ili tufikie lengo letu la uwakilishi wa asilimia hamsini ambalo Serikali ipo katika mchakato wa utekelezaji.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza, kwa kweli nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na ya kiutafiti, lakini pamoja na hayo, naomba niulize swali dogo.

Kwa kuwa wanafunzi wa kike, wa miaka 15 na kuendelea, wana mahitaji muhimu na ya lazima wanapokuwa mashulen na hasa mashule ya bweni na kwa kuwa baadhi ya wazazi wa watoto hawa hasa wale wanaotokea vijijini, hawana uwezo wa kuwapatia mahitaji hayo licha ya kwamba, hata na ada yenyewe inakuwa ni matatizo, Serikali itakubaliana na mimi kwamba, kuna haja ya kutenga bajeti ili kuweza kuwasaidia wasichana mahitaji yale ya muhimu tukizingatia kwamba, baadhi ya mahitaji huwa pia hayawekwi hadharani na sio rahisi kuomba kwa wazazi na kwa kuwa, mahitaji hayo ya muhimu yanawaletea wasichana *stress* ili wasiweze ku-*concentrate* vizuri katika masomo yao, je, Serikali itatenga bajeti hiyo ili kuwawezesha wengi waingie Chuo Kikuu? (*Makofi/Vicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru kwa kunishukuru kwa kutoa majibu mazuri. Ni kweli kwamba, hali ya uchumi Tanzania inafanya wazazi wengi washindwe kuwapa watoto wao mahitaji muhimu wanapokwenda shulen licha ya karo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali yetu ina mfuko unaosaidia watoto ambao wana mahitaji maalum. Kwa sasa hivi, nina taarifa kwamba, Wizara ya Elimu na Mafunzo, inapeleka fungu kwenye shule hizo ili Walimu na Kamati za shule ziangalie ni nani ambaye ana mahitaji zaidi na ninaamini wataangalia mahitaji ya watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, lakini ninapenda kusema kwamba, Serikali yetu imefanya kazi nzuri sana katika kuhakikisha kwamba, mazingira ya elimu, upatikanaji wa elimu kwa watoto wa Kitanzania hususani watoto wa kike, yanakuwa ni mazingira rafiki kwa sababu ile gharama ya shule imepungua.

Mheshimiwa Spika, unakuta watoto ambao wazazi wao wanasema hawawezi kuwalipia katika shule za Serikali, wanawapeleka kwenye shule za *private* na wanawapa mahitaji yote. Kinachonisikitisha ni kwamba, inapofika wakati huyu mtoto amebahatika kwenda kwenye shule ya Serikali, mzazi anasema hana uwezo wa kumsaidia. Mimi swali langu linakuja ni kwamba, huyu mzazi anasema vile kwa sababu hathamini huyu mtoto wa kike au kweli hana? Sasa kama kweli hana, lile fungu ambalo Wizara imepeleka kwenye mashule yetu kwa *Headmaster*, basi litawasaidia wale watoto kwa sababu watakuwa wameangaliwa kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninapenda kumweleza Mheshimiwa Mbunge, ni kuhusu watoto wa kike kuingia Vyuo Vikuu. Kwa kweli Serikali imelegeza masharti na inaelekea watoto wa kike sasa hivi wana fursa ya kupata mikopo kwa urahisi kuliko watoto wa kiume. Ninaamini kwamba, hiyo ni juhudii kubwa sana ambayo Serikali yetu imetoa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita.

Matangazo, nianze na wageni, wapo wageni wa Mheshimiwa Savelina Mwijage, kutoka Bukoba pamoja na mwanaye anayetwa Abeid Mwijage, naomba wasimame, wale pale, ahsante sana. Karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni 17, kutoka jimbo la Vunjo la Mheshimiwa Aloyce Kimaro, ambao ni Wenyeviti na Makatibu wa Kata wa CCM, wakiongozwa na Bwana Hussein Jamal, Katibu wa Siasa na Uenezi, Wilaya ya Moshi Vijijini. Naomba wageni hao wa Vunjo wasimame, wale pale, ahsante sana, ahsante. Karibuni sana, karibuni sana, tunafurahi sana kuwaona na tunawatachia mema huko Vunjo katika shughuli zenu. (*Makofi*)

Wapo wageni 20 wa Mheshimiwa Anna Abdallah, ambao ni Kikundi cha *Curser Film Production* chenye wasanii, wacheza filamu na kinaongozwa na viongozi watano; Mwanate Abdallah, Mlezi wa Kikundi, yule pale, Charles Magari, Kiongozi wa Kikundi, Bahati Tundu, Mwongozaji wa Filamu, Hussein Mwala, Mkurugenzi wa Kikundi na Kuruthum Juma, Katibu wa Kikundi. Basi wageni wote wa Mheshimiwa Anna Abdallah, naomba wasimame kwa pamoja. Ahsante sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Tahadhari tu, katika mambo yenu ya maigizo, msije katika hayo mliyoyaona leo, mkatuigiza, ahsante. (*Vicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa, Dkt. Haji Mwita Haji, ambao ni viongozi wa CCM kule jumboni kwake ambao ni Ali Miraji Hassan, Katibu mwenezi, Wadi ya Kikasini, yule pale, Makame Mwadini Makame, Katibu Fedha na Uchumi, kule Kikadini, Iddi Twalib Juma, Katibu wa Wadi Wazazi Kibigija, Haji Kitete, Katibu wa Wadi ya Paje na Salum Abdallah Chumu, Mwenyekiti wa CCM, Tawi la Jozani. Ahsante sana ndugu zetu kutoka Zanzibar karibuni sana, karibuni, nafurahi kuwaona mara kwa mara. (*Makofi*)

Mgeni wa Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, ambaye ni Ali Fuad Saleh, kutoka Tanga, yule pale upande wa kushoto, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame, wanafunzi wa *UDOM* ambao asili yao ni Mbozi, nitawataja; Andrew Namayala, Isack Mkondya, Kivansi Tujendage, Emmanuel Sambilimwaya na Waziri Mwakagwila, wale pale. Karibuni sana, karibuni sana, tunawatachia mafanikio katika mafunzo na masomo yenu. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa James Lembeli, kutoka Mamlaka ya Mji mdogo wa Kahama, ambao ni Mheshimiwa Jumanne Mayunga, Mwenyekiti wa Mji Mdogo na Mheshimiwa Furaha Kagoro, Diwani wa Kata Kahama Mjini. Eeh, ahsante sana Waheshimiwa, karibuni sana. (*Makofi*)

Yupo pia Felix Kimario, Mtendaji Mkoo wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kahama, Mheshimiwa Mathias Makashi, Diwani Kata ya Idahima, Paschal Lutare, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Mkoa Vijana na Joel Machanya, Katibu Kata CCM, Kata ya Kahama Mjini. Ahsante sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Hii ni mikakati mizuri kuwaleta wageni kama hawa hapa inasaidia, kwa hiyo na wengine mchangamkie mambo haya. (*Kicheko*)

Wageni wengine ni ndugu Gregory Theo, Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkoo wa Hesabu za Serikali, yule pale kwenye *Speaker's Gallery*. Amefuatana na Martin Madalu, Mkaguzi Mkazi, Dodoma, yule pale amekaa upande mwingine na Julius Shimori, Mkaguzi Mkazi TAMISEMI, yule pale. Karibuni sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Matangazo ya vikao, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa saba katika ukumbi Na 231.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anahitaji Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane saa saba katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Matangazo mengine, kuhusu baridi kwenye ukumbi, leo ni ajabu sana, leo walioleta malalamiko ni Wabunge wanaume watatu. Kwa hiyo, hii inadhihirisha humu ni baridi sana. Kwa hiyo, nimekwishawaomba Mafundi warekebishe lakini mwelewe kwamba mtambo huu jinsi ulivyo, hauleti joto mara moja, itachukua muda kidogo. Kwa hiyo, wamepandisha kidogo joto lakini tutaendelea kupata hali hiyo nzuri. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo kuhusu matatizo ya *internet*. Ni ajabu sana kwamba, kwa siku kadhaa sasa TTCL na VODA ambao wanatoa huduma ya *internet*, wote wamekuwa na matatizo ya kiufundi hapa Dodoma. Watumiaji wa *internet* na Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli wamepata usumbu mkubwa. Kwa hiyo, naomba wahusika, nimeambiwa linashugulikiwa kuweza kurekebishwa leo, naomba wahusika wafanye kila linalowezekana, kukaa ulimwengu wa sasa bila *internet*, ni matatizo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, alitaka mwongozo wa Spika kuhusu alichoona yeye kwamba, utaratibu umekosewa na Serikali baada ya shughuli za ujenzi wa barabara au ukarabati wa barabara ya Chalinze - Segera, kuanza kutumia fedha kabla hatujaidhinisha hapa Bungeni kwenye Kitabu cha mwaka 2009/10 kwa makadirio hayo.

Juzi jioni, nilipokea majibu ya Serikali, ambayo yamekaa vizuri, lakini kuna utata kuhusu kitabu cha makadirio, Kitabu cha Nne cha mwaka 2007/2008 ambapo ndiyo mradi unaanzia. Kwa hiyo, nimekabidhi kwa Katibu wa Bunge ili aweze kuangalia kuna tatizo lipi hapa, kwa sababu ikiwa fedha hizo ni zile zilizokwishatengwa, hasa zile za kigeni na mradi ukawa unaendelea basi hapa hatuna tatizo. Lakini kama kulikuwa hakuna

fedha na hizo zinazoelekea kutumika ni hizi ambazo zimeombewa mwaka huu, basi hapo tutakuwa na tatizo la Kikatiba. Kwa hiyo, nimempa Katibu, nadhani tutapa jibu baada ya muda si mrefu, niweze kulitolea mwongozo ili hili jambo lisiwe linatusumbua.

Ahsante, huo ndio mwisho wa matangazo, sasa Katibu, hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tumebakiza wachangiaji watatu, wawili hawamo humu ndani ya ukumbi, kwa hiyo amebaki tu Mheshimiwa Damas Nakei. Simuoni Mheshimiwa Mramba wala simuoni Mheshimiwa Mkono. Kwa hiyo, ni Mheshimiwa Nakei peke yake, nitampa nafasi yeche baada ya hapo Manaibu Mawaziri wa Fedha, kila mmoja robo Saa, halafu watafuatiwa na mtoa hoja. Kwa hiyo, naanza kuona kuna uwezekano mkubwa kabisa kura zetu za *row call* zikaanza asubuhi badala ya jioni. Mheshimiwa Nakei, Waheshimiwa nawaomba msitokomee sasa, maana wengine, chai haraka haraka na kurejea. (*Makofi*)

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa fursa hii ya asubuhi ya leo. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao kwa siku mbili, tatu zilizopita wamekuwa wakichangia hoja hii ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na afya njema asubuhi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa maandalizi ya bajeti hii, maandalizi ambayo ameyafanya vizuri na hatimaye kuwasilisha hotuba yake kwa umahiri mkubwa na kwa ufasaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya CCM kwa hatua yake ya jana, ya kuondoa au kurejesha misamaha ya kodi kwa mashirika ya dini na taasisi zake. Sasa ni hakika shughuli za ujenzi wa nchi yetu, zitaendelea bila matatizo kwa kushirikiana na taasisi hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi yetu Wabunge ni kuisimamia Serikali na kuishauri na kuhakikisha kwamba maamuzi yote ambayo tumeyapitisha humu ndani basi yanatekelezwa ipasavyo. Lakini kazi yetu vilevile, kama nilivyosema ni kuishauri Serikali kama ambavyo tunaendelea kuifanya kazi hii na hasa katika suala hili la kuitisha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia bajeti ya Serikali, sote tunazungumza ndani ya Dira ya Taifa 2025 (*vision 2025*) na naamini kabisa, utekelezaji na mikakati mbalimbali inayoendelea katika nchi yetu sasa hivi, ni kuelekea huko. Kuna shughuli mbalimbali, mikakati mbalimbali kama vile *Mini Tiger Programme of 2020* ambapo lengo

ni kuharakisha lengo la Serikali kufikia mwaka 2025 ambapo uchumi wa nchi yetu unalengwa kuwa umefikia au unapangwa kuwa umefikia uchumi wa kati na kuona kwamba, umasikini utakuwa umetokomezwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile ndani ya kipindi hiki cha kuelekea mwaka 2025, kuna suala zima la MKUKUTA, ambapo tunasema kuna vipaumbele mbalimbali nya Serikali ili kufikia malengo hayo ambayo tumeyalenga kuyafikia mwaka 2025. Lakini pia tumesema kwamba, ifikapo mwaka 2015, tuwe tumekwishaondoa umaskini ule uliokithiri, tunasema *abject poverty*. Sasa mimi najaribu kuiuliza Serikali, je, katika hatua tulio nayo sasa, miaka tisa katika kipindi hiki cha mpango huo wa Dira ya Taifa 2025, tathimini yetu inatwambia nini? Je, tumekwishafikia hatua ambayo tunaridhika nayo? Kama haturidhiki nayo na nina hakika haturidhiki nayo kwa sababu Serikali yenewe imekiri kabisa, ukiangalia ukurasa wa 21 & 22, kwamba, kasi ya kuondoa umasikini hapa nchini ni ndogo. Kwa nini? Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali sasa kuona kasi hiyo inaongezwa kwa kuelewa kwa nini tumefika hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri Serikali yetu sasa kwa kuona kwamba, mikakati yetu inawezekana isitufikishe kwa *speed* hii tuliyonayo mwaka 2025 kuwa na uchumi wa kati au uchumi ulioendelea, Serikali iwe inachukua hatua za haraka (yaani *contingency measures*) ili iturudishe tuwe *on track* kwa sababu inaelekeea tunaweza kuwa nje ya wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miaka 25 ambayo tumejiwekea kutimiza malengo hayo, tungeweza kufanya mambo makubwa sana lakini kama nilivyosema *speed* iliyopo inawezekana isitufikishe huko. Tungependa kuona wenzetu walikuwa wanafanya nini. Tunaambiwa kwamba, kule Malaysia ambako kuna wale wanaitwa *Tiger economies*, wamechukua miaka 16 tu. Kwa mfanu, Mahathir Mohamed, Waziri Mkuu wa nchi hiyo wakati fulani aliiwezesha nchi yake kupiga hatua kutoka kwenye hali tuliyonayo sisi lakini aliifikisha katika nchi ambayo sasa hivi inaheshimika pamoja na nchi zingine kama Singapore na kadhalika. Sasa tupate uzoefu kutoka kwao, wamefanya nini?

Mheshimiwa Spika, lakini tusiende mbali, jirani zetu hapa Rwanda, Rwanda pamoja na mazingira magumu ya kufanya kazi, mazingira magumu ya vita, wanaenda kwa *speed* kubwa sana. Kila mmoja wetu ni shahidi kwa kusikia ama kwa kuona, lakini ni kwamba wanaenda kwa *speed* kubwa pamoja na mazingira ya kufanya kazi kuwa magumu sana. Lakini sisi pamoja na utulivu wetu wa miaka yote hii bado *speed* yetu sio ya kutosha. Tutumie mazingira tuliyonayo ya hali ya utulivu wa nchi tuweze kwenda kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu kubwa ambalo nalionna, ni suala la utawala bora. Tunaweza kuwa na mipango mizuri katika kila jambo lakini bila ya kuwa na utawala bora, hatuwezi kufanikiwa. Naomba niishauri Serikali kuhakikisha kwamba kila mmoja wetu anakuwa na nidhamu katika maeneo mbalimbali tuwe na suala zima la uwajibikaji kwa kila mmoja wetu. Kila Mtanzania aweze kufanya kazi kwa uaminifu na kwa bidii kubwa. Haya ni mambo, kimsingi kama yanekuwa yanazingatiwa yanaweza kutufikisha kule ambako tunajaribu kulenga.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo ya ujumla, nikirejea katika bajeti yetu, kuna suala hili la Kilimo Kwanza, kilimo kwanza ni nini? Kilimo kwanza ni kauli mbiu lakini ikizungumzia mikakati mbalimbali ya kuweka kilimo katika hali ambayo itatutoa katika umaskini. Lakini ukiangalia hakuna jambo jipya katika kilimo, agenda ya kilimo ina muda mrefu katika nchi yetu, tumekuwa na siasa ni kilimo, tumekuwa na kilimo cha kufa na kupona na kadhalika lakini niseme kilichokuwa kinakosekana muda wote ni ile *integration* ya kilimo na mambo ambayo yanahusiana na kilimo chenyewe.

Mheshimiwa Spika, tumesema kuna suala la viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, hilo halikuzingatiwa kwa kiwango kilichotakiwa. Lakini vile vile miundombinu ya barabara vijijini, namna ya kufikia masoko au kuchukua mazao ya wakulima vijijini na kuyapeleka kwenye masoko, haikuzingatiwa. Napenda kuishauri Serikali, katika suala hili la barabara vijijini, kwenda na mkakati wa kujenga barabara wanaita (*low quality roads*) yaani za gharama nafuu ili ziweze kujengeka, kiuchumi wataalamu wanasema inalipa zaidi. Lakini vile vile suala zima la ujenzi wa reli katika nchi yetu, tulisema kama kungekuwa na *network* ya reli katika nchi hii kama inavyotakiwa basi ingeweza kutusaidia katika *logistics* za kuwezesha kilimo kuwa katika hali inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie labda suala la miundombinu. Katika suala hili, kwa ujumla nimeshataja barabara vijijini, lakini nizungumzie kuhusu barabara kuu. Niishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara ya Minjingu-Babati-Singida sasa unaendelea vizuri na habari inayonifurahisha zaidi ni kwamba mkandarasi aliyepewa kazi hiyo ambaye ni Mchima amepewa *contract* ya miaka mitatu lakini ye ye mwenyewe ameweka mikakati anavyodai kwamba ndani ya miaka miwili kuelekea mitatu atakuwa amemaliza hiyo kazi. Kwa hiyo, kwa kweli naishukuru Serikali kwa hatua hiyo ambayo inatufikisha leo pale.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, barabara ya kutoka Babati-Dodoma-Iringa, ni barabara muhimu sana, naomba tuhakikishe mtandao wa barabara kuu katika nchi hii zote zinakuwa za lami. Kitu ambacho nashauri hapa ni kwamba kuna tatizo la gharama za juu kabisa katika ujenzi wa barabara katika nchi yetu. Leo hii, barabara ya lami ni shilingi kati ya bilioni moja na bilioni 1.3, kwa mtaji huu, hatuvezi kujenga barabara katika nchi hii. Mimi nafikiri nitoe changamoto kwa Serikali na hasa Wizara ya Miundombinu, ifanye utafiti wa kutosha kwa sababu tuna habari kwamba jirani zetu Kenya au nchi za Afrika Mashariki, wao gharama za ujenzi wa barabara kwa kilomita moja ya lami si zaidi ya Dola 600,000 wakati sisi ni Dola milioni moja kwa kilomita moja, sasa kulikoni, kuna tatizo gani, kuna haja ya kuangalia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya elimu, niishauri Serikali, kwa kweli imejitahidi, imeweka elimu kama kipaumbele chake cha kwanza; lakini tatizo kubwa katika suala la elimu ni upatikanaji wa Walimu. Hili limesemwa na kila Mbunge lakini vile vile ujenzi wa maabara na hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike. Katika suala la Walimu angalau kila mkoa, nina hakika kuna Vyuo vya Ualimu lakini kwa Mkoa wa Manyara hatuna chuo hata kimoja cha ualimu. Naiomba Wizara ya Elimu au Serikali kwa ujumla itusaidie angalau na Mkoa wa Manyara tuweze kupata Chuo cha Ualimu au

Vyuo vya Ualimu angalau viwili ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa Walimu au vyuo ambavyo vinatoa walimu kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini ni kichocheo kikubwa sana katika kuleta maendeleo na kuondoa umaskini katika nchi yetu. Niiombe Serikali kwamba katika mpango wake wa umeme vijijini, iangalie maeneo ya vijijini kwa kasi kubwa zaidi. Mimi naomba kwa eneo langu la Babati Vijijini umeme uweze kufikishwa katika maeneo yafuatayo ambayo ni *satellite areas* muhimu katika maendeleo ya wananchi katika maeneo husika. Maeneo hayo ni Madunga, Ufana, Lokhmanda, Gidas, Riroda, Duru, Magara, Mamire na Qash.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa muda mfupi ulionipa na napenda niunge mkono hoja hii ya Serikali kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Muda sio mfupi, ndio wanaoupata kila Mheshimiwa Mbunge.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mwelekeo wa Bajeti ni mzuri kama ilivyo kawaida kwa kila mwaka. Tatizo kubwa ni utekelezaji wa yale masuala muhimu, ambayo pamoja na kupangiwa fedha nyingi sana, lakini hakuna kinachofanyika mbali na kujaribu kutekeleza. La kushangaza ni ile miradi mikubwa, hasa iliyoko kwenye Mikoa ya Kusini. Dhahiri ni mifano ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na Uwanja wa Ndege wa Songwe kuwepo kwenye Ilani ya Uchaguzi 2005, hadi sasa hakuna kinachoendelea, badala yake ni ahadi mpaka miaka mitano inamalizika. Fedha zilizopangwa miaka mitatu iliyopita; ziliishia wapi?

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Isanga/Mbeya – Chunya Makongolosi, hali ni ile ile. Mbaya zaidi ni kwamba, ghiliba imefanyika ya kuonesha kuwa, barabara hiyo inatengenezwa kumbe ni kama danganya toto. Si hivyo tu, wakati Jiwe la Msingi lilipowekwa na Mheshimiwa Rais, yule mkandarasi alionesha kuwekeana kwa kumthibitishia kuahidi kwamba, lazima barabara hiyo itakamilika. Yako wapi sasa? Aibu tupu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya Ilani ya Uchaguzi kuainisha ukamilishaji wa Barabara ya Mbeya - Makongolosi, Mheshimiwa Rais, kwa kauli yake, aliahidi kuwa Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni – Makongolosi, tumwachie yeye. Serikali iliahidi kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe; la kushangaza hadi sasa hakuna cha changarawe wala mchanga; kinachofanyika ni kuikwaruza tu wakati wa kiangazi, jambo ambalo huleta kero kubwa sana wakati wa masika!

Mheshimiwa Spika, katika barabara hiyo, Serikali vilevile iliahidi kuweka lami sehemu ya kilomita tatu kwenye mwinuko eneo la Mbala, ambako ajali hutokea kila mara, ingawa fedha tayari ilikwishatengwa sehemu hiyo, imeshindikana kuwekwa lami.

Wakati nikifuatilia, nilielezwa eti kokoto zinazofaa kwa kazi hiyo hazipatikani; hivi kweli hayo ndiyo majibu ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inasema nini juu ya *Mtwara Corridor* maana kwenye Bajeti imeendelea kutamkwa kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, madai ya walimu kutaka kulipwa fedha za bima zao zilizokwishaiva miaka minne iliyopita; mbona hawalipwi? Kinachoshangaza ni kwamba, mkataba ulio wazi kabisa kati ya wahusika na Bima ya Serikali ni kuwalipa walimu. Walimu ambao wameendelea kudai hasa ni wale wanaotoka Wilaya ya Chunya. Ni vyema ufanuzi ukatolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo matano, nasubiri Wizara husika itoe ufanuzi labda itaeleweka.

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Dini na *NGOs* lazima wawajibike. Naunga mkono uamuzi wa Serikali, kutoza ushuru wa kodi kwa vifaa na baadhi ya shughuli zinazoendeshwa na mashirika hayo. Kwa mfano, mashirika hayo yanazo shule, zahanati na vituo vya afya, ambavyo hutoza ada kubwa sana kuliko ile inayotozwa kwenye Serikali; hivyo, lazima walipe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nasubiri Wizara husika itoe ufanuzi labda itaeleweka.

**MHE. EMMANUEL J. LUAHULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa hotuba aliyohutubia Wananchi wa Dodoma, pamoa na Waheshimiwa Wabunge tarehe 10 Juni, 2009. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote, kwa kuandaa Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naishauri Serikali mambo mbalimbali ya kuongeza mapato ambayo inaacha yanapotea bure. Hoja au ushauri huu hata wakati wa Bajeti ya 2008/2009 nilishauri, lakin Serikali haizingatii. Maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo wapo, wanunuzi wa dhahabu wenyewe mitaji mikubwa hawachangii chochote katika Pato la Taifa. Serikali iwaweke wachimbaji wadogo wadogo kwenye mfumo mzuri ili walipe kodi, sasa hivi kila mtu anapopata, anafanya ajuavyo bila kuingiza mapato Serikalini.

Serikali iboreshe bandari zetu; ni vigumu sana kuyadhibiti mapato kama Kampuni ya *TICTS* itafanya kazi ya kutunza makontena badala ya kuyapakia na kuyapakua. Serikali lazima ikubali kuwa hapa kuna jambo; kwa nini makontena yanayoingia yasipelekwe bandari kavu? Tunapoteza mapato makusudi, Serikali iliamua *ICDs* zifanye kazi ya bandari kavu; kwa nini hazifanyi hivyo?

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali iondoe misamaha kwenye Makampuni ya Madini yanayochimba na yanayofanya utafiti lakin Mashirika ya Dini ni vizuri yaendelee na misamaha kama ilivyokuwa siku zote. Endapo Viongozi wa Dini

wanakiuka taratibu wawajibishwe. Mashirika ya Dini yanasaidia sana wananchi katika suala zima la kuondoa umaskini. Serikali lazima itueleze kwa nini inalazimika kufuta misamaha?

Mheshimiwa Spika, tatu, ni vizuri Serikali ifanye tathmini kujua kama wananchi wamefaidika na Fedha za JK. Viongozi wa *SACCOS* waliopata fedha hizi wamezitumia kwa faida yao wenyewe, Serikali isimamie urejeshaji wa fedha hizo ili wananchi wengine wakope. Vijiji vilivyopimwa ni vizuri vipewe hati za kumiliki ardhi ili ziwasaidie wananchi.

Mheshimiwa Waziri, aniambie hadi leo ni wananchi wangapi wamerasimishwa ardhi katika Wilaya ya Bukombe? Huwezi kuwaondolea umaskini wananchi wakati hawana dhamana ya kuwadhamini ili wapate mikopo.

Mheshimiwa Spika, nne, suala la upelekaji umeme Makao Makuu ya Wilaya katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2009/2010, ukurasa wa 45, Wilaya ya Bukombe haijasemwa; je, haiko katika mpango huu; na kama ipo kwa nini haioneshwi kwenye Kitabu cha Serikali?

Serikali iharakishe kupeleka umeme Bukombe, vinginevyo tuliyoshuhudia Busanda, tunaweza kupambana nayo Bukombe. Wananchi wamechoshwa na ahadi za kutafuta mkandarasi tangu Bajeti ya 2006/2007 hadi leo 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, tano, uamuzi wa Serikali wa kuwafidia makampuni ya kununua pamba na kuthamini mabenki ni mzuri sana, ambao utafanya makampuni yaendelee kununua pamba. Je, Serikali inamsaidiaje Mkulima wa Pamba wa Shinyanga ambaye hafaidiki na mpango wa kuyasaidia makampuni na benki? Kwa nini Serikali isimdhaminii mkulima kwa kumpatia angalau Tsh.100/= mpaka Tsh.150/= kwa kilo ya pamba uwe kama mtaji wake ili makampuni au soko bei itakayokuwepo, mkulima aongezee dhamana hiyo? Kama Serikali haitafidia kiasi chochote kwa mkulima wa pamba, tutakuwa hatujamsaidia. Watakaofaidika na mtikisiko huu wa uchumi ni mabenki na wanunuzi wa pamba. Fedha za wakulima kwenda *TIB*, imani yangu ni ndogo sana kwamba wakulima wa Bukombe watanufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali imesema katika Kitabu chake cha Mpango kwamba, itaendelea kutoa elimu. Katika Kitabu cha Bajeti, Mheshimiwa Waziri, haja sema lolote kuhusu wafugaji. Naomba Serikali iwaambie Wananchi wa Bukombe; ni maeneo gani yametengwa kwa wafugaji? Semina au elimu gani imetolewa kwa wafugaji hawa, majosho, madawa na mabwawa? Je, tunawathibitishia nini Wafugaji wa Bukombe wenye mifugo mingei sana?

Mheshimiwa Spika, saba, katika Wilaya ya Bukombe, Hifadhi ya Kigosi/Myowosi ambapo sehemu kubwa ya Wananchi wa Bukombe wanafuga nyuki, kumekuwa na tatizo la kuwataka waondo/waondoe mizinga yao. Hali hii itasababisha umaskini mkubwa sana kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, naomba Serikali itoe ufanuzi wa maelezo haya:-

Je, Mashirika ya Dini hayatatozwa kodi yataendelea na utaratibu kama ilivyokuwa zamani ili yahudumie jamii?

Je, kuwatoza kodi Mashirika ya Dini huoni kuwa ni njia ya kudhoofisha baadhi ya madhehebu kwa wananchi hali ambayo yaweza kuleta mtifaruku kwa jamii?

Kwa nini Serikali isiruhusu *ICDS* kushughulikia *containers* badala ya kuiachia *TICTS* ambapo tunapoteza mapato?

Kwa nini wafugaji wa nyuki Kidosi/Myowosi Bukombe wanasumbuliwa sana? Je, hatuoni tunakwamisha maendeleo yao? Je, wakulima wa pamba watadhaminiwa kwa kupewa angalau Tsh.100/= mpaka Tsh.150/=?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa waliofanya katika Jimbo la Bukombe, ambapo yaliyosalia naamini Serikali itatimiza kabla Ilani ya CCM 2005 kwisha hasa kuleta umeme Bukombe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Spika, naanza kuipongeza Serikali kwa Bajeti nzuri ambayo inaleta matumaini kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa misamaha ya kodi kwa Mashirika ya Dini, nayapongeza Mashirika ya Dini kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhusu ujenzi wa Vyuo Vikuu na Shule za Sekondari nchini. Kimsingi, Serikali inapunguziwa mzigo mzito kuhusu ujenzi wa vyuo. Mathalani, kama Serikali ingehitaji kujenga vyuo saba sasa inajenga vyuo vitatu, pesa nyingine zinatumika kwenye miradi mingine kama miundombinu na mingine mingi. Kwa ujumla, mashirika haya yanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mashirika haya yanapata misamaha ya kodi, lakini mbona kwa upande wa elimu misamaha hiyo haimnufaishi mwanafunzi/mzazi kutokana na gharama na ada za shule kuwa kubwa kuliko zile za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hebu tuanze mifano halisi kama ifuatavyo:-

Chuo Kikuu cha Tumaini Iringa ni shilingi milioni 2.800 kwa mwaka kwa masomo ya sheria; Chuo Kikuu cha St. Johns cha Dodoma ni shilingi milioni 1.860 kwa mwaka na mwaka huu 2009 ada inaongezwa sijui itakuwa kiasi gani; Chuo Kikuu cha St. Augustino Mwanza ni shilingi milioni 1.800 kwa mwaka; Shule ya Sekondari ya St. Mariam Bagamoyo kwa *O - Level* ni shilingi milioni 1.200 na *E - Level* ni shilingi milioni 1.400 kwa mwaka, wakati Shule za Serikali ada haifiki hata laki moja; gharama ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Dodoma ni shilingi laki saba hadi shilingi milioni 1.400 kwa mwaka, hizi ni za chini kuliko za Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mifumko mingi ya uanzishwaji wa makanisa mengi na makanisa hayo ni kujinufaisha binafsi, neno la Mungu halihitaji kuhama hama.

Tunajua wapo viongozi wengi wa dini amba o ni safi sana, lakini wapo wachache amba o wanataka kujinufaisha inabidi wadhibitiwe maana wanawaponza wenzao amba o ni safi. Nisingependa kuwataja kwani si mahali muafaka.

Mheshimiwa Spika, suala la sekta ya kilimo kupewa kipaumbele ni zuri sana. Nashauri uwepo ufuutiliaji wa karibu ili kuona mipango mizuri iliyowekwa na Serikali inatekelezwa, yaani Watendaji, Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, naomba niikumbushe Serikali ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwamba, tuisahau tulikotoka. Kwa kiasi kikubwa, huduma ya elimu na afya katika nchi hii, imetolewa na inaendelea kutolewa na Madhehebu ya Dini na *NGOs*. Viongozi wetu wengi walisoma katika Shule za Madhehebu ya Dini na kutibiwa bure katika Hospitali na Zahanati za Misheni.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Ngorongoro lenye mazingira magumu kijigrafia na miundombinu duni kupindukia, kama siyo Madhehebu ya Dini, maisha ya Wana-Ngorongoro wengi yangekuwa hatarini. Hata baada ya miaka 48 ya Uhuru wa Tanganyika na baadaye Tanzania, hakuna huduma yoyote inayotolewa na Serikali katika baadhi ya maeneo kama vile Naiyobi, Kapenjiro, Olpiro, Milima ya Goll, Pinying, Esilalei, Kesile na kadhalika. Madhehebu ya Dini yanatoa huduma za afya katika sehemu hizo kwa kutumia ndege (*Flying Doctors*). Kufuta misamaha ya kodi kwa Madhehebu ya Dini ni kutaka watu wafe katika maeneo niliyoyataja hususan akina mama na watoto. Huduma zao bado tunazihitaji sana.

Mheshimiwa Spika, wanaokiuka masharti ya misamaha ya kodi wakamatwe na kushtakiwa kwa vile hakuna mtu aliye juu ya sheria; si Askofu wala Sheikh.

Mheshimiwa Spika, ufuutiliaji na udhibiti makini wa vitu vinavyoagizwa na Madhehebu ya Dini kwa ajili ya huduma wanazozitoa ufanywe na Serikali kuititia vyombo vyake kama *TRA* ili kufichua udanganyifu na kuchukua hatua stahili za kisheria, badala ya kuadhibu watu wasio na hatia kwa makosa ya watu wengine wasio na maadili mema.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo (Mb), Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Mawaziri wote walioshiriki katika kazi nzito ya kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, haikugusia kabisa suala la wastaa fuwa ili yokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wazee hawa hadi leo wanadai fedha zao ambazo wengine hawajalipwa hata senti moja. Je, Waziri mhusika haoni kuwa bado wastaa fuwa hao hawajatendewa haki katika kulipwa fedha zao?

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Fedha na Uchumi atueleze ni lini wastaafu hawa ambao hawajalipwa haki zao watalipwa ukizingatia wengi wao wana hali duni za maisha na wengi wanateseka mno kupambana na ugumu huo wa maisha?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo kimepewa kipaumbele katika Bajeti, ningependa kufahamu kipaumbele kitatolewa katika kilimo cha aina gani? Kwa vile Tanzania tuna aina mbili za kilimo nazo ni kilimo cha chakula na kilimo cha biashara, ufanuzi utolewe ni aina ipi mojawapo ya kilimo itatiliwa mkazo zaidi?

Mheshimiwa Spika, kwa vile wakulima watalima mazao yao na wengine watayaiza; je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ili wakulima waweza kupeleka mazao yao katika masoko ukizingatia vijiji vingi miundombinu yake ya barabara ni mibovu?

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala zima la wananchi wa vijijini ambao ndio wakulima wakuu na wanaweka fedha zao nyumbani kutokana na umbali uliopo hadi kuyafikia mabenki na kuweza kuhifadhi fedha zao. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu miundombinu ya kuweka fedha zao katika hali ya usalama? Hivi Serikali haioni kuwa fedha za wananchi wanaishi vijijini zinapotea ikiwemo kuungua moto au kuibiwa zikiwa nyumbani?

Mheshimiwa Spika, kuna vyama vya ushirika ambavyo vinawasaidia sana wakulima vijijini lakini vyama hivi uwezo wake ni mdogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvii marisha vyama vya ushirika ili kuweza kujenga uwezo na baadaye kuwafikia wakulima ambao ndio walengwa?

Mheshimiwa Spika, hii Kampuni ya Reli (*TRL*), imekuwa ni mzigo mkubwa kwa Taifa; iwapo mkodishaji ameshindwa kuiendesha kampuni hii Serikali haioni umuhimu wa kuinyang'anya hao wakodishaji badala ya Serikali kuingia madeni kutokana na kampuni hii au hata kama Serikali ina ubia na kampuni hii; inanufaikaje na kampuni hii ambayo inajiendesha kihasara? Sasa hivi kampuni inajiendesha kwa ujanja ujanja tu; je, kuna nini Kampuni ya *TRL*? Huu ni mzigo mbiti kwa Serikali; wakati Watanzania wanateseka kutokana na ugumu wa maisha lakini bado kampuni inafikiriwa kutafutiwa mikopo kutoka vyombo vya Kimataifa na nchi wahisani.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (Mb), Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu wote, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye lengo la kumkomboa mwananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila, kama sitampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri aliyoitao tarehe 10 Juni, 2009 katika Ukumbi wa Kilimani wakati anaongea na Wazee wa Dodoma, pamoja na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, hotuba hiyo ilikuwa nzuri na ilitoa mwelekeo mzima wa bajeti hii, kwa lengo la kutekeleza Ilani ya Uchaguzi yenye nia ya kumkomboa Mtanzania; ninampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiarifu Serikali kuwa, nimefuatilia kwa makini sana Bajeti hii ya 2009/2010, lakini sijaona fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuweka lami Uwanja wa Ndege wa Mji wa Singida, pamoja na kwamba, tumekuwa tukiikumbusha Serikali mara kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukarabati uliofanywa na Serikali kwenye uwanja huu ambao umekiongezea ukubwa kiwanja hiki na kuwa na urefu wa kilometra 1.5. Ndege zenye abiria hadi 25 zinaweza kutua Singida na zitasaidia kuleta wawekezaji, wafanyabiashara na watalii, ambao watasadid a sana kuinua uchumi wa Singida ili nasi tuondokane na fedheha ya kuwa wa kwanza kwa umaskini. Ninategemea Waziri wakati wa majumuisho yake, atakumbuka kutenga fedha za kukiwekea lami kiwanja hiki.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha ahadi ya Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, aliyotoa ya kujenga Mahakama Kuu Singida, alipokuwa Waziri wa Sheria na Katiba. Uongozi wa Mkoa wa Singida chini ya Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Parseko Kone, walifarjika sana na wakaanza maandalizi. Ahadi hii ilitokana na ombi langu baada ya kugundua kuwa, kesi za makosa ya mauaji ni nyingi sana, suala ambalo linaathiri kesi hizi kusikilizwa mapema kwani mpaka Jiji atoke Dodoma au mtuhumiwa aende Mahakama Kuu Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa, nitakuwa nimekumbusha mapema wasije wakaanzisha msuguano na Wana-Singida; atafute fedha popote atenye ili ujenzi uanze.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa Serikali imejitahidi kuwapunguzia mzigo Watanzania maskini ingawa maeneo mengine yamesahaulika mfano soda. Napenda kuieleza Serikali kuwa vinywaji baridi vinatumwa sana na Watanzania maskini hasa wakati wa misiba, sherehe za harusi, semina, warsha, vikao mbalimbali na watoto wadogo nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kuweka VAT kwenye vinywaji hivi ni kuwafanya Watanzania maskini kushindwa kutumia vinywaji hivi. Ninaishauri Serikali iondoe VAT kwenye vinywaji baridi ili kuwasaidia wananchi maskini.

Mheshimiwa Spika, ninafaraja kuijulisha Serikali kuwa, Wakulima wa Mkoa wa Singida, wametoa kipaumbele sana kwa Zao la Alizeti kwani takwimu zinaonesha Singida mwaka 2006 Zao la Alizeti waliuza tani 28,000, mwaka 2008 waliuza tani 130,000, mwaka huu wa 2009 tunategemea kupata tani zaidi ya 140,000.

Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana Serikali bado haijaona umuhimu wa kutumia mafuta haya, pamoja na kuondoa VAT na kutafuta soko nje ya nchi. Vile vile

inasikitisha sana, tunapopokea mafuta mengine kutoka nje ambayo hatujui hata ubora wake.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kupunguza kuagiza mafuta nje, ninaishauri Serikali iondoe VAT kwenye mafuta ya alizeti, kutafuta soko la mafuta haya nje haraka, kwani wananchi wanaolima alizeti watakata tamaa kulima.

Mheshimiwa Spika, pia niikumbushe Serikali, ahadi ya kumleta mwekezaji kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta yetu ya alizeti ili yaweze kuingia kwenye soko la ushindani wa Kimataifa. Nasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake, natambua Waziri ni shemeji yangu, lakini awakumbuke wakwe zake Singida.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kuieleza Serikali kuwa, kilimo cha pamba kwa Mkoa wa Singida, kilisimama baada ya soko lake kuwa dogo bali sasa wakulima wa pamba Mkoani Singida wameanza kulima kwa nguvu sana, ingawa hadi sasa soko lake nje ya nchi bado ni dogo sana, kwa maana bei bado iko chini sana katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kutenga ruzuku kwa ajili ya zao la pamba ili kufidia hasara wanayopata wakulima wa zao la pamba Singida na maeneo mengine nchini kote, hii itasaidia wakulima kutokukata tamaa tena kulima zao la pamba kwani Serikali ya Mkoa imehamasisha sana na wakulima wameitikia, tuisiwakatishe tamaa watendaji na wakulima. Nasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kwa zao hili kutengewa ruzuku sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu, napenda kuikumbusha Serikali kuwa, Mashirika ya Dini, pamoja na *NGOs* yapo sambamba na Serikali katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, kwani wanajenga mashule, zahanati na hospitali, vyuo mbalimbali, kuchimba visima na kadhalika. Majukumu ambayo yanefanywa na Serikali. Sasa kuondoa msamaha wa VAT ni kuwakatisha tamaa juhudhi zao kuunga mkono Serikali. Inawezekana kabisa yapo mashirika na *NGOs* ambayo yanatumia nafasi hii vibaya, lakini kwa nini Serikali isidhibiti jambo hili kwa wanaokiuka taratibu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iyaondolee VAT Mashirika ya Dini na *NGOs* ili waendelee kutoa huduma zao nzuri na zenye kiwango cha juu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kutoa maoni yangu kwa Serikali, nikiwa nasubiri maelezo ya Serikali, napenda kutamka kuwa ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Pia pongezi kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuelezea juu ya *package* ya kunusuru uchumi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri vipaumbele hivi sita vimeendelezwa ili kuwe na *continuity* katika kuimarisha sekta hizi na kuwa elimu imebakia ya kwanza katika

kutengewa fedha za bajeti. Hata hivyo ni muhimu kuhakikisha fedha hizi zielekezwe kwenye maeneo yenye upungufu na matatizo; mfano, walimu bado wachache, vitendea kazi, maabara na kadhalika. Hili ndilo litaleta maana kamili katika kutenga fedha nyingi, isije ikawa sehemu kubwa ni kulipa madeni.

Mheshimiwa Spika, upande wa kilimo ni vizuri kuwa ruzuku ya mbolea imeongezwa, lakini pia kupatikana pembejeo za kisasa; matrekta, *tillers* na kadhalika, jambo hili ndilo litaleta Mapinduzi ya Kilimo. Kwa kuwa mikoa michache imechaguliwa kusaidiwa zaidi katika kilimo, mikoa hii itakuwa ndio *food baskets* za nchi yetu, kuweza kujitosheleza chakula na kusafirisha nje. Ni vizuri umwagiliaji utiliwe mkazo kuwa na mabwabwa madogo madogo, lakini pia kufufua mabwawa yale yaliyokuwepo tangu zamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makusanyo, mwaka jana lengo halikufikiwa na katika hali hii ya mporomoko wa uchumi Ulimwenguni, *challenge* ni kubwa sana. Utalii utaporomoka, mazao hayatauzwa nje na kadhalika, lakini kuwa na mipango ya hali ya juu na kuhakikisha malengo yanafikiwa kila mwezi. *Exemptions* zidhibitiwe kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kukopa lilishaachwa, limerudia tena kutokana na hali ya uchumi. Vilevile ni muhimu kutokopa kutoka Benki Kuu ili *interest rates* ambazo tayari ziko juu, zisiendelee kuongezeka. *Private Sector* ambayo imekua kwa kipindi hiki, isibanwe ili iendelee kukua, tayari mfumko wa bei upo juu, tusije kuongeza *inflation*.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka katika kuimrisha wakulima wetu katika uzalishaji wa alizeti, Serikali iliamua kuweka asilimia kumi kwa mafuta yanayoingizwa yakisemwa ni ghafi. Katika muda huu, bei ya alizeti inayonunuliwa kutoka kwa wakulima imeongezeka, wafanyabiashara wanaoagiza mafuta hawakufurahi, hata mwaka jana walijaribu kuiondoa. Jambo hili lilipozungumzwa katika kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Afrika Mashariki, ilikubaliwa kuwa ufanywe utafiti nchi za Malaysia kama kweli wanauzu mafuta ghafi. Je, matokeo ya utafiti huu yanasmaje? Ni muhimu hili lijulikane la sivo inaonekana ku-*contradict* dhana nzima ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Spika, fedha katika elimu zielekezwe zaidi katika maeneo yenye matatizo zaidi, ili kuweza kuimrisha Sekta hii ya Elimu. Tunajua kuwa, kuna matatizo mengi kuhusu uchumi, maabara na kadhalika. Isije shemu kubwa ikatumika kulipa madeni ni muhimu tukifika Juni mwaka 2010, mabadiliko yaonekane katika maeneo yenye matatizo katika elimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandika haya, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa Bajeti nzuri ya aina yake, yenye kuweka kinga na tahadhari kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa ufupi, naiunga mkono. Hata hivyo, nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, Hotuba ya Bajeti inaondoa kodi ya bandari (*Stevedoring Charges*) ili kutoa fursa kwa bandari zetu kutumika ipasavyo. Uamuzi huu ni wa msingi, lakini Serikali kufuta tu kodi husika bila kuweka mkakati maalum kwa ajili ya upakuzi na upakiaji wa mizigo katika bandari zetu za Mtwara na Tanga kuanzia Julai mwaka 2009 hakutasaidia. Yapo mazoea na ujanja wa Watendaji wa *TRA* na bandari, ambao hawako tayari kutumia bandari zetu za mikoani, kwa sababu hatua hiyo ni kuharibu miradi yao. Hivyo, uamuzi makini, mahususi na wenyewe dhamira ya kujenga uchumi wa nchi yetu ni lazima uchukuliwe. Kumbuka bandari zetu zinatumika chini ya kiwango, huku nchi jirani zikimezea mate uchumi uliopo kwenye bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, pili, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005, imetamka wazi juu ya kuboresha huduma ya maji vijijini na mijini, lakini hali ya maji vijijini hasa Tandahimba na Newala ni mbaya. Nilidhani ni vyema basi mradi kama ule wa Kahama, ungeanzishwa pia kwenye maeneo ya uhaba kama vile Tandahimba. Kumbuka maji ndio uhai.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haitoi fedha ya *export levy* ya korosho kwa Halmashauri? Ni muda sasa umepita, tangu sheria hii ipitishwe 2006 kwa ajili ya kuinua hali ya maendeleo ya Zao la Korosho, lakini wakati msimu wa 2009/2010 ndio unaanza kwa ajili ya palizi na upuliziaji wa korosho (dawa), fedha hazijatolewa kamwe; kuna ajenda gani?

Mheshimiwa Spika, naipongeza kwa Serikali kuamua kwa makusudi, kutenga fedha kwa ajili ya umeme kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi, lakini kwa nini basi Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi, isitengewe fedha za lami ili umeme uendane na barabara nzuri na uchumi ukue?

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kuweza kushiriki katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Spika, tunasema Kilimo Kwanza, lakini katika ugawaji wa fedha, kilimo kiko nafasi ya nne. Je, Kilimo Kwanza maana yake ni nini? Kilimo Kwanza kina tofauti gani na Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona, Kilimo ni Utu wa Mgongo na kadhalika. Hizi ni kaulimbiu ambazo zimekuwa zikitumika kwa nyakati mbalimbali, lakili kilimo bado hakijabadilika na hakijaweza kumkomboa mkulima wa Tanzania. Kilimo Kwanza kitaleta *impact* gani kwa Mkulima wa Tanzania na Taifa kwa jumla, hasa katika suala zima la kujitosheleza kwa chakula na kuweza kupata ziada ya kuza nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, mbolea ya ruzuku ikisimamiwa vizuri na kuwafikia wakulima kwa wakati, pamoja na mbegu, miche bora na madawa, yanaweza kumkomboa mkulima na kupatikana ziada. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda au viwanda vyta mbolea ili pembejeo hiyo iweze kupatikana kwa urahisi badala ya mbolea kutoka nje?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezaka kwa idadi ya madarasa na wanafunzi wengi kuingia sekondari, lakini maabara ni chache, vifaa vyta kusomea na kujifunzia ni vichache, pamoja na upungufu mkubwa wa walimu. Je, Serikali ina mikakati gani ya uhakika ya kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, kuna matunda mengi yanayozalishwa na wakulima kama vile maembe, apples, mananasi, machungwa, nyanya na kadhalika, lakini matunda haya na mengineyo, yanaozea shambani au majumbani. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda vyta kusindikia mazao au matunda mbalimbali ya wakulima ili kuwaongezea kipato na kupunguza umaskini?

Mheshimiwa Spika, kutokana na msukosuko wa uchumi Duniani, wafanyakazi na watumishi mbalimbali wamepoteza ajira katika nchi nyingi Duniani. Je, Serikali inasema nini kuhusu suala la ajira hapa nchini kwetu?

Mheshimiwa Spika, njia mojawapo ya kuendeleza na kukuza uchumi wetu ni utaratibu mzuri wa utoaji mikopo, inayozingatia upunguzaji wa riba katika mikopo. Riba katika mikopo ya mabenki mbalimbali ni kubwa kiasi kwamba, wananchi walio wengi hasa wakulima, wanashindwa kukopa ili kuendeleza kilimo na shughuli za kibiashara. Tunaiomba Serikali, iandae utaratibu utakaowezesha wananchi kukopa ili kukuza uchumi na hivyo kuchochea maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha, Uongozi na Watendaji wote wa Benki Kuu na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa kazi kubwa na muhimu zinazofanyika, ikiwemo maandalizi na mawasilisho ya Bajeti ya Serikali. Hongereni na Mungu awaongoze daima.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua ya kufuta misamaha ya kodi kwa Madhehebu na Taasisi za Dini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli misamaha hiyo imetumiwa vibaya na baadhi ya Taasisi na Madhehebu ya Dini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, si vizuri kujumuisha wote, hata walio na historia ndefu na nzuri ya kutumia misamaha hiyo. Taasisi nyingi za Kiislamu na Madhehebu ya Kikristo ya Kikatoliki, Kilutheri, Kianglikana, Moravian, AIC na mengine ni mifano mizuri ya walio na historia nzuri.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kuondoa misamaha ya kodi, yataonekana katika kudorora kwa huduma za kijamii kama vile elimu, afya, misaada kwa yatima, wajane na wengine.

Mheshimiwa Spika, nashauri Taasisi na Madhehebu ya Dini yanayofanya vizuri, yahakikishiwe kuendelea kupata misamaha hiyo, kwa faida ya wananchi wengi sana wanaonufaika na huduma zinazotolewa na Taasisi na Madhehebu hayo.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa matayarisho mazuri ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hatua alizozitangaza ili kulinusuru Taifa na janga linalotokana na kuyumba kwa uchumi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa kufuta misamaha ilio mingi, kwenye eneo la machimbo ya madini. Hatua zichukuliwe kufuta misamaha yote kwenye uingizaji mafuta ya aina zote. Misamaha ya kodi kwa Madhehebu ya Dini isifutwe/irejeshwe. Athari za kufuta misamaha hiyo zitakuwa kubwa mno kwenye utoaji wa huduma na misaada kwa jamii, kuliko manufaa ya kifedha yatakayopatikana. Katika uimarishaji wa miundombinu hivi sasa, kipaumbele kielekezwe kwenye uendelezaji wa reli na bandari zetu. Aidha, ujenzi wa *The Great North Road* (Iringa – Dodoma - Babati) upewe hadhi yake.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na wasaidizi wake, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010. Naomba kuchangia machache kuhusu Hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato, kuna mianya mikubwa ya ukwepaji wa kodi kutokana na baadhi ya wafanyabiashara ambao hawajasajiriwa na kupewa TIN Namba ili walazimike kutoa risiti kwa wote wanaonunua vifaa madukani na hao ni wengi sana. Nashauri Wizara iendelee kutoa elimu ya ulipaji kodi kupitia Redio, TV, sanaa za maonesho na kadhalika. Vilevile nashauri *inspectors* wa TRA wazunguke madukani kufanya ukaguzi, kubaini wale wote wasiota risiti katika manunuvi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Serikali imeondoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye chai na kahawa iliyozalishwa na kusindikwa hapa nchini. Suala hili halitasaidia wanywaji wa ndani, kwa kuwa matokeo yake ni kuongeza bei ya chai na kahawa na kukwamisha juhudhi ya Serikali ya kuhamasisha Watanzania kunywa chai na kahawa ya ndani. Matokeo yake, wanywaji wengi watanunua chai na kahawa kutoka nje. Hakuna mahali popote panapoonesha kuwa, kuna ongezako la kodi kwa chai na kahawa vinavyoingizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, kwa kujumuisha mapato ya vyanzo vya Halmashauri na Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kiwango kilichokadiriwa na Serikali za Mitaa ni kidogo sana. Hili linatokana na uwezo mdogo wa Watendaji wa Halmashauri za Wilaya wa kusimamia ukusanyaji wa malengo ya mapato

yao. Sera ya *D by D*, iendane na Serikali Kuu kuwapa uwezo wa kuitendaji watumishi katika Serikali hizo, hasa katika kubuni na kutumia fedha za umma. Kuna matatizo makubwa katika Halmashauri, lazima Serikali ichukue hatua za haraka. Kuna haja ya kubuni utaratibu wa kuwapa uwezo Watendaji wa Halmashauri za Wilaya katika kusimamia fedha za miradi. Wakati ambapo Serikali inapeleka fedha nyingi katika Halmashauri za Wilaya, Watendaji huelekeza fedha za miradi husika kwa matumizi mengine ambayo hayakupangiwa fedha. Huu ni ufujaji wa fedha za Umma. Watendaji katika Halmashauri za Wilaya nao wakubali kuwa wanahitaji msaada mkubwa kutoka Serikali Kuu, bila kuona kuwa Serikali inaingilia uhuru wao wa kujamulia na kutekeleza mambo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Lollesia Bukwimba, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Busanda. Natoa pole nyingi sana kwa Familia ya Marehemu Faustine Kabuzi Rwilomba, aliyefariki hivi karibuni. Mwenyezi Mungu, ampokee peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, alizungumzia kuhusu yafuatayo; nanukuu: “Kuondoa msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezako la Thamani (*VAT Special Relief*), kwa Asasi Zisizo za Kiserikali (NGOs) na Mashirika ya Dini, madhehebu yote na kadhalika. Hata hivyo, vifaa vya kiroho na ibada vitaendelea kupata msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, inaonekana Waziri na Serikali kwa ujumla, haioni umuhimu wa Madhehebu ya Dini katika shughuli zake nyingi ndani ya Jamii ya Tanzania. Shule nyingi hata kabla ya nchi hii kujitawala na hata baada ya kujitawala, zilianzishwa kuendeshwa na Mashirika ya Dini nchini kote na hata katika Kata, hususan Dini za Kikatoliki, Kilutheri, Kianglikana, Aghakhan, Kiislam na Bakwata. Bila madhehebu haya kujitolea kwa kuleta misaada mbalimbali kutoka nje, kwa huduma hizi, nchi yetu tusingefika hapa tulipo. Baba wa Taifa na wazazi wetu, walisoma katika shule za Madhehebu ya Dini na hata Vyuo Vikuu vimeanzishwa na madhehebu haya.

Mheshimiwa Spika, huduma za afya, vituo vya kutoa nasaha mbalimbali za mahospitali na zahanati nchini pote zimeanzishwa na kuendeshwa na Madhehebu ya Dini; kuna Hospitali za Kikatoliki, Kilutheri, Kiislam na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali isiposaidia Mashirika ya Dini katika kutoa huduma hizi, kweli Tanzania itarudi nyuma kimaendeleo. Serikali inapaswa kutoa misamaha maalumu na misaada kwa Mashirika ya Dini, kutohana na kazi nzuri zinazohudumia wananchi wengi. Ni kweli kuwa, wapo baadhi ya watu wachache wa madhehebu hayo, wanajinufaisha wenyewe. Serikali ni vyema ikatambua haraka na kuiondolea misamaha ya kodi na pia kuwafungulia mashtaka.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka jana iliyopita, mimi nilizungumzia kwenye maeneo kuhusu ununuzi wa samani (*furniture*) kutoka nchi za nje na kuuzwa hapa kwetu Tanzania. Serikali inatumia pesa za kigeni nyingi katika Bara la Asia kama China, India, Malaysia na kadhalika. Samani hizi zinapokuwa madukani, zinauzwa kwa bei kubwa sana kutoka shilingi za Kitanzania milioni mbili hadi shilingi za Kitanzania milioni tano na zaidi. Samani hizi zinazoingizwa Tanzania kutoka nje, zinatengenezwa kutoptera na vumbi la mbaao, mipodo na chache sana zinatokana na mbaao ngumu. Matokeo yake samani hizi hazidumu, huvunjika haraka au kupekechwa na wadudu haraka.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina mbaao nyingi sana zilizo imara, ngumu na zenye mvuto kama mninga, mikoko, mvute, mpingo, mtiki, misandali, mikaratusi, *micyprus* na kadhalika. Serikali ilifanya vizuri kuzuia magogo kuuzwa nchi za nje, hii inawapa wananchi fursa nzuri ya kutengeneza mbaao na kutengeneza samani bora, zenye mvuto na *good finishing* ili ziuzwe nchi za nje na kuleta biashara nzuri nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, inawajibika kuanzisha kwa wingi katika mikoa yote maeneo ya VETA na kadhalika, kuhakikisha wananchi na hasa vijana wetu wanapata mafunzo stadi ya kutengeneza samani kwa kutumia mashine za kisasa, kutoa samani nzuri ambazo zinaweza kushindana na nchi za nje. Ni vyema hata kama Serikali itaweza kuleta walimu wa ufundi wa samani kutoka nje ili kufundisha vijana wetu. Hali hii itaokoa sana pesa zetu za nchi kupelekwa nje ya nchi. Vijana wengi pamoja na watu wazima, watapata ajira na hii itasadia vijana wetu kutojiingiza katika uzururaji, wizi na ulevi wa madawa. Serikali yenye we iwe mfano wa kuanza kutumia samani za hapa nyumbani, zinazotokana na mbaao zetu za asilia.

Mheshimiwa Spika, iwe marufuku kwa Serikali kutumia samani za kutoka nje, Serikali iwe mfano wa kuanza kutumia samani zetu katika Maofisi yote ya Serikali, mahospitalini, mashulenzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini mpaka hii leo tangu nilipochangia hapa Bungeni mwaka jana, bado Serikali haijachangamka wala kufanya lolote katika kurekebisha hali hii? Je, halina umuhimu?

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutoridhika kwangu katika maeneo haya mawili niliyoayazungumza, naona itakuwa vigumu kwangu kuunga mkono katika eneo hili la bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Mungu aibariki Tanzania.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, jana nikichangia, nilizungumzia utalii. Mimi ni mdau katika utalii, inanihuzunisha sana kuona utalii badala ya kukua unateremka. Ili kukabiliana na ushindani uliopo hasa kutoka Kenya ni lazima tuchukue hatua za kurekebisha bei zetu ili tuende sambamba na jirani zetu. Kwa sasa Kenya wameteremsha bei zao za kukaa hotelini, kuingia kwenye mbuga zao na wanyama wakati sisi bei zetu bado ni juu sana.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri tuziangalie upya bei zetu za hoteli na kuingia kwenye mbuga zetu. Kwa sasa bei zetu ni kama ifuatavyo: *Entry fee* Mlima Kilimanjaro ni US \$ 60 kwa siku; *camping or hut charges* Mlima Kilimanjaro ni US \$ 50 kwa siku; *entry fee* Ngorongoro/Serengeti ni US \$ 50 kwa siku; *camping* Ngorongoro/Serengeti ni US \$ 50 kwa siku; kuingia Ngorongoro Crater ni US \$ 200 kwa siku *per car*, ili bei zetu angalau zifanane na za Kenya.

Mheshimiwa Spika, *entry fee* Mlima Kilimanjaro ziwe US \$ 30 kwa siku; *camping fee* Mlima Kilimanjaro ziwe US \$ 25 kwa siku; Ngorongoro Crater na *camping* iwe US \$ 25 kwa siku, kuingia Crater US \$ 100 *per car*.

Bei za Hoteli ya Ngorongoro na Serengeti ni nyingi mno, kwani hoteli nyingine zinatoza hadi US \$ 200 *per night*. Hii inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, bajeti imefuta kodi kwenye magari yaliyotengenezwa maalumu kwa ajili ya kubeba watalii. Hakuna kiwanda chochote Duniani, kinachotengeneza magari maalumu kwa ajili ya kubeba watalii kufuatana na mazingira ya nchi yetu. Magari tunayotumia hapa Tanzania hata Kenya, yanakuwa *modified either Nairobi au Arusha ili yaweze kubeba watalii*.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa *VISA* ni US \$ 50, kama nia ni kupunguza bei ya *VISA*, basi iteremke mpaka US \$ 25 au waruhusiwe waingie bure. Tukifanya hivi tutafufua utalii wetu.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Watendaji wote, kwa kuandaa na kuwasilisha Hotuba nzuri ya Bajeti 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, napongeza hatua ya Serikali, kusamehe ushuru wa forodha kwenye majembe ya mkono na pembejeo zote za kilimo, zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa kuwa wafanyabiashara wengi huwa hawapunguzi bei ya bidhaa hata baada ya ushuru wa forodha kuondolewa kwenye bidhaa hizo, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha bei ya bidhaa zilizosamehewa ushuru wa forodha zinashuka kulingana na kiwango cha ushuru kilichoshuka?

Mheshimiwa Spika, bei ya bidhaa hizi zisiposhuka, maana yake msamaha wa ushuru utakuwa umewanufaisha wafanyabiashara badala ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekiri kutambua udhaifu mkubwa uliopo katika Serikali za Mitaa wa kutosimamia vizuri matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, kuna uzembe mkubwa na wa makusudi, unaoendelea kufanywa na baadhi ya watendaji katika Halmashauri zetu nchini. Ili kuiondoa tabia hii ya uzembe, Serikali inapaswa kuwachukulia hatua au kuwaadhibu bila huruma mara moja, watendaji wote wanaozembea kusimamia vizuri matumizi ya fedha

za umma. Serikali inatakiwa kutoa adhabu kali kwa watendaji wazembe ili kuwaogopesha wengine na kuwafanya wawe makini zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali iachane kabisa na mtindo wa kuwahamisha watendaji wazembe kutoka alikozembea kazi kumpeleka kituo kingine cha kazi. Hii ni kuhamisha uzembe kutoka kituo kimoja hadi kituo kingine, huu sio Utawala Bora. Kwa hiyo, Serikali iwaadhibu vikali watendaji wazembe ili kuwatisha watendaji wengine wazembe ambao hawajabainika wazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Special Relief*), kwa Mashirika ya Dini na Asasi zisizo za Serikali (*NGOs*), naishauri Serikali iwape fursa ya kuomba upya msamaha wa VAT kwa shughuli wanazotoa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuagiza Mashirika ya Dini na *NGOs*, waombe upya msamaha wa VAT ni kuipa Serikali kuyachuja upya Mashirika ya Dini na *NGOs* ili yale ambayo Serikali inajua yanakiuka kanuni na taratibu za msamaha, yanyimwe msamaha, lakini yale ambayo yanajulikana hayakiuki taratibu na kanuni za VAT yapewe msamaha.

Mheshimiwa Spika, ninaamini sio *NGOs* zote au Mashirika ya Dini yote yanakiuka kanuni au taratibu za msamaha wa VAT.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwa, ili kuwatahadharisha Mashirika ya Dini na *NGOs* dhidi ya kukiuka kanuni za msamaha wa VAT, iweke katika hati ya msamaha kuwa Mashirika ya Dini na *NGOs* zitakazokiuka kanuni, masharti au taratibu za msamaha zitatangazwa hadharani na kuonesha wazi masharti yaliyokiukwa. Naamini hatua hii itawahamasisha wahusika kujizua kuvunja masharti ya misamaha.

Mheshimiwa Spika, *NGOs* na Mashirika ya Dini, yametoa mchango mkubwa sana na wa kipekee, kwa miaka mingi sana katika mazingira magumu nchini mwetu. Sio hekima kuhukumu Mashirika yote ya Dini na *NGOs* kuwa wakiukaji wa masharti ya misamaha.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwape nafasi, wakosaji wajirekebishe. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, kwa kuamini mchango wangu utazingatiwa.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri; ni Waziri makini sana na mchapakazi. Wizara imepata mtu hodari sana, pamoja na wasaidizi wake, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Omar Y. Mzee (Mb) na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari (Mb), nawapongeza sana. Pia niwapongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Ramadhani M. Khijjah, wakiwemo Manaibu wake; nimekuwa nao kwenye semina mbalimbali ni wazuri sana, wana mtazamo mzuri na dira, ambao ni Dr. Philip I. Mpango, John M. Haule na Laston T. Msongole pamoja na Gavana na Manaibu wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwapongeze Wakuu wa Idara pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake, ikiwemo *TRA* chini ya Mwenyekiti wa Bodi na Kamishna Mkuu, Ndugu Kitilya. Mchango wangu uko kwenye viwanda vyatatu kusindika mazao ya kilimo na viwanda vidogo vidogo (*SIDO*). Chonde chonde, bajeti kubwa iangalie sehemu hizo, kwani kuwepo kwa viwanda hivyo, hata kaulimbiu ya Kilimo Kwanza itawezekana, kwani hadi sasa mkulima ananyonywa sana kwenye mbolea za ulangizi na ulangizi wa mazao ghafi. Hivyo basi, kuimarisha kilimo kunategemea uwepo wa viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa. Bajeti iongezwe.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Masoko; nilipotembelea na Kamati Kiwanda vyatatu Viberiti kilichopo Moshi kuna tatizo la bei (Soko), viberiti vyetu bei iko juu kulinganisha na viberiti kutoka Asia, bei poa. Tatizo ni ukwepaji wa kodi (*under invoicing*), kutoka nchi husika. Naomba Wizara ya Fedha hasa *TRA*, ifuatilie tatizo la Kiwanda cha Kiberiti, ambacho Watanzania wamepata ajira pale.

Mheshimiwa Spika, nashauri viberiti na bidhaa toka nje, ziwekewe ushuru au kodi kubwa ili kulinda masoko ya ndani, viwanda vyetu vyatatu na kulinda ajira ya wananchi wetu kuliko ilivyo sasa, tunakuwa watumwa wa bidhaa za nje kwa njia ya machinga.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *General Tyres* cha Arusha kinakufa bila sababu za msingi na mimi nimekitembelea pamoja na Kamati. Ombi, tupeleke mtaji pale au ikiwezekana tupate mbia haraka ili kulinda ajira ya wananchi na kulinda utaalamu. Uchumi wa nchi utakua sana. Wafanyakazi wanalipwa mishahara bila kufanya kazi; hiyo bajeti inatoka wapi? Huko ni kumtesa sana mfanyakazi, mitambo ni mizuri na wataalamu wa kizalendo wapo. Tuimarishe pia *CAMATEC*, *TEMDO*, *NDC* na *SIDO*.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kwa ujumla, kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri wote na Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa. Nina maeneo machache ambayo ningependa nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Waziri juu ya msamaha Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Special Relief*), kwa makampuni ya madini, mafuta ya petroli na gesi.

Mchango wangu utahusu msamaha wa Kodi ya VAT kwenye gesi. Hivi sasa ukitoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, kuna matumizi mabaya ya misitu yetu kwa kuchoma mkaa. Kiasi cha mkaa kinachozalishwa katika barabara hii na sehemu nyingine katika nchi, kinaweza kuiweka nchi yetu katika matatizo ya kutengeneza jangwa. Ili kunusuru hali hii isitokee, napendekeza kuwa na msamaha wa VAT kwa majiko ya gesi yatumiwayo majumbani na gesi yenyewe. Sasa hivi vituo vingi vyatatu mafuta ya petroli vinauzwa pia majiko ya gesi. Tofauti ya majiko ya kisasa ya gesi na yale ya zamani ni kuwa ya sasa yako salama zaidi katika utumiaji, kwani hayahitaji kibiriti kuyawasha.

Mheshimiwa Spika, Wizara husika kama vile Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Nishati na Madini, waanzishe kampeni ya makusudi hasa kwa wakazi wa mijini ili waweze kuyatumia majiko haya, kwa lengo la kuhifadhi mazingira (misitu). Napendekeza wafanyakazi maofisini wakopeshwe majiko haya, ambayo gharama yake haizidi shilingi laki mbili na nusu. Miaka ya 1970, mikopo kama hii ilikuwepo kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kuondoa msamaha maalumu kwa Kodi ya Ongezako la Thamani (*VAT Special Relief*), kwa *NGOs* na Mashirika ya Dini: Mchango *NGOs* na Mashirika ya Dini katika Jamii ya Watanzania ni mkubwa sana. Sote tunafahamu kuwa, wamefanya kazi kubwa katika Sekta za Elimu, Afya na Ustawi wa Jamii kwa ujumla (*social amenities*). Mwaka jana nililieleza Bunge hili juu ya tofauti ya gharama za matibabu ya Hospitali ya St. Francis pale Mjini Ifakara na Hospitali za kawaida za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ikiwa msamaha huu utaondolewa, ina maana malalamiko niliyopewa ya gharama za matibabu kuwa juu, basi zitazidi kwani Serikali inafahamu kuwa *MSD* hazina dawa za kutosha na mashirika haya yanategemea misada kutoka nchi marafiki huko nje. Kuondoa msamaha huu, kutakuwa na maana ya kuwaomba wahisani wanaochangia vifaa na dawa, kuchangia pia fedha za kulipia kodi, hili litawakatisha tamaa na hatimaye kusitishwa na wananchi kupata makali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, aidha, mashirika haya yamejhishisha pia na utoaji wa elimu na huduma za ustawi wa jamii. Pale Mjini Ifakara katika Hospitali hiyo ya St. Francis, kuna huduma za utafiti (*Ifakara Research Centre*), kuna Chuo cha Waganga Wasaidizi (*AMO*) na hospitali yenyewe. Utafiti unahitaji vifaa vya maabara ambavyo vingi vinatoka nje. Msamaha huo ukiondolewa, taasisi kama hizi zitaathirika. Wanatusomeshea wananchi wetu, wanatibu wananchi wetu na wanafanya utafiti wa maradhi yanayowasumbua wananchi wetu. Wachache wanaodanganya juu ya misamaha hii wachukuliwe hatua za kisheria dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, kuondoa ushuru wa forodha wa asilimia kumi unaotozwa kwenye mafuta ghafi ya kula ya mawese (*Crude Palm Oil*) uondolewe, lakini kuwe na ukaguzi wa awali kule yanakotoka mafuta ghafi hayo (*pre-inspection*) ili kuzuia udanganyifu wa wafanyakishiashara wachache, kutumia nafasi hiyo kuleta nchini mafuta ambayo yamesafishwa ili kujiletea manufaa binafsi. Huko nyuma yalifanyika na yanaweza kujirudia. Inapodhirika kuwa, mafuta yaliyoingia siyo ghafi, wafanyakishiashara hao wachukuliwe hatua na mafuta hayo yasiruhusiwe kuingia nchini.

Mheshimiwa Spika, nguo za mitumba zimesaidia wananchi, kwani viwanda vyetu vya nguo havikuwa na uwezo mkubwa wa uzalishaji. Biashara hii ya mitumba, imeajiri vijana wengi mijini na vijijini na kusababisha hali ya utulivu katika maeneo hayo kwa vile ajira imepatikana. Napenda ushuru huo ushuke zaidi hadi senti 10 za dola ili wengi zaidi waajiriwe katika biashara hiyo na hivyo kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kutoa ajira milioni moja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, Wizara imejaribu kupunguza kuondoa VAT katika bidhaa mbalimbali katika bajeti hii. Jambo la kusikitisha, Wizara hiyo hiyo imeshindwa kuondoa au hata kupunguza VAT inayotolewa kwenye mbao laini zinazovunwa kwenye misitu yetu kwa mfano Sao Hill.

Mheshimiwa Spika, mbao laini hivi sasa hapa nchini zimekuwa ghali kuliko za kutoka nchi jirani. Hii imetokana kuwa, mbao hizo zinatozwa VAT mara mbili; VAT ya kwanza kwenye mti wenyewe na VAT ya pili ni mbao yenyewe. Ipo haja Wizara kuliona hilo ili wananchi waweze kujenga nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa kuzungumza Bungeni kwa bajeti ya Wizara hii, mwaka 2008/2009, nilielezea waziwazi juu ya Serikali kutoa misamaha ya kodi kwa baadhi ya bidhaa na punguzo hilo kutowafikia wananchi; mfano, ulikuwa wa mafuta ya MOTO POA.

Mheshimiwa Spika, bado ninaitaka Serikali iwe na mkakati maalumu juu ya hilo ili wananchi wafaidike na punguzo la bei pale Serikali inapofuta kodi kwenye bidhaa husika.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii tunaambwa Kilimo Kwanza, lakini mgao wa fedha wa Serikali, kilimo kimepewa kipaumbele cha pili huku elimu ikiwa ya kwanza. Je, hapa ieleweke vipi?

Mheshimiwa Spika, katika kutoa mkopo huo, wakulima Serikali imekusudia kuweka dirisha la mikopo katika Benki ya Rasilimali (*TIB*), ieleweke wakulima wametawanyika nchi nzima; sasa itakuwaje mikopo kupatikana kwake wakati Benki ya Rasilimali (*TIB*) ipo Dar es Salaam tu?

Mheshimiwa Spika, mimi sikubaliani na mpango wa Serikali kutaka kuendelea kuwasamehe petroli wachimbaji ambao wameshawekeza, kutegemea kuja kuwasamehe wawekezaji wapya kwa sasa kutokana na mtikisiko wa uchumi Duniani, liko mbali kwani uwekezaji bila shaka utakuwa mbali.

Mheshimiwa Spika, ili Taifa liepukane na kuwabana wananchi kiasi kikubwa kutokana na kodi ni lazima tabia ya kutoa msamaha kwa kodi kiasi kikubwa iachwe.

Mheshimiwa Spika, bado uwepo wa bandari zetu nchini, haujatumiwa ipasavyo na hasa ukitalia maanani, nchi yetu imezungukwa na nchi ambazo hazina bandari. Matatizo mengine si ya mtikisiko wa uchumi, bali ni kutokana na utendaji usiofaa; tujirekebishe.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara, kwa Bajeti nzuri, ambayo haina ubishi; ni ya kitaalamu na yenyе kutia matumaini makubwa ya kuondokana na umaskini. Nawapongeza Waziri, Mheshimiwa Mustafa H.

Mkulo, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee; Makatibu Wakuu na hasa Ndugu Ramadhani Khijjah na Wataalamu wote.

Pamoja na pongezi hizo, naomba nitoe ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe angalizo kwamba, madhara ya nadharia ya watu binafsi kutegemea waanzishe au wajenge viwanda sio sahihi kwani hawana uwezo wa kifedha na uzoefu. Ni vyema sasa Serikali ikaangalia tena uamuzi wake, kwa wale walioshindwa kufufua viwanda wanyang'anywe na Serikali kufanya kama ifuatavyo:-

Nashauri Serikali kutenga fedha kila mwaka ili Wizara ya Biashara ijenge Viwanda ambavyo vitaendeshwa kwa ushirikiano na Sekta Binafsi kwa hisa ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kusaidia Sekta ya Kilimo, kwa kusindika mazao yake na kutoa ajira kwa vijana wengi, ambao hivi sasa hawana kazi, jambo ambalo linaathiri Amani na Ustawi wa Nchi yetu.

Serikali itenye fungu maalumu la fedha na kuliweka katika Benki za Wazawa au za Serikali ili Watanzania waweze kukopa fedha hizo kwa Riba nafuu hasa kwa SACCOS zilizopo Nchini.

Kuweka fedha hizo kwenye mashamba makubwa ya Serikali ili kuwa na uhakika na mavuno kama vile Uyole, Ukiriguru na kadhalika, badala ya kuwa na Utafiti pekee ili kunufaika na Masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC.

Kiwanda cha Nyuzi Tabora ni kero kwa Wananchi, kwani kinaendeshwa kwa kuwaonea Wananchi/Wafanyakazi; hivyo, hao wawekezaji wasipewe msaada wowote na kulinda mikopo waliyokopa kwani hatuoni Wakazi wa Tabora tunafaidika vipi. Watumishi hawapati haki zao.

Kilimo ndio msingi mkubwa wa kulikwamua Taifa letu kutokana na lindi la umaskini, kama alivyotamka Rais wetu hivi karibuni.

Nashauri Bajeti ya Kilimo izingatie kwa kuona Nchi nyingine Duniani zimefanikiwa vipi, kama vile Nchi za Asia, India, Bangladesh, Pakistan, Indonesia na China. Nchi hizo zilizingatia sana katika kutoa mbegu bora, mbolea na zana za kilimo, ndio msingi wa kukuza kilimo bora. Nchi hizo zilipelekwa katika Kilimo cha Umwagiliaji, kwani Watanzania wengi hutumia kilimo cha kutegemea mvua kwa asilimia 60 na sehemu kubwa ya Nchi yetu haina mvua za kutosha hasa kutokana na tabia ya Nchi.

Kilimo cha umwagiliaji kipewe kipaumbele ili kitosheleze chakula Nchini. Matrekta yakopeshwe kwenye kila Halmashauri ili waweze kusimamia matumizi hayo au ukodishaji wa matrekta hayo. Kipaumbele kipewe kwa kutenga fedha za kuajiri Watumishi wengi wa Ugani na vitendea kazi (Pikipiki).

Fedha tunazokopa zipelekwe kwenye Mradi wa Umwagiliaji, kwa kuunda Shirika lenye Mamlaka kama vile TRA ili iwajibike kufanya utafiti wa kilimo hicho kwa makini.

Kwa kuwa Shirika la TFC ndilo lenye dhamana ya usambazaji wa mbolea; ni vyema wakapata fedha mapema ili wasambaze kwa wakati muafaka.

Zao la Tumbaku nalo lipewe Ruzuku ya Serikali ili Wananchi waweze kuondokana na umaskini. Naomba nipewe jibu.

Mheshimiwa Spika, shukrani kwa Serikali kwa kutenga fedha kwa Barabara ya Nzega – Tabora – Itigi – Tabora, tatizo kubwa ni utekelezaji wake, kwani fedha hutolewa kwa kuchelewa na ukiritimba wa kupata Wazabuni, inaweza kufika mpaka Desemba hajapatikana. Naomba Serikali itoe kipaumble, angalau kwa masika hii tuweze kupita wakati wote.

Naomba nipewe maelezo juu ya madai ya Watumishi wa TRC, ambao hawakulipwa kwa wakati huu, kwani Serikali ilikiri kuwalipa badala ya mwekezaji ili kuzuia migomo? Wanapogoma, wasafiri hupata shida.

Kabla Serikali haijatoa fedha kwa TRL ni vyema ikaangalia upya Mkataba na vifaa walivyoleta wawekezaji. Fedha hizo zielekezwe kutengeneza mabehewa na injini zake, kwani mpaka sasa hakuna mabehewa mapya kama ya Daraja la I – II. Serikali isimamie yenyewe hapa Nchini na yasipelekwe nje (India), yatengenezwe Morogoro kwenye karakana yetu.

Fedha za madawa zinazoplekwa MSD kwa ajili ya ununuzi ni vyema ziende mapema.

Madai ya Walimu ambayo ni kero ni vyema yakamalizika mapema, kabla ya Uchaguzi wa Vijiji na Vitongoji, ili wafanye kazi yao bila chuki na Serikali.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, issaidiwe kusimamia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufungua Benki ya Wanawake ili wakopeshwe kwa riba nafuu. Serikali ikitoa fedha hiyo, itakuwa imewekeza kwa kiwango kikubwa na kuondoa au kupunguza umaskini.

Mikopo ya Serikali Kuu inayotolewa na Wizara hii, haitoshi na haisaidii. Ni vyema Wizara hii iongezewe bajeti ili wanawake wafaidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/2009, barabara ya kutoka Tabora Manispaa iendayo Urambo kupitia Shule ya Sekondari ya Milambo (Ujiji), ambayo ilitengenewa fedha kama Barabara ya Mkoa kwa kila kilomita tatu kujengwa kwa lami na ilitegemewa kukamilika Aprili, 2009 mpaka sasa haijakamilika na imefungwa na hivyo, wananchi wanapata tabu kupita kwani imemwaga moramu. Naomba majibu kama ifuatavyo:-

Mkandarasi anayeitwa *Nyakirang'ani Construction Limited - Musoma*, analipwa fedha kiasi gani? Je, Serikali haiwezi kuvunja mkataba huo kwani kilometra tatu ni kiasi kidogo sana?

Mkandarasi huyo hana vifaa vya kutosha na vya kukidhi kazi hiyo. Kama anaidai Serikali ni lini atalipwa ili kuondoa kero hiyo kwa wakazi wa maeneo hayo na watumiaji wa barabara hiyo kwenda Urambo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kuwa katika hali ya uzima. Hii ni rehema yake Mungu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitaongelea kuhusu kilimo; nchi yetu imekuwa na kaulimbiu nyingi kuhusu kilimo. Tumekuwa na kaulimbiu Kilimo cha Kufa na Kupona, Siasa ni Kilimo, Kilimo ni Utii wa Mgongo na leo hii tusema Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kwamba, kauli zote hizo madhumuni yake ni kuhimiza kilimo nchini, lakini ilipaswa Serikali ifanye tathmini kwa kila kauli yake mbiu na kuona mafanikio na upungufu wake, kabla ya kutoa kaulimbiu nyingine; maana kauli tu na mipango mingi bila ya utekelezaji ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunayo kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, kwa maana Serikali imekusudia kuwahimiza wananchi kuhusu suala zima la kujipinda katika shughuli za kilimo. Lakini tuijulize je, bajeti imetoa kipaumbele kiasi gani juu ya kilimo? Ni kweli hela imeongezeka katika bajeti iliyopita, lakini matarajio ya wengi ni kwamba, kilimo kingetengewa fungu kubwa zaidi kuliko hilo lililotengwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe makini katika kutekeleza yale yote inayopanga. Kwa hiyo, lazima maneno yaendane na vitendo, maneno matupu hayajengi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa msamaha kwa Taasisi za Dini, hili lazima Serikali iangalie upya kwani taasisi hizi zimebeba jukumu kubwa la kuisaidia Serikali katika kuleta maendeleo. Taasisi za Dini hutoa misaada mingi kama vile ujenzi na kuendeleza shule, kuchimba visima hasa maeneo ya vijiji na zimejenga zahanati nyingi tu. Sasa kama msamaha utasitishwa kwa taasisi hizo, wao hawatakuwa tayari tena kuendelea kutoa huduma na kuleta maendeleo, jambo ambalo litasaidia kudumaza maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho atueleze ni misamaha ya vifaa vya aina gani vinavyoletwa hapa nchini na Taasisi za Dini vimeondolewa. Kwa mfano, Taasisi za Dini ya Kiislam, huleta hapa nchini vitabu kama vile Misahafu (*Quran*) na vifaa vya masomo mengine ya Kiislam, sasa ni vyema Waziri atoe ufanuzi juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, bandari ni kiungo muhimu sana kwa nchi yoyote Duniani cha kuongeza uchumi wa nchi. Bandari yetu ya Dar es Salaam ndio tegemeo letu kubwa katika kuingiza pesa ndani ya nchi, lakini utendaji wake unadorora kila kukicha na uدوروري wote huo unatokana na utendaji usioridhisha wa Kitengo cha Makasha (TICTS) pale bandarini. Hivi Serikali mbona inawaweka sana hawa *TICTS* au yenyewe inaridhika na utendaji wake? Mpaka leo hii, bado Serikali haijayafanya kazi maazimio (mapendekezo) ya hoja binafsi, ambayo Bunge iliridhia kuhusiana na utendaji usioridhisha wa kitengo hiki (*TICTS*). Muda sasa umefika, kwa Serikal kutoa kauli ya ama kuyatekeleza Maazimio ya Bunge au kutangaza kushindwa na hivyo kutoa baraka kwa TICTS kufanya wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, sote tunajenga nyumba moja, hatuna haja ya kugombania fito, lakini vile vile hakuna haja ya kuthamini na kujali fikra, mawazo na mipango ya wengine katika kujenga nyumba yetu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi ili kuitaka Serikali ikubali kuichukua mipango mizuri ya bajeti ya mwaka huu kutoka Kambi ya Upinzani, ambayo inaonesha vyanzo vya kuongeza mapato kutoka Bajeti ya Serikali shilingi za Kitanzania trilioni 9.513 hadi kufikia shilingi za Kitanzania trilioni 10.273. Hii ni kwa manufaa ya Taifa letu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. MAULIDAH A. KOMU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naomba niwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa WIzara hii muhimu na bila kuwasahau Watendaji wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu muhimu kwa miasha ya Taifa lolote lile, bila ya kuwa na vyanzo vya kupata fedha na kuwa na viongozi walio na uchungu na nchi yao na kutumia fedha zinazopatikana kwa maendeleo ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kuwakumbusha Waziri na Watendaji wake; mwaka jana, niliwaonya kwa kuwaauliza kwamba, kuna siku Watanzania wataamua kuokoka, hawatakunywa pombe wala kuvuta sigara; je, kodi wanayotegemea kujenga nchi hii ambayo siku zote hutoka kwenye sigara na pombe zitatoka wapi endapo hazitatoka humo?

Mheshimiwa Spika, huwezi kupata fedha bila kutumia fedha kwanza. Kwa hiyo, tuangalie jinsi ya kutoa fedha, kujenga na kuimarisha njia ya kupata fedha ili fedha ziingie kiurahisi.

Mheshimiwa Spika, takriban Wabunge wote, huongea kwa uchungu kuhusu ukusanyaji wa mapato katika nchi hii umezorota kupita kiasi. Vitega uchumi viko vingi nchi hi, lakini nani anajali; ni habari nyingi, maneno mengi, utekelezaji finyu.

Mheshimiwa Spika, naomba niorodheshe vitega uchumi ambavyo mimi naona kama tutavtilia maanani tukakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tukiimarishe reli na kujenga ya kisasa, tutapunguza fedha tunazokarabati barabara kila siku kwa ajili ya magari mazito, tutawasaidia wananchi kufanya biashara zao kwa urahisi wa kusafirisha mizigo yao, tutapunguza ajali za barabarani kwani wananchi wengi watatumia usafiri wa treni kwa kuwa nauli ni rahisi na uhakika wa kufika salama na la mwisho, tatarudisha heshima ya nchi na ajira za wananchi wetu zitaongezeka.

Mheshimiwa Spika, tukitengeneza bandari zetu zote na kuhakikisha tunaachana na uwozo wa *TICTS* na ukiritimba na rushwa zilizokithiri kwenye utendaji kazi za kutoa mizigo bandarini, bandarini ikiwa nzuri na mizigo inateremshwa kwa wakati muafaka sio mwezi mzima na zaidi, reli inafanya kazi vizuri basi bila shaka bandari itaongoza kuingiza fedha nyingi sana katika mfuko wetu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, maneno mengi ya methali yamepita katika hili jambo muhimu la kilimo; Kilimo cha Kufa na Kupona, Kilimo ni Utii wa Mgongo, Mapinduzi ya Kijani na sasa Kilimo Kwanza, yote haya ni kuboresha maneno kwani tumezowea mpaka nchi jirani huwa wanatuzonga kwa kutuita Watanzania maneno mengi, vitendo finyu.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa tunaongea mpaka lini; na lini tutaanza utekelezaji? Hebu Awamu ya Nne ianze mambo mapya ya utekelezaji kwanza maneno baadaye.

Mheshimiwa Spika, kilimo kikiimarishe kikweli kweli, kila mmoja anajua kwamba, shida, umaskini, njaa na maradhi, vyote vitaangamia. Hatuko wengi kama ndugu zetu wa China, lakini wanaringa kwa sababu ya kilimo. Naomba niilize Serikali; tunashindwa nini kuelekeza nguvu zote kwenye kilimo; tatizo liko wapi? Ardhi tunayo, nguvu kazi tunayo, vijana wamejaa wanazurura ovyo, wamebaki kuwa vibaka na sisi tukiendelea kuwaangalia na wananchi wanaojiita wenyewe hasira wanachoma moto na kuwauwa.

Mheshimiwa Spika, bahari yetu ina utajiri wa kutosha, lakini nani anaangalia wakati meli inakamatwa kwa kuhamisha utajiri wetu. Ilikamatwa meli moja, meli mia moja zimekimbia, sisi tulikuwa wapi? Je, tumekamata meli ikiwa na shehena ya samaki wengi na mashine za kusafisha na kuwakatakata zikiwa humo ndani ya meli?

Je, sisi tumefikiria nini mpaka sasa; tangu siku hiyo tumepanga kuweka mikakati ya kuwa na meli hizo sisi wenyewe ili tunufaikie? Ndani ya bahari hakuna samaki tu, kuna utajiri wa ajabu; je, tunafikiria nini na lini utajiri huo tutautafuta ili tuondokane na umaskini?

Mheshimiwa Spika, nina mengi lakini naomba niishie hapa kwani naona uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali itapoteza fedha nyingi bure katika mpango wa kufufua kilimo (Kilimo Kwanza), kama itaagiza matrekta na *power tillers* nyingi na kusahau kilimo cha maksai (plau). Baada ya muda, matrekta yatakayokopeshwa kwa wakulima yataharibika na kuwekwa juu ya mawe, kwa sababu wananchi wetu wengi hawana uwezo wa kuyaendesha (*service and maintenance*). Yanapoharibika hawana uwezo wala utashi wa kuyatengeneza wanayatelekeza lakini kilimo cha maksai (*ploughs*), hakina gharama za mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza fedha nyingi zielekezwe kwenye kilimo hiki nafuu, inawezekana kabisa kaya inaweza kupatiwa plau moja na maksai nne, tuna ng'ombe wengi wanaokaa na kulishwa bure, matrekta na *power tillers* chache yakopeshwe wachache wenye uwezo.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbeya – Chunya – Itigi ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa, imesahauliwa na kufanya eneo hilo kuwa pweke, lisilofikika na hivyo rasilimali zake nyingi za mbaao, asali na nta, madini, nyara, mazao na kadhalika, kuvunwa zaidi na walanguzi; ni shamba la bibi kwa walanguzi na majangiri. Serikali itenye fedha za kutosha kuitengeneza barabara hii muhimu kuliko inavyofanya sasa.

Mheshimiwa Spika, riba za mabenki bado ni kubwa na za juu. Mikopo ya mabenki ni mzigizo mkubwa sana kwa wananchi. Benki hizi zinanyonya wananchi; ni mirija ya hatari sana; ni kupe; napendekeza Serikali ilifanyie kazi suala la riba za mabenki.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe tamko linaloeweka kuhusu hatimiliki za kimila kama zinaweza kutumika bila utatanishi, kukopa kwenye mabenki. Bado Serikali ina kigugumizi, MKURABITA sasa hivi wanapima rasilimali ardhi za vijiji ili wananchi waweze kumiliki ardhi zao, lakini hatujapata majibu fasaha kuhusu suala la mikopo kwa kutumia hatimiliki za kimila. Serikali ielete wazi ili tupate jibu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ijengwe upya ili itumike zaidi kusafirisha mizigo, kuondoa *congestion* Bandari ya Dar es Salaam. Malori mengi yanepunguzwa katika barabara zetu na kupunguza uharibifu wa barabara kama reli itatumika kusafirisha mizigo kwenda nchi za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ndiyo nchi inayoongoza kuwa na bajeti kubwa zaidi ya Nchi za Afrika Mashariki za Kenya na Uganda, trilioni 9.5, lakini vipaumbele vyetu vinaifuja bajeti hii kwa sababu tunashindwa kutambua kwamba, nchi hii kubwa sana na hivyo *priority* ingekuwa ni ujenzi wa miundombinu madhubuti ya reli na barabara. Hata Mjerumani alipofika cha kwanza alianza na Reli ya Kati 1897 – 1905 – 1914 na baadaye Uingereza.

Mheshimiwa Spika, napendekeza sasa tuache mengine, tujenge miundombinu. Tufufue reli zetu, tujenge upya za kisasa, barabara zote za mikoa ziunganishwe kwa lami.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi ni kubwa, napendekeza baadhi ya shughuli kama Pensheni zihamishiwe Wizara ya Kazi. Wizara mpya iitwe Wizara ya Kazi na Pensheni, badala ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kutokana na uhaba wa ajira, shughuli kubwa zaidi ni masuala ya Pensheni, ambazo zingefanywa chini ya Wizara hii na kuiacha Wizara ya Fedha ishughulikie mambo ya Mipango, Uchumi na Fedha.

Wastaafu wengi wanasumbuka kupata malipo yao ya izeeni, baada ya kulitumikia Taifa kwa miaka yao yote. Shida kubwa ni urasimu na kumbukumbu. Wizara ya kazi haina shughuli nyingi, ipewe kazi hii. Napendekeza hilo.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni hali nikiwa mzima. Pia kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, kwa umahiri wako katika kutuongoza katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, ni ishara tosha kwamba, Serikali imejipanga vizuri katika kumfanya Mtanzania aishi maisha bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo, unaweza ukahofu utekelezaji kwa vitendo. Mimi napata wasiwasi mkubwa katika kutekeleza azma hii ambayo itamsaidia mtu wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, tukisema kilimo tujue tumegusa mambo mengi sana, ambayo ndio yanayoongoza katika nyanja za matatizo katika nchi yetu. Kilimo kinahitaji mambo yafuatayo: Miundombinu (Barabara), Miundombinu (Umeme), Pembejeo, Masoko, Viwanda, Maafisa Ugani na kadhalika.

Mambo haya katika Nchi yetu ndio tatizo sugu, ambalo Serikali kama inakonda, basi haya ndio sababu. Je, ukizingatia mambo haya na fedha iliyotengwa; Wizara itaweza kutekeleza azma yake kwa kusema Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Spika, ni kweli Dunia imepata mtikisiko wa uchumi, lakini Nchi yetu kama ingekuwa mwenendo mzuri wa kudhibiti uchumi wetu tusingetikisika. Tanzania tumezungukwa na vitega uchumi kama vile, Bahari, Utalii, Mbao, Madini, Mifugo na kadhalika, lakini bado bajeti yetu haikidhi haja, pamoja na msukumo wa Wafadhili. Mkulima huyu wa Kitanzania, ambaye anachangia kiasi cha asilimia 50 za fedha za kigeni, ndiye mtu wa kipato cha chini na mwenye maisha duni katika Nchi yetu.

Tunashuhudia kila msimu wa mazao ukifika, mazao ya wakulima mengi huharibika kwa ukosefu wa soko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la bidhaa katika huduma za simu za mkononi pale vocha au muda wa maongezi, kwa mtazamo wangu, najua watumiaji wa simu za mikononi katika Nchi yetu ni wengi sana, miongoni mwao ni wale wa vijijini

ambao pato lao kwa siku ni dogo sana. Serikali haioni kwamba, hili litamuua au kumfanya ashindwe kwani yeze ndie mtumiaji?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, napenda niseme, Mola atampa uwezo Mheshimiwa Waziri ili afanikishe azma yake.

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuunga mkono hoja hii. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba nieleze kidogo wasiwasi wangu juu ya Bajeti hii, hasa katika eneo la kufuta misamaha ya Kodi kwa Taasisi za Dini.

Mheshimiwa Spika, inaelekea Serikali haithamini au haijafanya utafiti wa kutosha katika huduma kubwa zinazotolewa na Taasisi za Dini.

Mheshimiwa Spika, thamani ya huduma zitolewazo na Taasisi za Dini ni kubwa kuliko hasara ambayo Serikali inapata. Hata hivyo, Serikali bado ina uwezo kwa uhakika, kudhibiti kasoro ndogo ndogo ambazo zinatokana na baadhi uya Viongozi wa Taasisi hizo kutokuwa Waaminifu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kufikiria upya uamuzi wake wa kufuta misamaha ya kodi kwa Taasisi za Dini.

Mwisho, naomba tena kuunga mkono hoja hii.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuamua mapato mengi yatoke ndani. Aidha, naipongeza Serikali kuona umuhimu kwa TRA kukusanya Kodi ya Majengo. Zoezi hili limeanza Dar es Salaam, nashauri hata mikoani kodi hizi zikusanywe na TRA.

Mheshimiwa Spika, ili tupambane na mtikisiko wa uchumi, nashauri mambo yafuatayo:-

TRA wapewe jukumu la kukusanya maduhuli yote Nchini; kwa mfano, mapato toka Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Mazingira na kadhalika, yakusanywe kituo kimoja tu TRA ili tudhibiti vizuri mapato yetu. Hii ni kwa sababu TRA wana uwezo wa kusimamia mapato hayo vizuri; wamesomea masuala ya mapato na mbinu wanajua; na pia wana ujuzi wa kupambana na wakwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, maendeleo yetu yatatekelezeka kama Wizara hii ya Fedha itapeleka fedha mapema katika Wizara nyeti mfano, Nishati na Madini na kadhalika; ni maeneo yaliyo na makusanyo ya mapato.

Kwa kuwa zamani tulitumia *Cash Budget*, utaratibu huu ni mzuri uendelezwe na tutengete fedha zetu za ndani ili mpango wa maendeleo utekelezekere.

Mheshimiwa Spika, nashauri mambo yafuatayo yafanyiwe kazi haraka: Wizara ya Fedha itoe mapema Fedha za *Revolving Fund*, kwa wachimbaji wadogo wa madini. Fedha za Maendeleo za Miradi mbalimbali katika Miundombinu, Afya na Maji, zitolewe mapema.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuona umuhimu sasa wa kufutilia mbali misaada. Naipongeza TRA, sasa wanaitoza kodi Kampuni ya Geita Gold Mine; nashauri hata Migodi mingine walipe kodi.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwawezesha Wananchi bado halijatekelezwa vizuri mwaka 2008/09, fedha za uwezeshaji ziliishia mijini tu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mwaka 2009/10, fedha zipelekwe katika *SACCOS* za vijiji ili kila mtu anufaike na mpango huo mzuri wa kupewa mikopo na waondokane na umaskini. Wananchi tayari wamejiunga katika *SACCOS*, wanasubiri mikopo wapewe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuamua sasa Kilimo Kwanza; ni safi, lakini tumejiandaa vizuri katika mabonde yetu? Tumejiandaaje kutumia maji ya maziwa yanayotuzunguka? Je, tumeandaa masoko ya kutosha mara watakavununa?

Nashauri maeneo yatakayobainishwa na kupimwa kwa ajili ya kilimo, yasibinafsishwe au kuuzwa kwa wageni; wapewe Watanzania na wasaidiwe vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, suala la mtambuka uk. 34 na 35; Serikali inaendelea kutekeleza Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu maendeleo ya Jinsia, kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za Uongozi za Kisiasa. Hii si kweli, hii ni kinadharia tu matendo si hivyo, TAKUKURU, hawasimamii haki za wanawake. Nasikitika, kama rushwa itaendelea kushamiri, katika chaguzi zijazo wanawake hatutapata nafasi yoyote . Nawauliza TAKUKURU; je, wako likizo? Naomba wasituvurugie mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana wewe, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa kazi kubwa mliyoifanya, kuandaa Mipango na hatimaye Bajeti ya Mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, nasita kuunga mkono hoja mpaka nitakapopewa ufanuzi kwa mambo machache sana yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kuona tena mwaka huu ikiwafutia Wafanyabiashara wanaoingiza mafuta ya kula hapa Nchini kwa kisingizio kwamba, hayo ni makubaliano ya Nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Nchi ni lazima tuwe na maamuzi ya kuwajenga wakulima wetu, lazima tuachane na maamuzi ambayo tukiyapitisha, yatawanufaisha wakulima wa Nchi nyingine na wakulima wetu wazidi kukwama na kudumaa kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wakulima wa Tanzania wanalima Mazao ya Alizeti, Ufuta, Mawese, Karanga na kadhalika. Mazao ambayo yanatoa mafuta ya uhakika, kwa ajili ya matumizi ya ndani na kuza nje. Sasa hivi hakuna Mtanzania anayelalamika kwa kukosa mafuta, kwa hiyo, wana mafuta ya kutosha na zaidi tena mafuta yanayofaa kwa afya zao.

Mheshimiwa Spika, hivi ni sababu zipi hasa zinazokufanya ufute kodi ya asilimia 10 kwa mafuta yanayotoka nje? Hii ya kusema ni makubaliano ya Afrika Mashariki, Watanzania hawakubaliani nayo. Hivi Serikali mnakubali kuendeshwa na Wafanyabiashara wachache, ambao kwa utashi wao, wanataka waagize mafuta toka nje ili waje kuangusha soko la Wakulima wetu?

Mheshimiwa Spika, ombi langu, waiteni hao wanaotaka kuleta mafuta toka nje, wapeni mashamba walime mawese, alizeti, karanga na kadhalika ili wafungue viwanda vya kutengeneza mafuta. Viwanda vyao vitatoa ajira kwa Watanzania na pia mabaki (mashudu), yatafaidisha wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa msamaha kwa Majericane ya kuhifadhia maziwa. Mimi inanishangaza sana, kwa sababu hatuna viwanda vya kutosha vya kusindika maziwa, badala yake tunatumia zaidi maziwa ya unga toka nje, maziwa halisi toka nje na maziwa machache yanayotengenezwa na kiwanda cha Tanga, Iringa na Musoma. Mimi nafikiri sasa umefika wakati wa kujenga viwanda vya kutosha vya maziwa hapa Tanzania. Pia tukizingatia kwamba, Tanzania ni nchi ya tatu kuwa na mifugo mingi Duniani, tunatakiwa tuwe na viwanda vingi vya nyama, ngozi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, juu ya misamaha ya kodi kwa Mashirika yetu ya Dini, nakuomba sana upite upya kwani tusipoangalia, maendeleo ya Nchi hii Kielimu, Kiafya na kadhalika, yatarudi nyuma. Nakubaliana kabisa na ufanuzi ulioutoa kwa waandishi wa habari hivi karibuni. Nakushauri unaposoma Bajeti, TRA na wengine, watoe mapema maelezo yanayohusu misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, naupongeza sana mpango wa Serikali kuweka kipaumbele kwa Miundombinu, Afya, Elimu na Sekta nyingine muhimu kwa faida ya Watanzaia hasa wanaokaa vijijini.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kukuomba sana, asilimia 10 ya mafuta yanayotoka nje irudishwe haraka sana.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, kwa kuniwezesha kuishika kalamu nami nikatoa mchango wangu katika Hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri inaonesha nia ya Serikali kutimiza ahadi yake ya Maisha Bora kwa kila Mtanzania. Kinachoonekana ni maneno mazuri ambayo ufanisi wake ni mgumu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kudidimia kwa uchumi katika Nchi yetu, unaweza ukajiuliza na ukapata jibu kwamba, tuna ukosefu wa usimamizi. Nchi yetu ina mambo mengi ambayo hadi leo hayajaweza katuondolea umaskini katika Nchi yetu na kumfanya Mwananchi aishi kwa hofu. Tanzania ina ardhi safi, ambayo kama itasimamiwa vizuri, nchi yetu itaondokana na umaskini. Mfano, mmojawapo ni pale tunapoangalia Mkonge, ulivyoweza kuota katika ardhi yetu na Michikichi.

Leo China ambaye ameanzisha jana kilimo hiki, ndiye anayejipatia fedha za kigeni, sisi tulidharau na yametushinda mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei utapelekea umaskini kila leo na kumfanya Mwananchi wetu aishi katika hali ngumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upandaji wa riba za mikopo Benki; ipo haja Serikali kwa makusudi, ipunguze riba katika Benki zake ili zimuwezeshe Mwananchi kukopa na kulipa.

Kuhusu kutoza ushuru wa bidhaa katika huduma za simu za mkononi pale vocha au muda wa maongezi unapouzwa; ni dhahiri eneo hili linambana mtumiaji wa simu hizi, jambo ambalo litapelekea watumiaji kushindwa kutumia simu na hapa patasababisha kukosekana kwa pato. Kwa kuzingatia umuhimu wa hili, ni vyema Serikali iangalie kwa jicho la rehema ili iwapunguzie mzigo wateja wa simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kumpungeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara, kwa kuandaa Bajeti ya Serikali na hatimae kuwasilishwa hapa Bungeni. Hata hivyo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kaulimbiu ya Kilimo Kwanza inatoa picha kwamba, kilimo sasa kimepewa kipaumbele cha kwanza. Hata hivyo, Bajeti halisi ambayo imetengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo, haiendani na kaulimbiu hiyo. Ukifuatilia jinsi ambavyo pesa zimetengwa kwenye Bajeti, kilimo kimetengewa Tshs. Bilioni 666.9, nyuma ya Sekta za Elimu shilingi bilioni 1,743.9, Miundombinu shilingi bilioni 1,096.6, Afya shilingi bilioni 963.0.

Mheshimiwa Spika, kwa mpangilio huo, utaona kwamba, kilimo kimepewa kipaumbele cha nne katika Bajeti ya Serikali. Kwa kaulimbiu hiyo ya Kilimo Kwanza na msisitizo uliotolewa, utadhani kwamba, kilimo kimepewa kipaumbele cha kwanza; lakini

ukweli siyo. Aidha, picha walijonayo Watanzania wengi, hasa Wakulima, wanajua kwamba, kilimo kimepewa nafasi kubwa; lakini si hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Ni nini hasa maana ya kaulimbiu ya Kilimo Kwanza wakati kibajeti ni Elimu Kwanza?
- (ii) Ni lini Bajeti ya Kilimo itafikia asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali kama ambavyo Wakuu wa Nchi za Kusini mwa Afrika walivyokubaliana kupitia Azimio la Maputo; kama ilivyooneshwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005?
- (iii) Ni kiasi gani cha pesa kati ya shilingi bilioni 666.9, zimetengwa kwenye Mbolea na Mbegu za mazao ya chakula?

Mheshimiwa Spika, Bandari nyingi Duniani, hutumika kama chanzo muhimu sana cha mapato na hivyo kukuza Uchumi wa Nchi husika. Bandari ya Mombasa nchini Kenya ni moja ya Bandari zinazofanya vizuri sana na hivyo kukuza uchumi wa Nchi hiyo.

Kwa bahati mbaya sana, Bandari yetu ya Dar es Salaam, pamoja na ndoto zetu za kuifanya kama *Hub* kwa Nchi za DRC, Malawi, Zambia na Burundi, lakini utendaji kazi wake ni mbaya sana. Matokeo yake, wafanyabiashara wengi wameacha kuleta meli zao katika Bandari ya Dar es Salaam kutokana na utendaji mbaya wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa, Kampuni ya TICTS haiwezi kukwepa lawama ya utendaji mbaya wa kazi katika Bandari ya Dar es Salaam. Mkataba kati ya TICTS na Bandari, uneleza wazi kabisa kwamba, iwapo TICTS itafanya mizunguko ya *crane* " chini ya 25 kwa saa, itakuwa imevunja Mkataba na inaweza kufukuzwa kazi. Jambo la ajabu sana, TICTS inafanya mizunguko 18 tu! Pamoja na Azimio la Bunge la kutaka Serikali ivunje Mkataba wa TICTS kutokana na utendaji mbovu, bado Serikali ina kigugumizi katika kuuvunja Mkataba huo mbovu sana! Hali hii itaendelea hadi lini na hii ni kwa manufaa ya nani? Je, uchumi wetu kupitia Bandari ya Dar es Salaam utakua kweli?

Mheshimiwa Spika, hatua ya Serikali kuondoa msamaha wa Kodi ya VAT kwa Asasi za Kidini siiungi mkono. Nasema hivyo, kwa sababu Taasisi za Kidini zimekuwa za msaada mkubwa sana katika kukuza Uchumi wa Nchi hii. Sekta ambazo zimefaidika sana na huduma za Kidini ni pamoja na Elimu, Maji, Afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itaendelea na azma yake hiyo, watakaoathirika na hatua hiyo ni Wananchi wanyonge wa Tanzania. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2008/09, Kanisa la Kinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde – Mbeya, ilichimba visima zaidi ya 300 katika Wilaya ya Mbozi. Walifanya hivyo kwa kuwa walipata msamaha wa Kodi ya VAT kwenye vifaa vilivyotumika katika ujenzi wa visima hivyo. Ukiiondoa msamaha huo, maana yake mwaka 2009/2010, Kanisa

halitakuwa tayari kuendelea na mpango wa kuchimba visima kwa manufaa ya Wananchi. Nashauri Serikali iliangalie vizuri suala hili, vinginevyo tutaharibu uhusiano mzuri uliopo kati ya Serikali na Taasisi za Kidini.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri awaeleze Watanzania, hasa wastaaifu wa kima cha chini, wataanza kulipwa shilingi ngapi kwa kipindi cha kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2009/2010? Aidha, urasimu uondolewe katika malipo ya Pensheni kwa wastaaifu, leo ukienda Hazina utadhani ni Hospitali! Hali hii siyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake. Naipongeza pia Wizara hii, pamoja na Wataalamu wake wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati mizuri na nia njema ya Wizara hii, hotuba ina mikakati na nia ya kuwaondolea Wananchi adha kubwa ya maisha magumu na kuwapa matumaini ya maisha mazuri ili kutimiza kaulimbiu ya Maisha Bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mimi kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia naomba kukiri kuwa, mimi ni mfanyakishara wa mafuta na usafirishaji wa aina zote za mizigo, mafuta na abiria. Kwa maana hiyo, nina utaalamu wa muda mrefu katika biashara hizi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, Waziri ameondoa ushuru kabisa wa magari ya mizigo yenye kuanzia tani ishirini na kuyapunguzia magari ya mizigo yenye tani tano na kuendelea hadi asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, sababu zilizotolewa za kuyaondolea magari ya mizigo ushuru si ya msingi sana. Ukiangalia kwa sasa, Nchi hii ina idadi kubwa sana ya magari ya mizigo ya tani zote kuanzia tani tano na kuendelea na mengi hayana kazi za kutosha.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu, siku zote Wabunge na Wananchi, pamoja na wadau, wanalamikia wingi wa ajali za magari ya abiria, ambayo hayana kiwango ambayo ni maroli yanayogeuzwa kuwa mabasi. Pamoja na ushauri wa Jeshi la Polisi kwamba, maroli kugeuzwa mabasi yanahatarisha maisha ya Watanzania na tafiti zinaonesha magari hayo ndio yanayoongoza kwa ajali.

Mheshimiwa Spika, je, kwa maana hiyo mizigo ina thamani kubwa kuliko maisha ya Watanzania na kupelekea kuondoa ushuru wa magari ya mizigo na kuacha mabasi?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Nchi kama Kenya, ushuru wa mabasi ni asilimia sifuri na malori ni asilimia 35%.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ni kuhalalisha Watanzania waingize malori na kuyageuza mabasi na kuhatarisha maisha ya Watanzania wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia manunuzi ya mabasi mapya kwa Nchi za Uganda na Kenya, utakuta ni ya juu ukilinganisha na Tanzania. Makampuni mengi ya Tanzania yanayonunu mabasi mapya, yanaishia kufilisika kwa mizigo ya madeni kutokana na bei kubwa inayosababishwa na kodi za mabasi.

Mheshimiwa Spika, nataka maelezo na takwimu za kutosha, zilizofanya Wizara ya Fedha kuondoaa ushuru kwenye magari ya mizigo na kutoondoaa kwenye mabasi yanayobeba dhamana ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nashukuru nangoja majibu.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Nashukuru kwa kupata nafasi hii, nami nichangie Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Kwanza, namshukuru Waziri na Wasaidizi wake, kwa Hotuba ya Bajeti.

Nianze moja kwa moja kwa upande wa Wakulima kama Serikali ilivyosema Kilimo Kwanza. Kwanza ni vizuri tufahamu kuwa, kwa Bajeti ya Mwaka 2008/2009, kilimo kilitengewa asilimia 7.1. Mwaka huo wa fedha, Serikali imetenga asilimia saba! Sijafahamu sababu ya kukipa jina la Kilimo Kwanza. Nafikiri kilimo kingepewa asilimia kubwa kuliko Wizara, ningekubaliana na Waziri kwamba Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mikopo kwa wakulima ni suala ambalo kwangu naona haliwezekani. Huyo mkulima maskini aliyeishi kijijini, ambaye hamiliki ardhi yake Kisheria, hana hati huko kijijini; nani atampa hati ya nyumba kwa nyumba za Nyasi? Mpango wa kukopesha Wananchi (Wakulima), umekuwepo tangu hapo zamani. Kuna swalii la kujuliza; ni wakulima wangapi walikopeshwa kutoka kwenye mabenki kwa ajili ya kununua matrekta? Benki gani itakuwa tayari kumkopeshwa mwananchi maskini ambaye ni mkulima?

Kwa ufahamu wangu, wale waliokopeshwa matrekta ni wafanyabiashara mashuhuri. Wafanyabiashara hao walipopata hiyo mikopo na kuinunulia matrekta, matrekta hayo yametumika kusomba mchanga, mawe, kokoto, wala hayakutumika kwa ajili ya kilimo. Kwa hiyo ni lazima Serikali itafute njia sahihi ya namna mkulima atakavyopata hiyo mikopo ya kununua matrekta.

Pili; ni vyema Serikali, ieleze Wananchi kuhusu ulipaji kodi kwa Mashirika ya Kidini na Mashirika Yasiyokuwa ya Serikali (NGO). Lazima Serikali ifahamu kuwa, haya mashirika yametoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya Nchi Kielimu, Kiafya, Kiroho na huduma mbalimbali kama maji na nyinginezo. Vilevile zimetoa wataalamu wengi sana, hata baadhi ya Mawaziri, Wabunge na Watendji wenye nyadhifa kubwa Serikalini wamesoma kwenye shule hizo za Mashirika ya Dini. Kama kuna Viongozi ambaao wametumia msamaha wa kodi kwa manufaa yao binafsi, wachukuliwe hatua za

Kisheria. Kosa la baadhi ya Viongozi wachache wasiokuwa waaminifu, isiwe sababu ya kuwalipisha kodi.

Uchumi hauwezi kupanda tu kwa kukusanya kodi, ni lazima nchi iwe na mkakati wa kuanzisha viwanda vingi hapa nchini ili Taifa liweze kuuza bidhaa nje ya nchi; mfano, viwanda vya nguo kwa vile tunalima pamba; na viwanda vya kusindika matunda kama vile maembe, ndizi, machungwa, mananasi na kadhalika.

Sikubaliani kamwe na msamaha kwa wachimbaji wa madini. Serikali iliingia mikataba isiyokuwa na faida kwa Watanzania na bado tunaendelea kuwapa msamaha (*Tax Holiday*). Wananchi wamesikitika sana, hasa wapiga kura wa Jimbo la Tarime, ambapo kuna Mgodi wa Nyamongo.

Serikali ina uwezo wa kuendesha Shirika letu la Reli (TRC) hivyo investor hana uwezo (TRC).

Naomba Mradi wa Umeme Vijijini (Tarime – Itiryo), utekelezwe kulingana na Bajeti ya Mwaka huu wa 2009/2010. Naishukuru Serikali kwa Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mwaka jana wakati wa kujadili Bajeti ya Miundombinu, niliuliza Serikali ni lini Barabara ya kutoka Musoma Mjini hadi Fort Ikoma kuititia Butiama alikozikwa Baba wa Taifa itajengwa?

Nilielezwe kwa kina kwani barabara hiyo ni muhimu sana katika Uchumi wa Wilaya ya Musoma, Bunda na Tarime. Pia nilihoji kwa nini Serikali ya CCM ingeweza kumsahau Baba wa Taifa katika Barabara hii pamoja na kuahidi kwa miaka isiyopungua 25? Serikali iliniahidi kuwa itaijenga.

Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana, kuona pamoja na ujenzi wa barabara zitakazojengwa mwaka 2009/10, hii Barabara ya Butiama - Fort Ikoma haimo. Hivi kwa nini Serikali haitaki kutekeleza ahadi hii? Mimi kama Mbunge wa Musoma Vijijini niwaambie nini Wananchi wangu?

Kwa kuwa hii ilikuwa Ahadi ya Serikali, sioni kwa nini niunge mkono Bajeti hii bila kupata maelezo ya kuniridhisha.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mungu, kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba mbili za Bajeti ya Taifa kwa Mwaka 2009/10; Hotuba ya Mipango na ya Fedha.

Nampongeza Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omary Yussuf Mzee, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Ramadhani Khijja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha, kwa kazi ya kuandaa Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu ya Tanzania ni ya Wakulima na Wafanyakazi, wakiwemo Wafanyabiashara kidogo. Asilimia kubwa ya mapato yetu inahitaji ielekezwe sana katika kada ya wakulima ambayo ni asilimia 80 ya Wanachi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Idadi ya Watanzania sasa inakisiwa kufikia milioni 40; hivyo, kutokana na makisio haya ni dhahiri idadi ya Wakulima ni takriban milioni 32 na idadi ya watu milioni 8 ndio inagawanywa kwa Wafanyakazi na Wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa Hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikielelza hali halisi ya Uchumi wa Nchi yetu na namna ya kukabiliana na hali ya msukosuko wa uchumi Duniani (*Global Financial Crisis*).

Mheshimiwa Spika, hatua zote zilizochukuliwa na Mheshimiwa Rais ni za kupongezwa, kwani zitatoa ahueni kwa Makampuni yetu ya uzalishaji ya ndani kuendelea na kazi za uzalishaji kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka huu, kipaumbele chetu ni kilimo kwa kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Ni dhahiri dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne ni nzuri. Pamoja na kuweka kipaumbele hiki, kipo kinadharia zaidi kwani ongezeko la asilimia 30 toka Bajeti ya Kilimo ya Mwaka 2008/09, bado ni ongezeko dogo sana kukidhi haja ya sekta nzima ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo haja kulingana na hali yetu ya sasa kiuchumi, kuona namna ya kuongeza Bajeti ya Kilimo kwa asilimia 100 toka Bajeti ya mwaka jana (2008/09). Ongezeko hili lingeweza kuongeza kasi ya ukuaji ya sekta hii muhimu ya kilimo, kwa minajili ya uzalishaji zaidi kwa mazao yote yale ya biashara na ya chakula kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka jana ya kilimo ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 513.0, iliyobeba kaulimbiu ya Mapinduzi ya Kijani, pamoja na mikakati yote ilioandaliwa Mwaka wa Fedha 2008/09. Kwa kaulimbiu hiyo, matokeo yake bado hayana manufaa yoyote kwa mkulima kufanya Mapinduzi ya Kijani. Matatizo ya kulima kwa kutegemea mvua za kubahatisha, bado yapo palepale; pia kuna ukosefu wa Wataalamu wa Kilimo (Maafisa Ugani. Suala la upungufu na ubora wa pembejeo bado linaendelea na miundombinu mingine ya kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji kama vile mabwawa ya uvunaji maji na kadhalika bado ni matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa hii ambayo Bajeti yetu makusanyo ya ndani yanakadiriwa kufikia trilioni 51096 na matumizi ya kawaida kufikia trilioni 6,688, ambayo kuna nakisi ya takriban trilioni 1.582, ambapo nakisi hiyo kwenye matumizi itatokana na fedha ya misaada na mikopo ya kibajeti na kisekta.

Mheshimiwa Spika, nakisi kubwa ya trilioni moja inatokana na hali ya nchi yetu kutokuwa na Mipango madhubuti ya uzalishaji kupitia kilimo. Iwapo juhudhi na tija ya

dhati itaelekezwa katika kilimo, basi nakisi kwa mwaka ujao wa fedha haiwezi ikawa na idadi kubwa ya fedha. Naiomba sana Serikali katika mipango yake katika kipaumbele cha kilimo, mipango ya kumruhusu mkulima iwe ya dhati. Naomba pamoja na Serikali kuteua Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Morogoro na Kigoma kama *Buffer Zone*, basi ni vyema pia ingeimarisha kimkakati Mikoa ya Kati; Singida, Dodoma, Manyara, Tabora, Shinyanga na mingine, hasa kuiimarisha katika miundombinu ya umwagiliaji. Mikoa inayo ardhi ya kutosha, udongo mzuri kwa kilimo na nguvu kazi ya kutosha kupatiwa fursa ya kuwa na kilimo endelevu cha umwagiliaji. Naamini kwa dhati kabisa, sekta hii itakuwa imepewa kipaumbele bila ubaguzi. Napongeza makusanyo ya TRA, lakini ni dhahiri tukiimarisha Soko la Eastern Congo, Burundi, Rwanda na kadhalika, soko hili linapaswa kuimashwa kwa kuwa na barabara bora, reli bora na huduma ya kuridhisha ya Bandari ya Dar es Salaam na hata kuwe na haja ya kuziimarisha Bandari za Tanga na Mtwara. Naamini mapato yataimarika zaidi na kuendelea kupunguza nakisi mwaka hadi mwaka.

Barabara ya Kati (*Central Road*), Dar es Salaam, Dodoma, Singida, Nzega, Kahama hadi Mpakani mwa Rwanda na Burundi, ziimashwe na eneo la Dodoma – Manyoni hadi Isuna likamilike.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza mtoa hoja, Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu wake wote wawili, Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na Mashirika na Mamlaka chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri.

Kipekee, nawapongeza Mamlaka ya Mapato, PPF na BoT, kwa mchango wao katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuyumba kwa Uchumi wa Dunia ni tishio kwa uhai na usalama wa Mataifa yenye uchumi duni (*Least Developed Countries*) kama yetu. Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, anastahili pongezi za dhati, kwa kuelewa vyema tishio la mtikisiko wa Uchumi wa Dunia na kuandaa Mpango wa Serikali ya Awamu ya Nne, kupunguza makali kutokana na athari za kiuchumi kwa nchi yetu. Tusipowasaidia wanaochocha uzalishaji wa mazao ya kilimo na kutoa ajira kwa Wananchi wetu, tutaanguka na kulazimika kuanza upya! Lazima tuunge mkono busara ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vilivyoainishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ni sahihi kabisa. Elimu, Afya, Maji na Miundombinu ni msingi kwa Kilimo bora. Kwa hiyo, Mpango Mkakati wa Serikali ulivyotafsiriwa katika mapendekezo ya Bajeti, haupingani hata kidogo na kaulimbiu ya Serikali kwa Mwaka 2009/10 (Kilimo Kwanza). Bila elimu bora hakuna kilimo bora; bila afya bora hakuna kilimo bora, bila maji hakuna kilimo bora na bila miundombinu bora hakuna kilimo bora.

Mheshimiwa Spika, ninao ushauri ufuatao kwa Serikali: Kwanza, kwa kuwa rasilimali fedha inatumika vibaya hasa katika Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji, usimamizi wa fedha na ufuatiliaji wa matumizi ni muhimu sana. Mfumo uliopo wa usimamizi hauheshimiki! Baadhi ya Watendaji ngazi za Wilaya na Vijiji, wanaiba waziwazi fedha ya ruzuku ya maendeleo na michango ya Wananchi! Kwa mfano, fedha haitumiwi kwa ufanisi katika miradi ya Elimu katika kujenga vyumba vya madarasa, miradi ya maji, afya na barabara! Serikali Kuu ina wajibu wa kurekebisha hali hii haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pili, nashauri Serikali iikamilishe haraka barabara ya lami toka Kagoma - Muleba Biharamulo - Lusahunga. Aidha, jitihada ziongezwe kuweka haraka lami kwenye njia ya ndege Uwanja wa Ndege wa Bukoba. Hali ya uwanja wa ndege inatishia usalama wa raia.

Mheshimiwa Spika, tatu, naishauri Serikali iuchukulie hatua umaskini wa kipato unaowakabili Wananchi wa Muleba Kusini. Tunahitaji mpango maalumu wa kuwawezesha Wananchi kushiriki kikamilifu katika uzalishaji. Wananchi wanao uwezo wa kujilisha, lakini hawana mazao ya kuuza. Zao la Kahawa kama linakufa; ndizi zinahitaji mbolea ya samadi; na ng'ombe hakuna!

Miundombinu ya barabara toka Muleba hadi Dar es Salaam ikiboreka kwa kukamilisha lami, halafu Wananchi wakasaidiwa kuboresha mashamba ya migomba, uzalishaji wa ndizi na maharage utaongezeka na kupunguza umaskini wa kipato. Aidha, Nishati ya Umeme utokanao na nguvu ya maji na upemo ikiongezwa, wawekezaji wa viwanda vya samaki na mazao ya kilimo na mifugo watavutika na kutoa ajira kwa vijana wetu. Hali ilivyo sasa inatisha sana. Wataalamu watumwe Muleba, kufanya utafiti na uchambuzi wa kisayansi. Wizara ya Fedha na Uchumi itusaidie. Halmashauri ya Wilaya ya Muleba haina Wataalamu wa kufanya kazi hii. Wananchi wanahitaji msaada toka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWINCHOUM ABDULRAHMAN MSOMI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi na Naibu Mawaziri wake, kwa kazi nzuri wanazofanya katika Wizara hii. Naipongeza Serikali kwa ujumla, bila kumsahau Katibu Mkuu wake na Wakuu wa Idara wote wa Wizara hii, kwa kuwasaidia vyema Mawaziri wao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa katika shule tulizojenga kwa kila Kata. Shule za Sekondari ambazo Wananchi wanashukuru, lakini maoni yanatolewa juu ya ujenzi wa nyumba za awali na maabara, ukiacha matatizo mengine madogo madogo, ambayo Halmashauri zinaweza kuyamaliza kama vile uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabweni pale inapohitajika.

Naishauri Wizara ya Fedha, iangalie uwezekano wa kuitumia Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii, kujenga nyumba hizo za walimu na maabara. Hii ni kutokana na uwezo ilionao Mifuko hiyo na mipango yao ya ujenzi kwa dhamana ya Serikali Kuu kama walivyofanya Miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Wananchi na Wawekezaji wenyewe maeneo Kigamboni, wamekopa fedha Benki mbalimbali, lakini aidha hawajamaliza miradi yao waliyoombea mikopo au hawaajaanza kabisa kutokana na Mpango wa Serikali Kuu kuupanga na kuujenga upya Mji wa Kigamboni na kuufanya wa kisasa. Mikopo ina riba na Serikali imezuia kutekelezwa mradi wowote kwa sasa; hivyo, Wananchi hao kupata hasara na pia malimbikizo ya riba. Naiomba Serikali itoe tamko, kwa Benki kusitisha/kufuta madai ya riba kwa kipindi ambacho Serikali Kuu kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imesitisha kuendelezwa chochote Kigamboni. Hili si kosa lao, lakini Wananchi wanaingia hasara na kazi zimesimama hivyo kukosa kipato walichokusudia.

Aidha, Wizara ya Fedha na Uchumi, izungumze na Mabenki kuzikubali Leseni za Makazi kuwa ni halali kwa dhamana ya mikopo. Jambo hili bado linawasumbua Wananchi kiutekelezaji, kwani baadhi ya Benki wanazikataa.

Naunga mkono maamuzi ya Serikali ya kutaka *NGOs* na Mashirika ya Dini, kuanza kulipa kodi. Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe, isipokuwa panahitajika kutoa ufanuzi jinsi litakavyoshughulikiwa jambo hili na kuweka bayana yatakayostahili kwao kwa misamaha ya kodi.

**MHE. LUCY FIDELIS OWENYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na shilingi ya Tanzania kuwa na thamani ya 1,244.1 mwaka 2007 na kupanda na kuwa shilingi 1,196.3 mwaka 2008; hii haitoshi kwa sababu bado katika hifadhi zetu mfano, TANAPA, Wakala wa Utalii wanalipa *park fees* kwa Dola za Kimarekani. Nchi jirani kwa mfano Kenya, huwezi kulipa *fees* yoyote iwe *park fees, hotel bills* na kadhalika; ni lazima utumie *Kenya Shillings* na hata kama mteja hana, analazimika kwenda kwenye maduka ya kubadilisha fedha na wanabdalisha fedha zao za kigeni na kwenda kufanya malipo hayo kwa fedha za Kikenya. Sisi Watanzania tuna Mashirika ya Umma ambayo bado yanatoza kodi za hifadhi kwa kutumia dola; kuna tatizo gani kutumia na kuthamini shilingi yetu ya Tanzania? Naomba nipiatiwe jibu la usahihi.

Mheshimiwa Spika, mimi sina pingamizi kabisa na dhana ya Kilimo Kwanza, lakini lazima iende sambamba na Elimu. Wakulima wakihimizwa kulima kilimo cha kisasa, kama hawana elimu ya kilimo hiyo, itakuwa ni bure. Itabidi tuwe na Mabwana Shamba wa kutosha (*Extension Officers*) ili waweze kuwasaidia Wakulima na kilimo hiki kisiwe cha kusubiri mawingu; tuachane na kilimo cha mvua tujielekeze katika kilimo cha umwagiliaji ambacho ni endelevu. Katika kilimo lazima tuwe na *Commercial Farmers*, yaani Wakulima Wakubwa, wa Kati na Wadogo. Mfano mzuri ni Kiwanda cha Sukari cha TPC, kilichopo Kilimanjaro. Kiwanda kile kimesaida sana vijana wengi kupata ajira (3500), sasa hivi wanazalisha umeme kwa kutumia mabaki ya miwa na kusaidia vijiji vya jirani; si hivyo tu tayari wanawaagiza wakulima wadogo wadogo (*Outgrower*), walime

miwa na wapeleke TPC. Tayari wale wakulima wadogo wana uhakika wa soko la kuuza miwa yao. Huu ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, Wakulima wengi hasa wa mazao ya nafaka kama mahindi, wanazuiliwa kuuza mazao yao nje ya nchi; lakini Serikali inaponunua mazao hayo kutoka kwa wakulima ili wayahifadhi kwa akiba, huwa wanunua kwa bei ya chini kuliko wakulima wanapokwenda kuuza nje ya nchi.

Wakulima hawapewi motisha kabisa na Serikali, mkulima huyu mtoto wake anatakiwa kulipiwa ada ya shule hana na anaweza kuuza mahindi yake ambayo yanaharibika kwa kukosa sehemu ya kuhifadhi. Tukumbuke hizi mbegu za mahindi za kisasa, huharibika haraka sana na matanki ya kuhifadhi mahindi yale yanauzwa ghali sana; mfano, kule SIDO Moshi, tanki la kubeba magunia 50 kulitengeneza siyo chini ya shilingi laki nne. Tunategemea mkulima huyu ateweza kuhifadhi mahindi haya? Hata akihifadhi bado bei yake siyo ya ushindani.

Mbona madini ambayo ndiyo yanayoweza kuliingizia Taifa fedha nydingi sana ambazo zingetosha kulisha Watanzania wote; wawekezaji wa madini wanaruhusiwa kubeba mchanga na kuupeleka makwao na baadae kutulipa mrabaha wa 3%? Je, aliyetakiwa kudhibitiwa ni mkulima au huyu mwekezaji kwenye madini?

Hivi hawa maafisa wa kupima viwanja huko vijiji; watafanyaje kazi wakati hawana vitendea kazi vyta kutosha? Kwa mfano, kuna vijiji vilivyopo mbali sana na Ofisi za Wilaya, Wafanyakazi hawa wangepatiwa hata pikipiki za kuendea kwenye vituo vyta kazi. Hiyo haitoshi, kuna Mkoa kama Kilimanjaro Darubini ipo moja; tunategemea nini?

Mategemeo yangu ni kwamba, kabla ya kipindi kijacho cha Bajeti (2009/2010), wastaa fu hawa watakuwa wameshalipwa haki zao. Hivi Serikali haiwaonei huruma wazee hawa amba ni Hazina ya Taifa? Katika Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, kumekuwepo na malipo mengi tu hewa ya wafanyakazi amba hawapo kazini. Serikali inatueleza nini kuhusu uzembe huu amba fedha hizo zingeweza kusaidia katika malipo ya Wazee hao?

Hili la kutoza kodi huduma zinazotolewa na Taasisi za Dini siyo sahihi; kama kuna Mashirika yaliyotumia misaada vibaya basi wapewe adhabu hata kufutiwa, badala ya kuadhibu wote wenye nia njema ya kulisaidia Taifa katika nyanja za Elimu, Afya na kadhalika. Iweke bayana ni huduma zipi zitakazotozwa kodi.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nashauri Kilimo Kwanza kizingatiwe. Tubuni mikakati ya *Mechanization of Agriculture*. Kilimo cha Mashine, yaani *tractors*, mbolea na pembejeo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hatuna kiwanda cha majembe ya mkono na tractor; je, ni sahihi? Nashauri Kilimo Kwanza kiwe na viwanda vya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa kuwalipa Wakandarasi mbalimbali kwa utaratibu wa *Certificates*, hasa katika kandarasi mbalimbali na hela hizo hutolewa na Hazina au Hazina Ndogo Mikoani. Nashauri umuhimu wa kuwalipa Wananchi kwa muda muafaka, kwani Wakandarasi na Wazabuni wengi hukopa hela kwenye Mabenki kwa riba kubwa. Wanavyochelewa kupokea hela zao, wanakuwa katika wakati mgumu sana.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa usimamizi na uongozi wako katika kuliendesha Bunge.

Nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa taarifa yake nzuri, iliyosheheni malengo ya kumpunguzia mzigo mwananchi. Pongezi hizi pia ziwahusu Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote kwa kufanikisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, uzuri wa Bajeti hii ni pale ilipoanzia Kilimo Kwanza. Ili Uchumi wetu uwe mzuri ni vyema kukiimarisha kilimo. Mambo muhimu yafuatayo yazingatiwe: Wataalamu wa kilimo, wawezeshwe na wakae vijijini kusaidiana na wakulima. Wakati huo huo tafiti zote zinapokamilika, zipelekwe vijijini zitumiwe na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ukiriguru ni muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo, lakini kimekuwa na matatizo ambayo sijafahamu kwa nini Serikali inawatesa Wataalamu hao? Lipo tatizo la maji la muda mrefu. Mradi wa kumaliza tatizo hilo ulishaanza, lakini kwa sababu zisizofafanuliwa na Hazina pia Wizara ya Kilimo wanafahamu. Naishauri Serikali kwa ujumla wake, kuinua kilimo ni pamoja na kuwajali Wataalamu wetu wa utafiti Ukiriguru na Chuo cha mafunzo Ukipriguru kuhusu tatizo lao.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Wizara yako (Hazina); ni wahusika wakuu katika kukwamisha mafanikio ya mradi. Shughulikia ili jibu lipatikane.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii inafurahisha, kwa kuzingatia matatizo ya watu wake. Kati ya sekta zilizopewa kipaumbele ni pamoja na Wizara ya Maji. Katika Wilaya yangu, suala la maji halijapata ufumbuzi wa kudumu; hata hivyo, hatua za Serikali kulishughulikia suala hilo zinatia moyo.

Ushauri kwa Serikali yetu ni kumaliza miradi inayioianzisha, kwani mradi uliopo Misungwi wa Nyahati ni wa miaka mingi; hivyo, Sekta husika ilitilie maanani suala hilo, Watu wa Misungwi waondokane na tatizo hilo.

Mradi wa Kahama – Shinyanga umeanzia Ziwa Victoria, eneo la Ihelele, Wialyani Misungwi. Vijiji vilivyopata maji ni sita tu, kitu hicho kinalalamikiwa na Wananchi wa Misungwi.

Ushauri wangu, Serikali ione umuhimu wa kuvipatia maji vijiji vilivyopo Tarafa za Mbarika vijiji 13 vilivyobaki; na Inonelwa vijiji 21 vilivyobaki.

Upande wa Tarafa za Usagara na Misungwi zitapata Maji kutoka Mradi wa Nyahiti.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ni muhimu kwa maendeleo ya nchi. Barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawi, inahitaji matengenezo kabla ya kuharibika na kujifunga. Hivyo, Bajeti ya Wizara iliangular hili, vinginevyo, mwakani haitapitika; kuipangia shilingi 60 milioni si sahihi iongezwe. Mkurugenzi wa Barabara (Iyombe) anaifahamu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya ni kitu ambacho kimepewa pia kipaumbele katika bajeti hii. Mikakati iangular maslahi ya Watumishi. Kazi za Watendaji hawa ni za saa ishirini na nne, wamekuwa na kipato kidogo sana ukilinganisha na kazi yao. Huu ni wakati wa kuangular kipato chao, sambamba na kukiboresha. Ipo haja katika bajeti hii, kununua vitendea kazi ili Watendaji hawa tuliuwasomesha kwa pesa za Watanzania wafanye kazi. Kufanya hivyo ni kuzuia pesa nyingi wanayoitumia Watanzania kwa matibabu nje ya nchi; hivyo, uwezeshaji wa vitendea kazi kwa Watendaji (Waganga) ni kuinua uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikuonesha ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Barabara za Halmashauri. TAMISEMI imekuwa ikitengewa pesa kidogo, hali inayowafanya washindwe kutengeneza barabara zilizo chini yao.

Ninaiomba sana Serikali, ione kila sababu ya kuongeza pesa kwenye eneo hilo ili barabara vijijini zipitike na hizo ni sababu za kuinua uchumi kwa maana mazao ya mkulima yatafika sokoni kwa wakati; hivyo kipato cha mkulima kitaongezeka. Huduma za akina mama kwenda Zahanati na kufuata maji zitakuwa rahisi.

Mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Namtakia Waziri, afya njema na utendaji mwemama katika Bajeti nzuri.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMISI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti, kwa kulisimamia Bunge vizuri. Mungu awabariki, mtuongoze vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono Bajeti hii ya Fedha na Uchumi kwa mwaka 2009/2010. Hata hivyo, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Nne (2009/2010), naomba tuwe makini sana hasa tukizingatia hali ya uchumi Duniani hadi ndani ya Tanzania yetu. Kwa hiyo, Serikali chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na wewe Waziri wa Fedha na Watendaji wa Wizara ya Fedha, msimamie na kutekeleza kazi vizuri kwa faida ya Tanzania na Wananchi wetu, pia muwajali Wakulima, Wafugaji na Wananchi wa hali ya chini.

Mheshimiwa Spika, Kilimo ni Utu wa Mgongo. Pia Kilimo Kwanza. Hata hivyo, maneno pekee hayatoshi, kupitia Bajeti hii basi niombe utekelezaji wote uliowekwa kupitia wataalamu, utumike vyema na itumike zaidi Ilani ya CCM na kutukuza maneno ya Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Nne, alipotoa hotuba juu ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Wazari wa Fedha, imeeleza kuhusu Utalii, Miundombinu na Biashara, lakini bado naiomba Serikali iwe macho zaidi, kuepuka hila za wajanja wenyewe uzembe utakaosababisha kuhujumu uchumi au kupoteza fedha ovyo na kukosa maendeleo na malengo mazuri.

Mheshimiwa Spika, Benki za ndani na za nje, pamoja na Benki ya Wakulima zisaidiwe na zitumie utaratibu mzuri kwa maslahi ya Wananchi wa Tanzania na Uzalendo uwepo zaidi na maisha bora kwa kila Mtanzania. Mambo ya Muungano yote na Sekta za mgao wa fedha na mambo kama hayo, yaendeshwe vizuri na kama bado kwa nini? Naomba Serikali isimamie na kumaliza au kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti hii.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu. Hotuba hii imeelekeza kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kukipa kipaumbale kilimo, kwa maana ya Kilimo Kwanza na kikitengea fedha za kutosha zisizopungua shilingi 20 bilioni.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa ni nyingi na zinaweza kuleta tija kubwa na kuongeza Pato la Taifa kama zitawafikia wananchi vijijini na kusimamiwa vizuri. Tatizo kubwa kwa wakulima ni pembejeo ambazo zitaboresha kilimo na kupata mazao ya kutosha na kuwapunguzia umaskini.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri fedha Wizara itoe mchanganuo mzuri unaoonesha mgawanyo wa fedha kwa kila Mkoa na kwa miradi husika. Mgawanyo huo uzingatie vilevile mikoa ambayo hali ya mvua zisizo na uhakika kwa kuwawezesha kujenga mabwawa na uvunaji wa maji ya mvua. Ninaomba Serikali, fedha hizi zinunulie matrekta, mbegu bora, madawa, kama ilivyojielekeza yenyewe na la msingi kabisa ni usimamizi, kitu ambacho ni tatizo tulilonalo. Lingine ni kuanzisha mashamba makubwa kwa kuwatumia na kuwashawishi wasomi, ambao wanawenza kutumia taaluma zao na mafanikio makubwa yakapatikana, badala ya kuwaacha wananchi vijijini, ambao hawawezni hata kutumia fursa za mikopo kwa kukopa.

Ili kuboresha ufugaji ambao ni muhimu sana ni vizuri ahadi zilizotolewa kwenye hotuba hii zisimamiwe vizuri na zitoe tija kwa wananchi. Tabia ya kupanga, kueleza, kuelimisha bila kusimamia utekelezaji, haitawawezesha wananchi kupata maendeleo. Hapa kubwa ni kununua madume bora na kuanzisha vituo katika vijiji ili yatumike

kubadilisha mifugo. Vituo hivi vihudumiwe na wataalamu wa kilimo na mifugo na madume haya yanaweza kutumika vilivyo.

Mikopo ni muhimu iweze kuwanufaisha wananchi vijijini, lakini kutohakana na masharti ya Benki, hawawezi kunufaika. Ili wanavijiji hawa wafaidike na mikopo hiyo ni vizuri Serikali iunde timu ya kuwasaidia wanavijiji wakamilishe vikwazo hivyo na waweze kupata mikopo.

Tunaomba suala la kurudisha JKT kwa mujibu wa Sheria liharakishwe ili kurekebisha nidhamu za Watumishi ambao wanaajiriwa. Vilevile somo kubwa linalotakiwa kufundishwa la uzalendo, limeathiri sana ndani ya Watumishi mbalimbali kwa kuweka maslahi binafsi mbele na kuacha maslahi ya Taifa; ndio maana kunakuwa na upotevu wa fedha nyingi. Ushahidi ni Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali.

Tunaomba Serikali iangalie umuhimu wa kuboresha kilimo cha zabibu kwani ni kilimo cha biashara pekee cha Mkoa wa Dodoma na ni tegemeo kubwa. Tunaomba tuone waziwazi, kazi ya Serikali ili kusukuma kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, hakuna Watendaji/Wataalamu katika ngazi za Vijiji wa Idara mbalimbali na hasa Kilimo, Maliasili, Mifugo, Maendeleo ya Jamii, Ushirika na Ardhi, ambao wangeweza kusimamia mipango ya Serikali ili iweze kuinua hali za wananchi kiuchumi na waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuongeza pensheni, ingawa hatujui imeongezeka kiasi gani. Ombi ni kwamba, kustaafu kwa mtumishi ni kwa yeoyote kama atabarikiwa kustaafu akiwa kazini; hivyo Mfuko huu utamsaidia asiathirike. Kiwango kikifikia shilingi 60,000 kwa mwezi kitamsaidia.

Hali ya chakula siyo nzuri. Tunaomba Serikali ijitahidi kupata taarifa za haraka kutoka maeneo mbalimbali Wilayani ili wapelekewe msaada wa chakula mapema, wananchi wasiathirike kwa kuchelewa kupata taaarifa za kweli.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali inavyojitahidi kusimamia mipango yake katika Wizara na Idara mbalimbali na mafao yanaonekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na uwezo wa kuchangia Bajeti iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa ufanuzi alioutoa kuhusu hali ya msukosuko wa kiuchumi. Pia nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze Wafanyakazi wa TRA, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu ni nzuri na inayojali Wananchi wa Tanzania. Ikitekelezwa kama ilivyopangwa, nchi yetu itapiga hatua kubwa kuwakomboa wanyonge.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mfumko wa bei ni mkubwa na hali hii itaondoka kutokana na utekelezaji wa mipango iliyopangwa katika kipindi hiki. Kwa hiyo, ninachokiomba haya yalioelezwa katika vitabu hivi viwili, yatekelezwe na yasiishie kwenye maandishi tu.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi iliyopendekezwa katika Mipango na Bajeti hii, naiomba Serikali iangalie tena msamaha wa kodi ya mafuta katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa imefika wakati, mashirika na makampuni yanayochimba madini, kulipa kodi kikamilifu kama yanavyolipa mashirika mengine ya ndani. Umefika wakati kila mmoja wetu ali pe kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye Bandari. Wachangiaji wengi wamezungumzia matatizo yaliyoko Bandarini na kutajwa TICTS kuwa ndio chanzo cha kuzorotesha utendaji mzima Bandarini hapo na kuikosesha fedha nyingi nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, Serikali ingefanya uchunguzi wa kutosha hasa kwa vile bandarini kuna vyombo vingi vinavyofanya kazi na isiwe lawama zote zinakwenda kwa TICTS na ikionekana kuna ukweli basi ichukue hatua za kufaa, pamoja na wengine wote wanaosababisha kasoro zilizozungumzwa na wachangiaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa bandari, lazima tuongeze kasi ya kutumia Bandari zetu nyingine za Tanga, Mtwara na Zanzibar ili kuongeza ufanisi wa kazi. Tukiendelea kung'ang'ania Bandari ya Dar es Salaam, tutaendelea kulaumu utendaji kutokana na ufinyu wa eneo na hasa kama majirani zetu wataamua kutumia Bandari za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu kwa kuelekea Hazina. Hazina ni chombo cha Serikali, lakini utendaji wa kazi yake nao unarejesha nyuma maendeleo na kuikosesha Serikali mapato baada ya wao kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, Hazina wanachelewesha kupeleka fedha kwenye miradi ambayo kama fedha zingetumwa kwa wakati, ingemalizika mapema na kuipatia mapato Serikali.

Mheshimiwa Spika, Hazina pia inalamikiwa kuchelewesha kutoa dhamana ya kuanza kwa miradi ambayo mashirika yetu ya Mifuko ya Jamii iko tayari kuiendeleza na wakati mwagine kuisababishia hasara Mifuko.

Mheshimiwa Spika, Hazina lazima ijisawazishe na namwomba Mheshimiwa Waziri, awachunguze wafanyakazi wake. Nahisi kuna wengine hawako tayari kuitetea Ilani ya Chama cha CCM, pamoja na utekelezaji wa Ahadi za Rais wetu, kutokana na kutokutolewa fedha kwa wakati, yanawakera wengi na kusema Hazina ni kikwazo.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na Wapiga Kura wa Jimbo la Fuoni, tunaunga mkono hoja.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii, kuipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa bajeti yake ambayo pamoja na msukosuko wa fedha ambao umeikumba Dunia, Wizara hii imeweza kuleta Bajeti ambayo ina lengo la kumsaidia Mtanzania kutokana na msukosuko huo.

Vilevile naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii, kwa utendaji wao ambao unaridhisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo ya uchumi, lazima tuipongeze Serikali kwa kuweza kukuza Pato la Taifa kutoka asilimia 7.1 mwaka 2007 na kufikia asilimia 7.4 mwaka 2008; ni jambo la kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Rais ya kuteua Wajumbe wapya wa Tume ya Pamoja ya Fedha, kwa ajili ya kukamilisha uchambuzi wa Taarifa za Tume, nimwombe Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho anipe *time frame*; ni lini tatizo hili litamalizwa na Serikali ili kuondoa maneno kati ya SMZ na SMT tukiwa Jamhuri moja?

Mheshimiwa Spika, pamoja na mashirikiano hayo, pia naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kwa makubaliano ya kuipatia SMZ asilimia 4.5 ya mikopo ya kibajeti kuanzia mwaka 2009/2010.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii, kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremia S. Sumary na Mheshimiwa Omar Yusufu Mzee, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia msukosuko wa uchumi duniani ni kwamba, Watanzania wote tutaathirika kutokana na misukosuko hiyo. Katika hali hii, mfanyakazi wa kima cha chini ametazamwa vipi? Gharama za maisha zitapanda, lakini kipato cha mfanyakazi wa ngazi za chini uko palepale; je, Serikali itawasaidiaje?

Mheshimiwa Spika, Kaulimbiu ya Serikali mwaka huu wa 2009/2010 ni Kilimo Kwanza. Naomba kujua mkakati uliowekwa na Serikali, kuhakikisha kuwa mkulima wa vijiji ananufaika na mabilioni ya pesa zilizowekwa TIB, kwa nia ya kuwakopesha wakulima.

Je, kuna utaratibu wowote wa TIB kuwa na matawi katika wilaya zetu ili tuwahamasishe wakulima kwenda kukopa katika matawi hayo ya TIB? Iwapo TIB itabaki kuwa Dar es Salaam, ina maana kwamba, watakaonufaika na fedha hizo za serikali ni watu wachache sana na kuna uwezekano wa fedha hizo kutotumika na wakulima.

Mheshimiwa Spika, Wahindi (RITES), wameshindwa kusimamia/kuendeleza Reli. Kabla ya Serikali kuingia ubia na Kampuni ya RITES kuendesha Reli, usafiri wa abiria na mizigo ulikuwa mzuri kuliko sasa; kwa nini utendaji wao usipimwe na ikionekana hawawezi kazi mkataba wao uvunjwe? Wananchi wanaotegemea usafiri wa reli wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka jana, Serikali ilitenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dodoma - Babati na kiasi cha shilingi milioni 524 kwa ajili ya Barabara ya Dodoma – Iringa. Katika bajeti ya mwaka huu, hakuna pesa zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara tajwa; je, hii ina maana kuwa nia ya serikali ilikuwa ni kujenga madaraja tu na siyo barabara? Napenda kujua ujenzi wa barabara tajwa utaanza lini kwani barabara hiyo inaunganisha Mikoa minne ya Arusha, Manyara, Dodoma na Iringa na inapita katika maeneo muhimu kwa maendeleo ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi duniani ni mbaya; hivyo kila mwananchi atatakiwa kubana matumizi ili kukabiliana na hali iliyokumba dunia. Nilitegemea Serikali yetu kuonesha mfano katika kubana matumizi yake kabla ya serikali kukopa kwa ajili ya matumizi yake ya kawaida. Waziri wa Fedha na Uchumi, atueleze jinsi serikali ilivyopanga kupunguza matumizi yake ya kawaida. Serikali ikope pesa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na si kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, napenda kunukuu katika ukurasa wa 52 (xiii) wa Kitabu cha Bajeti, iliyosomwa na Waziri wa Fedha na Uchumi: “Kuondoa msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Special Relief*), kwa Asasi zisizo za Kiserikali (*NGOs*) na Mashirika ya Dini.”

Mheshimiwa Spika, Waziri hakutaja vitu gani vitakavyoondolewa msamaha maalumu wa kodi. Mheshimiwa Waziri ataje maeneo husika ili waumini wa dini zote, pamoja na viongozi wao, waendelee kuwa na amani kuliko serikali kukaa kimya na kujenga uadui kati ya waumini, viongozi wa dini na serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, kwa kuandaa Bajeti yenye kuleta matumaini. Bajeti hii haiwezi kutosheleza na kukidhi mahitaji na kiu ya maendeleo walijonayo wananchi wengi. Kama alivyoituasa Baba wa Taifa, ninanukuu: “Kupanga ni kuchagua.”

Naipongeza Serikali, kwa kuweka vipaumbele na kuzingatia mikakati itakayochangia katika kuleta maisha bora kwa kuchochaea uchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu, napenda kutoa ushauri katika sekta zifuatazo:-

Pamoja na Serikali kuongeza Bajeti ya Elimu kwa asilimia 22, sekta hii bado inapanuka haraka. Wizara ya Fedha ijizatiti kwa kuweka akiba ya fedha za dharura ili kukabiliana na msukosuko kutoka Vyuo Vikuu. Tusingojee mpaka vurugu itokee.

Suala la mkopo kwa wanafunzi maelezo yatolewe mapema na wale wote ambao hawatapata nafasi ya kupata mikopo wajulishwe.

Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, ipate maelekezo ya kutosha. Kisimamiwe kwa vitendo kwa kutoa Elimu ya kutosha kwa Maafisa Ugani katika Kata; miongozo ya kufanyia kazi iandaliwe haraka na iwafikie wananchi haraka.

Naomba yatolewe maelezo ya kutosha kuhusu Fedha za EPA, ambazo zilipelekwa Wizara ya Kilimo kuitia Benki ya TIB kuwasaidia wakulima, kwa kuonesha mchanganuo jinsi fedha hizo zilivyotumika.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hotuba nzuri aliyoitoa Kilimani Mjini Dodoma, tarehe 10 Juni, 2009. Hotuba hiyo iliwayumuisha Wazee wa Mkoa wa Dodoma, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, ikiwa na lengo la kuwafahamisha wananchi kwa ujumla, kuhusu msukosuko wa uchumi ulioikumba Dunia na kuhusu Bajeti ya Mwaka huu wa 2009/2010.

Hotuba hiyo iliwaamsha wananchi wote kwa ujumla, kuhusu mwenendo mzima wa uchumi wa dunia na hali itakavyokuwa nchini Tanzania.

Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa Hotuba ya Bajeti, aliyoitoa tarehe 11 Juni, 2009 hapa Bungeni, ambayo imelenga msemo wa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka huu wa 2009/2010 ni nzuri na inalenga kuleta matumaini makubwa kwa Watanzania wote hasa wale walioko vijijini. Hivyo, napenda kuiomba Serikali ijiweke vizuri katika utekelezaji wa Bajeti hiyo.

Ikiwa Serikali itaweka msimamo, usimamizi na ufuatiliaji katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka huu, tutaweza kuwa juu nchini kuliko miaka ya nyuma iliyopita.

Mheshimiwa Spika, fedha ambazo zitatengwa kwa ajili ya kilimo ziwe endelevu na sio kusita sita. Mikopo isiwalenge wakulima wakubwa tu; na wakulima wadogo

wapatiwe mikopo hiyo wasiwe na kilimo cha kubahatisha. Mbolea ya ruzuku iwafikie wakulima kwa wakati unaotakiwa ili kuepusha malalamiko yanayojitokeza. Kilimo cha Umwagiliaji kiendelezwe na kuwekewa mikakati madhubuti. Mikoa inayozalisha chakula kwa wingi ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kipengele kinachosema msamaha maalumu wa kodi kwa makampuni ya madini; suala la kufuta kodi kwa makampuni ya madini, lingeangaliwa upya kwa sababu faida ambayo inaingia katika Serikali kutokana na madini ni ndogo sana. Kuondosha kodi kwa wawekezaji wa makampuni hayo ni kuendelea kuwaongezea utajiri makampuni haya, bila kuiangalia Tanzania inapata kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa sasa hivi Tanzania tunatakiwa kujiweka vizuri kwa kuzalisha zaidi, kuwa na ari ya kufanya kazi kwa uadilifu na mengineyo.

Je, katika msukosuko huu ulioikumba nchi kwa ujumla, kwa upande wa pili wa Tanzania, yaani Tanzania Visiwani; tumeandaa mikakati gani kama Jamhuri ya Muungano katika kuinusuru Zanzibar nayo isiyumbe na msukosuko huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Katika kuzingatia azma ya Serikali ya kuleta maendeleo nchini na maisha bora kwa Watanzania wote, Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2009/2010, imepanga kutekeleza pamoja na mambo mengine, kuboresha na kupanua Miundombinu ya Barabara, Reli, Bandari, Viwanja vya Ndege na Umeme hasa vijijini; kadhalika kutenga fedha za kugharimia miradi maalumu katika maeneo yenye mazingira magumu, yasiyovutia watumishi kufanya kazi kwenye maeneo hayo.

Pamoja na uwezekano wa kuanza mradi wa kuzalisha chuma ghafi (*Sponge Iron*), mwaka huu, mbona Barabara ya Itoni (Njombe) – Mkiu – Mwandindi (Wilaya ya Ludewa), haiko kwenye mpango wa kutengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuwezesha mizigo mizito kusafirishwa katika barabara hiyo, licha ya Mkao wa Iringa kuwasilisha andiko maalumu la mradi huo wa barabara ya lami katika Wizara ya Miundombinu mwaka jana? Inakuwaje eneo ambalo kunaanzishwa mradi mkubwa wa kitaifa kama huo, halifikiriwi kupewa barabara ya lami?

Ni miradi gani maalumu kwa mfano itakayotengewa fedha katika maeneo yenye mazingira magumu na fedha hii tutaiona kwenye Bajeti ya Wizara gani?

Katika sera za matumizi, bajeti hii inalenga kuendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Tatizo langu ni kwamba, licha ya mpango huu kuanza mwaka 2008/2009, sikuona fedha yoyote ilivoletwa na TAMISEMI kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa zahanati na vituo vya afya katika Wilaya ya Ludewa. TAMISEMI walisema hawakupatiwa gawio la fedha na Wizara ya Fedha na Uchumi. Fedha hiyo ilipitishwa na Bunge lakini haikutumika; je, imekwenda wapi?

Katika fursa kwa nchi yetu zitokanazo na msukosuko wa kifedha na kiuchumi duniani, bajeti hii inapendekeza kuainisha na kupima maeneo ya mashamba makubwa (*Land Bank*), kwa uzalishaji wa mazao ya chakula. Tatizo langu ni kwamba, sehemu kubwa ya ardhi inayodhaniwa kuwa haitumiki ni mali ya vijiji. Je, kuchukua ardhi ya vijiji kwa kiwango kikubwa hivyo haitapingana na Sheria ya Ardhi ya Nchi hii hususan *Village Land Act?* Je, hii haitafanana na *Land Acquisition* iliyofanywa na Wakoloni kwa Wazungu (*Settlers*) baada ya Vita Kuu ya Pili?

Bajeti hii inapendekeza kupunguza kiwango cha ukomo cha kutoa ushuru wa mazao kutoka asilimia tano ya bei ya kuuza mazao shambani hadi asilimia tatu ili kupunguza athari za msukosuko wa uchumi duniani kwa wakulima nchini, lakini kuanzia 2010/2011 baada ya Serikali za Mitaa kujiandaa kupata vyanzo mbadala vya mapato.

Je, vyanzo mbadala ni vipi hivyo kwa mfano ambavyo havitapingana na sheria ya nyuma ya kuondoa vyanzo vya ushuru mbalimbali vya Serikali za Mitaa?

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Pamoja na kuchangia kwa kuongea, naomba kwa niaba ya Wananchi wa Kyerwa, nizidi kusisitiza yafuatayo:- Serikali iyahimize Mabenki yaikopeshe Sekta ya Kilimo kwa riba yenyе tija. Naipongeza CRDB kwa kuonesha mfano.

Kunyauka kwa migomba na mikahawa; Serikali ngazi ya Wilaya imejitahidi, lakini ngoma bado nzito, migomba inaisha. Tunataka na kuomba Serikali ngazi ya Taifa ijihusishe, kabla mambo hayajazidi.

Umeme Vijijini ni ahadi ya muda mrefu, mpaka mwisho ameahidi Mheshimiwa Rais mwenyewe, alipotembelea na kuzunguka Wilaya ya Karagwe. Kila aliposimama, alirudia ahadi hiyo; Rwambaizi, Murongo, Kaisho, Nkwenda na Kuyanga. Tafadhali wananchi wanaomba utekelezaji.

Wananchi wanaendelea kunituma niombe Wilaya ya Karagwe igawanywe ziwe Wilaya mbili; Wilaya ya Kyerwa na Wilaya ya Karagwe. Wilaya inazidi kwa ukubwa Wilaya zote za Mkoa wa Kagera, pia inazidi hata ukiunganisha Wilaya mbili; chato na Misenyi au Bukoba Vijijini na Misenyi. Vigezo vingine ni muafaka. Tunaomba itengwe ili maendeleo yatolewe haraka.

**MHE. COL. FETEH S. MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa Hotuba yake nzuri; iliojaa busara na hekima juu ya dhana kuu ya kunyanya uchumi wa nchi yetu hasa kutohana na wimbi kubwa la kuyumba kwa uchumi katika dunia.

Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Manaibu wake, Makatibu Wakuu wa Wizara na Wataalamu wake.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, duniani kote, kwa zile nchi zilizobahatika kuwa na Bandari za Bahari na Maziwa Makuu, basi mara nyingi zinaneemeka sana kiuchumi, endapo bandari hizo zitatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mojawapo iliyobahatika kuwa na Bahari Kuu na Maziwa Makuu, lakini bado hatujaitumia fursa hiyo ipasavyo. Ninaomba sasa tuzitumie ipasavyo bandari zetu katika kuzitanua na kuzijenga kisasa, kwa manufaa ya nchi na wananchi wake, aidha, kudhibiti nyanja zote za ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina bahati ya Bahari yenye eneo kubwa sana kuanzia Capa de gado hadi Horohoro mpakani na Kenya na tuna bahati ya uvunaji wa samaki wazuri wenye minofu, ambao wanapendwa sana duniani. Sasa ni vyema tujiimarishe kwa kuwa na meli zenye uwezo wa uvuvi wa kisasa. Aidha, tuimarishe viwanda vya samaki vya kisasa. Vile vile tuweke bidii katika kukiimarisha Kiwanda cha Samaki kilichopo Mwanza na kiwanda cha utengenezaji wa zana za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, bado hatujawekeza hata kidogo kwenye uchumi wa Bahari na Maziwa yetu Makuu. Hivi sasa samaki wetu wanavuliwa ovyo ovyo na nchi za kigeni; hali hii tutaiacha mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu huu mdogo, ambao nina hakika, Waheshimiwa Wabunge wengi watakubaliana nami katika kuangalia sekta hizo ambazo bado serikali yetu haijazziimarishe ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na Wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, naiunga mkono hoja hii ya Waziri wa Fedha na Uchumi kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja. Pamoja na hayo, naomba yafuatayo yazingatiwe katika bajeti ikiwezekana:-

Katika ahadi zangu za kugombea Ubunge – 2005, niliahidi kulivalia njuga suala la upatikanaji wa Wilaya katika Jimbo la Kilwa Kaskazini. Pamoja na majibu nipewayo kuwa ufinyu wa Bajeti ndio ufanyao Jimbo hili isipatikane, lakini siku zinafikia ukingoni bila mafanikio yoyote. Ukikumbuka kwamba, vigezo vyote kama eneo, idadi ya watu, urefu wa mwanzo hadi mwisho wa Jimbo (Mpakani Rufiji Wilaya ya Liwale); hivyo inaniwiya vigumu sana kutembelea na kusikiliza matatizo ya wapiga kura wangu kwa kipindi cha miaka mitano kwani vijiji vingi na matatizo ni mengi sana; hivyo naona nawanyima haki wananchi kupata huduma ya Ubunge na maendeleo ya Jamii.

Kumbuka swalii langu la mwanzo kabisa katika Bunge hili Tukufu niliuliza, tuko kama yatima kwani maendeleo yote ya huduma za kijamii yanapatikana upande mmoja wa wilaya, kwa mfano, Hospitali, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Watendaji wake; Polisi, Magereza na hata Ofisi ya Mbunge, wao yapo Kilwa kusini; je, Mheshimiwa Waziri huoni busara ya kuipa Wilaya Jimbo la Kaskazini? Wananchi wamechoka kusikia jibu la

ufinyu wa Bajeti kwa kuwa Wilaya nyingine zinagawiwa. Nafahamu umoja ni nguvu, lakini haki ya Binadamu katika nchi yake, lazima pia iangaliwe kwa jicho la huruma.

Nitasema nini kwenye uchaguzi ujao endapo suala hili halikutatuliwa?

*Rural Electrification Project* katika Jimbo la Kilwa Kaskazini imekuwa kama ndoto ya kusadikika, japo gesi inapitia pale pale Jimboni kwetu (Somanga Fungu), lakini hata minong'ono ya kupata umeme mbali na lilipopita bomba au kituo, kama kuna uwezekano wa kupata nishati hiyo. Ninafahamu, inasemekana kuwa tutapata umeme kutoka mradi mkubwa kwa Songosongo, lakini lini waishio mbali na bomba hili watapata umeme? Naomba kauli yako.

Wananchi nimewahimiza kwa nguvu zote, wachangie ujenzi wa Shule za Sekondari, Vituo vya Afya na kadhalika, lakini bila nishati ya umeme si nitakuwa natwanga maji kwenye kinu!

Ninayo mengi lakini haya mawili yanatukera sana, ndio maana tunadiriki kusema tu watoto yatima katika nchi yetu.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wataalamu, kwa kuandaa Bajeti nzuri. Hata hivyo, kuna maeneo yanayohitaji kutazamwa vizuri na kwa karibu zaidi, kwa nia ya kuboreshwa. Hizi sehemu ni kama ifuatavyo:-

- (a) Wizara kupewa Tsh. 3,476,243,000,000 na Halmashauri zote nchini kupatiwa Tsh. 1,565,974,000,000, inahitaji kutazamwa upya. Huduma za jamii na shughuli za kiuzalishaji, zipo vijijini na ngazi ya Halmashauri; hivyo pesa zaidi ilipaswa kushushwa kwenye Halmashauri zaidi kuliko kubakiza Wizarani.
- (b) Taasisi/ Asasi za Kiraia na Madhehebu ya Dini yamekuwa yakitoa huduma nyingi za jamii katika maeneo mengi nchini, hivyo wazo la kuondoa msamaha wa Kodi ya VAT si sahihi. Hivyo, sehemu hii ibadilishwe na msamaha ubaki kama ulivyo hivi sasa.
- (c) Tofauti kubwa kati ya Mikoa kulingana na fedha wanayopangiwa irekebishwe. Fedha ipangwayo Mikoani hailingani, Mikoa michache inapendelewa na mingi hupatiwa fedha chache sana. Mifano ni Mikoa wa Dar es Salaam na Dodoma, Morogoro na Tabora, Tanga na Kigoma.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (Mb), Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba zake mbili za Hali ya Uchumi wa Taifa na ya Makadirio ya Mapato na Matumizi, ambapo zimeonesha hali halisi ya maendeleo ya nchi yetu na mwelekeo wa kwenda mbele (*way forward*). Hotuba zote zina takwimu muhimu na zimeelezwa kwa uwazi na zimelewaka, ndiyo maana michango inakuwa ya kina. Nampongeza sana na kuunga mkono hoja yake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwengine, nawapongeza wasaidizi wake wote, wakiongozwa na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Sumari (Mb) na Mheshimiwa Mzee (Mb), Katibu Mkuu, Bw. Khijjah, Naibu Makatibu Wakuu; Bw. Haule na Dkt. Mpango, Wakuu wa Idara na Wafanyakazi wote wa Wizara hiyo, kwa kumsaidia kwa uadilifu Waziri wao na kumuwezesha kusoma hotuba zote kwa ufanisi maana zimeandikwa vizuri sana. Hongereni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna sehemu ya hotuba ya bajeti, kifungu cha 72(vi), kuhusu kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye chai na kahawa iliyozalishwa na kusindikwa hapa nchini. Kodi hiyo ilikuwepo lakini ikaondolewa kwa sababu za msingi. Ikirudishwa basi Watanzania hawatanunua na kukimbilia chai na kahawa kutoka Kenya na Uganda. Aidha, watarejea kwenye kunywa chai wanayotengeneza wenyewe vijjini, inayoitwa SIDO. Napendekeza uamuzi huu upitiwe upya, tukizingatia kwamba, mazao haya hayauziwi mbolea yenyeye ruzuku, hivyo inaonekena kuwa Serikali haiyathamini bali inathamini mahindi tu. Chai na kahawa ni mazao ya chakula na biashara nje ya nchi. Pamoja na haya, nazidi kuunga mkono hoja hii kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, makombora yanayoelekezwa kwa Waziri na Serikali ni hali ya kawaida, inayoashiria kuwa muda wa Bunge la sasa unamalizika, kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011 hayatakuwepo bali kupongezana tu.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji wake wote, kwa Hotuba yake ya Bajeti, yenyeye mtiririko wenyeye kufahamika. Pia, naunga mkono hoja hii asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, naomba nifahamishwe kuhusu ile sehemu inayopelekwa Zanzibar; ingali hiyo hiyo asilimia 4.5 pamoja na ongezeko lote la Bajeti na mfumko wa bei? Imeshachosha kusubiriana, naomba tuelezwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, kuna haja ya kuendelezwa na kumalizwa ile miradi iliyokwishaanzishwa ya maendeleo kama vile ujenzi wa barabara, shule, zahanati na kadhalika, badala ya kuanzishwa miradi mipyä, matokeo yake kule hakuendelei wala hakuna kumalizika. Kwa hiyo, haya lazima yazingatiwe, la sivyo, tutakuwa tunapigishana kelele kila siku hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo ya msamaha kwa wawekezaji; inakuwaje tunatengeneza kwa wenzetu kwetu tunateketeza hasa kwa upande wa madini? Masuala ya ajira yapewe kipaumbele kwa watu wetu badala ya wagoni, mbona nasi tukienda kwao tunasumbuka, kwa hiyo, lazima tuwe na mikakati.

Mheshimiwa Spika, haya masuala ya bidhaa za kutoka nje, nyingine zingepigwa marufuku na zisiingizwe hapa nchini. Bidhaa nyingine tunaweza kuzalisha na kutengeneza wenyewe, ambazo zina ubora na uhakika zaidi kama vile mafuta ya kula.

Tunayo mafuta yetu mazuri ya alizeti, pamba na karanga, ambayo ni safi kabisa. Kwa nini tunawatajirisha watu badala ya kujitajirisha wenyewe? Kwa hiyo, hili lazima lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya kuojimudu kwa watu wenyewe ulemavu, viondoshewe ushuru na pia Serikali itusaidie kutuchangia kwani vifaa hivyo ni ghali sana na wengi wetu hatumudu kuvinunua. Kwenye bajeti hii sijasikia kuzungumzwa suala la watu wenyewe ulemavu!

Mheshimiwa Spika, naitakia Wizara kila la heri na mafanikio mema.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ya kutangaza mkakati wa kuhami na kunusuru uchumi wa nchi hii, hapo tarehe 10 Juni, 2009. Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hiyo na Taasisi zake, kwa kazi kubwa waliyofanya katika kutayarisha Bajeti wakati huu wa kipindi kigumu cha m dororo wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongozi hizo, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mbalimbali, waliokwishachangia hotuba hii na kuishauri Serikali yetu juu ya hatua mbalimbali za kuchukua katika maeneo mbalimbali ili kuinusuru kutokana na hali mbaya inayoendelea katika maeneo kama bandari, reli, barabara, taasisi mbalimbali kama Vyuo vya Elimu ya Juu na huduma za kilimo, maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Bandari yetu ya Dar es Salaam ingeweza kuingizia Serikali pato kubwa sana la fedha kama huduma zake zingetolewa kwa ufanisi. Hivi sasa kuna malalamiko kutoka kila pande za nchi hii na hata nchi mbalimbali zinazotumia bandari hii, kuhusiana na huduma mbovu zinazotolewa na bandari yetu. Mbaya zaidi, ucheleweshaji wa mizigo na dalili za rushwa, zinanukia katika kila kona ya eneo hili. Serikali inashauriwa kuchukua hatua za haraka za kuirekebisha hali hii ili kuweza kuinua uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, reli yetu, TRL, ambayo wengi wetu tulioomo ndani ya Bunge lako Tukufu, tuliitumia wakati wa kwenda na kurudi toka shulen, vyuoni na kadhalika ni mhimili mkubwa sana wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji nchini. Kwa wakati huu, reli hii iko taabani kwa kila namna, kiasi cha kwamba katika maeneo mengine, wahujumu wanabomoa mataluma na kuyauza kama vyuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, mwezeshaji wa reli hii wakati huu ni mchovu kuliko wazalendo waliokuwa wakiisimamia kabla ya ujio wake. Naipongeza Serikali kwa hatua inazochukua ili kuiweka katika hali nzuri reli hii. Lakini iko haja ya Serikali kufikiria upya, juu ya kuendelea kuwa RITES kama mwendeshaji wa reli hii.

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na wenzangu kuhusu kilimo, maji, umwagiliaji, elimu na huduma za afya kwa ujumla. Naomba nikubaliane na wenzangu

kuwa, fedha zinazotengwa kwa ajili ya maeneo haya, haziendi sambamba na la mgambo linalopigwa kuhusu maeneo haya; hazitosh na kwa kiasi kikubwa tunategemea misaada ya wafadhili, ambao wengi wao ama hawatimizi ahadi zao au hucheleva kuzitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kaulimbiu ya elimu kwanza au elimu ni ufunguo wa maisha, haitekelezwi ipasavyo. Upungufu wa vitendea kazi shulen, upungufu mkubwa wa walimu na ufinyu wa bajeti, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ni dalili mbaya ya ufanisi wetu katika uboreshaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuondolewa misamaha ya kodi kwa Mashirika ya Dini linahitaji kufikiriwa upya. Suala hili limefafanuliwa upya kuhusu huduma za afya na elimu. Natoa shukrani kwa Serikali kwa hilo. Juu ya kodi ya vifaa vya miradi ya utafutaji, uchimbaji na usambazaji wa hudua za maji hususan vijijini, inayotolewa na mashirika hayo, bado hakuna ufanuzi uliofanywa. Napenda kuishauri Serikali, itoe ufanuzi juu ya suala hili na kwa hakika iendelee kutoa misamaha kwa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, Jimboni Mbozi Magharibi, miradi mbalimbali ya maji vijijini, inaendeshwa na Mashirika ya Dini. Hivi ninavyosema, Shirika la CARITAS kuanzia mwezi huu limekubali kuendesha mradi wa kusambaza maji kwa vijiji 22 na vitongoji kadhaa kwenye kata nne zilizoko Tarafa ya Kamsamba na Msangano, baada ya Serikali kushindwa kutekeleza mradi huo ujulikanao *Mbozi West Water Supply Project*, uliosanifiwa mwaka 1980. Naamini kwa dhati, kama Serikali itaondoa kodi ya vifaa vya ujenzi wa mradi huu, wananchi wa vijiji hivyo 22 watapata maji safi katika miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo machache, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuendelea kusamehe *fuel levy* kwa makampuni ya madini ni kuikosesha nchi mapato dhahiri ya makampuni yanayofanya kazi kwa faida. Kuwasamehe ni kutotimiza wajibu. Nashauri misamaha hiyo ifutwe. Bunge lina haki ya kuikataa na kubadilisha sheria.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kusamehe ushuru kwa mafuta ya mawese ni msukumo wa wafanyabiashara tena watatu tu. Kila mwaka lazima wafanye hivyo, ni wakorofi wasisikilizwe. Ushuru urudishwe ili wakulima wa alizeti, karanga, pamba na ufuta, waweze kupata bei nzuri na kuongeza uzalishaji. Tuwalinde wakulima wetu na viwanda vyao.

Mheshimiwa Spika, mitumba iendelee kutozwa kodi.

Mheshimiwa Spika, tusigombane na Mashirika ya Dini, msamaha uendelee, lakini wadanganyifu wadhibitiwe na utitiri wa dini usiendelee kuruhusiwa. Magari ya Wachungaji ni muhimu yaendeleee kusamehewa ushuru, pamoja na bidhaa muhimu za kutoa huduma.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spiak, kimsingi au niseme awali, ninawapongeza kwa kazi ngumu mnayofanya, kwani kwa sekta kubwa kama hii ni dhahiri kunakuwa na upungufu mwingi.

Mheshimiwa Spika, kasi ya utekelezaji wa masuala mengi inakuwa ndogo sana, kiasi kwamba, wananchi tunajiuliza endapo pana upungufu wa wataalamu au uwezo mdogo wa wataalamu waliopo. *However*, kwa yale mafanikio, nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kuwa katika *Budget Speech* sikuona issue on pg. 16 ya *Speech* ya Rais, kuhusu uwezekano wa kuahirisha ulipaji wa mrabaha kwa wachimbaji wa vito. Kwa sisi wenye vito hivyo, tunashauri suala hili hata lisifikiriwe kabisa, kwani *revenue* yetu itayumba, nawashauri wenye mawazo ya aina hiyo wapuuzwe kabisa.

Mheshimiwa Spika, *slogan* ya Kilimo Kwanza kwa mwaka huu ingekuwa mikakati kuelekea Kilimo Kwanza ili tuelimishe wananchi, tuimalishe watenda kazi kwa maana ya wataalamu (Maafisa Ugani) na hali kadhalika kutengeneza au kuandaa bajeti inayoendana. *For now, it is too early*.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize, mapato ya ndani yataongezeka pale tu tutakapoweza kukusanya kodi kwa Watanzania wote wanaostahili kulipa kuliko ilivyo sasa hivi, watu takriban laki tano tu badala ya watu milioni kumi na saba kama ilivyo katika taarifa mbalimbali. Kisa ni kukosekana vitambulisho ili ku-*identify who are the Tanzanians and how to trace them*; sababu na soko huria litakalosababisha *free movement of persons*, bila vitambulisho tutafanyaje? Ahsante.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchukua fursa hii, kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza katika Bajeti hii, utakuwa katika azma ya kuboresha kilimo katika nchi yetu, ambapo tumekibatiza jina la Kilimo Kwanza. Naliunga mkono hili, kwa sababu asilimia themanini tutakuwa tumeishirikisha jamii hiyo kubwa kuchangia pato la nchi yetu. Pamoja na hilo, bado nina mashaka katika utekelezaji wa azma hiyo, kwa sababu tumeanza vibaya katika utekelezaji wake. Katika Bunge hili tulipitisha *mini-budget* ya fedha zilizorejeshwa na mkasa mzima wa fedha za *EPA* na tulikubaliana kiasi cha shilingi bilioni tatu ziende katika Benki ya *TIB*, dirisha la kilimo. Hadi sasa tuna habari kwamba, fedha hizo hazijakwenda na inasemekana zimejenga barabara. Labda Bunge lingeelezwa ukweli uko wapi ili imani yetu iwe pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania ni wapangaji wazuri sana wa mipango, lakini wazito sana katika utekelezaji wa mipango yetu wenyewe. Mfano, Mhesheshimiwa Rais, aliagiza Mkoa wa Morogoro uwe ghala la chakula Kitaifa, lakini hii leo ni maneno tu ya danadana za mizunguko ya lugha. Hivi sasa tuna changamoto kubwa katika Kilimo Kwanza, kwa sababu hivi karibuni baada ya uchaguzi wa Rais wa Malawi pia na wao wameanzisha Operesheni ya Kilimo Kwanza. Sasa hii iwe kigezo kwetu, kwani

tumeamua kwa pamoja mwaka huu wa 2009, lakini naamini *impact* ya Malawi itakuwa nzuri tofauti na sisi ambao ni wasemaji tu.

Mheshimiwa Spika, Balozi Sato alituasa alipomaliza muda wake nchini kwamba, tusipozingatia kilimo, uchumi wetu utakuwa duni na tegemezi hadi mwisho wa dunia hii nzuri. Lazima tujivunie rasilimali zetu, ambazo ni nzuri na pia tutumie ushauri tunaopewa na wenzetu walioendelea katika Mkutano wa Sullivan, Arusha. Wamarekani walishangaa na kusema, Tanzania haihitaji msaada pindi tu wakitumia njia za kisayansi ikiwemo kutangaza nchi.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwanzoni mwa mwaka 2006, Mheshimiwa Rais, alimteua Balozi Dokta Sharrif kuwa mtaalamu wa kuitanganza nchi, lakini hatuelewi, kwanza, alikubali uteuzi au *impact* ya kazi yake hiyo anawajibika wapi? Hivi karibuni Makamu wa Rais wa Kenya alikuja Tanzania na kuishukuru Tanzania kuwa Kenya inafaidika na kukuza uchumi wake kwa kutumia Mlima Kilimanjaro. Baada ya hapo, Makamu huyo katutukana Watanzania ambapo sio kweli, pengine alisema hivyo kutuamsha ili tujue utalii tuutumie vipi. Mimi bado nashauri, Katibu Mkuu Kiongozi, asaidie Wizara za Serikali kupitia Makatibu wa Wizara, wawajibike na mipango ya Serikali hasa inayopitishwa na Bunge badala ya ye ye kuwa kama mwanasiasa pale Ikulu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri uwepo utaratibu wa vikao baina ya Bunge na Makatibu Wakuu kila miezi mitatu. Ahsante.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waziri Mheshimiwa Mustapha Haidi Mkulo na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Sumari, Katibu Mkuu na Makamishna wote na Maafisa wa Wizara, kwa kuandaa vyema Bajeti ya Serikali yenye mwelekeo mzuri wa kwenda mbele kiuchumi na kunusuru pia uchumi wetu usitetereke katika msukosuko huu wa uchumi wa nchi za Dunia ya Kwanza.

Tunafahamu nia njema ya Serikali ya kufanya kila linalowezekana, kusaidia na kuunga mkono juhudzi za wananchi katika kupiga vita suala zima la kukabiliana na umaskini kutokana na kuongezeka kwa watu na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma ya Afya Vijijini. Serikali kupitia mpango wake wa utekelezaji MKUKUTA umeshirikisha, wananchi wamejenga Zahanati. Lakini kuna matatizo makubwa ya dawa kufika kwa wakati au zinapofika hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, lawama zilizopo kutoka kwa msambazaji dawa (*MSD*) ni kutopata fedha za gharama za dawa hizo kwa kucheleva kutoka Hazina, yaani hazifiki kwao kwa wakati. Kutotosha kwa kiwango cha Dawa zinazotolewa katika Zahanati zetu, kunaonekana sababu zake viwango vinavyopitiwa vyta kuongeza fedha za dawa kwa zahanati ni kidogo sana. Kwa mfano, kwa kipindi cha bajeti tatu; 2006/2007 (310,000/=), mwaka 2007/2008 (350,000/=) na mwaka 2008/2009 (390,000=). Viwango hivi ni kwa mwezi. Ukitazama kwa ujumla, viwango hivi kwa kipindi cha miaka mitatu ni shilingi 80,000 tu ndizo zilizoongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa ongezeko la watu kwa maana ya watoto wanaozaliwa, magonjwa yaliyopo na milipuko inayojitokeza na *inflation* iliyopo ambapo imesababisha hata dawa kupanda bei, kiwango hiki ni kidogo sana. Kwa kumsaidia mwananchi wa kijijini, anayetegemea huduma ya afya katika vituo vya Serikali tu na hakuna maduka ya dawa binafsi ambayo yangeweza labda kuwasaidia kuokoa maisha ya watoto wao.

Mheshimiwa Spika, nashauri tupitie viwango vya gharama za dawa kwa zahanati, kulingana na ongezeko halisi la watu na mahitaji ya dawa ikiwezekana mpate takwimu hizo kutoka katika zahanati husika kwa sababu zinatofautiana. Nashauri msimamie vizuri utaratibu huu wa kupeleka fedha *MSD* kwa wakati ili kuweza kuokoa ukosefu wa muda mrefu wa dawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kuwapongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake, pamoja na Watendaji wake katika Wizara, kwa hotuba nzuri na yenye kaulimbiu Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukipa kipaumbele kilimo, je, tumeandaa mipango gani ili kuki boresha? Je, nyenzo, huduma, pembejeo tumeziangalia kwa upana gani? Na je, hizo pembejep zinawafikia walengwa? Kwa sababu tatizo kubwa tulilonalo Watanzania ni kutokusimamia mipango yetu na hapa ndipo tunapofeli. Kwa mfano, fedha za *EPA* iliamuliwa zipelekwe kwenye kilimo; je, walengwa ziliwafikia? Je, ruzuku ya mbolea walengwa iliwafikia?

Mheshimiwa Spika, hizo ni aina ya kasoro za usimamizi wa mipango yetu kwa vile viongozi ama watendaji hatuko tayari kuwatumikia watu, tunajali zaidi maslahi yetu. Bado elimu ni suala ambalo limepewa kipaumbele, lakini hebu tujiulize wingi wa shule ndio kuboresha elimu? Shule ni ile yenye walimu kulingana na idadi ya wanafunzi na wenyewe uwezo wa kufundisha. Pia shule inahitaji kuwa na vifaa kwa mfano, kuna shule za sekondari ambazo hadi sasa hazina maabara, kwa maana hiyo, masomo ya sayansi yatakuwa ndoto kufaulu. Ama shule nzima yenye wanafunzi 300 ina mwalimu mmoja; je, tumeboresha Sekta ya Elimu?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali izingatie mambo hayo ili tujenge taifa lililo bora. Bajeti hii haikuonesha mipango thabiti ya kuboresha elimu kwa dhati kabisa. Wananchi wamekosa mbadala ndio maana wanajiunga na *DECI*, kwa sababu mikopo ya mabenki ina riba kubwa, hizo *SACCOS* haziwasaiddii. Maisha yamekuwa magumu kiasi ambacho Watanzania wanatafuta kila njia ya kujikwamua lakini wameshindwa. Ahsante.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Wizara (Watendaji) na Waziri, kwa hotuba nzuri yenye kutupa mwelekeo wa maendeleo ya Taifa letu kwa mwaka 2009/2010. Pamoja na pongezi hizo, nitapenda kuchangia kidogo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ili Taifa lipate kuendelea na kukuza uchumi wake ni lazima litambue na kutekeleza umuhimu wa elimu katika kuongeza mbinu au ujuzi au *skills*. *Development* inayokwenda sambamba na mahitaji (*Demand*) katika kipindi cha kuendeleza uchumi. Utekelezaji huu uende sambamba na ukuzaji au kupanua elimu ya juu kwa wanafunzi katika taaluma ambazo ni muhimu zaidi katika kuchangia Uchumi wa Taifa. Taaluma hizo ni pamoja na Sayansi ya Binadamu, Kilimo, Teknolojia na Sayansi Jamii.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sayansi ni msingi wa maendeleo kwa taifa lolote linaloendelea, kwani elimu ya binadamu, itatusaida kuwa na madaktari wa kutosha kwa ajili ya afya ya wananchi ambao ndio chimbuko la maendeleo au ukuaji wa uchumi. Hatuwezi kuinua uchumi kwa kiwango tunachotarajia, endapo hatutakuwa na madaktari wa kutosha ambao wamepata mafunzo au mbinu zinazoendana na mazingira ya wakati, kwani mfumko wa magonjwa hurudisha nyuma hali ya uchumi. Hivyo, tuwe na usimamizi mzuri katika kulinda afya za wananchi, hususan kina mama na watoto. Ushauri wangu ni kuwa, mbinu mbalimbali zitolewe kulingana na wakati ili kukabiliana na maradhi kwa faida ya taifa. Ni vyema kuyabaini maeneo haya na kuyapa *new skills every time*, kulingana na hali halisi ya uchumi na mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu ya kilimo na kuzingatia usambazaji wa wataalamu ambao ni muhimu kwa kutoa mafunzo na kuonesha mfano katika kata na vijiji kwa wakulima, ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula. Zipo shule nyingi sana za kilimo hapa nchini, lakini wataalamu hawaonekani vijijini. Ushauri wangu ni kwamba, naomba kuwe na *incentive package* itakayowafanya wakubali au washawishike kukaa vijijini. Hii itakwenda sambamba na Sera ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sayansi ya Jmii ipewe umuhimu pia ili tuweze kuwa na taifa lenye siasa safi, watendaji wanaojituma na kuwajibika; utawala bora na uendeshaji wa shughuli zote za kukuza uchumi zitakuwa ni zenye tija katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kukusanya mapato, hatua mbalimbali zimeainishwa ambazo zitatekelezwa. Nasikitika sana kuwa, Sekta ya Sanaa imesahaulika na wala haipo kabisa katika ndoto za Serikali kuwa ni sekta mojawapo inayoweza kuipa Serikali mapato katika kukusanya kodi. Jambo la msingi ni Serikali kuweka utaratibu mzuri au mazingira mazuri. Kwanza, kuwaweka wasanii wote katika mazingira ya kujipatia kipato kuititia sanaa yao. Pili ni kuweka utaratibu utakaowezesha kila wanaojishughulisha na sanaa, kuweza kulipa kodi. Hivyo basi, naomba Waziri (Serikali), iwaeleze wasanii wote Tanzania, ina nia gani nao au haiwahitaji.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kigezo gani kilichotumika katika kuipangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, fedha za mwaka 2009/2010 na ni kitu gani kilichopelekea kutotenga fedha za mikopo kwa wanafunzi wanaoingia vyuoni mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, upungufu wa fedha za Bodi ya Mikopo utapelekea watoto 65,000 kushindwa kupata mikopo ya kuingia vyuoni, je, ni kweli Serikali mko makini kweli na elimu? Inasikitisha sana punguzeni mambo mengine lakini elimu ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, je, fedha za kujenga nyumba za Walimu nchi nzima ziko wapi na ni nyumba ngapi zitajengwa katika Mikoa gani na maeneo gani?

Mheshimiwa Spika, je, fedha za kununulia usafiri wa pikipiki, bajaji za kubebea wagonjwa hasa wanawake wajawazito zipo na ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, Watendaji wa *TRA* ambao wamepewa dhamana ya kukusanya kodi ya majengo (*Property Tax*), katika Mkao wa Dar es Salaam, hawawajibiki kama ilivyotarajiwa. Majengo ni mengi na yenye thamani kubwa, makusanyo yamekuwa chini kuliko ilivyokuwa awali. Je, ni sababu gani zinazokwamisha? Halmashauri imeshindwa kutimiza malengo yake; inaonekana wahusika hawana ari ya kufanya kazi katika Halmashauri hizo. Je, Mtendaji Mkuu wa *TRA* ametoa maelezo gani?

Mheshimiwa Spika, ni jambo la msingi kama *TRA* itajikita katika kubuni vyanzo vipyta vya mapato kuliko kuendelea kuongeza kodi kwenye vyanzo vya zamani. Kuna vyanzo kama *Carbon Tax*, itasaidia kuzuwia uharibifu wa mazingira kwa kutoza kodi katika mitambo inayozalisha uchafuzi wa hali ya hewa. Kwa mfano, meli, viwanda, magari, treni, mashine, *petrol station*, ndege, mitambo mbalimbali ambayo ingeweza kutoza kodi angalau shilingi 10,000 kwa magari madogo na mitambo mikubwa, viwanda, na kadhalika, shilingi 50,000 kwa mwaka. Mapato hayo yakikusanya, yatasaidia kuongeza mapato na pia kupunguza Serikali kutumia fedha nyingi za kupanda miti kila mwaka na kuhifadhi mazingira. *TRA* ipeleke vijana nje ya nchi, kuangalia wenzetu wanavyobuni vyanzo vipyta vya mapato ambayo hayataleta kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpungeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mustafa Mkulo, Naibu wake, Mheshimiwa Sumari na Mheshimiwa Omari, kwa kazi nzuri ambayo imefanyika katika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nami pia niseme machache tu kuwa, hata siku moja bajeti haitakidhi mahitaji yote kwa kuwa, uwezo wetu ni mdogo. La msingi na jambo kubwa ni kuhakikisha kuwa, hiyo mipango iliyopo inatekelezwa kwa ukamilifu na uadilifu ili mwaka kesho, mipango mingine ipate nafasi.

Mheshimiwa Spika, angalizo langu kuu ni juu ya uharakishaji wa utoaji wa pesa katika maeneo husika, ili utekelezaji uende mapema. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kufuta Kodi ya Taasisi za Kidini, maana Makanisa na Misikiti,

yangekwama kuendesha shughuli zake. Lakini hata hivyo, lazima tubane *loop holes* zilizopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA M. JECHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kubuni mikakati mbalimbali ya kuiongezea Serikali yetu vyanzo nya mapato, Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2009/2010, imeandaliwa wakati Dunia imekumbwa na msukosuko wa kiuchumi, hivyo, ni dhahiri na nchi yetu imeathirika. Hivyo basi, tunaipongeza Serikali kwa juhudhi za makusudi zilizochukuliwa za kutafuta vipaumbele na kuvipangia mikakati mahususi ya utekelezaji, ili wananchi wetu waendelee kupata maisha bora.

Mheshimiwa Spika, suala la ‘Kilimo Kwanza’ ni muhimu kwani ndio Utu wa Mgongo wa Taifa letu. Lakini tunaiomba Serikali kuwa na mpango wa kilimo wa muda mfupi, wa Kati na wa mrefu, ili Kilimo chetu kiwa endelevu na Serikali iwakopeshe wakulima ili waweze kumiliki viwanda vidogo vidogo na nya kati ili waweze kusindika mazao yao na kuyauza nje ya nchi na hivyo kuiongeza kipato, ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa kwa na Bahari Kuu, je, Serikali ina mipango gani katika kuvuna mazao ya Baharini, ambapo bahari yetu ina hazina kubwa ya zao la samaki, Lulu, Kilimo cha Mwani ambapo mazao yote haya, yana soko kubwa nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali kuwa, mipango ya kuiendeleza Taasisi hii ya Wavuvi kwani, mapato yake ni makubwa na tukijipanga vizuri, sekta hii itaiongezea Serikali yetu mapato. Mfano mzuri wa mazao hayo, meli iliyokamatwa ikivua Samaki wetu kwa wizi. Katika mtikisiko huu wa uchumi, ni vema tukadhibiti mapato yetu na mianya yote ya uvujaji wa mapato yetu lazima idhibitiwe.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba suala la bei ya mbao (*soft wood*), milingoti ya nguzo za umeme (*poles*) liangaliwe upya. Serikali inamlipisha mvunaji malipo yafuatayo; *Royalty*, *LMAD*, *VAT*, *CESS* ya Halmashauri na michango ya sekondari ya Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa *VAT* hulipishwa mara mbili, yaani wakati wa kununua miti na wakati wa kuuza mbao laini. *LMDA* haikutakiwa kutozwa ila inafanyika hivyo kwa vile Hazina inachukua *Royalty* yote bila kurejesha chochote kile kwa ajili ya

kuotesha, kupanda na kukuza miti hasa katika *commercial plantation*, matokeo yake mbao za Malawi ndio zenye bei nafuu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili liangaliwe na Hazina ifute VAT katika miti na *electrical poles*, kwenye *stage* ya kabla ya kununua mti na ibakie katika mbao na '*pole*' iliyo tayari kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kongwa, tunaomba miradi miwili ya umeme vijijini. Mradi wa kwanza ni wa Mkoka-Matongoro-Norini, Mlanje –Mageseni – Makawa (30 Kms). Mradi wa pili ni wa Kibaigwa –Manyata- Ngomai –Njoge (20 Kms).

Mheshimiwa Spika, suala la Bandari, *TRA*, *TICTS* liangaliwe kipekee, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi kwa kuwasilisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kama ifuatavyo. Naiona nia njema ya Serikali, kudhibiti mapato ya Serikali kila inapoona inafaa. Hata hivyo, naishauri Serikali iachilio mbali suala la kufuta msamaha wa kodi kwa mashirika ya dini. Mgogoro wa suala hili ni moto usioweza kuzimika haraka. Tanzania imefikia hapa kielimu, kiafya na kijamii, kutokana na mchango mkubwa sana wa mashirika ya dini. Hata sasa bado mguu mmoja wa Serikali umesimamia katika mashirika ya kidini, hasa kiafya na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano wa Jimbo langu mwenyewe, ni mwaka 2002 tu, nilipopata kibali cha kuwa na vituo viwili vyta afya vyta Serikali (ambavyo bado havina majengo). Huduma ya afya ya wananchi wangu na mimi mwenyewe, tunategemea Hospitali za Ndolage na Kagondo, zote za *mission*. Vilevile, Zahanati za Rwigembe kule Ngege, Kishuro, Kelebe ni *mission* na ziko maeneo ya mipakani na ngumu kufikika na Serikali haitoi huduma huko.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali na washirika wake wote, mfano *TRA*, kuwachukulia hatua kali wanaojificha katika misamaha ya kodi ya mashirika ya dini na kujinufaisha. Hao ni hatari, wadhibitiwe haohao mmojammoja, bahati nzuri baadhi wanajulikana kwenu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kwenye Chai na Kahawa inayozalishwa na kusindikwa hapa nchini. Kwa maoni yangu na wadau wa Chai na Kahawa, tunaona havikubaliki. Tunatoaa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunahimiza ongezeko la kilimo cha Chai ambacho kilikufa na Serikali ni shahidi. Wakati ndio kwanza mwelekeo unaanza kujitokeza,

Serikali inasema tutoze kodi ya VAT, hii itaua kukua kwa zao la Chai ambalo tunataka liongezeke.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa Kahawa hivi sasa imeshuka, baada ya soko kuwa la chini sana. Sasa badala ya kuwapa moyo wakulima ambao bado wanalima kahawa, ili walime na wengine wavutike, unataka kuwatoza VAT. Naishauri Serikali katika hili, ifikirie upya, VAT ifutwe kwa Chai na Kahawa.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii, Serikali ijue itawatoza VAT wale wachache sana waliojiandikisha kulipa VAT, wengi ambao ni wadogowadogo hawatalipa kitu. Kwa hiyo, Serikali haitapata kipato kikubwa kama inavyodhani, isipokuwa itawabana na kuwaumiza kina *Tanica Coffee, Tanzania Tea Blenders, Kilimanjaro Tea n.k*

Mheshimiwa Spika, vilevile tujue leo kauli mbiu yetu ni Kilimo Kwanza, sasa ni mgongano wa hoja. Tunataka nani alime na alime nini? Tuwahimize wananchi walime Chai, Kahawa na mazao mengine, pale palipo na unafuu wa bei. Tukiwatoza VAT, Chai ya Tanzania haitazalishwa na matokeo yake, kipato chao kitashuka. Wakati huohuo tutafunga soko la wageni kuleta Chai na Kahawa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kagera ni Mkoa unaozalisha Kahawa na Chai, nina maslahi katika hili. Naomba wananchi wa Kagera, wafikiriwe kuongezewa nguvu ya kazi ya kilimo cha Chai na Kahawa na si vingenevyo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ilitazame suala hili pamoja na mafuta ya kula yanayozalishwa Tanzania. Mafuta ya Alizeti, Karanga, Mawese, Pamba na Korosho, hayana *cholesterol*. Hayo mnayotaka kuyapa soko yana *cholesterol*, ni hatari kwa afya zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba, VAT iondolewe kwenye Chai, Kahawa, Alizeti, Karanga, Mawese, Pamba, na Korosho, nchini mwetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Mawaziri wote wawili pamoja na watalaam na watendaji wote ambao kwa namna moja au nyingine, wamewezesha kutayarisha hotuba hizi mbili, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwenye sekta ya Kilimo. Kama tunavyoelewa kwamba, Serikali ilitoa kauli mbiu ya ‘Kilimo ni Utu wa Mgongo’ na sasa hivi imetolewa kauli mbiu ‘Kilimo Kwanza’, kauli mbiu hizi zote zimetolewa ili kuweza kuwahamasisha wananchi, wakulima waweze kujikita zaidi katika kilimo. Kauli mbiu hizi hazitaweza kuwatia moyo wakulima kwa kuwapatia pembejeo pekee kama vile mbolea, matrekta, watalaam na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi ninapata wasiwasi kama kweli Serikali imeshaamua kuboresha kilimo na kwenda sambamba na kauli mbiu ya KILIMO KWANZA, kwa sababu tunamtaka mkulima azalishe mazao kwa wingi kwa kumpa pembejeo, lakini Serikali yenyewe bado hadi sasa hajawezza kuwahakikishia wakulima hao masoko ya uhakika ya kuuza mazao yao, Serikali bado hadi sasa hajajiandaa kujenga viwanda kwa ajili ya kusindika mazao yao na pia kuwepo miundombinu ya uhakika na iliyobora zaidi kama vile maji, umeme na barabara ili kuwawezesha wakulima kusafirisha mazao yao kwa urahisi, uhakika na kwa haraka ili yasiwaharibikie njiani au mashambani .

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haitaweza kujikita kweli kweli katika kuwajengea wananchi ama wakulima wetu mambo hayo ili wakulima wetu wapate moyo wa kuzalisha na kuwa na uhakika wa mauzo na usafirishaji wa mazao yao, basi sidhani kama wakulima wataweza kuhamisika na badala yake kaulimbiu hiyo ya KILIMO KWANZA itakuwa “KILIMO MWISHO” .

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie sana masuala hayo ya masoko na miundombinu ya uhakika ili wakulima wetu nao waweze kuhamasika na kuweza kuzalisha kwa wingi na wao kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato, naona Serikali haijakusudia vema kuweka mkakati wa kukusanya mapato hasa kupitia katika bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania imejaliwa na kila hali ya utajiri na kama Serikali itakusudia kweli kuimarisha bandari zake za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar, basi ni dhahiri nchi yetu itaweza kukusanya mapato ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kama bandari ya Dar es Salaam itaweza kupanuliwa ili kuruhusu meli nyingi na kubwa kuingia bandarini na kutoka kwa wakati na uwepo ufanisi mzuri wa utendaji yaani kupakia na kupakua mizigo kwa haraka ili wafanyabiashara nao wapate bidhaa zao kwa wakati, jambo ambalo litawatia moyo na kupenda kuitumia bandari yetu ya Dar es Salaam na kwa hali hiyo tutaweza kukusanya mapato kwa wingi kama wafayavyo nchi za wenzetu amba wanategemea sana mapato yao kupitia bandari kama vile Singapore na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kupanua bandari ya Dar es Salaam, ni vyema pia Serikali ingeanzisha mpango wa kuweka bandari kavu (*dry port*) kwa Mikoa ambayo ina uwezo wa kuendesha bandari hizo kama vile Mkoa wa Kigoma na mingineyo imepakana na nchi jirani ambazo zimeonyesha kuwa na harakati kubwa za kibiashara na nchi yetu ya Tanzania. Naamini kama Serikali itafanya kazi kwa umakini maeneo kama hayo ni wazi nchi yetu itaweza kupiga hatua kubwa kiuchumi na kuacha kutegemea bajeti yetu sehemu fulani kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakupongeza wewe Katibu na wataalam wote wa Wizara, kwa bajeti ambayo inajibu hali ya sasa ya jamii. Ninaunga Mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu uwekaji lami barabara ya Iringa – Dodoma. Mheshimiwa Waziri, ulinidokeza kwamba, kuna fungu la fedha lililotengwa kwa ajili hiyo mwaka 2009/2010. Kama ndivyo, naomba sana, utakapohitimisha hoja hiyo, tafadhali utamke hivyo. Hii itaijenga sana Wizara na papo hapo, utajibu kiu ya muda mrefu ya Mikoa yote ya Kusini, ya kufungua milango ya uchumi, kati ya Mikoa hiyo na Mikoa ya Kati na Kaskazini.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kupongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kazi nzuri na hasa kwa bajeti ya mwaka 2009/2010 ambayo ni ya aina yake. Kusema kweli haijawahi kutokea, Serikali kuchukua madeni ya wafanyabiashara au tuseme ushirika ili kusaidia benki kuweza kuwakopesha tena wafanyabiashara ili nao waweze kununua mazao kama pamba, tumbaku, kahawa, korosha, chai na kadhalika. Kwa kweli ni ubunifu wa hali ya juu sana.

Hongera sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne ikiongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ikifanya kazi bega kwa bega na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwa kifupi, nawapongeza wote, moja tu ambalo naona linaleta dosari nzuri ya bajeti hii, nalo ni lile la kutoza kodi Mashirika ya Dini na NGO's.

Mheshimiwa Spika, nimepokea simu nyingi sana kutoka kwa Mapadri, Maaskofu na Masheikh bila kutowasahau Wachungaji wote, wanositika na suala la kuambiwa walipie kodi vifaa ambavyo mara nyingi wanaomba msaada toka nchi za nje. Kwa mfano, wanaomba msaada kama Kanisa au BAKWATA, ili kujenga shule au hospitali, wakipewa fedha hizo ambazo ni kodi za wafadhili toka nchi za Ulaya au Uarabuni, zikifika hapa tena vifaa vya kujengea au vya kupasulia au vitanda vya kujifungulia (*Labour Beds*), mradi si vya ibada vilipiwe kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunawavunja nguvu wafadhili wetu, Ndugu zetu katika maendeleo, kwani kuna sehemu hakuna Hospitali za Serikali, unakuta Hospitali za Misheni ndio zinatusitiri. Mfano, Ndala Misheni, wagonjwa wanashindwa kwenye zahanati za Serikali kutoka Wilaya ya Nzega nadhani hata Tabora, wanapelekwa Ndala. Pili, Hospitali ya Misheni ya Pentekoste ya Nkinga, Igunga wagongwa wa Wilaya ya Nzega wanapelekwa Nkinga kama hospitali ya “*Referral*” na ziko nyingi mfano ya St. Gaspar – Itigi, ni hospitali ya Kitaifa lakini ni ya Misheni.

Mheshimiwa Spika, naomba chonde chonde kodi hii iondolewe. Najua kuna wachungaji Pwagu, lakini hawa si wengi, naomba wengine wasiadhibiwe sababu ya

wachache. Wale wanaofanya madudu, Serikali iwachukulie hatua/sheria, waadhibiwe ipasavyo na wengine wasaidiwe kwa kuondoa kodi hii kama zamani kwa lugha nyingine, msitoze kodi Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho lakini si kwa umuhimu. Ile ahadi ya Mheshimiwa Rais, ya umeme wa kutoka Nzega kwenda Bukene, tuhitimishe. Sasa kuna nguzo zimelundikwa pale Ijanija, inaleta matumaini, lakini Wapinzani wanasema ni geresha tu, naomba iwe *real*. Nguzo zipo tayari zimekwishalipwa, basi kazi ifanyike tupate umeme ili tupate maendeleo, ajira, ushirika wetu wa Igembensabo ukoboe mchele pale pale Bukene, Bukene ichanganye kibiashara na hivyo tujkwamue kiuchumi. Mwalimu aliseme “*It can be done, play your party*” na Rais Barrack Obama anasema, “Yes we can”.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa matumaini, umeme Bukene unawezekana.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, bajeti ni nzuri, ni bajeti ya kutia moyo, lakini wasiwasi upo katika utekelezaji. Maendeleo yetu Watanzania ni kusuasua kwa sababu ya utekelezaji duni, tunapanga vizuri lakini utekelezaji wetu mdogo. Nashauri tuwe watendaji na tufuatilie mno utendaji wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Serikali inajitahidi kusomesha watoto wetu na vijana hawa wanapata elimu lakini inakuwa ni elimu ya kujua kusoma na kuandika tu na sio elimu ya kumletea maendeleo Mtanzania. Nashauri elimu iwe ya kumfanya kijana wa Kitanzania awe mwenye uwezo wa kubuni mambo ya kujitegemea, hata kama ni elimu ya darasa la saba.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote haiwezi kuwa ya kimaendeleo bila ya kuwa na viwanda endelevu. Viwanda vyetu hapa nchini, ni vya kuvunja moyo sana kwani viwanda vingi utendaji wake ni mdogo na vingine vimefungwa kabisa mfano *General Tyre* na kadhalika. Nashauri viwanda vipewe kipaumbele cha kufufuliwa ili vilete manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na bandari nzuri sana lakini uimarishaji na kuzithamini bandari zetu haupo, kwani hali hiyo ingekuwepo, basi wala nchi yetu isingekuwa yenyе bajeti tegemezi. Nashauri Serikali izitengeneze kwa kuzitanua bandari zetu za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na kadhalika. Wakusanyaji wa mapato *TRA* wanajitahidi kukusanya mapato vizuri lakini Serikali imeridhika na ukusanyaji huo?

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wa madini hapa nchini wasiwe wenye kuchukua madini kwa kujinufaisha wao na nchi zao zaidi, lakini madini hayo yaye kwa manufaa ya Watanzania zaidi. Nashauri mali zote zilizopo nchini petu ziwe kwa manufaa ya Watanzania na sio kwa manufaa ya nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ili iwe ya watu wenye maisha bora basi iwasogezee Mabenki Mikoani hadi Mawilayani. Mwaka jana niliuliza swali langu kuhusu Serikali ya Muungano kutujengea Benki za *NMB* na *CRDB* kule Zanzibar na pia Jimboni kwangu Nungwi, lakini Serikali hajaonesha lolote kuhusu hilo. Nashauri pia naiomba Serikali ituletee huduma hiyo na kule kwetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuipongeza bajeti hii na bila kuchelewa naunga mkono hoja.

Kwanza nampongeza sana Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii. Pia naipongeza Kamati husika hususan Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Shinyanga na wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudhi kubwa waliyofanya kwa kutupatia maji ya kutosha. Tunasema tutayatunza kwa nguvu zetu zote.

Pili, kuhusu kutoa msamaha wa kodi kwa Taasisi ya Kidini ni vizuri lakini nina hoja ifuatayo. Taasisi hizi zinatusaidia sana ila tu wanaoleta vurugu ni wale wanaofukuzwa katika taasisi hizo na hivyo naye anaanzisha Kanisa/Msikiti wake. Ombi, Wilaya ziainishe Makanisa/Misikiti gani ambayo inafaa kupewa misamaha hiyo, hii itaondosha vurugu hii ambayo Serikali imeona.

Tatu, kuhusu *TRL*, napendekeza Wahindi (*RITES*) waondoke kwani wananchi wanahangaika sana, ni afadhali tulivyokuwa tunaendesha wenyewe. Hivyo, Wizara husika ni vyema ikafikiria kutafuta fedha kwa kutumia vyanzo vyta ndani kama tulivyofanya Mradi wa Maji Shinyanga, jambo hili linawezekana. Pia naishauri Serikali kuwa Shirika la *TRL*, ni vizuri tulihudumie wenyewe Watanzania kwani tuna uchungu na wananchi wetu.

Nne, naishukuru Serikali hasa Wizara ya Miundombinu kwa kuukumbuka Mkoa wa Kigoma kwa kujenga barabara. Kwa Mkoa wa Shinyanga, tunafurahi sana kwani tumepata kiunganishi cha kuitishia chakula kwani Mkoa wa Shinyanga hauna mvua ya kutosha na wenzetu Mkoa wao ni wa neema kipindi chote cha mwaka, hivyo nashukuru sana.

Tano, napenda kuzungumzia kuhusu kilimo kwanza. Ombi langu ni kwamba Maafisa Ugani wawe na nyenzo na pia wawe na mashamba ya mifano ili wananchi wajifunze kutoka kwao kwa maneno na vitendo kwa kuona mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kurudisha JKT. Suala hili ni zuri kwani vijana kwa mujibu wa sheria ni vizuri wakapata mafunzo ya kilimo na wawe wakakamavu, kwa sasa vijana wetu ni nyoronyoro sana. Nami naamini vijana wakitoka JKT mambo ya migomo itapungua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata fursa ya kuchangia hoja hii, nitapenda wakati wa majumuisho ya Waziri kupata maelezo ya ziada katika maeneo yafuatayo. Niliomba kupata maelezo baada ya Mheshimiwa Rais kubaini na kueleza upungufu wa *TRL* ikiwa ni pamoja na menejimenti ni hatua gani ameagiza ichukuliwe?

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kupata maelezo juu ya DECI, nini hatma yake hususan fedha za wananchi? Kadhalika *Bayport* ambayo imewakopesha Walimu wengi nchini na haifuati mikataba baina yao na wanawakata fedha nyingi zaidi na hakuna utaratibu mzuri wa marejesho na makato ya muda mrefu. Pia urasimu wa kulipa mafao ya wastaafu na mirathi, usumbufu huu utaisha lini na je, malimbikizo na madai ya Walimu kucheleweshewa na hasa mishahara kwa waajiriwa wapya, yatashughulikiwa lini? Fedha ambayo Serikali imekuwa ikiongeza kwa mishahara ya wafanyakazi wa Reli je, ilikuwa imeidhinishwa na Bunge? HAZINA wametoa wapi mamlaka ya kutumia fedha za wananchi wanavyotaka?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa utayarishaji wa bajeti hii tunayoichangia.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii naiunga mkono asilimia mia moja na kwa kuwa niko Kamati ya Fedha na Uchumi, ninaielewa vizuri sana. Bajeti hii kwa ujumla wake, ni tofauti na ya miaka iliyopita kwa kuwa ina *deficit*. Kwangu mimi, naona ndiyo bajeti iliyopangiliwa kwa umakini mkubwa. Sio kwamba Mheshimiwa Waziri hajaona hiyo *Deficit – Gap*, bali amepanga na kupangua hadi kufikia alipoitao ikiwa na nakisi. Hii inadhihirisha Serikali itakuwa makini sana kuzuia *over-expenditure* na ubadhirifu wa aina yoyote huku ikitafuta namna ya kufidia *deficit*. Kwa hiyo, mimi naona ni bajeti nzuri!!

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu ya “Kilimo Kwanza”, tulipokuwa tunasema “Kilimo ni Utu wa Mgongo” sikuwa naelewa kwa sababu sikuwa naona ni kwa namna gani tutaweza kupima mafanikio au matarajio ya Serikali lakini “Kilimo Kwanza” inapimika. Naishauri Serikali kwamba tunapoweka kauli mbiu twende *deeper* zaidi kuweka *Bench-mark*. Tuweke wazi namna ya kupima hii kipaumbele. Kwa mfano:-

- Ifikapo mwaka 2010 tuwe na kaya 2,000,000 zinazojitosheleza kwa chakula;
- Tuwe na viwanda 100 vya kusindika kahawa;
- Tuwe na viwanda 100 vya kukamua alizeti;
- Tuwe na lita kadhaa za alizeti, pamba, ufuta za kuuza nje;

- Tuwe na ekari kadhaa za umwagiliaji na kadhalika;
- Tuwe na mipango yetu kwa sura ya kupimika ili tuweze kuhoji Serikali, tuweze kujiipima ili kujisahihisha tusiishie tu na kauli mbiu.

Mheshimiwa Spika, nchi ikikosa chakula, itaweza kuagiza kutoka nchi jirani au Ulaya au hata Marekani na kadhalika lakini wananchi wanapokosa maji si rahisi kuomba msaada wa maji kutoka nje. Mimi nadhani kauli mbiu ingekuwa “Maji Kwanza” kwa kuwa hata kilimo chenyewe kinategemea upatikanaji wa maji. Mimi ningesema tuboreshe kilimo, lakini maji kwanza kwa kuwa “Maji ni Uhai”. Tuboreshe kilimo kwa maana ya “Kilimo cha Umwagiliaji”.

Mheshimiwa Spika, *value for money*, kutotimiza malengo ya kutekeleza mipango ya Serikali inaweza kuchangiwa na haya yafuatayo:-

- (i) Watumishi/watendaji walio chini ya viwango
- (ii) Kutokuwa na watumishi wa kutosha, hasa Idara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kujenga uwezo wa watendaji ili wafanye kazi kwa viwango vinavyotarajiwa (*capacity building*), uwezo wa kumudu majukumu ili fedha zinazotolewa zitoe matarajio ya Serikali. Naishauri Serikali pia kuondoa tatizo sugu la kukosa watumishi kwenye Idara ya Serikali kwa kufanya ifuatavyo:-

- Bunge kutunga sheria ili mishahara yote ya watumishi bila kujali ni ya Serikali, NGO's au Taasisi zozote za maendeleo kuwa na *scale* sawa. Hii itapunguza tatizo sugu la watumishi wa Serikali kuhamia kwenye NGO's kwenda kutafuta *greener pastures*.

- Idara za Serikali (Afya, Elimu, Miundombinu na kadhalika) zitakapokuwa na watumishi wa kutosha na wenge viwango, fedha za Serikali zitatumika ipasavyo (*Value for Money*)

- Tuweke vigezo vya kupima mafanikio na kuhoji pale ambapo hatukufanikiwa la sivyo tutaendelea kulalamikia utekelezaji wa bajeti kwa Idara zote (Miundombinu, Maji, Umeme, Kilimo na kadhalika) mwaka hadi mwaka bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa kuangalia uwezekano wa kuahirisha kodi kwa NGO's na Madhehebu ya Dini.

Hata hivyo, makundi haya yatozwe kodi kwa shughuli zote zinazoendeshwa kibiashara kwa mfano mahoteli, mabwalo, shule zenyé karo za kibiashara na uwekezaji mwingine wowote wa kibiashara zaidi kuliko kiroho.

**MHE. MCHUNGAJI DR. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii asilima mia kwa mia.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Watendaji wake wote kwa bajeti nzuri sana ya mwaka 2009/2010. Imegusa kila kona, tunachangia na kukazia tu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, *ATCL* imekwisha kabisa na inalitia aibu Taifa letu. *ATCL* ina wafanyakazi 300, lazima wapunguzwe. Kwa nini *Precision Air* itushinde? Kwa nini Kenya itushinde? *ATCL* isaidiwe? Tuondoe aibu ya Tanzania. Nunua ndege iwe *priority*

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu Shirika la Reli. Inashangaza mmewaachia Wahindi. Pesa na reli ni za Tanzania. *management* ya Wahindi tu, tubadilishe utaratibu ili *management* iwe *fifty fifty*.

Mheshimiwa Spika, tatu, nashauri misamaha ya kodi kwa Mashirika Dini, iendelee. Tunapongea kwa ufanuzi mzuri. Wote tumeshuhudia kazi kubwa ya Mashirika ya Dini, Mashule na Mahospitali, wengi tumesoma shule hizo. Serikali lazima junge mkono hujudi hizo.

Mheshimiwa Spika, nne, DECI imekufa. Tunaomba Serikali iunde chombo mbadala kwa kusaidia maskini. Bank siyo rafiki wa maskini, *SACCO's* inahitaji mtu aweke hisa, maskini hawana. Tubuni kitu mbadala cha kuwasaidia wananchi wetu.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Suala la msamaha wa Mashirika ya Dini na NGOs. Naomba nitoe rai kwa Serikali ili kurejea upya uamuzi wake wa kuondoa msahama maalum wa VAT kwenye Asasi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, asasi hizi zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa huduma za jamii hususan elimu, afya na maji. Kwa kuwa, maeneo haya yanawagusa wananchi walio wengi moja kwa moja, kufutwa kwa msamaha huu, kunaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa uchangiaji na utoaji wa huduma hasa vijijini. Ni vema Serikali ikakaa na Mashirika haya ya Dini na kutoa mwongozi na ufanuzi mzuri wa namna ya kuziba mianya ya ukwepaji kodi ili msamaha huu uendelee kutolewa na si kwa vifaa vya koroho tu iguse pia maeneo yanayosaidia Serikali hasa katika eneo la afya, elimu na huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali iimarishe VICOBA. Naipongea Serikali kwa mkakati wake mzuri wa uvezeshaji wa wananchi kiuchumi. Aidha, Serikali ianzishe utaratibu wa kuimarisha VICOBA kwani umeonyesha matokeo mazuri kwa wale ambao wamepata huduma hiyo.

Serikali pia ihakikishe kuwa inaweka utaratibu wa kuwafikia walengwa hasa wale wenye hadhi ya kuwezesha na wananchi wenye kipato cha chini, mkakati huu ndiyo njia pakee ya kuwawezesha wananchi kupata ajira na mapato.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. MWAKA A. RAMADHANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuianda hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, nainze kuichangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Kuhusu *TRA*, kama inavyojulikana kuwa uchumi umeshuka dunia nzima, kwa maana hiyo hata magari yanayonunuliwa nje yameshuka bei kidogo, cha kushangaza ushuru kwetu umezidi kupanda kiasi cha kwamba mtu ameleta gari yake lakini ushuru mkubwa sana mpaka anashindwa kuitoa na *storage charges* pia ni kubwa. Naomba *TRA* Ifanye imani kwa wananchi wake kwa kupunguza ushuru.

Pia kinachosikitisha zaidi, ni kuona kwamba unapoleta gari Dar es Saalam kutoka Zanzibar, unatakiwa lazima ulipe *difference* wakati nchi ni moja na *TRA* ni moja! Kwa nini bei ya ushuru Tanzania nzima isiwe moja ili wananchi waondokane na manyanyaso hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *ATCL*, imekuwa ni mzigzo kwa Serikali, ndege ziko mbili (2) lakini wafanyakazi 364, wote hao wa nini? Naiomba Serikali kufanya juhudzi za makusudi ili kulinusuru shirika hili. Kwa mfano, watoe pesa za kulipa mafao ya baadhi ya wafanyakazi ili waweze kupunguzwa kwani watu 364 ni wengi sana katika kuendesha shirika hili ambalo bado ni changa. Pia ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar hakuna kwa nini wakati abiria wapo wengi? Naomba Serikali ifuatilie masuala haya na kuweza kuyapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *TICTS*, ni kuwa kampuni hii haifai kuwapo peke yake kwani haina uwezo wa kuendesha shughuli hii. Kwanza, haina vifaa vyta kutosha inavyotumia ni vyta *TPA*. Pili, huduma zake haziridhishi kwani waliahidi watatengeza gati kiliongezea kina kirefu cha maji, mpaka leo hawaajaonesha nia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini kampuni hiyo inang'ang'aniwa haitolewi maamuzi, tunaiomba Serikali ichukue hatua inayofaa kwa manufaa ya nchi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ya tarehe 10 Juni, 2009 aliyoitoa Ukumbi wa Kilimani hapa Dodoma. Ni hotuba iliyotupa hali halisi ya nchi yetu kiuchumi baada ya mtikisiko wa kiuchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake ya bajeti ambayo kwa hali yetu ya kiuchumi Tanzania, hotuba hiyo ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo manne yafuatayo:-

Kwanza, mikakati ya kupunguza matumizi. Nashauri Serikali pia iangalie namna itakavyoweza kupunguza matumizi kwa kuacha mazoea yaliyopo ya kutumika Washauri Waelekezi kwa baadhi ya miradi. Baadhi ya miradi haina haja ya kutumika Washauri Waelekezi kwa sababu Wataalamu waliopo Serikalini wnatosha kufanya kazi watakazofanya Washauri hao. Kwa mfano, kuna haja gani ya kutumika Mshauri Mwelekezi kwa kugawana Haki za Muungano kati ya sehemu mbili za Muungano? Kumekuwa na mazoea hapa petu Tanzania kila Wizara hata kila Idara lazima itumie mfumo wa Washauri Waelekezi.

Mheshimiwa Spika, pili, fidia kwa makampuni na vyama vya ushirika. Utaratibu huu si mbaya lakini unahitaji tahadhari kubwa sana ili wajanja wasiitumie nafasi hii vibaya. Mara nyingi fidia za namna hiyo hukosa usahihi na baada ya kuleta faida huleta hasara na kuwatahirisha watu bila ya kutoka jesho. Uhakika wa kina unahitajika ufanyike ili kuyajua makampuni na mashirika yaliyopata hasara wakati wa kununua mazao.

Mheshimiwa Spika, tatu, pensheni kwa wastaifu. Pamoja na jitihada za Serikali za kuondosha usumbufu wa pensheni za wastaifu lakini bado usumbufu upo. Wastaifu wetu wengi hulazimika kutafuta msaada kwa nguvu za Viongozi ili wapate haki zao hizo kwa wakati. Kwa wale ambao hukosa nguvu za Viongozi na hasa Wabunge, huchelewa sana kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake nzuri iliyozingatia kwa kiasi kikubwa maslahi ya Watanzania wengi ikiaweka pembeni wafugaji Watanzania ambao kwa sehemu kubwa wanategemea ufugaji peke yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika bajeti hii na zile zingine zilizotangulia, imesahau suala zima la ufugaji na miundombinu yake. Inasikitisha kuwa sijafanikiwa kuona fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuchimba mabwawa (malambo), majosho, chanjo ya mifugo dhidi ya *Ndigara East Coast Fever (ECF)* na chanjo zingine. Aidha, hakuna fedha kwa ajili ya kuboresha mifugo kwa maana ya kuwapatia wafugaji madume bora ya mbegu kutoka Ranchi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wetu wengi wanaishi na kufuga mifugo katika nyanda kame. Maeneo haya ya nyanda kame kwa kawaida hayina maji na upatikanaji wake ni wa gharma kubwa. Hivyo ni jukumu la Serikali yetu kuchukua hatua za makusudi kutenga fedha kwa ajiil ya mifugo na kuwafanya wafugaji waache kuhamahama kufuata maji na malisho na kujenga uwezekano wa kuzuka migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wilaya ya Simanjiro, Serikali inaombwa kutimiza ahadi yake ya kupeleka maji makao makuu ya Wilaya ya Orkesemet na kuwapatia maji safi na salama wananchi wa kata ya Mererani. Aidha, ombi langu la dharura ni kuomba fedha kwa ajili ya kuwaokoa wananchi wa kata ya Orkesement Ruvu-Remili na Kitwai kutokana na kukosekana kwa maji na kupelekea wafugaji kuhamia Wilaya ya Kilindi Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika narudia kuomba Serikali iwatazame wafugaji kwa jicho la huruma, hii ni pamoja na kupewa upendeleo kwenye ujenzi wa nyumba za Walimu kutokana na jiografia ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iondoe au ifute msimamo wake wa kuziondolea msamaha wa kodi Taasisi za Dini ambazo kwa kiasi kikubwa hutoa huduma muhimu kwa wananchi wetu. Ni imani yangu, Serikali italitazama jambo hili na kubadilisha msimamo wake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMTI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Wasaidizi wake wote kwa jinsi walivyojitalidi kufafanua masuala nyeti ya kitaifa ili yaeleweke vizuri kwa umma, lakini jambo la ziada, ni jitihada ya kuyazingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa madhehebu ya dini na wananchi wote waliota michango yao. Huo ndiyo uzalendo wa kweli.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuongeza makusanyo ya kodi nchini, ni vizuri tukajitahidi kuongeza wigo wa walipakodi kwa kuweka viwango ambavyo havitawafanya wakwepe kodi za wastani bila bugudha. Wakwepa kodi wapewe adhabu kubwa ili waogope kukwepa kulipa kodi na kusimamia wale wote wanaokwepa kwa kutotoa risiti za mauzo yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu kubwa kwa bajeti hii ni, tumejiandaa kiasi gani kukabiliana na hali ya upungufu wa hali mbaya ya upungufu wa chakula katika mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo katika vyombo na taasisi za kimataifa zinaonyesha kuwepo na hali mbaya ya hewa na hivyo lazima Serikali zote husika zijiandae kununua na kuendeleza upatikanaji wa chakula katika nchi zao, chakula kilichopo nchini kinatosheleza kwa kipindi cha miezi miwili tu, kutokana nai mvua za vuli zinazoanza miezi ya Septemba na Oktoba, kama haitakuwa nzuri basi mimi nashauri tuijandae vizuri zaidi kwa chakula, ama siyo maafa yanaweza kuathiri nchi hii. Siasa na mafanikio ya bajeti yetu, ni lazima iendane na upatikanaji wa chakula, yote tunayoyaandaa, bila uhakika wa chakula, tutakuwa tumepteza nguvu zetu bure.

Mheshimiwa Spika, napenda kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu kwa kukubali kila wakati na kuzikubali hoja na hisia mbalimbali za wananchi wake, tunazidi kuiombea Serikali yetu na bajeti hii imemalizike vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa nguvu zangu zote.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kupidia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta bajeti ambayo inamgusa mwananchi. pamoja na pongezi hizo, napenda nitoe mchango wangu ambao nina hakika utazidi kuisaidia Wizara iboreshe baadhi ya maeneo ili kuleta tija zaidi kwa wananchi na Taifa.

Mheshimiwa Spika, vitu ambavyo vinalifanya Taifa liweze kusonga mbele zaidi ni afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara na kilimo na umeme. Naishukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua iliyofikikia katika vitu vyote hivyo lakini bado jithada iongezeke kwani maeneo mengi bado hayana maendeleo kutokana na kukosekana kwa vitu hivyo nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo kubwa sana kwani sote tunajua kwamba maji ni haki ya msingi kwa kila mtu, lakini unakuta kiasi cha fedha kinachoretengwa ni kidogo kwa Wizara husika, hivyo kuifanya ishindwe kupeleka mahitaji hayo kwenye vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo mengi hayana maji katika ardhi au mito na mabwawa, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kwa maeneo hayo na hasa kwenye shule kwa sababu kiasi kinachotengwa ni kidogo kwa Wizara husika, hivyo kuifanya ishindwe kupeleka mahitaji hayo kwenye vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, maeneo mengi hayana maji katika ardhi au mito na mabwawa, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kwa maeneo hayo na hasa kwenye shule, vituo ya afya wakawekewa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ambayo yatatumika wakati wote? Ni hasara kiasi gani tunapata kwa kuyaacha maji yanazagaa hovyo? Naomba nipatiwe maelezo.

Mheshimiwa Spika, afya bora ndiyo msingi wa maendeleo lakini fedha zilizotengwa ni ndogo na mikakati iliyowekwa haitoshelezi kwani idadi ya waganga na wauguzi, ni ndogo sana ukilinganisha na idadi ya wagonjwa wanaowahudumia. Hii ni kutowatendea haki wafanyakazi hao na hata wananchi. Kama vile haitoshi, vifaa vya huduma mbalimbali za afya na vyuoni ni haba hasa katika vituo vya afya na zahanati za kwenye Wilaya na Kata zetu. Mtu anapotibiwa anatarajia apate dawa na aanze kuzitumia lakini maeneo mengine ni kinyume kabisa, mtu anatibiwa na kuambiwa akatafute dawa, je, ni lini Serikali itahakikisha dawa za kutosha zinawafikia wananchi katika vituo vya afya na zahanati zilizo karibu nao?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuhimiza kila kata ijenge shule na zoezi hilo la ujenzi wa shule limefikia asilimia 80, lakini kuna tatizo la Walimu, vifaa vya shule vya kusomea na kusomesha, usumbufu wa mishahara kwa Walimu, ni lini Serikali itaongeza juhudi za kuhakikisha inaongeza fedha kwa Wizara husika ili kupunguza matatizo hayo ili watoto wetu wapate elimu bora na si bora elimu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake za kuhimiza suala la kilimo, kazi ambayo inaikabili Wizara ya Kilimo na hasa kuitia Wizara ya Fedha, ihakikishe kwamba zana za kilimo, pembejeo na mbegu, zinawafikia wakulima kwa wakati. Ni lazima Serikali iweke msisitizo wa kilimo cha biashara na chakula. Ardhi tunayo, nia tunayo kitu gani kinapelekea nchi yetu kutegemea chakula cha misaada wakati ardhi yetu ni nzuri sana na kubwa. Mikopo itolewe kwa wakulima ili ilete tija kwa Taifa

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayawezi kupatikana endapo barabara za vijiji hazitaimarishwa, ni kweli Serikali inatengeneza barabara lakini nyingi zake ni za mijini, juhudi za kutengeneza barabara za vijiji ili wakulima wapeleke mazao yao kwenye masoko ya mjini na kujipatia kipato, zinahitajika. Haya yote yanahitaji fedha zipelekwe kwenye Wizara husika ili iweze kutekeleza mambo haya kwa mafanikio. Naomba nipiatiwe majibu ni vipi masuala haya yatafanikiwa na Taifa kuzidi kupiga hatua?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri aliyoitao hapa Dodoma kuelezea wazi kuhusu wazi mwelekeo na hasa pale alipolezea wazi kuhusu bajeti na mtikisiko katika mfumo wa fedha duniani kwa uchumi ambao haujawahi kutokea zaidi ya miaka 60.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Waziri wa Fedha na Manaibu pamoja na timu yote ya Wizara ya Fedha kwa maandalizi ya bajeti hii. Pia nimpongeze Waziri Kivuli kwa kuleta bajeti mbadala ambayo ni nzuri, mengi yatasaidia kuleta faraja kwa ule upungufu uliopo na kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2009/2010, ni ya wastani si nzuri na si mbaya, ina upungufu lakini mipango iliyopangwa pamoja na fedha zilizopangwa zikitumika kama zilivyokusudiwa basi itapunguza ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuipa kipaumbele bajeti kuhusu kilimo. Kwa kweli kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu. Kama tunataka kuboresha kilimo, kwanza tuwe na mikakati thabiti, tuwe na watalaam wa kutosha na waende mashambani, wasikae maofisini tu na tuwapatie mbolea mapema, pembejeo na zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wakulima itawawezesha wakulima kupata mikopo kwa ajili ya kupanua kilimo na kuzalisha mazao mengi kwa ajili ya Taifa letu na vilevile wataweza kujiwekea akiba zao.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji nacho kipewe kipaumbele ili tusitegemee kilimo cha mvua kwani mvua tunaweza tukakosa kabisa na tukapata njaa. Kuboresha kilimo ni manufaa ya Watanzania na njia moja ya kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, afya ni muhimu katika maisha ya binadamu, kama mtu hupati matibabu kwa wakati, ni usumbufu mkubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali hii kwanza ielekezwe vijijini kwa kuhakikisha kuwa zahanati zimeboreshwa na zimepatiwa wafanyakazi wa kutosha, madawa pamoja na vitendea kazi na nyumba za Madaktari ili waweze kutoa huduma kwa ufanisi kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kama nchi haina miundombinu, haiwezi kuinua uchumi wa Taifa, ni lazima kuwe na mipango kabambe ya kutafuta Wakandarasi wazuri sio wababaishaji na kupelekeea kuipa hasara Serikali na nguvu kubwa ipelekwe vijijini ambako ndiko uchumi wa nchi hutegemea kwa chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya vijijini ni mibovu, wakati wa mvua wakulima wanapata hasara kubwa kwa kusafirisha mazao yao na pia kupeleka hasara kwa mkulima na Taifa, pamoja na kuzorotesha shughuli zote.

Mhehsimiwa Spika, miundombinu ya reli ni mibovu na inahitaji iboreshwe ili wasafiri wanaosafiri kwa kutumia usafiri huo wawe na imani kwa usalama wa maisha yao na mali zao. Suala la *SUMATRA* liangaliwe kwa makini na kuhakikisha vyombo vinapoondoka bandarini viwe vinakaguliwa ili ajali zisitokee mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, kila mtu anahitaji kupata elimu lakini bado tuna upungufu wa Walimu, vitendea kazi, vikalio vya wanafunzi na nyumba za Walimu. Huo ni upungufu hasa vijijini. Kwa hivyo, naomba Serikali, bajeti hii ielekeze nguvu vijijini kupanua elimu kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu, napenda kukupongeza wewe pamoja Wenyeviti wako wote na namtakia kila la kheri Waziri na Manaibu wake katika kazi yao na Mungu awabariki, amen.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, kilimo kwanza kama mkakati au kauli mbiu ya kuendeleza kilimo, naomba kupata ufanuzi, je Serikali mbona haijonyesha katika bajeti yake mkakati wa kutenga fedha za kutosha kwa upatikanaji wa matrekta ili kuendana na mapinduzi ya kilimo na kuondokona na kilimo cha jembe la mkono?

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali mbona haikuonyesha mwelekeo wa takwimu zinaonyesha na kufafanua bei za mbolea na pembejeo ili kuendana na dhana ya kilimo kwanza, mbali ya kusubiri siku ya kuwasilishwa sekta husika?

Mheshimiwa Spika, kilimo kwanza ni jambo zuri isipokuwa wakulima bado wana hofu na kujiuliza maswali kadhaa na Serikali ni vema itoe ufanuzi wa yafuatayo:-

- (i) Viwanda nya mazao vitakuwepo?
- (ii) Masoko ya uhakika ya mazao yatakayozalishwa yatakuwepo?
- (iii) Je, miundombinu ya kufikisha mazao ya kilimo katika masoko itaimarishwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari zetu, bado Serikali haijapanga mkakati madhubuti wa kuziendeleza ili kuweza kuleta tija na ufanisi kwa viwango vinavyotakiwa ili kukidhi haja ya meli kubwa kuweza kutoa huduma mfano bandari ya Dar es Salaam ilihudumia shehena jumla ya tani 2,316,000 ikilinganishwa na tani 5,703,000 mwaka 2007 sawa na upungufu wa asilimia 59.4, nini sababu ya kushuka kwa tija ya kupakia na kupakua mizigo? Hivi tunajifunza nini juu ya upungufu huo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi katika bahari, imedhihirika kwamba bado haujaleta tija na pato kwa wananchi na Serikali. Ninashauri Serikali kuandaa mazingira ya kutafuta mkopo wa bei nafuu wa meli za uvuvi ili kuweza kuvuna rasilimali zetu zilizokaa muda mrefu.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, kwa hotuba yake iliyotangaza hatua mbalimbali zinazolenga kuunusuru uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi pia kwa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake pamoja na wataalamu wake wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri na hasa katika kipindi hiki cha aina yake ambapo uchumi wetu kama ulivyo wa dunia, umepata msukosuko.

Mheshimiwa Spika, *this is ex-ordinary moment and I therefore expect extraordinary measures* na ndivyo Wizara ilivyofanya. Hata hivyo, naomba Wizara irekebishe baadhi ya hatua hizo kama ninavyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, kufuta misamaha ya kodi, *NGO's* na Mashirika ya Dini ni wadau wakubwa wa maendeleo, kama kuna *abuse* ya misamaha hiyo, dawa si kufuta bali ni kutafuta hao wahalifu na kuwashughulikia. Serikali siku zote inapaswa kuangalia ni wapi tulipojikwaa na si wapi tulipoangukia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi ya magari, katika bajeti ya mwaka huu, Serikali haijasema lolote ili kuwapa watu uwezo wa kulipa. Serikali ifikirie uwezekano wa watu kulipa kwa awamu kama wanavyofanya wafanyabiashara wanalipa kodi kila baada ya robo mwaka. Vijana wetu wengi wanamiliki magari na kumiliki gari si utajiri watu wakalipe kwa awamu. Kiwango ni kile kile lakini itaonekana ni kidogo kwa sababu analipa kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu VAT kwenye mauzo ya kahawa na chai, siku zote hizi tunalazimisha unywaji wa kahawa ya hapa nchini ili kupunguza utegemezi wa soko la nje, kweli VAT ni kufanya mazao yanayosindikwa hapa nchini kuwa ghali zaidi, hii ni *counter productive* na inaua kabisa moyo wa usindikaji wa mazao ili kuongeza thamani, haiendi sambamba na kauli mbiu ya kilimo kwanza, inasaidia sana viwanda vya nje ya nchi zetu. Sababu inayotolewa ya kufanya mazao haya sawa na mengini ni dhaifu. A good Government always improves lives of its people not otherwise. Pengine hatua nzuri ingekuwa mazao mengine pia yasiwe na VAT ili kuleta huo usawa. Hivi tutapeleka mazao ghafi nje mpaka lini, wafanyabiashara wamekuwa *bailed out* na Serikali, sioni ni kwa nini Serikali hiyo hiyo iwakandamize wakulima!

Mheshimiwa Spika, kuondoa ushuru asilimia 10 kwenye mafuta ghafi (*grude palm oil*), hii pia ni kuwakandamiza wakulima wa alizeti waliohamasihwa sana na ari yao sasa iko juu, kwa nini tutekeleze matakwa ya wachache kuumiza wananchi wetu walio wengi? Tunamtumikia nani hapa?

Mheshimiwa Spika, tatizo si *East Africa*, nani analima *palm oil* hapa Afrika Mashariki? Natumai Tanzania (Kigoma) tunaongoza. Ni nini hatma ya alizeti na mawese ya Kigoma sasa na miaka mitano ijayo? Alizeti imeongeza ajira na kipato katika Mikoa ya Kati, vyote hivi vitapotea na hii haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imefanya vizuri kuondoa tozo na ushuru katika mashine na mitambo ili kusaidia uchumi hapa Tanzania. Sasa tusiharibu tena kwa kuweka tozo na ushuru kwenye mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, *TEMDO*, *CAMARTEC*, *SIDO* wamebuni mashine, mitambo na teknolojia mbalimbali hasa kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha *agro-process industry*. Naomba tubuni mpango utakaowezesha uzalishaji wa teknolojia hizi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza, *Mwananchi Empowerment Fund*, ipewe fedha ili wazalendo wazitumie kuendeleza viwanda hivyo kwa mfano, *CAMARTEC* wametengeneza trekta, tunafanyeje kuwa na uzalishaji mwangi wa matekta?

Mheshimiwa Spika, kuanzisha mfuko wa uzalishaji wa technolojia hizi. Kwa njia hii, tutaanza safari ya kuifanya nchi hii kuwa ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, namtakia Waziri na Wizara yake baraka tele na ufanisi bora wa kazi.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Nne, kwa hatua kubwa iliyofikia katika kuleta maendeleo ya wananchi wa nchi hii. Nashukuru watendaji wote, wananchi wote pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais, maana kama yeche amefanya vizuri lakini waliobakia wanabeza jitihada hizo, basi nchi yetu itabakia kwenye umaskini.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tujali jitihada hizo na tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 kwa nguvu zote. Naunga mkono hoja asilimia 100.

**MHE ABDUL JABIRI MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, kwa kiasi kikubwa imelenga kuunusuru uchumi wetu ambaou unadorora kutokana na msukosuko wa uchumi duniani (*Global Financial Crisis*). Ili kunusuru uchumi wetu, Serikali imeweka vipaumbele mbalimbali, ambavyo endapo vitatekelezwa kwa umakini na ufanisi wa hali ya juu, kuna uwezekano mkubwa sana wa kuinusuru nchi hii kutokana na msukosuko huo.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu yetu ya mwaka huu ni ‘Kilimo Kwanza’, ambayo Serikali imeiweka. Nchi hii, ambayo asilimia zaidi ya 80 ni wakulima kwa muda mrefu, sekta hii ilikosa msukumo wa Kitaifa na hatimaye kulifikisha Taifa letu kuwa omboomba wa chakula. Ni matarajio yangu kuwa endapo Serikali itafuatalia kwa karibu tatizo la uendelezaji wa sekta hii, italeta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu suala la Kilimo linasisitizwa hasa kwenye mikoa minne tu, ambayo imepewa jina la “*The Big Four*” na kusahau Mikoa mingine ambayo ina ardhi ya kutosha na yenyе rutuba nyingi mfano Bonde la Mto Rufiji. Tafiti nyingi zimefanyika kuhusiana na bonde hili chini ya RUBADA na kuonyesha kuwa kama bonde hili litaendelezwa, kuna uwezekano mkubwa wa kuweza kuzalisha chakula cha nchi nzima kwa mwaka mzima. Ni vizuri sasa Serikali, iangalie upya Mikoa hiyo, kwa kuongeza Wilaya ya Rufiji katika uzalishaji wa chakula. Wananchi wapo tayari kuzalisha iwapo tu zana za uzalishaji hasa matrekta pamoja na wataalam wa kilimo, watapelekwa kwa wingi katika Wilaya hii ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia, ni elimu. Kwa muda mrefu, elimu inapewa kipaumbele na Taifa hili na matunda yake kwa sasa yanaonekana. Jambo ambalo napenda kuunga mkono ni maamuzi ya kujenga nyumba za Walimu, hasa maeneo ya pembezoni. Uamuzi huu, naomba utelekezwe kwa uaminifu, kwani Walimu wetu wengi ambaou hufundisha shule za pembezoni wanateseka sana kwa kukosa nyumba bora za kuishi na kusababisha familia zao kukaa maeneo mengine na hivyo kumfanya mtumishi huyu, kuchukia mazingira hayo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujengaji wa nyumba za Walimu, ni vizuri basi kwa Serikali kutekeleza azma yake ya kuwapatia “posho ya mazingira magumu” watumishi wote walio katika mazingira hayo. Kwa kufanya hivyo, Walimu hao, kwa kiasi fulani wataweza kuyakabili mazingira hayo. Posho hizi, zizingatie watumishi wote, yaani Walimu wa shule za msingi na sekondari; pamoja na wauguzi na watendaji wengine wa Serikali.

Aidha, ni vizuri pia kwa watumishi wa maeneo ya *Delta* ya Mto Rufiji ambapo kuna kata nne na shule za msingi ishirini na mbili za sekondari, wakapewa hudumu ya

boti, ili ziwasaidie kufika katika maeneo hayo ya *Delta*. Kwa kufanya hivyo, kutawezesha watumishi hao kusafiri na kufurahia mazingira hayo magumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wa Fedha na watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri ya fedha. Naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi ni maskini sana kwa maana zote za neno hilo. Hali ya umaskini ni mbaya zaidi vijijini kuliko ilivyo mijini. Inatia moyo kuona kwamba Serikali inachukua hatua mbalimbali zenyelengo la kupunguza hali ya umaskini nchini. Njia sahihi ya kupambana na umasikini ni kudhibiti vyanzo veya umaskini wetu. Katika bajeti hii, Serikali inaendelea kuongeza ruzuku katika pembejeo za kilimo na kuchukua hatua madhubuti za kuongeza uingizaji wa matrekta ya uwezo mbalimbali nchini. Hatua hizi, zitakuwa na manufaa kwa wakulima, hasa kama utawekwa utaratibu mzuri wa kuanzisha vituo veya zana na pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa dirisha la mikopo ya kilimo litakaloanzishwa *TIB*, ni dhahiri kwamba wakulima wadogo wanaolima heka moja hadi tano hawatafaidika na mikopo isipokuwa wakiwekewa utaratibu utaratibu wa makusudi wa kuwafikia kuititia kwenye vyama vyao veya ushirika, *SACCOS* na vikundi. Hii ina maana kwamba *TIB* ikopeshe asasi hizo. Wakati huo huo, dirisha la mikopo la *TIB* litumike kukopesha wakulima wa kati na wakubwa – watu wanaotaka kuanzisha kilimo cha biashara. Ufumbuzi wa tatizo la mikopo kwa wakulima wadogo, utapatikana kwa kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambayo itakuwa na mtandao kuititia kwenye asasi za fedha, hususan *community banks*, *SACCOS* na kadhalika. Hatua mahsusizi zichukuliwe mapema. Ikiwa ni pamoja na kutunga sheria ya benki hiyo. Tumechelewa sana kuanzisha benki hii.

Mheshimiwa Spika, suala la kuondolewa kwa misamaha ya kodi kwa mashirika yasiyokuwa ya Serikali, *NGOs*, yakiongozwa na Mashirika ya Dini, limeleta hali mbaya sana ya kisiasa nchini. Hatua zilizochukuliwa kukanusha na kufafanua suala hilo, hazijafanikiwa kuonesha wasiwasi uliojengeka. Mheshimiwa Waziri alipaswa kutambua kwamba suala hilo ni nyeti na kwa hiyo kulizungumzia kwa uangalifu mkubwa. Nina hakika kwamba Serikali haitaki ugomvi na Mashirika ya Dini na ugomvi wa aina hiyo hauna manufaa kwa nchi yetu. Napendekeza Waziri atoe tamko maalum Bungeni kufafanua suala hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Taifa halina uwezo wowote wa kutengeneza zana za kilimo baada ya *UFI* na kiwanda cha Mbeya kuacha kuzalisha zana hizo. Tunakiweka kilimo chetu katika hatari kubwa kwa kutegemea zana za kuagizwa kutoka nje. Aidha, viwanda veya kutengeneza mbolea vilikufa miaka mingi iliyopita na hivyo hivyo viwanda veya kusindika mazao kuyaongezea thamani. Inabidi Serikali ichukue hatua za makusudi kuhamasisha kuanzishwa kwa viwanda veya kilimo. Hili ni jambo muhimu na la haraka.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie upya suala zima la msamaha wa kodi. Nadhani ni busara kufuta misamaha ya kodi kwa Makampuni yote yanayojihuisha na shughuli za uchimbaji wa madini. Inashangaza na inasikitisha kuona msamaha umefutwa kwa wale tu watakaoingia mikataba mipyä au wapya na si wale wa zamani. Katika dhana nzima ya ulipaji kodi, lazima kuwe na usawa, haiwezekani watu wanaofanya shughuli moja/biashara moja wengine wafutiwe kodi wengine walipe kodi.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza na makampuni ya zamani yalipe kodi kwani Serikali ilitoa tangazo la msamaha hivyo, itoe tamko rasmi kuwa sasa msamaha umefutwa ili nchi ianze kupata mapato kwani hali ya uchumi ni mbaya tunahitaji pesa! Kwani hakuna sheria inayomtaka mwekezaji asitoe kodi bali ni moja ya kivutio tu ili waje kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuchangia kuhusu suala la misamaha ya kodi kiholela, Serikali iangalie upya wanaosamehewa kama wanastahili kusamehewa? Kwani upungufu wa ukusanyaji wa mapato unachangiwa na misamaha holela na ile ya wawekezaji ambapo Waziri mwenyewe amekiri nchi inapoteza zaidi ya trilioni 2, sawa na 30% ya mapato ya Serikali. Kwa hiyo, mianya yote ya upotevu wa pesa zinazostahili kukusanywa kama mapato ya nchi izibwe kwani nchi yetu bado inategemea 100% ya bajeti ya maendeleo kwa wafadhili.

Mheshimiwa Spika, *Stimulus Package* ya Tshs. 1.7 trilioni, ni wazo zuri lakini itawanufaisha wenye Mabenki na inazipa mwanya wa kufanya biashara nzuri na Serikali kwa kutuma fedha za Serikali. Nashauri Serikali yetu ione ulazima wa kuwa na hisa ili kuhakikisha kuwa fedha iliyotolewa ambayo inatokana na kodi za wananchi inadhibitiwa na kurudi kwa walipa kodi Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashauri Serikari iweke wazi kuwa hiyo trilioni 1.7 Tshs inatoka ndani ya bajeti ambayo ni Tsh 9.5trioni hivyo basi bajeti halisi ni 7.8 trilioni ambayo itatumika katika shughuli za maendeleo na utendaji wa Serikali na kama sivyo Serikali iweke wazi juu ya bajeti halisi.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashauri pesa hii itungiwe sheria na Bunge ili utekelezaji wake uweze kusimamiwa na Bunge ili kuzuia matumizi mabaya ya fedha na kuepuka EPA Na.2 Kwa maana hiyo, nashauri Bunge lishirikishwe kikamilifu juu ya matumizi ya hiyo *Stimulus Package*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la mfumuko wa bei, (*Inflation*), ni kubwa sana na wasiwasi upo kuwa yawezafikia zaidi ya 25%. Sasa Serikali itueleze ni mikakati gani imefanyika ili kupunguza *inflation* ili kunusuru maisha ya Watanzania na kulinda thamani ya shilingi yetu? Serikali ilieleze Bunge hili mikakati ikoje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kilimo na kaulimbiu zinazozaliwa kila kukicha, sasa tunasikia KILIMO KWANZA, tumesikia kauli mbiu nyingi ‘kilimo ni uti wa mgongo’ na kadhalika sasa tutaendelea kubadili kauli mbiu mpaka lini bila

utekelezaji? Inashangaza kauli mbiu zipo kilimo hakiendelei. Kilimo kimepewa asilimia 7 tu, sawa sawa na bajeti ya mwaka jana, sasa mkakati wa kilimo kwanza utafanikiwa kweli?

Mheshimiwa Spika, nchi haina viwanda vya pembejeo, au zana za kilimo mfano UFI na ZZK (Mbeya) vimekufa na hatuna viwanda vya usindikaji. Umeme wa matatizo, njia za usafirishaji zikiwemo barabara, reli, ni mbou na zisizoaminika hasa maeneo ya vijijini palipo na shughuli za kilimo. Nashauri Serikali iboreshe hayo ili kilimo kifanikiwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile kilimo cha umwagiliaji ni wimbo usiotekelzeza ingawa tuna mabonde mazuri mengi mfano Bonde la Mto Rufiji na Malagarasi. Kwa Mabonde hayo mawili tunaweza kulisha nchi za Kusini na Mashirika ya Afrika lakini maneno mengi vitendo sifuri.

Mheshimiwa Spika, bajeti ni makisio ya mapato na matumizi na Bunge lako liliidhinisha bajeti ya mwaka ulioisha wa 2008/2009, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, alieleze Bunge lako kuhusu utekelezaji wa bajeti iliyopita 2008/2009 na atueleze ni kiasi gani kwa maoni yake kilibaki katika bajeti ile bila kutumika na fedha hizo zina athari gani kwenye bajeti tunayoijadili sasa.

Mheshimiwa Spika, pia namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, atueleze ni kiasi gani kulitumika katika Akaunti ya Amana yaani *deposit* na miadi mingine yaani (*Commitments*), ili Bunge hili liweze kutolea maoni na kuondoa dhana ya matumizi ya bajeti mbili wakati mmoja yaani (*running two parallel budgets*).

Mheshimiwa Spika, bajeti hii inaonyesha kuwa Serikali itatumia trilion 9.5, Mheshimiwa Waziri ameleeza kuhusu hatua alizopanga kuchukua ili kupunguza matumizi makubwa kwenye Wizara, Mkoa, Idara mbalimbali, ili bajeti hii ionyeshe uwiano katika matumizi na fedha nyingi zaidi kutoka kwenye vyanzo vya ndani kwenda kwenye bajeti ya maendeleo hasa kwenye Kilimo, elimu na miundombinu, naomba atueleze pia ni jinsi gani matumizi ya magari kwa viongozi yataadhibitiwa kwani wengi wao wana magari mawili, la Ofisi na la nyumbani. Vile vile atueleze au afafanue kuhusu utaratibu wa kuwakopesha watumishi wa Serikali magari.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ni uingizaji bidhaa kutoka nje, haina udhibiti na huigharimu Serikali pesa nyingi za kigeni, Serikali imejipanga vipi kudhibiti suala hilo? Serikali pia itueleze mipango yake ya udhibiti wa matumizi ya pesa za kigeni kiholela kwani si halali kwa wafanyabiashara kuuza bidhaa na huduma zao kwa fedha za kigeni, hii ipo mahotelini kwa kiasi kikubwa, je, Serikali haioni kuwa inaendelea kusababisha shilingi yetu ikose thamani kila kukicha, hivyo hatua zichukuliwe haraka. Tujifunze kutoka kwa wenzetu Kenya na South Afrika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi, ishirikiane na kitengo kinachojishughulisha na mipango, wafanye utafiti wa kina wakati

wa kuandaa bajeti ili kuleta Bungeni bajeti inaoyoonyesha vitendo yaani *action orriented budget!*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa kufafanua jambo la uchumi wa nchi yetu. Vyanzo tulivyonyavyo ni vya kutosha kabisa kukuza uchumi wetu, tuna Bandari zetu, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara. Naomba kujua pesa zilizotengwa kwa kilimo ni kiasi gani? Kwa kuwa Mkao wa Kagera umesahaulika, je, ina sehemu katika bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye Benki ya Wakulima, kuna mikakati gani ya kusimamia kutenda haki sawa kwa wote isiwe ya watu wachache?

Mheshimiwa Spika, suala la madhehebu ya dini, tusitake kuwakorofisha kwa jambo dogo sana. Naomba Wizara ikae chini, ijaribu kurekebisha. Mkao wetu wa Kagera, Hospitali nyingi pamoja na shule, ni za dini, ajira nyingi ni za dini, leo hii tuisiwathamini, ni ajabu kubwa sana. Chonde chonde, naomba legeza kamba.

Mheshimiwa Spika, pesa zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi uwanja wa ndege, je, ni kwa nini zinachanganywa na uwanja wa Mpanda? Naomba kujua uwanja ndege wa Bukoba umetengewa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, naomba kujua zao la kahawa, kuna tatizo gani kuhusu bei? Uganda wanaiza soko gani au wana soko tofauti? Je, Wizara hii inatusaidiaje sisi watu wa Mkao wa Kagera kwenye Kilimo cha Kahawa pamoja na kilimo cha Umwagiliaji? Pesa zilizotengwa, je, mkao huo umo?

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji pensheni kwa wastaifu wetu, suala hili sisi Wabunge lipo kwenye Majimbo yetu, je, Serikali inasemaje kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la fidia ya wakulima wetu wa kahawa. Wanaiza kahawa zao kwenye vyama vya ushirika, wanapunjwa sana, naomba waruhusiwe kuuza popote penye kipato kizuri kulingana na umuhimu wa zao hilo ambalo ni tegemeo letu, zao hilo ndilo lililotusomesha sisi tulio wengi.

Mheshimiwa Spika, je, barabara ambazo zimetelekezwa tunapata shida sana, kwa mfano barabara ya Muleba – Lusahunga, wananchi wanateseka sana pamoja na kutekwa mara kwa mara. Je, imetengewa shilingi ngapi ili tuweze kuondokana na matatizo haya?

Mheshimiwa Spika, mikakati yote iliyomo ndani ya bajeti hii iwe na usimamizi mkali sana kuweza kusimamia watendaji kwa sababu sio wazuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya matibabu hasa Wizara ya Afya yameshughulikiwaje maana kuna malalamiko mengi sana, kuhusu Manesi, Madaktari, kwenda kutibiwa wananyimwa pesa, wanasubiri bajeti, je, afya imetengewa pesa ya kutosha, wanadai pesa za nyuma na za kurudi kutibiwa.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kukumbusha hivi, *TICTS* iondolewe mara moja pamoja na watendaji wake. Mimi na Kamati tumeona mambo mengi mabaya sana.

Mheshimiwa Spika, naomba tumalize mgogoro wa kidini wa kujiletea ambao umeleta sura mbaya kwetu.

**MHE.DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mustafa Mkulo (Mb), Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Manaibu wake na watendaji wa Wizara yake kwa kuandaa Bajeti ya Serikali na kuwasilisha hotuba yake vizuri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mgawo wa fedha za bajeti mwaka huu, unaonyesha jinsi vipaumbele vya Serikali vilivyowekwa. Cha kwanza, ni elimu iliyotengewa shilingi billion 1,743.9, pili ni miundombinu iliyotengewa shilingi 1,09.6, kipaumbele cha tatu ni qfya yenye shilingi bilioni 963 na cha nne ni kilimo iliyotengewa bilioni 666.9, ikifuatiwa na Maji na Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya elimu, napenda Serikali itilie mkazo suala la upatikanaji wa Walimu katika shule za msingi na Sekondari, pamoja na ujenzi wa maabara na hosteli katika shule za sekondari ili angalau kila Mkoa uwe na Chuo cha Ualimu, Mkoa wa Mara nao ufikiriwe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu ya barabara za lami na hata changarawe hapa Tanzania, ni wa gharama kubwa. Inaonyesha kwamba katika Afrika ya Mashariki gharama zetu ni za juu zaidi, Serikali ifanye utafiti katika hili, ni kwa nini inakuwa hivyo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Serikali.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake, kwa kuandaa hotuba pamoja na bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuitia katika misamaha ya kodi za Petroli, hasa upande wa madini, kwani msamaha wa kutolipa kodi yaani kutozwa kodi katika petroli kuanzia tarehe 1/7/2009, naona ni kama kiini macho. Kwani utawezaje kumtoza kodi mtu ambaye hujafunga naye mkataba wala hujui atakuja lini?

Mheshimiwa Spika, cha muhimu, ni kutoza makampuni yaliyopo kwanza ili kuweza kukusanya kodi ya uhakika kuliko kupanga kodi kwa mtu ambaye humuoni na hayupo karibu. Tunaposamehe kodi ya kiwango kikubwa ndio tunawaumiza wananchi wetu kwa michango. Bajeti hii inaonekana makusanyo ni madogo na matumizi ni makubwa, Angalizo, tusije kuta tunawabebesha wananchi wetu mzigo mkubwa wa bajeti hii kama haitatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, mambo mliyoahidi ni mengi kama maabara katika sekondari, nyumba za Walimu, zahanati na n.k. Kama hapo awali, Serikali ilisema wananchi

wachangie shule, nyumba za Walimu, mabweni na kadhalika, sasa basi katika kuyumba kwa uchumi mambo haya yatakekelezeka, isiwe ni bajeti ya kisasa kuelekea Uchaguzi na tukawapa wananchi matumaini.

Mheshimiwa Spika, tunaposema kipaumbele chetu ni KILIMO KWANZA, bei za wakulima katika soko la dunia zimeanguka. Mfano katika baadhi ya Wilaya na Mikoa ya Mwanza, baada ya kushuka kwa bei ya pamba, sasa wakulima hawataki hata kutoa pamba mashambani, hivi ni nani anafidia hasara za wakulima hawa, kwani wanaona kutoa pamba mashamabani ni gharama kuliko mauzo ya pamba ambayo iko shamabani. Haya ni mateso kwa mkulima ambaye ametumia gharama kubwa kwa kulima tena kwa jembe la mkono, Mtanzania wa leo bado analima kwa jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania ya leo hata mtu akiagiza trekta, litakaa bandarini kwa muda wa miezi miwili au zaidi ndio litoke kwa kuwa kodi na gharama za utoaji, ni zaidi ya milioni moja. Angalieni sana hiki kitengo cha *TRA* na *TISCAN*, hawa ni watu wa ajabu, kama hata trekta kutoka tu ni zaidi ya miezi miwili.

**MHE. SHALLY J.RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kuunga mkono hoja kwani hotuba hii ni nzuri na inaeleweka vizuri japo kuna maeneo ambayo yamenikwaza na ninamuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha ayatolee tamko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa fedha za umma, pamoja na maelezo mazuri ya Waziri kuhusu usimamizi wa fedha za umma, hakuzungumzia kabisa mashirika ya umma. Katika kitabu chake ukurasa wa 13/14, amesisitiza kuwa “mafanikio yamepatikana katika usimamizi wa fedha za umma, inadhihirika katika maeneo kadhaa moja wapo ikiwa ni kuimarishwa kwa Kamati za Bunge za Mahesabu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa (*PAC* na *LAAC*), kwa kupatiwa mafunzo nje na ndani ya nchi”, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumuuliza Mhesimiwa Waziri wa Fedha, je, fedha za mashirika ya umma hazihitaji usimamizi wa uhakika? Endapo jibu ni ndio kwa nini Kamati ya Mahesabu ya Mashirika Umma (*POAC*) haijapewa kipaumbele kwenye mafunzo ya nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, kwa kukusitiza jambo hilo, Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 15(27), alizungumzia tena *PAC* na *LAAC* bila kutaja lolote kuhusu taarifa ya *POAC* iliyotolewa hapa Bungeni kwenye Bunge katika Mkutano wa Kumi na Sita, je, ni kwa nini hakuzingatia mapendekezo ya Kamati kuhusu kuyanusuru mashirika hayo?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Waziri kutozungumzia *POAC*, ninapenda kusikia toka kwake mambo yafuatayo:-

Kwanza, kati ya mashirika 159, ni mangapi ameyaongezea fedha za kuyaimarisha? Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alitamka wazi kuiwezesha Benki ya *TIB*. Kwa hili tunashukuru Mungu kwani itanufaisha wengi. Bila

kusahau uamuzi alioufanya kuinusuru benki ya *CRDB* kwa niaba ya wakopaji wakulima na vyama vya ushirika. Wana hisa wa *CRDB* wamemshukuru na kumpongeza Rais wetu mchumi aliyebolea.

Pili, ni lini Serikali itauza hisa zake kwenye mashirika ya umma yaliyobakia ili kujitoa kabisa kwenye biashara. Hususani kwenye taasisi za fedha kama benki? Hapa niulizie rasmi benki ya Twiga Bank Corp.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya kutoa fungu la hela ili kuuwezesha umma kupitia *SACCOS*, waliofaidika ni wachache kwa kurudiarudia tena katika ngazi za Mkoa na Wilaya. Ni lini sasa fedha hizo zitawafikia wananchi kwenye kata zao na vijiji vyao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufutwa kwa misamaha ya kodi wa Taasisi za Dini na NGO's. Nashauri jambo hili liangaliwe upya. Eimu iitolewe na wadau wote wahuishwe kikamilifu, ahsante.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Naomba nichukue fursa hii kuipongeza bajeti ya Waziri wa Fedha inayohimiza Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, nayakubali yote yalisemwa na bajeti hiyo. Napenda kushauri Serikali kwamba kama inapenda kuona matunda ya mpango huo, wakulima katika Mikoa sita iliyotajwa wapewe kipaumbele katika masuala ya kilimo. Wapewe pia elimu ya matumizi ya zana za kilimo na pembejeo. Kama hili halitafanyika, pesa iliyotengwa kwa ajili ya kusaidia kuinua kilimo, haiwezi kuonyesha mafanikio ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ugomvi wa wakulima na wafugaji ni tatizo la Kitaifa. Pamoja na tamko la Serikali kuhusu jambo hilo, bado wakulima hawajatendewa haki. Naiomba Serikali iongeze juhudhi ya kutenga fedha /kutafuta fedha ili zoezi la kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima yapimwe kwa haraka nchi nzima hususani maeneo yenye wakulima na wafugaji. Bila hili, wananchi wengi hasa wakulima wataendelea kuuwawa na wafugaji, hili ni tishio kwa amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia fedha nyingi sana ndani na nje ya nchi kutengeneza barabara za lami nchini kote kwa gharama kubwa. Nataka kujuu ni vipi barabara hizi haziwekewi alama za barabarani kama zilivyo nchi zingine, badala yake barabara hizo (*high ways*) zinachimbwa kwa sululu na kuwekewa matuta, je Serikali haioni kuwa, kufanya hivyo ni kinyume na matumizi ya *high way road*, Serikali haijagundua kwamba matuta hayo yameongeza uharibifu wa magari na matuta hayo mengine yamewekwa katika maporomoko ya milima ambapo waporaji/majambazi hungojea magari na kuyavamia hususani barabara ya Tunduma - Mbeya, hii ni hatari sana. Naomba Serikali itazame upya suala hili, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI A. MZEE:** Mheshimiwa Sika, mgawo wa 4.5% kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, bado halijapatiwa ufumbuzi. Matokeo yake ni kuendelea kuwa

kero za Muungano, je ni wakati gani muafaka wa kero hii itapatiwa ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipokuwa akiwahutubia wananchi wa Dodoma, alisema Serikali yake inatarajia kutumia shilingi trillion 1.7 kukabiliana na msukosuko wa uchumi. Je, fedha hizo zinatoka wapi na mbona hazionekani katika kitabu cha matumizi wakati Bunge ndio chombo kinachoidhinisha matumizi ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, kina mama bado ni tatizo, kina mama wengi wanapoteza maisha kutopteka na ujauzito wakati wa kujifungua. Ili kukabiliana na lengo la tano la *MDGS*, lazima Serikali itenye fedha za kutosha katika sekta ya afya ili kuwepo na afya bora. Mikakati ipangwe ili kuwe na zahanati zenye vifaa vya kutosha kujifungulia, usafiri, wahudumu, wauguzi na madaktari pamoja na kuimarisha hospitali zote ili kupunguza vifo vitokanavyo na kujifungua.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya elimu, elimu ya awali imefikia lengo lakini tatizo kubwa lipo kwenye elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu. Madarasa, nyumba za walimu, vifaa na Walimu pamoja na Wahadhiri hawatoshi, je Serikali ina mpango gani mahsusii kukabiliana na changamoto zote hizo hasa hasa katika bajeti hii ili kupunguza matatizo pamoja na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu ina mipango gani?

Mheshimiwa Spika, mionganii mwa malengo ya *MDGS*, ni kupungza umaskini na njaa, Serikali imekuja na *theme* mpya ya KILIMO KWANZA, nakuacha ile ya kwanza ya KILIMO NI UTI WA MGONGO, Serikali lazima itenye bajeti ya kutosha katika sekta ya kilimo ambacho kitakuwa endelevu na kutoa tija kwa Tanzania kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, Mikoa yote ambayo ina uwezo wa kuzalisha zaidi ipangiwe mikakati ambao utaondokana na jembe la kutumia mkono, badala yake Serikali itenye bajeti ya kutosha ya pembejeo, zana za kilimo yakiwemo matrekta na mbolea ili uzalishaji uwe bora zaidi ili kuondokana na umaskini na njaa.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninawapongoza watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi kuanzia Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu Manaibu Makatibu Wakuu na wote walioshiriki katika machakato wa kuandaa bajeti hii. Ni bajeti nzuri yenye lengo la kuleta maendeleo ya kiuchumi lakini pia ya kijamii. Hata hivyo, yapo maeneo ambayo ninapenda yaboreshwe.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi. Kodi ni moja ya vyanzo vya mapato ya Mataifa yote duniani. Pamoja na utaratibu ambao umekuwepo, ni mianya ambayo inakosesha taifa pesa nyingi. Kwa maoni yangu, ukiacha taasisi za kidini, mashirika, idara na watu wote wenye uwezo wa kulipa kodi, walipe. Binafsi siungi mkono mpango wa kuzitaka taasisi za dini zilipe kodi. Nitaiunga mkono hoja hii pale tu Serikali itakapokuwa imejitoshaleza katika kutoa huduma za elimu, afya na kadhalika katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa vile katika maeneo mengi ya nchi yetu yanapata huduma kama za afya na elimu kupitia taasisi za kudini – basi vitendea kazi vinavyotumiwa na taasisi za kidini kutoa huduma hizo zisitozwe kodi. Serikali itakuwa na sababu ya kulipisha kodi taasisi za kidini itakapokuwa imefikisha tu vijiji vyote huduma za afya, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda lizingatiwe ni misamaha mingi ya kodi kwa makampuni ya madini hapa nchini hasa iliyoko kwenye mafuta. Ni katika kulipa kodi nchi hii itanufaika na madini yetu. Hivi sasa sekta ya madini inachangia kidogo sana pato la taifa ukilinganisha thamani ya madini yanayochimbiliwa na kuuzwa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya kilimo pamoja na kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu kuwa Kilimo Kwanza, bado, kwa mfano zao la pamba Serikali imedhamiria kufidia wafanyabiashara wa zao hilo lakini imekaa kimya katika suala zima la kustawisha bei ya pamba pale ambapo bei yake iko chini kwenye soko la dunia. Kama Serikali haitasadidua kurekebisha bei ya pamba, kwa hakika wakulima wa pamba hawatalima pamba msimu ujao. Serikali ni muhimu ikaliona tatizo hili kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

**MHE. FELIX N. KIJKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kabla sijatoa ushauri wangu kuhusu Bajeti hii ya Serikali, napenda kutamka wazi kuwa naunga mkono kwa asilimia mia moja. Baada ya kuunga mkono bajeti, naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, napenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kwanza kuzitengeneza barabara za Mkoa wa Kigoma kwa kiwango cha lami. Ombi kwa Serikali sasa ni kutafuta fedha za kujenga barabara hizo bila kusimama na hasa ile barabara ya kutoka Kigoma kwenda Nyakanazi ambayo imekuwa kikwazo kikubwa kinachochangia kwa kiasi kikubwa kuongeza umaskini kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Aidha, zitafutwe fedha na Serikali ili kutengeneza barabara ya Manyuvu hadi Kigoma ili kurahisisha mzunguko wa usafiri, anayetoka Dar es Salaam kwenda hadi Kigoma badala ya kupitia Singida, Kahama, Nayakanazi hadi Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia kuhusu usafiri wa reli, napenda kushauri kwamba kwa makusudi mazima Serikali iboreshe huduma ya reli kwa kuwa imekuwa kero kubwa na kwa umuhimu wa Bandari ya Kigoma kwa ajili ya mizigo inayokwenda nchi jirani za *DRC*, Burundi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudini kubwa za kujenga sekondari za kutosha kwa nchi nzima. Katika hili, ninashauri kwa makusudi mazima, Serikali ipange kozi nyingi za kwenye Vyuo vya Elimu ya Ualimu ili kuwa na Walimu wa kutosha.

Aidha, kwa makusudi mazima, Serikali iweke mkakati wa kujenga ama kuanzisha Chuo Kikuu kwa Mikoa ya Magharibi na hususani Mikoa kama vile Kigoma, Rukwa, Tabora na Kagera. Ninaamini juhudini za Serikali zilizotumika Dodoma, zikitumika kwa

Mikoa hiyo, inawezekana. Hii ni baada ya kuona kuwa wanafunzi wa Kigoma walio wengi baada ya kuhitimu elimu ya Kidato cha Sita wanashindwa kupata nafasi ya kuendelea na elimu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri Serikali kuwa kuliko kujikita kwa kupeleka umeme kwenye vijiji vya miji mikuu na baadhi ya Mikoa yenye umeme, Mikoa na Wilaya zisizo na umeme ipewe kipaumbele. Kwa kutokufanya hivyo ni kuzidi kuwasononesha wananchi wa maeneo hayo. Natoa mfano kwa Mkoa wa Kigoma ambao umekua ukipewa ahadi zisizotekelzeza tangu uhuru. Naishauri Serikali iwaonee huruma wananchi wa Mkoa huo ambao wanaishi maisha kama ya wakimbizi katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji ni sugu kwa Mkoa wa Kigoma hususani Wilaya ya Kibondo. Wilaya ya Kibondo haijawahi kuwa na maji ya uhakika tangu uhuru. Ninaomba Serikali iwaonee huruma wananchi hawa kuanzia Kibondo Mjini, Jimbo la Buyungu pamoja na vijiji vyote vya Wilaya.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu wa kuongea, napenda kuongeza hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kuondoa kodi kwenye nyuzi za kufuma. Kwa maoni yangu, kitendo hiki kitaleta ushindani usio sawa baina ya nyuzi zisizo za pamba na nyuzi za pamba pamoja na nyingine za *natural fibre* kama vile katani. Hali hii inaweza kuzorotesha uzalishaji wa nyuzi za pamba katika viwanda vyetu kama TABOTEX na hivyo kuathiri ufanisi wa viwanda vyetu hapa nchini. Aidha, ununuzi wa pamba inayolimwa na wakulima wetu hapa nchini kwa matumizi ya viwanda vyetu yataathirika pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza Serikali ama isitishe kuondoa kodi hii kwenye *imported synthetic yarn* au *VAT* kwenye *locally produced cotton yarn* iondolewe pia.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nashukuru kupata fursa hii kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Nampongeza Waziri wa Uchumi kwa kuwasilisha bajeti aliyojali sana wananchi wa kawaida na kwa ajili hiyo sina sababu ya kutounga mkono hoja hii. Bajeti hii imizingatia yale yaliyopewa kipaumbele katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 10 Juni 2009. Hata hivyo, naomba kuchangia yafuatayo ili kusaidia maendeleo ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuhami na kunusuru uchumi kukabili matatizo ya mpito na dharura na hasa yale ya ukwasi, kuna haja sasa hivi sasa nchi yetu ichukue kila juhudi ya kuifanya *credit rating* ili na sisi tujulikane kama tunakopesheka katika ulimwengu huu. Pamoja na hatua zitakazochukuliwa ili kuwapatia mikopo wawekezaji wakubwa na wa kati kuna haja pia ya kuhakikisha kwamba wajasiriamali hao wanapata

mikopo kutoka nje. Fedha za hapa nchini peke yake hazitoshi, kuna umuhimu wa kuangalia Sheria za *BOT* na fedha kwa kuzingatia utapatikanaji wa dhamana kwa Benki za nje kutoka BOT na sio kwa benki za hapa hapa tu. Dhamana ya aina hiyo zipewe “*private investors*” vilevile. Kuna mabenki ya kimataifa ambayo yako tayari kutoa mikopo kwa dhamana ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna umuhimu pia hivi sasa Wizara Fedha ichukue fursa na juhudi ya kutafuta mikopo kutoka Mabenki ya nje kwa riba muafaka ili kuzitumia kwa maendeleo ya miundombinu mbalimbali badala ya kutegemea *WB, IFM ADB*, wafadhili wakati umefika sasa kuingiza fedha nyingi za kigeni kwa maendeleo yetu kwa kila hali.

Mheshimiwa Spika, kilimo bila ya viwanda hakitaendelea lazima yote mawili yaboreshwe sambamba wakati tunataka kuwekeza. Katika kilimo lazima tuhakikishe kwamba tunavyo viwanda vya mbolea na pembeleo muhimu na vile vya zana za kilimo na umwagiliaji. Sambamba na hapo uwekezaji kwa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yetu vipewe kipaumbele katika uwekezaji. Hapa ndipo tunahitaji fedha za nje kwa kila hali.

Mheshimiwa Spika, hapo nyuma Bunge lako Tukufu lilipendekeza kuweka ushuru kwa mafuta ghafi kutoka nje. Tulipeleka ujumbe kwenda Malaysia kutafiti aina ya *crude oil*, inayosafirishwa kupelekwa nje na ikathibitika kwamba hakuna mafuta ghafi. Hivyo tukiamua hutoza ushuru ili kuwashamasisha wakulimwa wetu na viwanda vinavyotumia malighafi yetu, mimi binafsi siafiki kuondolewa ushuru mafuta ghafi yanayotoka nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, naunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja sambamba na kumpungeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wake na Watendaji wote wa Wizara hii. Naomba kuchangia hoja katika vipengele vifuatavyo ambavyo napenda vipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, mkopo wa J.K. na A.K., napenda kuishauri Serikali yetu pamoja na kuwapongeza viongozi wetu wakuu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Aman Karume, kwa kuanzisha mikopo hii hapa nchini. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na viongozi wetu hawa lakini ni kweli mikopo hii haiwafikii walengwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalamika kuhusu urasimu mkubwa unafanywa na watendaji katika kuwapatia mikopo hii, wajasiriamali hawa wanawake. Nashauri elimu ya biashara itolewe kabla kutoa mikopo na kuwashamasisha wananchi waweze kulipa ili wengine waweze kupata mikopo kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Spika, kilimo. Kwa kuwa bajeti hii imeweka mbele sekta ya kilimo, ni jambo jema kwa maendeleo ya nchi yetu. Jambo ninalosisitiza ni kupatiwa elimu, vifaa

na mikopo kwa wakulima hasa wanawake ili waweze kuondoakana na matatizo ya kutumia majembe ya mkono. Kwa kuwa wakulima wengi hawana uwezo wa kununua vifaa kama trekta basi waweze kukopeshwa vifaa hivyo ili kilimo kisonge mbele. Pamoja na kutafutiwa soko la bidhaa zao kwa haraka.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri. Hotuba imezingatia kikamilifu mpango mzima wa bajeti unaotoa fursa kwa dhana nzima ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, pongezi za ziada, nazitoa kwa kuongeza pesheni ya wastaa fu, ongezeko la bajeti kwenye sekta za kilimo, elimu, barabara na afya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utaanza kwenye sekta ya kilimo. Kauli mbiu ya kilimo kwanza inawezekana kabisa kuitekeleza endapo yafuatayo yatazingatiwa:-

Matumizi mazuri ya wataalam wa kilimo, njia mojawapo katika hili, ni kuanzisha au kuimrisha mashamba darasa ili kuonyesha kilimo bora kwa vitendo. Wakulima waelekezwe matumizi mazuri ya mbolea ya Minjingu badala ya kuonekana kuwa ina athiri mimea kumbe ni matumizi mabaya. Uanzishwaji wa Benki ya Kilimo uharakishwe. Kilimo cha umwagiliaji kiimrisha zaidi. Kuwe na punguzo la bei kwa zana na pembejeo za kilimo, kuwe na mpango maalum wa viwanda vidogo vya usindikaji mazao ili kuyaongeza thamani. Haya yote yanawezekana kama tutadhamiria kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili nitaaelekeza kwenye sekta ya barabara. Mtando mzuri wa barabara hususani za vijijini, ni kigezo muhimu kwa mkulima kumuondolea umaskini. Ili mkulima aweze kudhibiti vizuri bei ya mazao yake, inabidi aweze kuyafikisha kwenye soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuimrisha barabara za vijijini, kunahitaji fedha za kutosha, mgao kutoka mfuko wa barabara (*Road Fund*), ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kulitambua hilo, katika bajeti ya mwaka 2008 Septemba, 2009 zilitengwa zaidi ya Tshs bilioni 18 kama mfuko maalum (*LGTP VTPP Budget for councils*) kwa ajili ya barabara zilizo chini ya Halmashauri na zile vijijini.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ambazo zilikuwa mchango kutoka Serikali Kuu na msaada kutoka *DANIDA FUNDS* hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2008 Septemba, hakuna Halmashauri hata moja iliopokea fedha hizo zaidi ya Mikoa miwili tu Dodoma na Iringa. Hii inaonyesha wazi ni jinsi gani tulivyo na mipango mizuri lakini isiyoteklezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono bajeti hii, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini, naomba nipate maelezo ya kutosha, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya *LGTP* na *VTPP* zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHIRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pungezi kwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na viongozi wote wa Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi 2005 ya CCM.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pungezi kwa Waziri wa Fedha, Naibu wote wawili; Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa bajeti nzuri; bajeti ambayo inayomjali Mtanzania. Sitaki kusahau kwa hiyo, nasema naunga mkono hoja hii ya bajeti kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba nitoe yangu machache. Nashukuru kuona katika bajeti hii kilimo kimepewa kipaumbele. Mwananchi hasa Mtanzania kuishi kwake kunategemea kilimo, uwe mkulima au mfanyakazi, mambo yote yanaweza kungoja lakini sio kilimo. Namshukuru Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu walioona hili na kuamua kuwa kuwepo kipaumbele katika kilimo kwanza. Naamini kuwa kilimo kikiwa kwanza kwa vitendo wananchi/Watanzania hawatapata shida, mwananchi atapata chakula cha kutosha mwaka mzima, atauza ziada na pato la Mtanzania na la nchi kwa ujumla litapanda.

Mheshimiwa Spika, sote tunaamini na tunajua kuwa uchumi wa nchi umeyumba. Kwa kusema hivyo, nachukua nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake aliyoitoa kwa wazee wa Dodoma na Wabunge na hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha kwa kuwapanua Watanzania uelewa, kufahamu ni nini na ni wapi chanzo cha uchumi wa dunia kuyumba. Nchi yetu bahati nzuri inayo ardhi ya kutosha, kwa hiyo, tukiamini na kusema na kutia kwenye vitendo kilimo kwanza, uchumi wetu Watanzania utakuwa nafuu, hautayumba sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza sera ya nchi yetu hasa Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu kwa kupendekeza au kuipatia kipaumbele Mikoa sita kwa uzalishaji wa chakula. Mikoa hii ni Ruvuma, Morogoro, Rukwa, Kigoma, Mbeya na Iringa. Wakulima/wananchi wa Mikoa hii wameipokea kwa furaha sana na wako tayari kutekeleza agizo la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mbolea, wananchi ili wazalishe wanahitaji pembejeo, bajeti hii kwa kuwajali wakulima, tunashauri mbolea ifike kwa wakati. Maana yake kabla ya mwezi wa tisa kwa Mkoa wa Morogoro tunapata mvua mara mbili kwa mwaka. Kwa hiyo, mkulima hasa analima mara mbili kwa mwaka. Kwa Mkoa wa Ruvuma wako tayari kulima chakula cha kutosha ili mradi mbolea ifike kwa muda muafaka, kabla ya Septemba. Kilimo cha Ruvuma kwa kutegemea mvua ni mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mbegu bora zipatikane madukani kwa wakati wa kilimo, kila kitu kikipatikana kwa muda muafaka na kanuni bora za kilimo zikifuatwa, Morogoro na Ruvuma, Mikoa hii kweli itakuwa ghala la chakula. Ruzuku za pembejeo hizi hasa

mbolea ziongezeke kwani bado wakulima wanaona licha ya ruzuku bado mbolea ni ghali (*Mijingu phosphate na urea*) etc.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji maji, tunashukuru Serikali yetu, kwani kwa kupitia mpango *ASDP*, zipo fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya kilimo. Kwa hiyo, wananchi wakishauriwa, wataibua miradi ya umwagiliaji. Kufuatana na kubadilika kwa hali ya hewa, inabidi tujikite na kubadilika kwa hali ya hewa, inabidi tujikite sana kwa kilimo cha umwagiliaji. uvunaji wa maji utiliwe maanani. Kwa hiyo, nashauri Serikali, fedha katika miradi hii hasa chini ya *DADPS* ziwahi kupatikana kwa wakati. Kwa hiyo, kwa Mikoa inayotumia kilimo cha umwagiliaji, mbolea inabidi ipatikane wakati wowote. Mikoa ya Morogoro na Ruvuma wanatumia kilimo cha umwagiliaji na wakulima wakubwa ni wanawake tukichukua kuwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi kijiji na wanategemea kilimo nia zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, zana ya kilimo, natoa pongezi kwa Waziri Mkuu, kwa kutoa agizo kwa Wilaya/Halmashauri kuwa kila Halmashauri inunuwe trekta ndogo 50 *power tiller* kila mwaka kwa kuanzia na bajeti ya mwaka huu. Nashauri fedha hizi zitolewe mapema na matrektta yaagizwe mapema ili wananchi wanufaike na bajeti ya mwaka huu na watumie *tractor* hizi mwaka huu. Naamini kwa kufanya hivyo, kama hali ya hewa itakuwa nzuri, Mikoa mingi itazalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini na mijini, ili tuwe na maendeleo ni muhimu kupata umeme wa uhakika vijijini. Serikali inajitahidi kufikisha umeme vijijini lakini bado. Ili tuwe na viwanda vidogo na vikubwa vyakula ni lazima tuwe na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri jambo hili tulipe kipaumbele kwenye bajeti zetu. Mko wa Morogoro unazalisha matunda na mboga kwa wingi. Wakiptiwa umeme vijijini, usindikaji vijijini utakuwepo na tutaongeza ajira hasa kwa kina mama na watoto. Mko wa Ruvuma hata mjini kuna tatizo la umeme kwani Mko unatumia umeme wa jenereta, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na viongozi wengine wanayo habari na uzalishaji wake na hali ya umeme Mko huu uangaliwe kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Serikali yetu kwa kutoa/kuweka kipaumbele cha pekee kwa elimu. Kweli Serikali yetu inamjali mtoto wa ki-Tanzania. Shule za sekondari tunajenga kila kata sasa bajeti yetu na Wizara pia kwa kusaidiana na wananchi tutilie mkazo katika kujenga shule za kidato cha tano na sita. Kama ilivyoagizwa kila Wilaya kuwa na angalau sekondari moja au mbili, nashauri kuelekeza macho katika ujenzi wa maabara, fedha tuitumie vizuri na haraka katika kujenga maabara. Naamini Serikali imeishaanza kwa kupitia kwa Wizara husika lakini tuweke bidii, kwani watoto wanaomaliza kidato cha nne sasa, ni mchepuo wa *arts*.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuuu kwa sasa ni wengi ukilinganisha na miaka ya nyuma. Haya yote ni mafanikio mazuri ya

Serikali yetu, mikopo ichambuliwe vizuri, wapewe wahitaji kwa wakati kusudi wanafunzi wapate kuendelea na masomo yao bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, benki ya wakulima, hayo yote ni mambo mazuri yanayopangwa kutekelezwa kwa Serikali yetu, pamoj na uanzishwaji wa benki ya wanawake, haya yote ni mambo mazuri, nashauri benki hizi zianzishwe haraka, ili wananchi waweze kukopa na hasa wanawake.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ni muhimu kwa kuleta maendeleo, mawasiliano ya simu na radio ni muhimu sana. Katika Wilaya ya Tunduru na Namtumbo ni taabu sana kupata Radio Tanzania ni radio Malawi/Msumbiji zinaptikana kwa urahisi. Nashauri wananchi hawa wasaidiwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawaomba sana wanawake wa Mkoa wa Morogoro waweke bidii katika kilimo na tushirikiane kwa pamoja katika kuleta mapinduzi ya kilimo cha kijani, ghala la chakula na kuinua uchumi wa familia zetu.

Mheshimiwa Spika, narudia kumshukuru Waziri wa Fedha, Naibu wote wawili na watendaji wa Wizara, Mawaziri na wafanyakazi wa Serikali kwa bajeti nzuri ya trilion 9.5. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, natoa hongera nyingi kwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa kutuletea bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kilimo kwanza, kwa sasa mchango wa kilimo ni 25.7% lakini kilimo kinakua kwa 4.6% ingawaje wakulima wetu ni kati ya 70 – 80%. Kwa hiyo, kilimo ni muhimu kwa maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Rufiji ina ardhi yenye rutuba nyingi na maji mengi ya mto Rufiji basi Kamisheni ya Mipango ikubali kuiingiza Rufiji katika mpango mkubwa wa kilimo kwanza. Tunahitaji matrekti mengi, umwagiliaji mkubwa wa mashamba, mbegu bora, madawa na mbolea. Naomba kuwa mradi wa kilimo kwanza, uwafikie wakulima mmoja mmoja na kuhakikisha kuwa mikopo ya masharti nafuu inapatikana kwa sababu hawa *peasants* ndio wanaolisha taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mifugo, Kamisheni ya Mipango, ijaribu kuigawa nchi yetu katika *area za kilimo (agricultural land)* na *area ya mifugo (pastoral land)* ili ardhi ya kilimo isitumiwa kwa mifugo kwa vile kilimo kinachangia 25.7% kwenye pato la taifa lakini mifugo inachangia 4.7% kwenye pato la taifa. Kwa hiyo, ni muhimu kulinda ardhi ya kilimo isiharibiwe na kugeuzwa jangwa. Kilimo kwanza kinatupa chakula na vilevile kilimo kinatoa mazao ya biashara, naomba *Planning Commission* inusuru ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipange fedha zaidi katika kushughulikia janga la UKIMWI katika nchi yetu. Mpaka sasa zaidi ya 90% ya fedha ya kuhudumia janga la

UKIMWI, zinatoka kwa wafadhili – *Global Fund for HIV, TB and Malaria, CDC* ya *USAID, CLINTON FOUNDATION* na nchi zingine. Hatari ni kuwa, iko siku wafadhili watakataa kubeba mzigo wa kuhudumia UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, uvuvi, kule Rufiji, ndani ya Hifadhi ya *Selous* kuna mabwawa ya asili yaliyojaa samaki wengi. Hapo zamani kabla ya *operation* uhai, wananchi walikuwa wanapewa *permit* ya kuvua ndani ya *selous* kwa muda maalum, bwawa kwa bwawa kwa mzunguko kwa miezi maalum. Lakini sasa ruhusa hiyo haitolewi na kuna samaki wengi kule *selous* wakati wananchi wana matatizo ya njaa na umaskini. Naomba Serikali irudie utaratibu wa zamani wa kutoa *permit* kwa wananchi ili wakavue ili wajipatie riziki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania kwa bajeti iliyojaa matumaini na nia ya kukomboa Watanzania wengi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, msimamo ama mtazamo wa Serikali, umeonyesha kwa makusudi mema kabisa na ya kulenga zaidi ama kutoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo. Ni kweli tena ukweli usiopingika kwamba ajira kubwa ya Watanzania ipo kwenye sekta hii. Hata msimamo wa Mheshimiwa Rais wa kutaka makusanyo ya pesa za *EPA* yaelekezwe kwenye sekta hii, ni ushahidi tosha.

Mheshimiwa Spika, napendekeza yangu ya nyongeza na kuitaka Serikali hebu ione uwezekano na kuongeza ruzuku ama *subsidization* zaidi kwenye seta hii. Mbali ya mbolea Serikali ingezipa Serikali za Vijiji matrekta ya kulimia na ya kupandia kutegemea na aina ya mazao maana hii itaongeza ufanisi sana katika Taifa letu kuwa na kilimo bora. Hili ni pendekezo langu kwa bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995, wakati baba wa Taifa akihutubia Taifa kwenye Maazimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (*Mei Day*), aligusia umuhimu wa nchi yetu kufufua viwanda. Tamko hili lilitokana na umuhimu wa viwanda katika ukuzaji wa uchumi. Nchi zote zilizoendelea duniani zinazotegemea sana sekta hii kama muhimili wake, ziangalie nchi za G8 Marekani, Canada, Urusi, Japani, Italia, Uingereza, Ujeruman na Ufaransa, zote hizi zinategemea sana viwanda. Lakini China, nchi ambayo ilikuwa kwenye mfumo wa kikomunisti, ndio mfano mzuri sana wa kuigwa na nchi yetu, wengi wa wananchi wa China walikuwa maskini lakini kutokana na umakini wa kisera na usimamizi na utekelezaji wake, nchi hii imefaidika na kuwa tajiri mkubwa duniani. Leo hii watu kutoka nchi mbalimbali wanakwenda kununua bidhaa China.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali ipaswa kutambua hili kwa vitendo, tushirikiane na wawekezaji kutoka ndani na nje na kuhakikisha kuna ruzuku (*subsides*) kutoka Serikalini. Ufufuaji na uanzishaji wa viwanda, ni njia kubwa ya kututoa hapa tulipo. *Export/Market/Soko* la nje ni muhimu sana katika kukuza pato la taifa. Fedha za kigeni *foreign currency* zitapatikana kwa wingi zaidi ya iliyo sasa na soko la ajira (*labour*

*market)* litakua. Naelewa kuwa Serikali kwa bajeti hii haikujipanga kwa utekelezaji, ninaopendekeza hapa lakini kwa bajeti ya mwakani tukianza na sera hii, basi tutapiga hatua kubwa sana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni utengaji wa fedha kwa sekta ya ulinzi, hapa naongelea Wapiganaji ama Askari wetu. Siku zote tumekuwa tukitoa kipaumbele kwenye vifaa ama silaha katika upangaji wa bajeti. Askari wetu bado wanaendelea kuishi kwa taabu sana wanapokuwa wamestaafu, hasa wale wa vyeo vya chini. Tukumbuke kuwa Askari hawa akili zao zote hazijui maisha mengine zaidi ya yale ya Uaskari. Hii inapelekea kuwapa taabu sana wanapostaafu. Naiomba Serikali ifanye mambo mawili.

Kwanza, walipwe kwa mwezi viwango ambavyo vimebadilika kwa kuendana na upandaji wa ghamama za maisha. Kila bajeti ya Wizara ya Ulinzi izingatie hili, Askari anayeishi katika dhiki, kwa kweli ni sana na *time bomb*. Kuna uwezekano na ushahidi umeonyesha jinsi baadhi ya Askari wastaafu wa vyeo vya chini walivyojihusisha na vitendo vya kiujambazi. Pili, iko haja ya kutatua tatizo tajwa hapo juu kwa kufikiria nje ya utaratibu wa kigeni kwa kuuongeza umri wao wa kustaafu. Wengi wanastaafu wakiwa na nguvu za kutosha, hii itasaidia kutatua tatizo la hapo juu.

Mheshimiwa Spika, nitafikiria juu ya kuunga mkono bajeti hii baada ya kusikiliza upitishaji wa vifungu.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara husika kwa kuandaa hotuba vizuri na kutuwezesha kuijadili kwa kina kwa lengo la kurekebisha upungufu mbalimbali uliojitekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla sura ya bajeti ni nzuri ila napenda kupata ufanuzi kwa maeneo yafuatayo. Ukurasa wa 20 kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi kama sera imefanikiwa kidogo kwa vile suala la kutumia mashamba ya wananchi wa vijiji ili yawe dhamana ya kuombea mikopo, nina wasiwasi kama taasisi za kifedha zinakubaliana na hati hizo. Bado wananchi wanahangaishwa sana na vyombo vya fedha hasa wananchi wanyonge ambaa ndiyo wengi kinyume kabisa na lengo la sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kuanzisha mifuko ya vijana wanawake wa TASAF lakini kwa masikitiko makubwa, Halmashauri nyingi hazifanyi jithada zozote kuhamasisha watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi ili waweze kukidhi vigezo vya kuweza kukopesha kama wananchi wengine wanavyofaidika na mifuko hiyo. Kwa msingi huo, nashauri Wizara na msimamizi wa fedha hizo itoe mwongozo wa jinsi ya kuhusisha vikundi vya wajasiliamali wenye ulemavu kikamilifu, (Uk. 23).

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuchukua hatua mbalimbali za kulinda ajira, suala hili linanifaraji kwa sababu kwa sasa viwanda muhimu vilivyobinafsishwa, bado havifanyi kazi kama *general tyre* na kadhalika kiasi kwamba waajiriwa wengi mpaka sasa hawana ajira.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 35 – 40 Serikali, imetoa matumaini ya kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania, lakini wasiwasi wangu ni kwamba utekelezaji wa malengo hayo yote utafikia viwango katika hali ya kutegemea fedha za miradi ya maendeleo kutoka kwa wafadhili zaidi kuliko fedha za ndani. Nashauri tuwe na utaratibu wa kutenga fedha za ndani kidogo kidogo ili hatimaye kuweza kugharamia miradi yetu kadhaa.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 52, kuhusu kuondolewa msamaha maalum wa kodi ya VAT kwa mashirika mbalimbali yakiwemo ya kidini, kwa vile kumekuwa na malalamiko mengi tangu bajeti ilipowasilishwa, yafaa Serikali itoe ufanuzi wa kuwaelewesha wananchi juu ya vipengele vilivyofutiwa kodi hizi ili huu mkanganyiko uliotokea uondoche kwa wanasiasa ambao wanajitafutia umaarufu tu usio na tija. Ni kweli kuna taasisi kadhaa ambazo zimetumia misamaha hii isivyo kwa faida yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza kuwa iko kwenye mchakato wa kuandaa MKUKUTA II, rai yangu ni kuwa nakumbusha umuhimu wa kuwahuishisha na kuwashirikisha kwa dhati jamii ya wenyewe ulemavu ili nao watoe mchango katika mchakato huu. Nakumbusha hivyo kwa sababu katika MKUKUTA I, kundi hili la jamii lilijumuishwajumuishwa tu bila kulishughulikiwa kwa undani tena kipekee kwa vile linaishi ndani ya umaskini uliokithiri na changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa upande wa Serikali Wizara ya Fedha tutaanza na Manaibu Mawaziri ambapo kila mmoja ana haki ya robo saa, dakika 15. Naanza na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nitoe shukrani zangu za dhati, kwa michango ambayo tumeipokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Pili, napenda niunge mkono hoja ambazo ziliwasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, siku ya alhamisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba Serikali hii ni sikivu na ndio maana muda wote tumekuwa makini sana kusikiliza hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge na ni jana tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameamua kufuta kodi kwa Taasisi za Dini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijachambua hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa muhtasari, nitoe maelezo nini maana ya bajeti. Bajeti sio mapato na matumizi tu bali ni mchakato wa kuibua vipaumbele na hatimaye kuvipatia fedha vipaumbele hivyo ili viweze kuwa vichocheo vya ukuaji wa uchumi na maisha bora ya Mtanzania. Kutokana na *definition* hiyo, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwamba na wao wameshiriki kikamilifu katika mchakato huu. Nchi ni yetu sote na bajeti

ni yetu sote Kwa hiyo, nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge sasa muipe nafasi Serikali, msikilize majibu ya hoja ambazo mmetupa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika hoja zifuatazo. Hoja ya kwanza ambayo imeulizwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni kwa nini mapato yetu hayajafikia malengo wakati uchumi umekua kwa asilimia 7.4. Nataka niseme tu kwamba wakati Mheshimiwa Waziri Mkulo akiwasilisha hali ya uchumi ya mwaka 2008, ukurasa wa 42, alieleza katika ripoti ile kwamba uchumi utakua kwa asilimia 7.8. Ile *base* tulioikadiria ilikuwa ni kubwa ya asilimia 7.8 baadaye uchumi ukakua kwa asilimia 7.4 kutokana na misukosuko hii iliyotokea, hali hii imesababisha vile vile mapato yetu kupungua kwa asilimia 10. Lakini hata hivyo, mapato yetu yamepungua kutokana na makisio ambayo sisi tumeyaweka. Lakini ukilinganisha na mapato ya mwaka jana na mwaka huu tunaomalizia, utaona kwamba mapato yetu yameongezeka kwa asilimia 23.

Mheshimiwa Spika, vile vile kama hiyo haitoshi, Pato la Taifa, mara zote linakuwa *computed* katika kipindi cha mwaka tunaita kwa Kiingereza *Calendar Year* yaani kuanzia Januari mpaka Desemba lakini mapato yetu tunayakusanya kwa kutumia *Fiscal Year* kuanzia Julai mpaka Juni. Kwa hiyo, mtikisiko wa uchumi umeanza kutuathiri zaidi katika *quarter* ya kwanza ya mwaka huu kuliko hata *quarter* ya mwisho ya mwaka jana. Kwa hivyo, hii nayo ndiyo iliyosababisha vile vile mapato yetu kuweza kushuka kwa asilimia 10. Hoja hii imeulizwa na wachangiaji wengi lakini nimenukuu baadhi yao Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa, Mheshimiwa Mwanne Mcemba na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imeulizwa na Waheshimiwa Wabunge, ni suala zima ambalo wameitaka Serikali isimamie na idhibiti mfumuko wa bei usiongezeke. Hapa nataka niseme tu kifupi ni kwamba mfumuko wa bei Tanzania unachangiwa zaidi na chakula kwa asilimia 55.9. Kwa hiyo, tuna tatizo la uzalishaji mdogo. Vile vile, gharama za usafirishaji na usafiri, nazo zimeonekana kuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kudhibiti mfumuko wa bei, kuna haja kubwa ya kuzalisha zaidi na hapa nataka niseme ndiyo ile azma ya Serikali ya kusema kilimo kwanza. Tukifanikiwa katika kilimo kwanza na sina wasiwasi kwa nini tusifanikiwe, tutafikia hatua ya kupunguza mfumko wa bei kwa kiwango kikubwa sana hasa tukizingatia kwamba asilimia 55.9 ya mfumko wetu wa bei unachangiwa na chakula. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na kaka yangu, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge walitutaka tutoe ufanuzi, ni suala la kwa nini umaskini haupungui kwa kasi na wengine waliongezea zaidi wakasema MKUKUTA toka umeanzishwa haujafikia malengo. Nataka niseme kwamba MKUKUTA toka tumeuanzisha, huu ni mwaka wa nne na kupungua kwa umaskini *it is a process*. Lazima umaskini wetu upungue kidogo kidogo na hatimaye utafikia mahali sisi sote kwa umoja wetu, tataridhika kwamba umaskini umeweza kupungua. Lakini nataka nieleze tu kwamba sehemu kubwa ya Watanzania

wanategemea kilimo. Kama nilivyoeleza wiki iliyopita kwamba kilimo chetu ni cha kutegemea jembe la mkono. Kama sehemu kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo na kilimo chetu ni cha kutegemea jembe la mkono, ni dhahiri kwamba lazima tuwe na mapinduzi katika kilimo ili tuweze kupunguza umaskini kwa kasi kubwa zaidi. Nataka nieleze tu kwamba ushiriki wa sekta binafsi hasa katika kilimo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka nioanishe mtazamo huo wa umaskini na hali halisi ya utamaduni wetu. Watanzania lazima tujitume kama tunataka tuongeze kasi ya kupunguza umaskini. Lakini vile vile, nataka niseme kwamba Wachina wamefikia hapa walipofikia leo kwa sera yao ya “*one child policy*”. Leo Watanzania tunazungumzia familia zetu kwa wastani wa watu watano. Utakapozungumzia wastani wa watu watano lazima umaskini utashuka taratibu. Tuiangalie hii Serikali haiwezi ikakupangia watoto wangapi lakini tunasisitiza mpango katika familia kwa sababu tunachokihitaji sote tunataka *quality children not quantity*. Tukifikia hatua hii, tukajiangalia ndani ya familia zetu, umaskini utashuka kwa haraka sana. Leo Wachina katika ile sera yao, wanazungumzia kwamba hakuna kaka, hakuna dada, hakuna mjomba, hakuna *aunt* kwa sababu umezaliwa peke yako. Una babu, bibi, mama, baba na mtoto, lakini sisi hatusemi tufikie huko lakini Watanzania tuweze kuiangalia hali hiyo vile vile.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninapenda nilizungumzie, ni hili kilimo kwanza. Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wanataka kuelewa maana ya kilimo kwanza na kwamba hakuna *reflection* katika bajeti. Nataka niseme tu kwamba katika bajeti hii, kilimo tunesema kwanza na kina *reflection* ndani ya bajeti. Nitoe takwimu sahihi kabisa ambazo ziko kwenye bajeti. Bajeti ya Serikali, katika vitabu vyetu inaonekana ni shilingi 666.944 bilioni lakini vile vile katika mpango ambao ameutangaza Mheshimiwa Rais kuna fedha za dhamana ambazo Serikali inabidi ichukue dhamana ni shilingi bilioni 398.6 kwa ajili ya kudhamini mikopo ya kilimo, riba nafuu pamoja na dhamana za *TFC* katika mbolea ya Minjingu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna mkopo ambao tunautarajia kutoka India wa shilingi bilioni 54.36 ukijumlisha zote hizi una trilioni 1.119 sawa na asilimia 13.24. Kwa mtazamo huu, tumezidi hata lile lengo lililowekwa na *SADC* la asilimia 10 katika bajeti yetu. Kwa hivyo, nataka niseme kwamba hoja ile ni ya msingi na ni dhahiri kwamba Wabunge wanataka kufahamu lakini Serikali iliposema kilimo kwanza, ilimaanisha kilimo kwanza na fedha hizi zipo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge walitaka kuelewa, ni suala la kupanua wigo ikiwa ni pamoja na kujumuisha sekta isiyo rasmi. Nasema wazo ni zuri na *TRA* kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, wameshaanza kulifanyia kazi. Aidha, azma za Halmashauri nyingi ikiwemo Halmashauri ya Ilala ya kujenga majengo kwa ajili ya wafanyakishara wadogo wadogo, azma ile inamwondoa kutoka *informal sector* kumpeleka kwenye *formal sector* nayo vile vile itasaidia katika kuendeleza kodi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge walitaka kulielewa ni suala la kuchangia gharama na kugawana mapato ya Muungano. Nataka niseme Serikali zote mbili kupitia wataalamu wao, tayari wameshazipitia zile ripoti kutoka *Joint*

*Finance Commission*, kinachosubiriwa sasa hivi ni Mabaraza ya Mawaziri kuweza kutoa maamuzi yao. Tunategemea katika kipindi kifupi, maamuzi yatatoka na tutapata maelekezo kutoka kwa viongozi hawa vipi mgawanyo baina ya Serikali hizi mbili uende na vipi tutachangia katika zile gharama za Muungano.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni lile ambalo Waheshimiwa Wabunge walitaka nalo ni ZRB (*Zanzibar Revenue Board*) kuwa na mjumbe katika Bodi ya *Tanzania Revenue*. Ushauri sio mbaya kwa kuwa unahitaji kupelekwa katika Bodi ya *TRA*. Sisi Wizara ya Fedha tumeuchukua ushauri huo na tutauwasilisha na tuna imani kubwa sana kwamba ushauri wetu huu ambaeo mmeutoa unaweza ukazaa matunda na hatimaye ikawa ni faraja kwa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka niseme kwamba mafunzo kwa ajili ndugu zetu wa *Zanzibar Revenue Board*, kwa kweli wana ushirikiano mzuri sana baina yao na *Tanzania Revenue Board* na wameshafanya mafunzo kwa pamoja na tutawasisitiza kwamba waendelee kufanya mafunzo ili kuwashirikisha ndugu zetu wa *Zanzibar Revenue Board* kwa faida na manufaa ya Taasisi zetu mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nasema tena naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja mbili za Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, alizowasilisha hapa Bungeni tarehe 11 Juni, 2009 na nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja zote mbili.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake ya kihistoria aliyoitoa alipowahutubia wazee wa Mkoa wa Dodoma na wananchi, tarehe 10 Juni, 2009. Ninampongeza sana Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na Wanakamati wenyewe kiujumla. Nampongeza sana Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa maoni yake. Maoni ya Upinzani yalikuwa mazuri na bila shaka, yatatusaidia wakati ujao, wakati tunapojiandaa tena kuandaa makisio ya Serikali. Nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwenye hoja zote mbili, waliozungumza hapa Bungeni na wale ambaeo waliochangia kwa maandishi na ninawaomba kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi atawatambua basi mimi nisifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza inayohusu uamuzi wa Serikali wa kukopa fedha za ndani ili kufidia pengo la bajeti, ichukuliwe kwa uangalifu ili kuhakikisha kuwa hatua hiyo haitawafanya wale walio kwenye sekta binafsi kutoweza kupata mikopo kutoka kwenye Mabenki na kama ikitokea hivyo, basi itachochea viwango vya riba kuongezeka na mfumko wa bei kuwepo. Nakubaliana na rai kwamba kama tusipokuwa waangalifu, ni kweli inaweza kutokea hivyo lakini niseme kwamba uamuzi wa Serikali wa kukopa fedha za ndani, ni moja tu ya jitihada za kukwamua uchumi wa taifa na

kuwezesha kuendelea kukua. Hata hivyo, uamuzi huo utafanywa kwa makini kuhakikisha hautoi nje sekta hiyo ya binafsi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha azma hii, kiasi kikubwa zaidi kitakuwa ni mkopo kutoka Benki Kuu. Jumla ya shilingi bilioni 506 tunatarajia kukopa katika mwaka 2009/2010, shilingi bilioni 300 ambazo tunatarajia ndizo tutakopa kutoka Benki Kuu na zilizosalia bilioni 206 kutoka kwenye masoko ya fedha. Kwa hiyo, kiwango hiki cha mikopo ya ndani kinawiana na Sera za Fedha ambazo zinalenga na mambo mengine kuwa na ongezeko la kiwango cha mikopo kwa sekta binafsi cha asilimia 28.7 na kiwango cha chini na tulivu cha mfumuko wa bei cha asilimia isiyozidi 10 ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, lakini ninapenda kusisitiza hapa kuwa kumekuwa na uoanishaji mzuri kati ya Sera za Fedha na Sera za Kodi na matumizi ya Serikali (*Monetary Reports na Fiscal Policy*) kwa kiasi ambacho tunaamini kwa pamoja basi malengo ambayo yanakusudiwa ya Kitaifa kwenye uchumi yatapatikana. Niseme kwamba Serikali na Benki Kuu katika kipindi hiki cha msukosuko wa fedha na uchumi duniani, itachukua hatua zisizo za kawaida za kuongeza ukwasi katika uchumi ikiwa ni pamoja na Serikali kukopa toka Benki Kuu na soko la wazi la mitaji ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, labda niseme kidogo kwamba kule nyuma imesikika kwamba Serikali haitakopa kwenye vyombo vya fedha haswa Benki za Biashara kwa kuogopa kwamba kufanya hivyo basi uwezo wa Benki zile utapungua na kwa hiyo hawatakuwa na fedha za kuelekeza kwenye sekta binafsi kwa ajili ya viwanda. Hapa tunasema kwamba tutakopa kutoka Benki Kuu na ukifikiria kwa haraka haraka naweza kudhani kwamba kwa hiyo tutakachokuwa tunafanya ni kuongeza ujazi wa fedha kwenye uchumi na kwa hiyo utaongeza mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili hapa, la kwanza ni kwanza mfumuko wetu wa bei una sehemu mbili na sehemu iliyo kubwa ni ile ambayo inahusu chakula. Kama tulivyosikia Naibu Waziri mwenzangu alivyosema kwamba ukichukua uzito wa chakula kwenye lile kapu la kukokotoa kiwango cha kasi ya mfumuko wa bei cha asilimia 55.90 ukaongezea pale uzito wa nishati na maji ambaa ni asilimia 8.5 halafu ukaongezea mafuta kwa ajili ya usafirishaji ambaa ni asilimia 9.7 basi unapata uzito wa jumla ambaa moja kwa moja unakwenda kwenye gharama za chakula kwa asilimia 74.10. Maana yake ni kwamba sera za fedha zina sehemu ndogo katika ule mfumuko wa bei. Kwa mfano, ujazi wa fedha kwenye uchumi, kwa mfano uuzaji wa fedha za kigeni kwenye soko la fedha za kigeni (*Inter Bank Exchange Markets*) na yale mambo mengine ambayo Benki Kuu inaweza kufanya ili kudhibiti mfumuko wa bei, inajielekeza kwenye asilimia 25.9 kwamba asilimia 74.4 ni kutokana na chakula. Kwa hiyo, kwa sisi kukopa kutoka Benki Kuu hatuoni kwamba kutapelekea kuongezeka kwa mfumuko wa bei ili mradi vilevile ajenda yetu ya kilimo kwanza itakwenda kama ambavyo tumepanga na tunaamini kwamba itakwenda hivyo. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kiasi cha mkopo huu cha bilioni 506 kutoka Benki Kuu na kutoka kwenye soko la wazi ni takriban asilimia 30 ya pato la Taifa na ni

asilimia ndogo sana ukilinganisha na nchi nyingine ambazo zenyewe kasi ya kukua kwa uchumi ni kubwa kuliko sisi. Kwa mfano Canada, deni la Taifa kwa pato la Taifa ni karibu asilimia 70, Japan wanaelekea kwenye asilimia 200, Uingereza karibu asilimia 47, Marekani wenyewe asilimia 62. Kwa hiyo, hakuna sababu kwa kweli ya kuogopa kukopa kwenye soko ili mradi tulichokopa kitaelekezwa kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili inahusu Tanzania kuweza kukusanya mapato ya asilimia 20 - 25 ya pato ya Taifa na kwamba kama tukifanya hivyo misamaha ya kodi ambayo imewekwa kisheria, itapungua kwa asilimia 50. Mapato ya Serikali yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, mapato ya Serikali yalikuwa ni asilimia 15.9 ya mapato ya pato ya Taifa na mwaka 2009/2010 tunategemea yatakuwa ni asilimia 16.4. Misamaha ya kodi ni asilimia 3.5 ya pato la Taifa. Kama misamaha ingepungua kwa asilimia 50 basi tunakiri kwamba mapato ya Serikali yangefikia asilimia 17.6 ya pato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kwamba kupunguza misamaha ya kodi kunaweza kuongeza mapato. Katika kutekeleza azma hii ya kuongeza mapato ya Serikali, Serikali imekua ikifanya mapitio ya misamaha yake mwaka hadi mwaka ili kuhakikisha inabakiza vivutio muhimu tu. Aidha, Serikali inatia mkazo katika kudhiti namna ya matumizi ya misamaha inayotolewa kwa kuzingatia umuhimu wa misamaha ya kodi katika kuvutia wawekezaji. Kuwezesha utoaji wa huduma za kijamii na kutekeleza sera mbalimbali za kitaifa baadhi ya misamaha itaendelea kubaki. Hata hivyo, zoezi la kuipitia misamaha hiyo utafanywa mara kwa mara ili kubaini kama bado inahitajika au la.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu utaratibu wa utoaji fedha kwa kutumia *cash budget* ambao unadaiwa kwamba unadhoofisha sana nidhamu ya bajeti na mara nyingi miradi ya maendeleo inaathirika sana na utaratibu huu kwani za mwanzo kupunguzwa ni matumizi ya miradi ya maendeleo. Naomba niseme kwamba chimbuko la utaratibu huu wa *cash budget* uliana pale ilipobainika kwamba nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali ilikuwa imeshuka sana na utaratibu huu kwa kiasi kikubwa umesaidia sana kurekebisha hali hii. Chini ya utaratibu huu, fedha za matumizi hutolewa kila mwezi kulingana na mapato na vilevile kwa kuzingatia mipango kazi ya Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Kwa upande mwingine, fedha za maendeleo vigezo muhimu vya ziada vinavyotumika katika utoaji wa fedha ni pamoja na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi husika pamoja na hati za madai ya malipo kuhusiana na miradi hiyo. Kwa kuwa mara nyingi miradi hii ya maendeleo inategemea misaada, misaada ikichelewa kupokelewa, ni dhahiri kwamba na malipo kwa ajili ya miradi yenyewe itachelewa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo napenda kuizungumzia, katika mpango wa kunusuru uchumi, Serikali ililieleza Bunge lako kwamba riba nafuu ni kiasi gani na hili kama tunavyokumbuka ilitajwa na Mheshimiwa Rais. Serikali katika mkakati wa kunusuru uchumi, imepanga kutoa mitaji ya uendeshaji kwa riba nafuu. Mpango huu utatoa mikopo nafuu kwa mabenki ambayo yatakopesha yenye shughuli zilizokumbwa na msukosuko na hivyo kushindwa kuhimili masharti ya soko na mikopo. Kwa kila shilingi moja itakayotolewa na Serikali, Benki shiriki zitatoa shilingi 1.5. Mikopo hiyo itatolewa

kwa Benki shiriki kupitia Benki Kuu kwa riba ya asilimia 2. Benki shiriki zitatakiwa kutoa mikopo kwa wakopaji walioathirika na msukosuko kwa riba isiyozidi kiwango watakachokubaliana na Serikali. Kwa hiyo, kinachosemekana ni kwamba hatimaye kile kiwango cha riba ambacho kitatozwa, kitakuwa chini ya kiwango cha riba kwenye soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine, niunge mkono hoja hii. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, kwa Naibu Spika na pia Wenyeviti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiko, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtipura, kwa jinsi mlivyosimamia na kuongoza Bunge wakati wa majadiliano ya hoja za Serikali nilizozitoa tarehe 11 mwezi huu hadi kufikia leo, kuhusu taarifa ya hali ya uchumi pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

Aidha, nawashukuru kipekee Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuwasilisha kwa ufasaha maoni ya Kamati yake. Vilele namshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo katika masuala ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, kwa maoni na ushauri wao juu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru wote waliochangia kwa njia mbalimbali wakiwemo wale waliota maoni yao kwa kuzungumza hapa Bunge, waliota maoni yao kwa maandishi na waliota maoni nje ya ukumbi huu, kwa michango yao mizuri ambayo itasaidia katika kusimamia utekelezaji wa bajeti hii na katika kuandaa bajeti ya miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, napenda niwataje Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Naanza na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoma, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Willibroad P.Slaa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Lukas L. Selelili, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Mheshimiwa Suleiman H. Saddiq, Mheshimiwa Ahmed A. Salum, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Omari S. Kwaangw', Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Fred T. Mpandazoe, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Zubeir A. Maulid, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Khadija S. Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Mohamed H. Mnyaa, Mheshimiwa Joyce M. Machimu, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa

Archt. Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Susan J. Lyimo, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Kilonsti Mpologomyi, Mheshimiwa Dora H. Mushi, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma na Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Salum Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Salum H. Khamis, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Ludovick Mwananza, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Wilson M. Massilingi, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri na wa mwisho kwa kuzungumza hapa ni Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Naibu Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Wabunge wafuatao walichangia, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Frolence Kyendesya, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Yono S. Kevela na Mheshimiwa Castor Ligalama. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Kanali Feteh Mgeni, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Steven Galinoma, Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Christine Ishengoma. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Eliatta Switi, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Alyoce Kimaro, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika,

Mheshimiwa Luka Siyame, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Riziki Juma, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda na Mheshimiwa Charles Keenja. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi walikuwa mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze, maoni, ushauri na maelezo yaliyotolewa na Kamati, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, yatasaidia sana utekelezaji bora wa bajeti ya mwakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, aliyewasilisha bajeti yake mbadala hapa Bungeni. Napenda kumhakikishia kuwa Serikali itaifanyia kazi bajeti hiyo na mapendekezo yake na kubaini yale yanayotekelvezka, nawashukuruni wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo, zipo baadhi ya hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani, Kamati na Waheshimiwa Wabunge ambazo ni muhimu nikazitolea maelezo ili tuweze kwenda pamoja. Nashukuru kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Jeremiah Sumari, wameweza kuchangia katika hoja kadhaa, naomba nijibu hoja hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwanza kueleza hoja zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha, Mheshimiwa Abdallah Kigoda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilihusu Serikali pamoja na Benki Kuu ziandae mazingira ya kuyawezesha mabenki kuwa na vyanzo nafuu vya fedha. Aidha iharakishe utaratibu wa kuwa na *Credit Reference Bureau* ili kupima hali ya wakopaji kutokana na viwango vyao vya hali ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vikuu vya fedha ni viwili, navyo ni mtaji unaotolewa na wawekezaji au wamiliki wa mabenki hao na amana. Chanzo kingine, ni faida wanayoipata kutoka kwenye biashara yao. Chanzo chenyeh gherama sana hapa, ni *deposits* kwa sababu Mabenki yanalamika kulipia riba, hii haipangwi na Serikali wala Benki Kuu bali soko la fedha ndilo linalopanga. Hata hivyo, nataka niwahakikishie

Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa riba zinazotolewa na soko ni nafuu na zinaendana na hali halisi ya fedha ili kuhakikisha kuwa riba ya masoko ni nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuanzisha *Credit Reference Bureau*, Benki Kuu imeshakamilisha miongozo ya kuandikisha au kutoa leseni na kusimamia *Credit Reference Bureau* hapa nchini. Miongozo hiyo inapitiwa na Wanasheria ili kuhakiki ubora wake kisheria kabla hajatolewa katika gazeti la Serikali. Aidha mchakato wa kuanzisha *Credit Reference Bank*, umefikia hatua nzuri. Sasa hivi Benki inamtafuta mshauri wa muda mrefu ambaye atasaidia kuweka mifumo ya kompyuta na kujenga uwezo wa kuiendesha *data bank* hiyo. Baada ya hatua hizo, sekta binafsi itakaribishwa kuleta maombi ya kuanzisha na kuendesha vyombo vya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihuhi Serikali iweke kipaumbele katika kusukuma utekelezaji wa maeneo yafuatayo, mikopo ya makazi, mikopo ya karadha, mageuzi katika mifuko ya pensheni na uboreshaji wa *microfinance*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ikishirikiana na Benki Kuu chini ya *Financial Sector Support Program*, imeandaa na kupitisha mwongozo wa mikopo ya makazi ya mwaka 2009 ambao ulianza kutumika rasmi tarehe 1/5/2009. Wizara sasa inaandaa mkakati wa kutoa mafunzo yaani *public awareness* kwa wadau mbalimbali ili ueleweke na kuanza kutumika ipasavyo na mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuchochaea utekelezaji wa mageuzi katika mifuko ya pensheni, Benki kuu imeshaandaa *draft investment guidelines* ambazo zipo katika hatua ya kuangaliwa na mshauri mwelekezi wa mambo ya pensheni. Miungozo ya kusimamia pensheni, itatolewa baada ya kuundwa kitengo cha usimamizi wa mifuko ya pensheni kazi ambayo inafanywa na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana. Harakati za kuanzisha kitengo hicho, zimefikia hatua nzuri kwani Wizara imeshatangaza magazetini ikitafuta wataalam watakaoendesha kitengo hicho. Taarifa kamili itatolewa na Wizara husika itakapowasilisha bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha *microfinance*, Benki Kuu kwa kushirikiana na *Financial Sector Deepening Trust*, inafanya utafiti ili kubaini matatizo yanayozuia matumizi ya huduma mbalimbali za kifedha nchini. Taarifa ya utafiti huu itatolewa kwa umma mwishoni mwa mwaka 2009. Benki Kuu pia inaandaa miongozo itakayowezesha uandikishaji, utoaji leseni na usimamizi wa asasi zinazotoa mikopo tu nchini. *Microfinance Regulatory Framework* ipo tayari na Benki Kuu ipo katika zoezi la kuwahamasisha wadau juu ya taratibu hizo na tayari kongamano moja lililohudhuriwa na *SACCOS* mbalimbali lilihafanyika.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma ya kifedha, Serikali imeandaa mkakati wa kitaifa wa kuboresha huduma hizi chini ya *National Rural Financial Services Strategy*. Mkakati huu, unahusisha Tanzania Bara na Visiwani na unalenga maeneo makuu mawili. La kwanza, kuongeza kasi ya kuwepo kwa taasisi za fedha zilizo na ufanisi na endelevu kwa wakazi wa kijiji na ya pili kujenga uwezo wa kiufundi na

usimamizi wa kifedha na kiutawala wa taasisi za kifedha zinazohudumia maeneo ya vijijini. Mkakati pia unalenga kutatua matatizo ya huduma ya fedha vijijini katika pande mbili yaani upande wa utoaji huduma na upande wa utumiaji na upokeaji huduma. Kutokana na umuhimu wa *SACCOS* katika kutoa huduma ya kifedha vijijini, ndani ya mkakati huu wa kitaifa, kuna mkakati mdogo wa *SACCOS* utakaosaidia kuboresha huduma za asasi hizo nchini. Pia Benki Kuu chini ya mpango wa *Financial Sector Support Program*, imeandaa mpango kabambe wa kutoa elimu itakayowawezesha wananchi wa kada zote kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya kifedha na utumiaji mzuri wa huduma za kifedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliulizwa, je, Serikali ina uhakika gani mikopo inayofidiwa kwa vyama vya ushirika na makampuni yaliyonunua mazao kwa wakulima ilitumiwa vizuri? Je, wakulima waliopata hasara na athari kutokana na mtikisiko wa uchumi watafidiwa? Jibu ni kwamba uamuvi wa Serikali wa kufidia vyama vya ushirika na makampuni yaliyonunua mazao kwa wakulima na kuyauza kwa hasara, una nia ya kusaidia vyama au makampuni hayo ili yaendelee kununua mazao ya wakulima msimu ujao. Uamuvi huo, utatekelezwa kwa makini na fidia itatolewa pale tu ambapo uhakiki umefanyika na kuonyesha bayana mikopo hiyo ilitumika vizuri na pia hasara iliyopatikana ni ya kweli na ilitokana na msukosuko wa kiuchumi duniani na si vinginevyo. Hivyo napenda kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge kuwa uamuvi wa Serikali wa kufidia hasara hiyo, hauna kasoro yoyote na utekelezaji wake utafanyika kwa umakini mkubwa.

Aidha, napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa, takwimu tulizonazo, hazonyeshi kuwa kuna mkulima yoyote aliyepeata hasara msimu uliopita. Wakulima walifanikiwa kuyauza mazao yao kwa bei nzuri kabla ya athari ya msukosuko hazijawa bayana. Kwa hiyo, kwa msimu uliopita, vyama vya ushirika na makampuni yaliyokuwa yamenunua mazao ya wakulima, ndiyo yalikuwa yakipata hasara kwa sababu taarifa za msukosuko zilijitokeza baada ya kununua mazao kutoka kwa wakulima. Vyama hivi na makampuni haya, aidha ilibidi wayauze mazao hayo kwa hasara au washindwe kuyauza kabisa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni fedha za mkopo kutoka India hazionekani kwenye bajeti. Aidha shilingi bilioni 20 kwa Hifadhi ya Chakula ya Taifa, hazikutengwa kwenye bajeti. Sehemu ya swali hili, lilijiwi na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini napenda niseme kwamba ni kweli fedha kiasi cha shilingi 54.36 bilioni ambazo ni mkopo kutoka India kwa ajili ya ununuzi wa matrekta hazionekani kwenye bajeti. Hii ni kwa sababu taratibu za kupata mkopo huo hazijakamilika na zikikamilika, Serikali itawasilisha Bungeni Muswada wa Matumizi ya Ziada kwa mwaka 2009/2010. Hii ni njia ya kawaida tunapofika wakati hatujathibitisha kwamba pesa hizo zimepatikana hatuweki kwenye bajeti mpaka hapo zitakapopatikana ili tusije tukajipa matumaini, fedha zisipopatikana, matumizi yatakosa chanzo cha pesa.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi bilioni 19.6 kwa ajili ya hifadhi ya chakula zimetengwa kwenye Fungu 43, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kifungu 5001 yaani Hifadhi ya Chakula.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliuliza hatua ya Benki Kuu kukopesha mabenki shilingi bilioni 270 na kisha kutoa *T-Bills* kiasi cha bilioni 205 si ya kuziwezesha benki hizo kutumia fedha hizo kufanya biashara na Serikali?

Mheshimiwa Spika, Kikosi Kazi kilichofanya kazi ya kuchambua athari za msukosuko wa fedha na uchumi duniani, kilitoa mapendekezo matano yanayohitaji kutengewa fedha. Mapendekezo hayo ni haya yafuatayo:-

- (i) Kufidia hasara waliyopata wanunuvi wa mazao msimu wa 2008/2009 yenye jumla ya shilingi bilioni 21.9
- (ii) Kuto udhamini wa kuahirisha mikopo ya waathirika yenye jumla ya shilingi bilioni 270.6.
- (iii) Kutoa mitaji ya uendeshaji (*Working Capital*) kwa riba nafuu itakayokuwa na jumla ya shilingi bilioni 80.
- (iv) Kuboresha mikopo ya dhamana ambayo itakuwa na jumla ya shilingi bilioni 350.
- (v) Kupunguza gharama za vito vya thamani, kuahirisha ulipaji wa mrabaha (*royalty*) ya 2009/2010 hadi 2010/2013.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo hayo, hakuna pendekezo la kuzikopesha benki shilingi bilioni 270. Pendekezo la pili, linaongelea kuwa Serikali itoe udhamini (*guarantee*) na siyo pesa taslimu shilingi bilioni 270.6. Ileweke kuwa dhamana haitatumika kufidia hasara ya mikopo itakayoahirishwa malipo yake (*re-scheduling*) mpaka uhakiki wa kutosha ufanywe na wataalamu. Kwa hiyo, mabenki hayataweza kutumia nyaraka za udhamini (*Guarantee Documents*), kununulia *T-Bills*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliuliza je, mkopo utakapotolewa na Benki Kuu wa shilingi bilioni 300 kwa Serikali ni *advance payment* ya mrabaha wa Serikali; kama ndivyo, SMZ inapata nini katika mpango huo?

Mheshimiwa Spika, jibu tunasema kwamba, kiasi cha shilingi bilioni 300 kitakachotoka Benki Kuu ni mkopo na siyo *advance payment* ya mrabaha. Katika mantiki hiyo, mkopo huo umeainishwa katika bajeti ya mwaka 2009/2010 na SMZ itaendelea kupata mgao wake wa pesa za bajeti, ikijumuisha mikopo kama ilivyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine inasema, kwa nini Serikali ililipa shilingi bilioni 4.4 kwa RAHCO ili kufuta madeni mbalimbali ya lililokuwa Shirika la Reli bila kibali cha *National Debt Management Committee*? Kufuatia kubinafsishwa kwa Shirika la Reli Tanzania (TRL), Serikali ililazimika kuchukua madeni yote ya TRC. Lengo la uamuhi huo likikuwa ni kuiwezesha Kampuni ya Reli Tanzania, kuanza kutoa huduma upya *on a clean state*. Hata hivyo, baadhi ya makampuni yaliyokuwa yakiidai TRC, hasa

yale ya mafuta, yalinkataa kutoa huduma ya mafuta kwa TRL hadi walipwe. Kufuatia uamuzi huo, Serikali ililazimika kulipa madeni ya mafuta jumla ya shilingi bilioni 4.4, kuiwezesha TRL kuanza uendeshaji mara moja.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyofuatia inasema, makampuni ya madini yaliyoingia mikataba na Serikali kabla ya tarehe 1 Julai, 2009, yahusishwe na kufuta Tangazo la Serikali Namba 99 la Mwaka 2005. Aidha, Serikali itekeleze mapendekezo ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, msamaha wa ushuru wa bidhaa za mafuta (*fuel levy*), ambao pia unajumuisha diesel, upo kwenye mikataba husika ya kuendeleza madini (*MDAs*), ambayo Serikali imeingia na makampuni ya madini. Bajeti ya Serikali ya 2009/2010, imependekeza kufuta msamaha wa ushuru wa mafuta na ushuru wa bidhaa (*Excise Duty*), kwa bidhaa za petroli. Kwa kuwa ushuru wa mafuta kwa makampuni haya upo kwenye miakataba, suala hilo litapelekwa kwa wanasheria wetu kwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010, Serikali imeanza kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini. Baadhi ya mapendekezo haya ni pamoja na:-

- (i) Kupitia Sera ya Madini ya Mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 kama itakavyoelezwa na Waziri wa Nidhati na Madini, atakapowasilisha bajeti yake hapa Bungeni.
- (ii) Kupunguza wigo wa nafuu maalumu wa VAT kwa makampuni ya madini ili nafuu hii ibakie tu kwa makampuni ya utafiti.
- (iii) Kufuta Tangazo la Serikali Namba 29 la Mwaka 2005 linalotoa msamaha wa ushuru wa mafuta ya petroli.
- (iv) Kufuta msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli kwa makampuni ya madini kwa kufuta Tangazo la Serikali Namba 480 la Mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihu Serikali kuahidi kuhamisha usimamizi wa shughuli za Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini, pamoja na Bodi ya Usimamizi wa Vifaa kutoka Wizara ya Miundombinu na kuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Iliulizwa jambo hili limefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, kinachosubiriwa ni mabadiliko ya hati ya mgawanyo wa majukumu (*instrument*), ili majukumu yawekwe chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Tayari Idara Kuu ya Utumishi, imewasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya hati ya mgawanyo wa majukumu kwa mamlaka husika. Hata hivyo, wakati mabadiliko hayo yakisubiriwa, Wizara ya Fedha na Uchumi, imeendelea na matayarisho yote muhimu ya kuyapokea majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu kwa nini fedha za EPA zimejumuishwa katika deni la ndani: hadi Desemba, 2008, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 1929.3, ikiwa ni ongezeko la asilimia 1.8 ikilinganishwa na deni lilokuwepo Desemba, 2007. Ongezeko la deni hili limetokana na kujumuishwa kwa shilingi bilioni 137.5 inayotokana na kulipia malimbikizo ya madeni ya nje (*EPA Stock*). Itakumbukwa kuwa, chimbuko la fedha za EPA ni gharama ambazo wafanyabiashara wa Tanzania walikuwa wanalipia bidhaa ambazo waliagiza nje ya nchi kupitia NBC na Benki Kuu.

Kutokana na shida ya upatikanaji wa fedha za kigeni wakati huo, wafanyabiashara wa Tanzania walikuwa wanalazimika kulipia bidhaa zao kwa shilingi za Tanzania na Benki kulazimika kutafuta fedha za kigeni ili kulipia bidhaa hizo. Katika mchakato wa kutafuta fedha za kigeni, kulikuwa kunatokea hasara ya kubadilisha shilingi ya Tanzania ili kupata fedha ya kigeni kulikosababishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi. Serikali ilikuwa inalazimika kulipa hasara hii kwa kutoa dhamana za Serikali kupitia Akaunti ya *External Payment Arrears (EPA)*, iliyokuwa inasimamiwa na Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikifuta ushuru wa forodha wa asilimia 10 kwenye mafuta ya kula kutoka nje kutadumaza kilimo cha mbegu za mafuta nchini kama vile alizeti, ufuta, mbegu za mawese, karanga na kadhalika. Kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ushuru wa forodha kwenye mafuta ghafi ya mawese ni asilimia sifuri. Hata hivyo, Tanzania imekuwa ikiomba na kuruhusiwa kutimiza kiwango cha asilimia 10 ili kulinda wakulima wa machikichi na mbegu nyingine za mafuta nchini na pia kuziba mwanya wa ukwepaji ushuru.

Kufuatia hali hii, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, liliagiza ufanyike utafiti ili kutathmini mahitaji ya mafuta ya kula na uzalishaji wa mbegu za mafuta ili kukidhi mahitaji ya viwanda vya usindikaji. Utafiti huu ulibaini kuwa uwezo wa uzalishaji wa mbegu za mafuta ndani ya Jumuiya ulikuwa hautoshelezi mahitaji ya soko na hivyo kupendelekeza kuwa, ushuru wa forodha wa kiwango cha asilimia sifuri uendelee kutumika ndani ya Jumuiya kwa mafuta ghafi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi ya soko kwa sasa, kuendelea kutoza ushuru wa asilimia 10 kwa mafuta ghafi, wakati nchi nyingine ndani ya Jumuiya zinatoza asilimia sifuri, kunaviweka viwanda vyetu vya kusindika mafuta katika hali ngumu kiushidani. Kwa kuwa kuanzia mwezi Januari, 2010, hakutakuwa na ushuru wa forodha katika biashara ya ndani kwa nchi zote za Jumuiya ni dhahiri kuwa, mafuta ghafi ya mawese yanaweza kuingizwa katika nchi nyingine za Jumuiya kwa ushuru wa asilimia sifuri, kusindikwa katika nchi hizo na hatimaye kuleta Tanzania bila kulipa ushuru. Hali hii inaweza kusababisha viwanda vyetu kufungwa, wananchi kukosa ajira na wakulima kukosa soko la mbegu wanazozalisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya *stimulus package* ikiwa ni pamoja na kutoa ruzuku ya shilingi 100 kwa kilo moja ya pamba. Serikali imeipokea hoja hii na itaifanyia kazi, kwa sababu inaweza kuhusisha mazao mengi zaidi. Serikali kwa maana ya Wizara ya Fedha na Gavana wa Benki Kuu, Prof. Ndullu, tumeanza kulishughulikia

suala hili na Waheshimiwa Wabunge, watajulishwa nini kitafanyika kadiri tutakavyokuwa tunaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri imeelezwa kuwa fedha za sekta ya elimu zimetengwa shilingi trilioni 1.7, lakini zinazoonekana kwenye vitabu vyta bajeti ni shilingi bilioni 507. Je, fedha hizo zimetengwa wapi? Tunapoichambua Sekta ya Elimu ni muhimu kuangalia mapana yake. Huduma ya Sekta ya Elimu hutolewa na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Vyuo vyta Maendeleo ya Wananchi chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Vyuo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Vyuo vyta Fedha chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010, jumla ya fedha zilizotengwa katika Sekta ya Elimu ni shilingi trilioni 1.743, sawa na asilimia 21.8 ya bajeti yote, ukiondoa deni la Taifa. Fedha hizo zimetengwa kupitia mafungu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu shilingi bilioni 507.5, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto shilingi bilioni 5.132, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) shilingi trilioni bilioni 2.105, Tume ya Utumishi wa Umma shilingi 2.280, Taasisi mbalimbali za mafunzo kama vile TIA, IFM, IAA, RDB, Hombolo na kadhalika shilingi bilioni 132.443, Mikoa shilingi bilioni 5.286 na Halmashauri za Wilaya shilingi 1,086,265,000,000.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa bandari unakwazwa na TRA kwa zaidi ya aslimia 80 kwa kuwa mlolongo ni mrefu; mfano, TISCAN, ASCAN na TRA, waangalie namna ya kupunguza mlolongo na kurahisisha utoaji mizigo. Serikali imepokea ushauri na utazingatiwa katika miradi mbalimbali ya maboresho ya TRA, kwa mujibu wa Mpango Mkuu wa Tatu, ambao tayari umeshaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tunduma - Sumbawanga iliyokuwa ijengwe kwa kutumia fedha za MCC, haijaanza kujengwa licha ya kuahidiwa hivyo na Serikali tokea mwaka jana. Kauli za ahadi hiyo, zimekuwa zikirudiwa mara kwa mara na Mheshimiwa Makamu wa Rais na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu; ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tunduma - Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 224 ni moja kati ya barabara zitakazojengwa katika Mpango wa *Millenium Challenge Cooperation*, unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani. Barabara nyingine ni pamoja na Tanga - Horohoro (kilomita 65), Songea - Namtumbo (kilomita 61) na ile ya Njiapanda ya Peramiho - Mbunga (kilomita 78). Barabara hiyo imepita katika hatua mbalimbali ya utekelezaji na kwa sasa zoezi linaloendelea ni kufanya mapitio ya usanifu wa barabara na pia kukamilisha nyaraka za kuitisha zabuni kulingana na miongozo ya MCC. Kazi hii inafanywa na kampuni ya Kihandisi inayoitwa AFRICON ya Afrika Kusini, zoezi ambalo lilianza mapema mwezi Aprili mwaka huu na linatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti mwaka huu. Zoezi hili ambalo ni mwendelezo wa usanifu wa awali uliofanywa na Wakala wa Matengenezo ya Barabara nchini

(TANROADS), ni lazima likamili like kwanza kabla ya kuitisha zabuni za wakandarasi wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua ya maendeleo ya mapitio hayo yanayofanywa na Mhandisi Mshauri, tunatarajia kazi itaanza kama ilivyokuwa imepangwa awali na ujenzi wa barabara hii umegawanywa kiutekelezaji katika maeneo matatu kama ifuatavyo:-

- (i) Barabara inayotoka Tunduma - Ikana (kilomita 64), zabuni za ujenzi zitatolewa mwezi Agosti, 2009, mkataba wa ujenzi unatakiwa kusainiwa Februari, 2010 na ujenzi kuanza Machi 2010 na kukamilika Februari, 2012.
- (ii) Barabara ya Ikana - Laela (kilomita 64), utekelezaji wa sehemu ya barabara hii utakuwa sawa na ule wa Tunduma - Ikana.
- (iii) Barabara ya Laela - Sumbawanga (kilomita 96.5), zabuni zitatolewa mwezi Agosti, 2009, mkataba wa ujenzi utasainiwa mwezi Desemba na ujenzi kuanza rasmi hapo Januari, 2010 na kukamilika ifikapo Septemba mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuona kuwa, barabara hii inakamilishwa mapema iwezekanavyo. Hii ni pamoja na miradi mingine inayogharimiwa na Serikali ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu kwa nini *flow meter* inaharibika mara kwa mara? Je, ikiharibika tunafanyaje kukadiria mapato? Awali Mamlaka ya Bandari iliweka *flow meter* moja, ambazo ikiharibika ilibidi kukokotoa kodi kwa kutumia utaratibu wa kizamani. Kwa sasa Mamlaka ya Bandari Tanzania, imeweka *flow meters* tatu zenye ubora wa kutosha, ambazo hupokezana moja inapoharibika. Aidha, TPA imeshamwajiri Mshauri ambaye atatoa mafunzo ya kusimamia ukarabati wa *meter* hizo. Kwa hiyo, Serikali haitarajji *flow meters* zote kuharibika kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu mlundikano wa shehena za mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, TICTS hawana vifaa vya kutosha kufanya kazi, Serikali iifanyie kazi. Suala hili limezungumzwa na Wabunge wengi, tunakubaliana na ushauri wa Wabunge wote, tutalifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza kodi katika sigara, je, bei ya tumbaku kwa mkulima itaongezeka ili kumnufaisha mkulima? Ushuru wa bidhaa kwenye sigara umeongezwa kwa kiwango cha mfumko wa bei ili kulinda mapato ya Serikali. Utaratibu huu ni wa kisera na ulifikasiwa kwa makubaliano kati ya Serikali na wadau wote wanaozalisha bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa. Bei ya mazao inapangwa na nguvu za soko na siyo Serikali. Hata hivyo, Serikali inaweza sera mbalimbali ambazo zinawawezesha wananchi kupata bei nzuri zaidi sokoni kama kuimarisha vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, fedha za uwezeshaji za JK, hazijawafikia wananchi wengi na hivyo kuwafanya kukimbilia DECI.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuongeza ajira (mabilioni ya JK), unalenga mtu mmoja mmoja, SACCOS na vikundi hususan vijana na wanawake, kwa ajili ya kujiongezea kipato na ajira. Wajasiriamali waliolengwa, hawalazimiki kuweka fedha ili wapate mikopo.

Aidha, mikopo ya Mfuko huo, haiwalengi waajiriwa na wafanyabiashara wa kati. Iteleweke kwamba, wengi wa waliopanda mbegu DECI ni wafanyakazi na wafanyabiashara wa kati, ndio maana wengi wao wanalia kwamba, wamepoteza mamilioni ya fedha. Hivyo, siyo kweli kwamba, walikimbilia huko kwa kokosa fedha kutoka mabilioni ya JK, kwa sababu walengwa wa mabilioni ya JK hawana mamilioni.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Pamba imepewa kiasi gani cha fedha kunusuru Zao la Pamba? Uchambuzi unafanywa, kubainisha kiasi halisi kitakachohusika na utaratibu huu, kwa kushirikisha mabenki yaliyohusika. Hivyo, kiasi kamili kitajulikana baada shughuli hiyo kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, TRA inatumia takwimu za zamani kuthamini magari wakati bei za magari zimeshuka kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani. Tanzania ni Mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) na inatekeleza mkataba wa kuthamini bidhaa zinzoingia nchini katika bei ya soko (*agreement on customs valuation*). Utaratibu huu unataka bidhaa zote, yakiwemo magari, zitathminiwe katika bei zake za kununulia. Zipo hatua sita za msingi ambazo zinapaswa kufuatwa kwa mlolongo wakati wa kutathmini bidhaa. Hatua hizi zinazingatiwa kikamilifu na TRA katika kutathmini mizigo yote ya forodha.

Vilevile ni kweli kuwa, TRA inayo benki ya takwimu za thamani ya mizigo, ambayo inatumika kutathmini na kudhibiti hatari ya uvujaji wa mapato ya Serikali na siyo kama kiashiria cha thamani ya mizigo hiyo. Aidha, benki hii inafanyiwa marekebisho mara kwa mara, kupitia kwenye mtandao wa kompyuta. Marekebisho hayo, yataisaidia Idara ya Forodha kupata bei mpya wakati wowote inapotokea kuwa zimebadilika katika masoko mbalimbali ya bidhaa zitokazo nje.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali haijaonesha kiwango cha ongezeko la pensheni kwa wastaafu wa kima cha chini. Aidha, kuna usumbufu wa ucheleweshaji wa mafao ya wastaafu. Kama nilivyoeleza katika Hotuba ya Bajeti, Serikali inayowajali wastaafu wake, itaongeza kiwango cha chini cha pensheni kutoka shilingi 21,601.5 kwa mwezi za sasa na kuwa shilingi 50,114 kwa mwezi kuanzia Julai, 2009. Ongezeko hili ni karibu mara mbili na nusu ya kima kilichopo hivi sasa. Ongezeko hili haliwezi kukidhi mahitaji yote ya mstaafuli, lakini kwa Bajeti ya Serikali ilivyo, Serikali inaamini kwamba, angalau itakuwa ni mwanzo mzuri wa kuwasaidia wastaafu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa malipo ya mafao kwa baadhi ya wastaafu, unasababishwa na uwasilishaji wa nyaraka na taarifa pungufu zinazowezeshwa kulipwa kwa mafao ya wastaafu; hali hii huilazimisha Wizara kurejea kufanya mawasiliano na Wizara zinazohusika ili kupata nyaraka na taarifa zilizopungua. Hoja hizo huchukua

muda mrefu kujibiwa na Wizara zinazohusika au kutojibiwa kabisa na hivyo kuendeleza ucheleweshaji wa mafao kwa wahusika. Katika jitihada za kuondoa kero hii, Serikali ilifanya semina za kikanda, zilizowahusisha waajiri, ambapo maafisa wanaoshughulikia mafao ya kustaafu na mirathi, walielezwa wajibu wao wa kushughulikia mafao ya kustaafu na mirathi na matunda yake yameanza kuonekana. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa watumishi wote kuwa na kawaida ya kukagua kumbukumbu zao kabla ya tarehe za kustaafu kufikia.

Mheshimiwa Spika, kwa nini STAMICO hawajapewa kibali cha kukopa fedha kutoka NDC? Ni kweli kwamba, baada ya STAMICO kuna *specified* sheria, ambayo iliwataka wakitaka kukopa, lazima wapate idhini PSRC. Hata hivyo, Serikali iliamua Shirika la Madini la Taifa liendelee kuwepo na kusimamia Sekta ya Madini; hivyo, lilikubaliwa kuingia katika makubaliano na *South African Enterprise Fund*, kuwapatia mitambo miwili ya kuchongea miamba kwa utaratibu wa *lease financing*. Mashine hizo zimeshawasili Dar es Salaam na tayari zimeanza kutumika. STAMICO sasa hivi wamekuwa *de-specified* na wanaruhusiwa kukopa.

Mheshimiwa Spika, kodi ya bidhaa za simu za mikononi kwa kuangalia thamani iliyopo kwenye kadi ya muda wa maongezi, haitaongeza bei ya watumiaji na kuwaumiza wenyе kipato cha chini. Mabadiliko yaliyofanywa kwenye Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2009/010 katika utoaji wa ushuru wa bidhaa na kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za simu za mikononi, hayabadili viwango vya kodi husika. Kodi zinazotozwa kwenye huduma hizo zinabakia kuwa ni VAT na ushuru wa bidhaa tu. Kiwango cha ushuru wa bidhaa kikibakia kuwa asilimia 10, kiwango cha VAT kitapungua kutoka asilimia 20 hadi asilimia 18. Mabadiliko haya yanalenga katika kuhakikisha kuwa, Serikali inapata mapato yake halali. Kwa misingi hii, mabadiliko haya hayategemei kubadilisha bei ya watumiaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania ipewe jukumu la kukusanya kodi za majengo hadi mikoani na mapato mengine yasiyo ya kodi. Mamlaka ya Mapato Tanzania, inakusanya kodi ya majengo katika Mkoa wa Dar es Salaam kama mpango wa majaribio (*Pilot Project*) ili kupima mafanikio na changamoto zitakazojitokeza. TRA bado inajipanga vizuri zaidi katika utekelezaji wake kwa nchi nzima. Tunashauri Mheshimiwa Mbunge, asubiri matokeo ya mpango wa majaribio, kabla ya kuanza utekelezaji wa nchi nzima na katika Wizara nyinginezo, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Maliasili na Wizara ya Nishati na Madini kama alivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenye fungu maalum la fedha za kuziweka katika benki za wazawa au za Serikali ili Watanzania waweze kukopa kwa riba nafuu hasa kupitia SACCOS. Serikali imejitahidi sana kutoa fedha za kuweka katika benki za wazawa na za Serikali ili kukopessa Watanzania kwa riba nafuu. Kwa mfano, mabilioni ya JK, shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa, fedha za Mfuko wa Pembejeo na Vifaa vya Kilimo na kadhalika, pia kuna Mfuko wa Dhamana wa SMEs ambao unadhamini mikopo inayotolewa na mabenki kwa wajasiriamali wadogo wadogo. Watanzania wanawenza kutumia fursa hizo na kupata mikopo wanayoihitaji kwa shughuli za maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kabla Serikali haijatoa fedha kwa TRL ni vyema ikaangalia upya mkataba na vifaa walivyoleta wawekezaji. Kutokana na hali ya uendeshaji wa TRL, Serikali imeanza kupitia upya Mpango wa Biashara (*Business Plan*), kwa lengo la kuiboresha pamoja na kupitia upya Mikataba ya Ukokishaji (*Consension Agreement*) na Kanuni za Kampuni (*Memorandum Of Association*), kabla ya kuidhinisha TRL ianze kupewa tena fedha za IFC na kufikia kudhamini mkopo wanaoomba kutoka Shirika la India.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipunguze riba katika mabenki ili kumuwezesha mwananchi kukopa na kulipa. Benki na taasisi za fedha hufanya biashara, ambapo hutozwa riba kwa kiwango ambacho hutegemea nguvu za soko na uwezo wa kulipa wa mteja. Kwa mantiki hiyo, Serikali haiwezi kupanga kiwango cha riba ambacho kitatozwa na mabenki kwa wateja wake. Aidha, Benki Kuu inaweza kutumia dhamana za Serikali na mauzo ya fedha za kigeni ili kupunguza msukumo wa kuongeza viwango vyta riba, kwani mabenki mengi yanaangalia mwenendo wa riba za dhamana za Serikali na bei za fedha za kigeni yanapopanga riba zao.

Mheshimiwa Spika, kiasi gani cha pesa kati ya shilingi bilioni 666.6 kimetengwa kwenye mbolea na mbegu za mazao ya chakula? Jumla ya shilingi bilioni 118 zimetengwa kwa ajili ya mbolea na mbegu za mazao ya chakula. Kati ya kiasi hicho, Serikali imetenga shilingi bilioni 58 na Benki ya Dunia imechangia shilingi bilioni 60.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ushuru umeondolewa kwenye magari ya mizigo badala ya magari ya abiria kama mabasi? Hoja hii iambatane na takwimu za kutosha. Wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri, tumeanza na zoezi hili kwa magari ya mizigo na pendekezo kuhusu ushuru wa mabasi tutalipela kwenye Vikao vyta Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao. Kwa kuanzia, tayari zoezi la kuhakiki taratibu za usajili wa bidhaa kwa mabasi yanayotoka Kenya umeshafanyika na utambuzi wa mabasi yanayokidhi masharti umekamilika. Kutokana na hatua hii ni wakati muafaka sasa kwa Serikali yetu kufikiria kuipeleka hoja hii ya kupunguza ushuru wa mabasi mbele ya vikao vinavyohusika vyta Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa MMAM 2008/2009, hatuoni fedha zimetengwa kwa TAMISEMI kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vyta afya hasa katika Wilaya ya Rudewa. TAMISEMI wamesema hawakutengewa fedha na Hazina. Utekelezaji wa MMAM, ulianza mwaka 2007/2008 na unahusisha wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Sekretarieti za Mkoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wadau wengine. Kulingana na mgawanyo wa majukumu kwa kila mda, Serikali hutenga fedha ili kutekeleza shughuli za MMAM katika kutekeleza Sera ya *Decentralization by Devolution*. Fedha za Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa MMAM katika Bajeti ya 2009/2010, zimetengwa chini ya kila Halmashauri, ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedumaza utoaji wa huduma za afya katika Hospitali ya KKKT Seriani, baada ya kuifanya kuwa Teule (*Desgnaited District*

*Hospital).* Kwa nini Serikali haijalipa mishahara ya wafanyakazi inayokaribia shilingi milioni 560 kwa miezi saba mfululizo?

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Seriani iliyopo Mkoani Arusha, ilikuwa Hospitali ya Hiari (*Voluntary Agency Hospital*) hadi tarehe 5 Desemba, 2008 ilipopandishwa hadhi na kuwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Arusha. Baada ya kupandishwa hadhi, Uongozi wa Hospitali ya Seriani, uliandaa mahitaji ya gharama za mishahara na kuwasilisha Serikalini mwezi Aprili mwaka huu. Kwa kuwa taratibu za kupandisha hadhi hospitali hiyo zilikamilika wakati utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2008/2009 unakaribia kumalizika na watumishi hao hawakuwa kwenye ikama kwa mwaka husika, ilikuwa ni vigumu kulipwa mshahara. Hata hivyo, kwa mwaka 2009/2010, mishahara ya watumishi wa hospitali hiyo imejumuishwa katika bajeti. Mishahara ya Watumishi wa Hospitali Teule ya Seriani, itanza kulipwa mwezi Julai, 2009, pamoja na mabadiliko ya miezi saba, kuanzia Desemba, 2008 hadi Juni, 2009.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haikuonesha kiasi gani kimetengwa katika barabara za Halmashauri, pia TAMISEMI imetengewa fedha kidogo kuzitengeneza, hivyo Serikali iongeze fedha hizo. Utaratibu unaotumika kibajeti kuhusu barabara za Halmashauri ni kwa fedha kutengwa kupitia Wizara, Idara na Programu mbalimbali ambazo zinatekelezwa na mafungu mbalimbali, kutegemeana na hadhi na madhumuni ya barabara husika. Barabara za Serikali za Mitaa, hutengewa na kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), ambao kwa mwaka 2009/2010, jumla ya shilingi bilioni 85.2 zimetengwa katika Fungu 56 (Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, zimetengwa Fungu 56, yaani Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Aidha, Mifuko mbalimbali kama SDP, DAC na PADEP, inayotekelawa na Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula, pamoja na Halmashauri, zimetenga fedha kwa ajili ya barabara ziendazo mashambani. Programu ya LGTP, imetengewa jumla ya shilingi 25.8 bilioni kwa ajili ya uendeshaji wa barabara; hoja je, kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya maeneo yenye mazingira magumu na hizi fedha tunazoziona ni Bajeti ya Wizara gani?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua za makusudi, kuboresha mazingira katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuwavutia watumishi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, ilitenga kiasi cha shilingi bilioni ishirini kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu, ikiwa ni pamoja na nyumba za walimu. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni ishirini na tatu kwa ajili ya Halmashauri thelathini na sita zenye mazingira magumu kama vile Ludewa, Ngorongoro, Mafia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zipo kwenye Kitabu cha Nne cha Bajeti kwa kila fungu la Mkoa na Halmashauri husika. Hoja kwa nini Serikali imetenga fedha nyingi kwenye kifungu cha *personal allowance in kind* ambacho ni kwa ajili ya *food and refreshment* wakati vifungu vingine muhimu havikutengewa fedha ya kutosha?

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mabadiliko ya mfumo wa takwimu za fedha za Serikali, yaani *Government Financial Statistics* kama *210500 and Personal allowance in kind*, imeundwa kubainisha matumizi yanayofanywa Serikalini kulingana na stahili za Viongozi na Watumishi mbalimbali. Stahili hizi zinagharimiwa na Serikali kwa kuzingatia sheria, hadhi na mikataba ya ajira au shughuli maalumu wanazofanya. Kwa maana hiyo, kasma *210500 - personal allowance in kind*, pamoja na kuhusisha *food and refreshment* pia inajumisha gharama za umeme, simu, samani, vyombo vya ndani, maji safi na maji taka, posho ya nyumba na gharama za pango.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha zilizotengwa kwa kasma hii kwa kila fungu, zimezingatia idadi ya Viongozi na Watumishi wanaolipwa stahili hizo.

Katika kuboresha miundombinu ya reli, Serikali inashauriwa kuboresha Reli ya Kati. Kwa ujumla, kuna haja ya kukarabati reli kutoka Isaka hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ingawa suala hili linamhusu Waziri wa Miundombinu, napenda nitoe maelezo mafupi kuhusu juhudzi za Serikali katika kuboresha Reli ya Kati. Serikali inatambua umuhimu wa Reli ya Kati kwa uchumi wa nchi yetu, ikiwa kama kiungo muhimu kati ya Bandari yetu Kuu ya Dar es Salaam na nchi za jirani kupitia Bandari ya Mwanza na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali tayari inatekeleza hatua kadhaa zenyenye lengo la kuboresha reli hiyo muhimu. Kwa sasa Serikali inakamilisha upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*), kwa lengo la kupanua reli hiyo kati ya Dar es Salaam na Isaka, kwa kuongeza upana wake kutoka mita moja hadi mita 1.435. Kazi hii inayotekelawa na Kampuni ya Baniton Northen Saint Afee, inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti mwaka huu. Aidha, Serikali ina mpango wa kujenga reli mpya kutoka Isaka hadi Kigali na Bujumbura, kwa kushirikiana na nchi za Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu wa reli hii pia unatarajiwa kukamilika mwaka huu. Kazi ya upembuzi yakinifu itakapokamilika, itatuwezesha kufahamu gharama halisi ya miradi hii miwili na huo ndio utakuwa msingi wa mazungumzo yetu na wadau watakaochangia kugharimia miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ingawa mpaka sasa hatujui gharama halisi ya miradi hiyo miwili, Serikali inaamini gharama ya kutekeleza miradi hii ni kubwa kuliko uwezo wa bajeti yetu ya Serikali au mchango wa mfadhili mmoja. Ili kupata fedha za kutosha kutekeleza miradi hii mikubwa, Serikali yetu kwa kushirikiana na nchi za Rwanda na Burundi, zinaendeleza mazungumzo na wafadhili mbalimbali ili kuwaomba wachangie gharama za miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Julai, 2008, ulifanyika mkutano mkubwa wa Wafadhili Mjini Tunisia, chini ya uratibu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Wafadhili mbalimbali wakiwemo Benki ya Dunia na ADB na sekta binafsi walishiriki. Baadhi ya Wafadhili walionesha nia ya kuchangia gharama ya ujenzi wa pamoja na Benki ya Dunia,

Benki ya Maendeleo ya Afrika, Kampuni ya BNSF ya Marekani, Serikali ya Japan na Benki ya Rasilimali ya Ulaya. Mazungumzo na Wafadhili mbalimbali yatakamilika baada ya gharama halisi ya miradi hiyo kujulikana.

Mheshimiwa Spika, ili Reli ya Kati iweze kuleta manufaa yanayokusudiwa, Serikali inaamini ni muhimu pia kuboresha sehemu ya reli kati ya Isaka na Kigoma na kati ya Isaka na Mwanza, pamoja na Bandari za Dar es Salaam, Kigoma na Mwanza. Maelezo ya kina kuhusu mipango ya Serikali kuhusiana na miradi hii, yatatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya 2007/2008, ilishauriwa liundwe jopo la wataalamu wa ndani na nje, kutathmini usahihi wa takwimu mpya za upande wa Taifa na kuendeleza taratibu za kuboresha takwimu hizo; je, utelezaji wake ukoje?

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu, iliunda jopo la wataalamu wa ndani na nje ili kutathmini usahihi wa takwimu mpya wa Pato la Taifa kama ilivyoagizwa katika Bajeti ya 2007/2008. Uhakiki huo ulisimamiwa na mtaalamu wa utayarishaji wa takwimu wa Pato la Taifa kutoka Shirika la Maendeleo la Uingereza, yaani NDFD, akishirikiana na Wataalamu wa Utayarishaji wa Pato la Taifa kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa na Wataalamu wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, wataalamu kutoka Wizara, Idara na asasi mbalimbali za Tanzania Bara kama vile Wizara ya Fedha na Uchumi, Kilimo na Chakula, Viwanda na Masoko, Elimu, Afya, Mawasiliano, TRA, Benki Kuu na TICRA, walifanya tathmini. Aidha, Umoja wa Mataifa, umeridhia ubora wa usahihi wa takwimu hizo mpya na tayari umechapishwa kwenye Kitabu cha Takwimu cha Umoja wa Mataifa. Uwezeshaji wananchi kiuchumi, haujatekelezwa vizuri na fedha za uwezeshaji ziliishia mijini tu.

Mheshimiwa Spika, fedha za uwezeshaji; mabilioni ya JK awamu ya kwanza ambazo ni shilingi bilioni kumi nukta tano, zilitolewa kupitia Benki za CRDB na NMB, ambazo zilikopesha zaidi ya mara tatu ya kiasi hicho. CRDB ilikopesha jumla ya kiasi cha shilingi bilioni ishirini nukta tisa, kupitia SACCOS ambazo nydingi ziko vijijini. Kwa upande wa NMB, ilikopesha shilingi bilioni kumi na sita nukta mbili kwa Wajasiliamali mmoja mmoja, ambao wapo ndani ya umbali ya kilometra ishirini kutoka kwenye Tawi la Benki.

Aidha, awamu ya pili ya mpango huo, imelenga kunufaisha Wananchi wengi zaidi vijijini, ambapo asasi za kifedha na kibenki na benki kumi na mbili zenye uwezo wa kuwafikia wananchi wengi vijijini zinatumika na hivyo kuondoa kasoro hiyo hasa katika zile Wilaya ishirini na moja ambazo hazikupata mkopo katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba, fedha hizi zinakopeshwa kwa utaratibu wa mzunguko (*revolving*). Hivyo, kadiri mikopo hiyo inavyorejeshwa, ndivyo zinavyoweza kukopeshwa kwa wananchi wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya uamuzi wake wa kuondoa msamaha maalumu wa VAT kwa Asasi Zisizo za Kiserikali na Mashirika ya Dini; jibu ni kwamba, Serikali inatambua na kuthamini mchango unaotolewa na Asasi Zisizo za Kiserikali na Mashirika ya Dini katika kutoa huduma za kijamii kama vile afya, elimu na maji. Kama nilivyoeleza hapo awali, msamaha maalumu wa VAT unaotolewa kwa Asasi Zisizo za Kiserikali na Mashirika ya Dini, umekuwa ukitumika vibaya na baadhi ya mashirika na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali. Hata hivyo, baada ya kupata maoni ya Waheshimiwa Wabunge, Serikali kwa kuongozwa na Waziri Muu, ilifanya mazungumzo na Viongozi wa Dini zote hapa nchini na tulikubaliana kwamba, lipo tatizo katika matumizi ya misaada inayopatiwa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumekubaliana kwa pamoja kuwa, misamaha ya kodi iwe na tija na wananchi waielewe kuwa ina faida. Utengenezwe utaratibu wa wazi, utakaoweza kuziba mianya yote ya matumizi mabaya ya misamaha hiyo. Tumekubaliana kuunda kamati ya pamoja, itakayotengeneza utaratibu huo na utaanza kutumika mara tu baada ya kukamilika. Kamati itajumuisha Wawakilishi wa Madhehebu ya Dini, TRA na Serikali. Mazungumzo yalifanyika katika hali ya maelewano makubwa, kwa hiyo, Serikali imeamua msamaha wa VAT kwa Asasi zisizo za Kiserikali na Mashirika ya Dini, uendelee kama ulivyo hivi sasa hadi hapo utaratibu utapokamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya hoja tumeyajibu, lakini kwa sababu ya muda, nimeshindwa kuyajibu yote kama tulivyoyatayarisha. Imani yangu ni kwamba, taarifa nzima hii ya majibu itachapishwa kwenye *Hansard*, kwa wale ambao hamkuona yale mliyoyaauliza, nadhani mtayaona kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

### **WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Natumaini kama kawaida, utachapisha nakala za kutosha za majibu hayo ili hata yale ambayo hayajafikiwa, yatusaidie kuwa mwongozo katika mahusiano yetu na Wananchi. Nakushukuru sana kwa kazi kubwa uliyoifanya ya kujibu hizo hoja.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono, lakini hoja hii inaamuliwa kwa misingi ya Katiba na kwa hiyo, inabidi kwanza chini ya Kanuni ya 79(8)(8), sasa nimwombe Katibu wa Bunge, igongwe kengele kule nje ili Mbunge ye yote ambaye yupo kwenye maeneo ya Bunge aweze kuingia ndani.

Baada ya hapo, tutaitwa kwa majina ambayo tunayo hapa. Nimepata orodha ya Wabunge walioaga, lakini haijumlishi Mawaziri; kuna wengine ambao wana udhuru na hatuwezi kuwa nao. Tayari kengele imepigwa, wakati tunasubiri nataka nisaidie tu kwamba, ibara ya tisini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema, nitainukuu ibara hii inaelezea ni nyakati zipi Bunge linaweza kuvunjwa.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mengi mengine, ibara ya 90(2)(b) inasema: “Rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote isipokuwa tu kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali.” Kwa hiyo ni hatua inayoweza kuchukuliwa wala siyo hiari tena, kama Bajeti imekataliwa basi Bunge linavunjwa na Mheshimiwa Rais. Sasa maneno hayo hayo yamechukuliwa kwenye Kanuni ya 98(2), nitainukuu inasema: “Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutopitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.”

Sasa hiyo ndio hatua inayofuata, ambayo kama nilivyosema, inatawaliwa na Kanuni ya 79(8) inayosema: “Katibu atapiga kengele ya kuwaita Wabunge kwa muda wa dakika moja na baada ya muda huo, Spika atamwagiza Katibu kumwita Mbunge mmoja mmoja kwa jina lake na kumuuliza anapiga kura yake upande gani na kurekodi kura hiyo.”

Waheshimiwa Wabunge, kura zipo za aina tatu ambazo zinatakiwa ziandikwe. Kura ya ndio, siyo au hana uamuzi, kwa kweli ipo na ya nne ni kwamba, hayupo tu, sasa inawezekana hayupo kwa sababu mbalimbali. Wenzetu wa Baraza la Wawakilishi, wamekwenda kuhudhuria Baraza la Wawakilishi. Wengine wamekwenda kwenye misiba na kuna mmoja amesema yuko Biharamulo kwa shughuli binafsi, lakini nadhani hii inaeleweka.

Katibu muda umekwishapita, nakuomba sasa utuite jina moja moja kwa ajili ya kura.

(*Hapa kengele ilipigwa ili Wabunge waliokuwa nje waingie ndani ya Ukumbi wa Bunge*)  
(*Hapa upigaji wa kura kwa kutaja jina moja moja ulianza*)

Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda	Ndiyo
Mheshimiwa Philip Sang'ka Marmo	Ndiyo
Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu	Hakuwepo
Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Mark James Mwандосya	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi	Ndiyo
Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati	Ndiyo
Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta	Hakuwepo
Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla	Hakuwepo
Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa	Ndiyo
Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia	Hakuwepo
Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian	Ndiyo
Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe	Ndiyo

Mheshimiwa	Mathias Meinrad Chikawe	Ndiyo
Mheshimiwa	Dr. Diodorus Buberwa Kamala	Ndiyo
Mheshimiwa	Shamsa Selengia Mwangunga	Ndiyo
Mheshimiwa	Mustafa Haidi Mkulo	Ndiyo
Mheshimiwa	Lawrence Kego Masha	Ndiyo
Mheshimiwa	William Mganga Ngeleja	Hakuwepo
Mheshimiwa	Capt. George Huruma Mkuchika	Hakuwepo
Mheshimiwa	Celina Ompeshi Kombani	Ndiyo
Mheshimiwa	Johnson Paulo Mwanyika	Hakuwepo
Mheshimiwa	Anne Semamba Makinda	Hakuwepo
Mheshimiwa	Dr. Maua Abeid Daftari	Hakuwepo
Mheshimiwa	Hezekiah Ndahani Chibulunje	Hakuwepo
Mheshimiwa	Balozi Seif Ali Iddi	Hakuwepo
Mheshimiwa	Dr. Emmanuel John Nchimbi	Ndiyo
Mheshimiwa	Mwantumu Bakari Mahiza	Hakuwepo
Mheshimiwa	Dr. Cyril August Chami	Hakuwepo
Mheshimiwa	Dr. Milton M. Mahanga	Ndiyo
Mheshimiwa	Dr. Aisha Omar Kigoda	Ndiyo
Mheshimiwa	Joel Nkaya Bendera	Hakuwepo
Mheshimiwa	Dr. David Mathayo David	Ndiyo
Mheshimiwa	Christopher Kajoro Chiza	Ndiyo
Mheshimiwa	Gaudentia Mugosi Kabaka	Ndiyo
Mheshimiwa	Jeremiah Solomon Sumari	Ndiyo
Mheshimiwa	Mohamed Aboud Mohamed	Ndiyo
Mheshimiwa	Omar Yussuf Mzee	Ndiyo
Mheshimiwa	Balozi Hamis Suedi Kagasheki	Ndiyo
Mheshimiwa	Dr. Lucy Sawere Nkya	Ndiyo
Mheshimiwa	Dr. James Mnanka Wanyancha	Hakuwepo
Mheshimiwa	Ezekiel Magolyo Maige	Ndiyo
Mheshimiwa	Adam Kighoma Ali Malima	Ndiyo
Mheshimiwa	Aggrey Deaisile Joshua Mwanri	Ndiyo
Mheshimiwa	Dr. Abdallah Omar Kigoda	Ndiyo
Mheshimiwa	George Malima Lubeleje	Hakuwepo
Mheshimiwa	Wilson Mutagaywa Masilingi	Ndiyo
Mheshimiwa	Anne Kilango Malecela	Hakuwepo
Mheshimiwa	John Momose Cheyo	Hapana
Mheshimiwa	Dr. Willibrod Peter Slaa	Hapana
Mheshimiwa	Kabwe Zuberi Zitto	Hakuwepo
Mheshimiwa	George B. Simbachawene	Hakuwepo
Mheshimiwa	Lediana Mafuru Mng'ong'o	Hakuwepo
Mheshimiwa	Abdisalaam Issa Khatib	Ndiyo
Mheshimiwa	Omar Shabani Kwaangw'	Ndiyo
Mheshimiwa	Jenista Joakim Mhagama	Ndiyo
Mheshimiwa	Job Yustino Ndugai	Ndiyo
Mheshimiwa	Gideon Asimulike Cheyo	Ndiyo
Mheshimiwa	Mohamed Hamisi Missanga	Ndiyo

Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo	Ndiyo
Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed	Hapana
Mheshimiwa Halima James Mdee	Hakuwepo
Mheshimiwa Shoka Khamis Juma	Hakuwepo
Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu	Hapana
Mheshimiwa Riziki Omar Juma	Hapana
Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali	Hakuwepo
Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo	Hapana
Mheshimiwa Said Amour Arfi	Hakuwepo
Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi	Hakuwepo
Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani	Hapana
Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya	Hapana
Mheshimiwa Salim Hemed Khamis	Hapana
Mheshimiwa Anna Maulidah Komu	Hapana
Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha	Hakuwepo
Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya	Hapana
Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya	Hapana
Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa	Hakuwepo
Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi	Hakuwepo
Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim	Hapana
Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary	Hakuwepo
Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya	Hakuwepo
Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji	Hakuwepo
Mheshimiwa Ania Said Chaurembo	Hakuwepo

**SPIKA:** Katibu, naomba umwite Mheshimiwa Joseph Mungai, anawahi Hospitali anataka kupiga kura.

Mheshimiwa Joseph J. Mungai	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Ali Mzee	Hapana
Mheshimiwa Ali Said Salim	Hakuwepo
Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili	Hapana
Mheshimiwa Bakari Shamis Faki	Hapana
Mheshimiwa Mohamed Ali Said	Hapana
Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga	Hapana
Mheshimiwa Juma Said Omar	Hapana
Mheshimiwa Ali Khamis Seif	Hapana
Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage	Hapana
Mheshimiwa Khadija S. A. Al-Qassmy	Hapana
Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika	Hapana
Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah	Ndiyo
Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah	Ndiyo
Mheshimiwa Mohammed Abdi Abdulaziz	Hakuwepo
Mheshimiwa Bahati Ali Abeid	Ndiyo

Mheshimiwa Ali Haji Ali	Hakuwepo
Mheshimiwa Fatma Othman Ali	Ndiyo
Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally	Ndiyo
Mheshimiwa Ame Pandu Ame	Ndiyo
Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir	Hakuwepo
Mheshimiwa Ameir Ali Ameir	Ndiyo
Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan	Ndiyo
Mheshimiwa Rostam Abdulrasul Azizi	Hakuwepo
Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar	Ndiyo
Mheshimiwa Feetham Filipo Banyikwa	Ndiyo
Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga	Hakuwepo
Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes	Ndiyo
Mheshimiwa Lollesia J. M. Bukwimba	Ndiyo
Mheshimiwa Felister Aloyce Bura	Ndiyo
Mheshimiwa Pindi Hazara Chana	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni	Hakuwepo
Mheshimiwa Andrew John Chenge	Ndiyo
Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo	Ndiyo
Mheshimiwa Samuel Mcchele Chitalilo	Hakuwepo
Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh	Ndiyo
Mheshimiwa Paschal Constantine Degera	Hakuwepo
Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji	Ndiyo
Mheshimiwa Mohammed Gulam Dewji	Hakuwepo
Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo	Hakuwepo
Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel	Abstain
Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah	Hakuwepo
Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama	Ndiyo
Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke	Ndiyo
Mheshimiwa Ali Juma Haji	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji	Ndiyo
Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji	Ndiyo
Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed	Hakuwepo
Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa	Hakuwepo
Mheshimiwa Parmukh Sing Hoogan	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma	Ndiyo
Mheshimiwa Issa Kassim Issa	Ndiyo
Mheshimiwa Yahya Kassim Issa	Ndiyo
Mheshimiwa Athumani Said Janguo	Hakuwepo
Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha	Ndiyo
Mheshimiwa Rajab Hamad Juma	Hakuwepo
Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga	Ndiyo
Mheshimiwa Janet Bina Kahama	Ndiyo
Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi	Ndiyo
Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu	Ndiyo
Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe	Hakuwepo

Mheshimiwa Eustace Osler Katagira	Hakuwepo
Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa	Ndiyo
Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo	Ndiyo
Mheshimiwa Charles N. Keenja	Ndiyo
Mheshimiwa Yono Stanley Kevela	Ndiyo
Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis	Ndiyo
Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis	Hakuwepo
Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib	Hakuwepo
Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo	Ndiyo
Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko	Ndiyo
Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi	Hakuwepo
Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah	Hakuwepo
Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro	Ndiyo
Mheshimiwa Halima Omar Kimbau	Hakuwepo
Mheshimiwa Archt. Fuya Godwin Kimbita	Ndiyo
Mheshimiwa Paul Peter Kimiti	Ndiyo
Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini	Ndiyo
Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba	Hakuwepo
Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya	Ndiyo
Mheshimiwa William Jonathan Kusila	Ndiyo
Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir	Ndiyo
Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya	Ndiyo
Mheshimiwa Michael Lekule Laizer	Ndiyo
Mheshimiwa James Daudi Lembeli	Ndiyo
Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama	Ndiyo
Mheshimiwa Devota Mukwa Likokola	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu	Ndiyo
Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto	Ndiyo
Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa	Ndiyo
Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula	Ndiyo
Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi	Ndiyo
Mheshimiwa Riziki Said Lulida	Hakuwepo
Mheshimiwa Anna Richard Lupembe	Ndiyo
Mheshimiwa John Paul Lwanji	Ndiyo
Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba	Ndiyo
Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina	Ndiyo
Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu	Ndiyo
Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge	Ndiyo
Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba	Hakuwepo
Mheshimiwa Jackson Muvangila Makwetta	Ndiyo
Mheshimiwa Benito William Malangalila	Ndiyo
Mheshimiwa John Samwel Malecela	Hakuwepo
Mheshimiwa Halima Mohammed Mamuya	Hakuwepo
Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno	Hakuwepo
Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya	Ndiyo

Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi	Ndiyo
Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa	Ndiyo
Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa	Ndiyo
Mheshimiwa Haroub Said Masoud	Ndiyo
Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi	Ndiyo
Mheshimiwa Joyce Martin Masunga	Ndiyo
Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid	Ndiyo
Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga	Ndiyo
Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka	Ndiyo
Mheshimiwa Monica Ngezi Mbega	Ndiyo
Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchomba	Ndiyo
Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji	Ndiyo
Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki	Ndiyo
Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni	Ndiyo
Mheshimiwa Laus Omar Mhina	Ndiyo
Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita	Ndiyo
Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi	Ndiyo
Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga	Ndiyo
Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa	Ndiyo
Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono	Hapana
Mheshimiwa Rita Louise Mlaki	Hakuwepo
Mheshimiwa Martha Mosses Mlata	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa	Ndiyo
Mheshimiwa Herbert James Mntangi	Ndiyo
Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed	Ndiyo
Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed	Hapana
Mheshimiwa Elisa David Mollel	Ndiyo
Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda	Ndiyo
Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe	Ndiyo
Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya	Ndiyo
Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina	Ndiyo
Mheshimiwa Kilontsi Muhamma Mpologomyi	Ndiyo
Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba	Hakuwepo
Mheshimiwa Felix Christopher Mrema	Ndiyo
Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha	Ndiyo
Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri	Ndiyo
Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela	Hakuwepo
Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama	Ndiyo
Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai	Ndiyo
Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi	Ndiyo
Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia	Ndiyo
Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir	Ndiyo

Mheshimiwa Joseph James Mungai	Ndiyo
Mheshimiwa James Philipo Musalika	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Sheha Mussa	Ndiyo
Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa	Ndiyo
Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu	Ndiyo
Mheshimiwa Dorah Herial Mushi	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe	Hakuwepo
Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi	Ndiyo
Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa	Ndiyo
Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila	Ndiyo
Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro	Ndiyo
Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda	Ndiyo
Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale	Hakuwepo
Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu	Hakuwepo
Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha	Ndiyo
Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera	Hapania
Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya	Ndiyo
Mheshimiwa Damas Pascal Nakei	Ndiyo
Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro	Ndiyo
Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa	Ndiyo
Mheshimiwa Philemon Ndesamburo	Hapania
Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa	Ndiyo
Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu	Ndiyo
Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru	Ndiyo
Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye	Ndiyo
Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi	Ndiyo
Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan A. Ngwilizi	Ndiyo
Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga	Ndiyo
Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka	Ndiyo
Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba	Ndiyo
Mheshimiwa Said Juma Nkumba	Ndiyo
Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko	Ndiyo
Mheshimiwa Tatou Musa Ntimizi	Hakuwepo
Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu	Ndiyo
Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami	Ndiyo
Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa	Hakuwepo
Mheshimiwa Ussi Ame Pandu	Ndiyo
Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan	Ndiyo
Mheshimiwa Shally Josepha Raymond	Ndiyo
Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatire	Ndiyo
Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq	Hakuwepo
Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said	Ndiyo
Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila	Ndiyo
Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe	Ndiyo
Mheshimiwa Ahmed Ally Salum	Ndiyo

Mheshimiwa Salum Khamis Salum	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi	Ndiyo
Mheshimiwa Lukas Lumambo Selelii	Ndiyo
Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka	Ndiyo
Mheshimiwa Haji Juma Sereweji	Hakuwepo
Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba	Hakuwepo
Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby	Hakuwepo
Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah	Hakuwepo
Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo	Ndiyo
Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti	Ndiyo
Mheshimiwa John Magalle Shibuda	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Said Sinani	Ndiyo
Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame	Ndiyo
Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman	Hakuwepo
Mheshimiwa Abdallah Salum Sumry	Ndiyo
Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi	Ndiyo
Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir	Ndiyo
Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim	Ndiyo
Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele	Ndiyo
Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla	Ndiyo
Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu	Ndiyo
Mheshimiwa Anastazia James Wambura	Ndiyo
Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi	Ndiyo
Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir	Ndiyo
Mheshimiwa Mussa Azan Zungu	Ndiyo

**SPIKA:** Katibu, kuna orodha ya Wenyeviti, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid hakutokea popote

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, imekaa sawa alinitaja

**SPIKA:** Kumbe alishakutaja vizuri. Naomba tushauriane suala la kisheria wakati tunasubiri matokeo; ni dhahiri kabisa kwamba, akidi ipo, kwa mujibu wa Kanuni ya 77; kura ya maamuzi lazima tuwepo zaidi ya nusu na hata kabla ya kuhesabu nilikuwa najua kwamba, tupo zaidi ya nusu, kulingana na jinsi tulivyokaa. Wale ambaao wametamka tu nadhani kwa utundu kwamba, Samweli Sitta hajapiga kura, jibu lao lipo katika Kanuni ya 79(2): “Spika, wakati amekalia Kiti cha Spika, hatakuwa na kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za ndiyo na siyo zitalingana.” Kura yangu itategemea haya matokeo, kwa hiyo, nasubiri. (*Kicheko*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Nakusaidia, Kanuni ya 68, endelea.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, nimeleta kimemo hapo kwako; wakati unazungumza hapa ulisema tuseme Siyo au Ndiyo, kwa hiyo, mimi nilitamka Siyo, lakini sikueleweka imeelewaka nimetamka Ndiyo; kwa hiyo, naomba kurudia tena kwamba, nimesema Siyo na sikusema Ndiyo. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kila Mbunge aliyemo humu, wakati wa kupiga kura ana kura moja tu, kama ulisema Ndiyo au Siyo, basi chochote kilichoandikwa ndiyo hicho hicho. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Naam endelea.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ulipokuwa unatuelezea hapa kwamba, kura zitakazopigwa ni Ndiyo, Siyo na Sina Uamuji; ninatambua kwa lugha ya kawaida kwamba, siyo inaweza kuwa ni hapana lakini kwa kuwa Bunge letu linaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni zetu na kanuni inasema Ndiyo na Siyo, kwa wale Wabunge waliosema Hapana; je, kwa tafsiri rahisi sio kwamba hawa wameharibu kura zao? (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utamaduni wa Bunge letu, umekuwa ukitafsiri ile Hapana ni sawasawa na Siyo. Ndiyo utamaduni wa Bunge, tumeukuta na tunaendelea nao. Hata kama mtu angesema nakubali, basi tungeitafsiri ni Ndiyo. (*Makofi*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Enhe, Kanuni yetu ni ile ile.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68; wakati tunasubiri matokeo ya kura tulizopiga, naomba unipe mwongozo wako juu ya jambo linalonitatiza, kuhusiana na Sheria ya *Provisional Revenue Collection Act, 1962*, ambayo inaipa Serikali ruhusa ya kuanza kutumia na ku-*collect* kabla Bunge halijafikia mwisho kwa utaratibu wetu wa zamani na kupilisha *The Finance Bill*; kwa kuwa tumetengua utaratibu na sasa *Finance Bill* tunaitela kesho, naomba mwongozo wako; ile sheria inayoiruhusu Serikali tuitengue Serikali ianze ku-*collect* na kutumia kabla Bunge halijaisha; na je, ile sheria ambayo inaruhusu Serikali kuanza ku-*collect* na kutumia kabla kama ilivyokuwa zamani imetenguliwa?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kaboyonga, anawahisha shughuli ambayo tutaanza kuishughulikia kesho. Kesho ndiyo tutajadili *Finance Bill* na maelezo yote kuhusu shughuli hii, yatatoka moja kwa moja kwa Serikali yenyewe. Kwa hiyo, kwa mujibu wa kanuni zetu, nisingetakiwa sasa kutoa mwongozo wakati shughuli yenyewe inakuja kesho na majibu yote yatapatikana kesho. (*Makofi*)

Kuna pendekezo limekuja hapa kwamba, kwa sababu Bunge hili lina nyenzo za kuweza kupiga kura kwa mpango wa *electronic*, Katibu aharakishe utaratibu huo ili tusiwe katika hali kama hii; nadhani itakuwa jambo zuri. (*Makofi*)

## **MATOKEO YA KURA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hesabu za Katibu Mezani Mwanaume na Katibu Mezani Mwanamke hazikubaliani, kwa hiyo, pengine nichukue hesabu za mwanamke ni waaminifu zaidi. (*Kicheko*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kuna *rigging*?

**SPIKA:** Nawaangalia vizuri hapa.

Waheshimiwa Wabunge, matokeo ni kama ifuatavyo: Jumla ya Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba tulivyo sasa ni 318 (ukimtoa Spika); hakuna kura iliyoharibika kwa sababu ni kutamka; kura zisizo na uamuzi ni 2; Hapana ni 33; Wasiokuwepo 63; na kura za Ndiyo ni 221. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa matokeo hayo, nawaarifu kwamba, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limepitisha Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2009/2010. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimewasiliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, imeonekana si rahisi kwa Wizara ya Fedha kuleta Muswada Fedha saa kumi na moja, kwa hiyo, amenishauri kwamba, tubaki katika ratiba.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na uamuzi huo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 06.55 mchana Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 19 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)